# UBAADAUSASA KAMA KUNGA YA UANDISHI KATIKA RIWAYA ZA *DUNIA YAO* (2006) NA *NYUSO ZA MWANAMKE* (2010) ZA S. A. MOHAMED NA *UNAITWA NANI?* (2008) YA K. W. WAMITILA

**NA**

**MUIGAI MARY NJAMBI**

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA, KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2024**

# IKIRARI

**MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa katika chuo kikuu kinginecho ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamifu. Haki zote zimehifadhiwa na hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:________________________________ Tarehe:______________________

**Muigai Mary Njambi**
**SASS/DPHIL/KIS/02/11**

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa kibali chetu kama wasimamizi kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi:________________________________ Tarehe:______________________

**Prof. Issa Y. Mwamzandi**

Idara ya Sanaa na Elimu,

Chuo Kikuu cha Kabianga,

Kericho-Kenya.

Sahihi:________________________________ Tarehe:______________________

**Prof. Robert W. Oduori**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi

Eldoret- Kenya.

# TABARUKU

Kwa marehemu babangu, Geoffrey Muigai Njoroge

Kwa kunipeleka shuleni na kunitia shime ya kusoma hadi kileleni.

Na mamangu mpendwa, Gladys Njoki Muigai

Kwa kunipenda na kunifunza kuwajibika maishani.

Na kwa ndugu na jamaa

Kwa kuwa nguzo muhimu maishani mwangu.

# SHUKURANI

Kukamilika kwa tasnifu hii hakungewezekana bila msaada, ushirika na wosia niliopokea kutoka kwa watu mbalimbali. Sina budi kuwatolea shukurani zangu wote waliohusika kwa njia moja au nyingine.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hekima, nguvu na afya njema hadi nikaweza kuikamilisha tasnifu hii.

Natoa shukurani kwa wasimamizi wangu Prof. Issa Mwamzandi na Prof. Robert Oduori kwa kunielekeza katika kila hatua ya uandishi wa kazi hii. Nawashukuru kwa kunivumilia na kunipa shime wakati nilihisi kama ningelemewa.

Ningependa kuwatolea shukurani za dhati walimu wangu wote katika masomo haya ya uzamifu kwa kuniongezea maarifa na kunielekeza katika hatua tofauti za kuiandika tasnifu hii. Shukurani za pekee ziwaendee Bw. Collins Mumbo na Dkt. Emmanuel Satia kwa mwongozo wenu.

Pia nawashukuru wahadhiri na wafanya kazi katika idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi kwa kunihimiza na kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu nilipokuwa katika hali ya kukata tamaa.

Natoa shukurani za dhati kwa familia yangu kwa kunitia moyo hadi nikaikamilisha kazi hii. Mlijitolea kwa hali na mali na mchango wenu daima utabaki katika kumbukumbu zangu. Maombi yenu kwangu na yawe manukato mazuri mbele ya Mungu na awajalie kwa kila njia. Bila msaada wenu nisingeweza kuikamilisha kazi hii.

Siwezi kuwasahau marafiki zangu kwa mchango wenu katika mchakato mzima wa kuiandika tasnifu hii.

# IKISIRI

Riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika miaka ya hivi karibuni zinakaidi uandishi uliozoeleka wa kimapokeo uliopendekezwa na akina Aristotle, na kugeukia mtindo mpya wa uandishi wa kimajaribio wa kibaadausasa. Utafiti huu basi unachunguza uandishi wa kibaadausasa katika riwaya zilizoteuliwa za Kiswahili zilizoandikwa katika K21, yaani, *Dunia Yao, Nyuso za Mwanamke* na *Unaitwa Nani*? Riwaya hizi zina matumizi mengi ya uhalisia mazingaombwe ambayo huenda kinyume na kaida za uhalisia. Licha ya hayo, waandishi wa riwaya hizi hurejelea matini nyingine katika kazi zao zikiwemo za kifasihi, kidini, kisanaa, kihistoria, kifalsafa na kisaikolojia. Hata hivyo, uandishi huu mpya haujafanyiwa utafiti wa kutosha ili kuubainisha katika maandishi ya fasihi ya Kiswahili na kuonyesha athari zake kwa msomaji wa kazi hizi. Lengo la utafiti lilikuwa ni kubainisha na kuhakiki vipengele vya ubaadausasa katika riwaya zilizotafitiwa kama vile matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi, matumizi ya uhalisia mazingaombwe na matumizi ya mwingiliano matini. Utafiti huu uliegemea katika falsafa ya ubaadausasa na kuongozwa na nadharia ya ubaadausasa ambayo hupendekeza uanuwai wa mawazo kwa kukaidi kuwepo na mtazamo mmoja wa kueleza ulimwengu na tajriba za binadamu, au simulizi kuu. Usampuli wa kimaksudi ulitumika kupata data kwa kujikita katika riwaya zilizoandikwa katika K21 na ambazo zilidhihirisha vipengele vya ubaadausasa. Data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa riwaya zilizoteuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa iliyodhihirika kwa wingi katika riwaya hizo. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa na kuwasilishwa kwa lugha ya nathari. Utafiti uligundua kuwa baadhi ya vipengele vya kibaadausasa vilitumiwa kimaksudi na waandishi ili kukaidi simulizi kuu zilizotawala. Riwaya za kibaadausasa zilitumia uchopekaji wa vipande vya simulizi kuvuruga urazini, mshikamano na muumano wa usimulizi wa riwaya za kimapokeo. Kimaudhui, riwaya hizi zinapuuza na kutilia shaka simulizi kuu inayohusiana na maana ya uhuru katika mataifa mengi ya Afrika kwa kusaili mwelekeo chanya uliohusishwa uhuru kuwa ungeleta maendeleo katika mataifa na badala yake kuonyesha hali ya utamauishi inayotawala mataifa haya. Riwaya hizi pia zinasaili hali ya utumwa miongoni mwa Waafrika wanaohamia ughaibuni kutafuta maisha bora humo kwa kuonyesha changamoto ambazo wahamiaji hupitia. Hali kadhalika, riwaya hizi zinafichua itikadi zilizofichika ndani ya misaada inayoletwa katika mataifa ya Afrika kutoka mataifa ya Ulaya na kuibainisha kama chambo cha kueneza ukoloni mamboleo kwa urahisi katika K21. Hali kadhalika, katika riwaya zilizotafitiwa mipaka kati ya uhalisia na umazingaombwe imezibwa kupitia matumizi ya wahusika na matukio ya ajabu kama vile mizuka, vivuli, wafu pamoja na wahusika wenye nguvu za kiajabu ili kuwakilisha hali halisi ya dunia ya sasa ambayo imejaa mambo mengine ya ajabu yasiyoelezeka. Fauka ya hayo, utafiti uligundua kuwa riwaya zilizoteuliwa zilitumia mwingiliano matini kwa wingi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunahitimisha kwa kusema kuwa mtindo wa uandishi wa ubaadausasa umetumika sio tu kama mbinu ya kiumbuji bali katika kudhihirisha fujo, ghasia na ukosefu wa mshikamano katika ulimwengu wa K21 kwa kukaidi simulizi za awali. Utafiti huu unatoa mchango katika taaluma ya usomi kwa kueleza vipengele vya ubaadausasa katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu na namna ya kuzisoma kwa jumla.

## ABSTRACT

Kiswahili novels written in the recent past have a tendency that breaks away from conventionality and have turned to more experimental forms of literary composition. This form of writing is a shift from the traditional Aristotelian mode of representation that has dominated the literary space for a while now and there is a discernible trend towards postmodernist writing of literary works. This study examines the postmodernist style of composition in selected Kiswahili novels of the twenty first century, namely, *Dunia Yao*, *Nyuso za Mwanamke* and *Unaitwa Nani*? These novels are replete with the use of magical realism that subverts the rules of conventional realism. Further, the writers allude to other texts, be they literary, religious, artistic, historical, philosophical and psychological in nature. Compared to other conventional writing modes, little, however, has been done to appreciate the new dimension that authorship has taken in Kiswahili literary composition and what these portend to the reader. The objectives of the study were to identify the respective postmodern techniques and examine how they have been used in the selected novels, namely the use of fragmentation, magical realism and intertextuality. The study was grounded on the postmodernism philosophy and guided by the postmodernism theory which advocates for diversity and multiplicity rather than an all-encompassing world view of human experiences, referred to as metanarratives. The data was sampled purposively with specific emphasis placed on literary texts that were composed in the 21$^{st}$ century and with a leaning toward postmodern tendencies. Data was collected through a critical reading of the novels. Tenets of postmodernism that featured most in the selected novels informed the main topics for discussion. The data was qualitatively analyzed using the tenets of postmodernism theory and presented in prose form. The study revealed that some of the postmodernist styles are deliberately used by writers to show skepticism towards dominant metanarratives. The postmodernist novel uses fragmentation to disrupt the rationality, unity and linearity of the traditional narrative fiction. Thematically, the novels show skepticism toward the meaning of independence in post-colonial Africa by challenging its optimistic view and portraying a state of disillusionment as far as national development is concerned. The novels also question the state of servitude among African immigrants to western countries in search for greener pasture. In addition, the novels unearth the ideology that punctuate aid by the West to African countries and depicts them as baits to easily propagate neo colonialism in the 21$^{st}$ century. Further, the boundary between the real and the magical is blurred through the use of characters such as ghosts, spirits, the dead and human beings with magical powers to represent the unexplainable experiences of the world today. Moreover, the postmodern novels use intertextuality immensely. The study concludes that the postmodernist style of writing has been used deliberately by the writers not only for aesthetic purposes but more importantly to depict the chaos, disorder and fragmentation of the world in the 21$^{st}$ century. This study makes a contribution to scholarship through the understanding of the tenets of postmodernism in Kiswahili novels and the approach that readers can enlist for a successful reading of these novels.

# YALIYOMO

IKIRARI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKURANI ..... iv
IKISIRI ..... v
ABSTRACT ..... vi
YALIYOMO ..... vii
ORODHA YA VIFUPISHO ..... xi
UFAFANUZI WA DHANA ..... xii
TAFSIRI YA ISTILAHI ..... xiii
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**MISINGI YA UTAFITI ..... 1**
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli wa Utafiti ..... 1
1.2 Suala la Utafiti ..... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ..... 5
1.4 Maswali ya Utafiti ..... 6
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 8
1.7 Upeo wa Utafiti ..... 8
1.8 Misingi ya Kinadharia ..... 9
1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti ..... 17
1.10 Mbinu za Utafiti ..... 32
1.10.1 Usampuli ..... 33
1.10.2 Ukusanyaji data ..... 34
1.10.3 Utafiti Maktabani ..... 35
1.10.4 Uchanganuzi wa Data ..... 37
1.10.5 Changamoto katika Utafiti ..... 35
1.11 Hitimisho ..... 38
**SURA YA PILI ..... 39**
**DHANA YA UBAADAUSASA NA SIFA ZAKE BAINIFU KATIKA FASIHI ..... 39**
2.0 Utangulizi ..... 39
2.1 Dhana ya Usasa ..... 40

2.2 Dhana ya Ubaadausasa ........................................................................................ 44
2.3 Ubaadausasa Katika Muktadha wa Kihistoria ...................................................... 46
2.4 Ubaadausasa katika Muktadha wa Kinadharia na Kifalsafa ................................. 48
2.4.1 Jean-Francois Lyotard: Uhakiki wa Simulizi Kuu ......................................... 49
2.4.2 Jean Baudrillard: Uhakiki wa Uwakilishaji wa Ishara katika Ulimwengu wa Kiteknolojia ........................................................................................ 52
2.4.3 Jacques Derrida, Michel Foucault, Luce Irigaray, Gilles Deleuze & Felix Guattari na Fredric Jameson ........................................................................ 53
2.5 Ubaadausasa kama Mtindo Maalum wa Kiuandishi na Kisanaa .......................... 57
2.6 Ubaadausasa Katika Fasihi ya Kiswahili ............................................................. 58
2.7 Sifa Bainifu za Ubaadausasa katika Fasihi .......................................................... 62
2.7.1 Uhakiki wa Simulizi Kuu ................................................................................ 63
2.7.2 Ukosefu wa Udhabiti katika Vipengele vya Ukweli na Maana ...................... 64
2.7.3 Mwingiliano Matini ......................................................................................... 65
2.7.4 Uanuwai wa Mawazo ...................................................................................... 65
2.7.5 Uhalisia Mazingaombwe ................................................................................. 66
2.7.6 Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi ............................................................. 67
2.8 Hitimisho ............................................................................................................. 69
**SURA YA TATU ........................................................................................... 70**
**MATUMIZI YA MBINU YA UANDISHI YA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI NA UHAKIKI WA SIMULIZI KUU ........................................ 70**
3.0 Utangulizi ............................................................................................................ 70
3.1 Dhana ya Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi kama Mbinu ya kiubunifu ......... 71
3.2 Uhakiki wa Maana ya Uhuru katika Mataifa ya Afrika ........................................ 73
3.2.1 Ukosefu wa Haki na Usawa ............................................................................ 75
3.2.2 Ukosefu wa Maendeleo ................................................................................... 79
3.2.2.1 Ukosefu wa Usalama ..................................................................................... 81
3.2.2.2 Uchafuzi wa Mazingira na Ukosefu wa Ajira ............................................... 82
3.2.2.3 Miundo Misingi Duni na Umaskini Uliokithiri ............................................. 84
3.3 Ajenda za Mataifa ya Ulaya na Mashirika yasiyo ya Kiserikali Barani Afrika ..... 89
3.3.1 Uenezaji wa Kasumba Potovu Dhidi ya Mataifa ya Afrika ............................ 89
3.3.2 Utoaji wa Misaada na Uanzishaji wa Miradi Tofauti ..................................... 97
3.3.3 Uwekezaji katika Mataifa ya Afrika ............................................................. 104
3.3.4 Amri na Masharti Kutoka Mataifa ya Ulaya ................................................ 109

3.4 Uhamiaji katika Nchi za Ulaya: Kiini na Changamoto Zake ..............................114
3.4.1 Sababu za Uhamiaji ........................................................................115
3.4.2 Changamoto zinazoambatana na Uhamiaji ..........................................118
3.4.3 Mahitaji ya Kifedha ........................................................................118
3.4.3.1 Ukosefu wa Ajira ........................................................................122
3.4.3.2 Ukosefu wa Makazi Bora ..............................................................124
3.4.3.4 Kukumbwa na Magonjwa ...............................................................124
3.5 Hitimisho ........................................................................................127
**SURA YA NNE ....................................................................................130**
**UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UHALISIA MAZINGAOMBWE.130**
4.0 Utangulizi ........................................................................................130
4.1 Dhana na Sifa za Uhalisia Mazingaombwe ...........................................130
4.2 Uhalisia Mazingaombwe katika Riwaya za Utafiti ..................................136
4.2.1 Binadamu wa Kawaida wenye Uwezo wa Kiajabu ..................................136
4.2.2 Matumizi ya Wahusika na Matukio ya Ajabuajabu ...................................140
4.3 Hitimisho ........................................................................................149
**SURA YA TANO ..................................................................................151**
**UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA MWINGILIANO MATINI ..........151**
5.0 Utangulizi ........................................................................................151
5.1 Dhana ya Mwingiliano Matini katika Fasihi ...........................................152
5.2 Dhima ya Mwingiliano Matini katika Kazi za Kibaadausasa .............................154
5.3 Mwingiliano Matini katika Riwaya za Utafiti ..........................................156
5.3.1 Urejeleaji wa Kazi za Fasihi ya Kiswahili ..............................................157
5.3.2 Urejeleaji wa Fasihi ya Kiingereza ......................................................165
5.3.3 Urejeleaji wa Filamu ........................................................................169
5.3.4 Marejeleo ya Kidini ..........................................................................170
5.3.5 Marejeleo ya Mashujaa wa Kihistoria ...................................................173
5.3.6 Marejeleo ya Wanafalsafa na Wanasaikolojia .........................................175
5.4 Hitimisho ........................................................................................181
**SURA YA SITA ....................................................................................183**
**MUHTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ............183**
6.0 Utangulizi ........................................................................................183
6.1 Muhtasari wa Matokeo ......................................................................183
6.2 Hitimisho ........................................................................................194

6.3 Mapendekezo ........................................................................................... 196
MAREJELEO ................................................................................................. 197

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **DY** | - | Dunia Yao |
| **K21** | - | Karne ya ishirini na moja |
| **n.w** | - | Na Wengine |
| **NZM** | - | Nyuso za Mwanamke |
| **Ty** | - | Tafsiri Yangu |
| **UNN** | - | Unaitwa Nani? |

## UFAFANUZI WA DHANA

**Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa-** Ni mtindo wa uandishi unaokaidi mtindo uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Badala yake unatumia vipengele vya ubaadausasa kuwasilisha kazi ya fasihi. Vipengele hivi vinatokana na mihimili mikuu ya nadharia ya ubaadausasa kama vile matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi, matumizi ya uhalisia mazingaombwe na matumizi mengi ya mwingiliano matini. Kimaudhui, mtindo wa uandishi wa kibaadausasa hulenga kupuuza na kusaili simulizi kuu za aina mbalimbali .

**Simulizi kuu** – ni jumla ya imani na mambo yaliyozoeleka na kukubalika kama ukweli au yanayodai kuhodhi ukweli halisi.

**Uchopekaji wa vipande vya simulizi** – ni mbinu mojawapo ya uandishi wa riwaya za kibaadausasa ambao unakiuka uandishi wa kimapokeo wa uhalisia ambapo matukio yalifuatana kiwakati. Badala yake unatumia vipengele vya simulizi vilivyochupwa huku na kule kama njia ya kudhihirisha ukosefu wa mshikamano katika K21

## TAFSIRI YA ISTILAHI

Ilikuwa muhimu kutoa tafsiri ya baadhi ya istilahi zilizotumika katika utafiti huu kutokana na sababu kuwa uwanja huu wa utafiti haujaandikiwa sana kwa lugha ya Kiswahili. Wataalamu mbalimbali wa Kiswahili hivyo basi hutumia istilahi tofauti kwa dhana moja. Tafsiri hii basi itampa msomaji ufahamu wa istilahi hizi kama zilivyotumika katika utafiti huu.

Baadausasa – *Postmodern*

Enzi za Kati - *Middle Ages*

Itikadi- *Ideology*

Jamii tumizi – *consumer society*

Kibaadausasa – *Postmodernist*

Kipindi cha Mwamko mkuu – *Reinaissance*

Kipindi cha Ulimbwende- *Romanticism*

Maarifa kamili- *absolute knowledge*

Maigizo/uigaji - *simulacra/ simulation*

Mwamko wa Kitaaluma - *Enlightment project*

Mwingiliano matini – *Intertextuality*

Nadharia ya udodosinafsia – *psychoanalytic theory*

Nakshi - *decoration*

Sanaa za kimaono - *visual arts*

Siasa za kifalsafa - *Philosophical politics*.

Simulizi kuu – *Grand narratives*

Simulizi ndogo – *mini narratives*

Tamaduni pendwa - *Popular culture*

Tamaduni za juu - *High culture*

Tanzo la Edipode – *Oedipus complex*

Uanuwai - *Pluralism*

Ubaadausasa – *Postmodernism*

Ubidhaishaji wa vitu - *Consumerism*

Ubunaji – *fabulation*

Ubunaji wa visasili – *myth creation*

Uchopekaji wa vipande vya simulizi – *Fragmentation*

Uhakiki Makinifu wa Mazungumzo – *Critical Discourse Analysis*

Uhalisia mazingaombwe – *Magical Realism*

Uhalisia- *Realism*

Uigaji/wigo – *Pastiche*

Ujumi - *aesthetics*

Ukuaji wa viwanda – *industrialization*

Ukweli halisi – *absolute truth*

Upingaji kaida - *Antifoundational*

Usasa- *Modernism*

Usimulizi usiokuwa na mshikamano imara - *discontinuous narratives*

Utafiti kiustahilifu/wa kithamana – *Qualitative research*

Wizi wa maadishi- *Plagiarism*

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inahusu misingi ya utafiti iliyotumika katika utekelezaji wa utafiti na uchanganuzi wa data. Sura hii imegawika katika sehemu kumi: Sehemu ya kwanza imefafanua usuli wa suala la utafiti huku sehemu ya pili ikiangazia suala la utafiti. Katika sehemu ya tatu, tunapata malengo ya utafiti ambapo malengo matatu yamebainishwa. Maswali ya utafiti yaliyoongoza utafiti huu yamefafanuliwa katika sehemu ya nne. Sehemu ya tano inaeleza sababu za kuchagua mada ya utafiti. Umuhimu wa utafiti umefafanuliwa kwa kina katika sehemu ya sita huku sehemu ya saba ikiangazia upeo na mipaka ya utafiti. Katika sehemu ya nane misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu imeelezwa kwa tafsili. Maoni na maelezo ya wataalam mbalimbali pamoja na tahakiki zinazohusiana na mada ya utafiti zimeangaziwa katika sehemu ya tisa. Mbinu za utafiti zilizotumika kutekeleza utafiti huu zimejadiliwa katika sehemu ya kumi. Katika sehemu hii mbinu na vifaa vilivyotumika katika kukusanya data vimejadiliwa. Vilevile, mikakati iliyotumika katika kufikia sampuli wakilishi imejadiliwa. Sehemu hii imehitimishwa na ufafanuzi kuhusu namna data ilivyokusanywa, ilivyochanganuliwa na hatimaye ilivyowasilishwa.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Mtindo wa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa ulianza kuwa maarufu katika fasihi ya kilimwengu tangu miaka ya sitini ulipoanza kutumika katika nchi za kimagharibi (Lewis 2001). Hata hivyo, katika fasihi ya Kiswahili mtindo huu umeanza kutumika katika mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini kama njia ya kuonyesha mabadiliko yanayotokea katika dunia ya sasa hasa kutokana na utandawazi (Khamis 2005; Traore 2014). Kuzuka kwa mtindo huu wa uandishi kumeleta mabadiliko makubwa katika

uandishi wa fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya. Kwa mujibu wa Senkoro (2011) kila utanzu huambatana na kanuni au mambo yanayojitokeza mara kwa mara katika uwanja husika. Katika riwaya, hususan riwaya ya Kiswahili, mtindo wa uandishi uliozoeleka ni ule wa kimapokeo na ambao ulijikita katika uhalisia. Hata hivyo, baadhi ya riwaya za Kiswahili hasa zile zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja zinaenda kinyume na mtindo huu wa uhalisia na badala yake kutumia mtindo wa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa.

Akizungumzia kuhusu fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio, Senkoro (2011) anasema kwamba, kazi yoyote ile inayoweza kuitwa ya kimajaribio, haina budi kuambatana na upya ambao unaweza kuelezeka kinadharia. Upya unaojitokeza katika riwaya za kimajaribio za kibaadausasa umejitokeza katika muundo na mtindo wa riwaya zenyewe. Kwa kuzingatia muundo, baadhi ya riwaya za kibaadausasa hazina muungano na muumano wa hadithi tangu mwanzo hadi mwisho; matukio yanaonekana kama vipengele vinavyojitenga na vingine badala ya vipengele hivi kuingiliana, kujengana na kukamilishana. Kuna vipande vidogovidogo vya visa ambavyo hutumika kama malighafi ya kuunga simulizi hizo zilizochupwa huku na huko (Bertoncini 2006; Khamis 2008). Aidha, kimtindo kuna wingi wa urejeleo matini na matumizi ya uhalisia mazingaombwe (Mwamzandi 2013; Khamis 2007; Lewis 2001). Kazi hizi hazilengi kuhodhi ukweli kama zilivyo simulizi za jadi za akina Plato na Aristotle[1] na zinakiuka kaida za uhalisia zilizozoeleka na kutumiwa katika riwaya ya Kiswahili.

[1] Plato na Aristotle walichukulia sanaa kama chombo cha kufunza maadili na kifaa muhimu kilichoathiri tabia za mtu binafsi. Kutokana na hali hii, kazi za kifasihi zilipaswa kuuwakilisha ukweli, sio kama ulivyo hasa, bali kama unavyopaswa kuwa. Hivyo basi, Mhusika katika kazi ya kisanaa alipaswa kumiliki sifa zinazoambatana na taaluma, cheo au tabaka lake katika jamii. Kwa mfano, majagina wakuu hawangepaswa kuwakilishwa kama watu fisadi, wasioaminika na waovu kwa sababu jambo hili lingeathiri maadili ya hadhira lengwa kwa njia hasi (Tilak 1993).

Katika misingi ya kihalisia, sanaa lazima iaminike; matukio huakisi hali halisi ya maisha ya watu na usawiri wa wahusika husadiki maisha yao ya kila siku. Vilevile, kazi za kihalisia husisitiza mantiki na muundo wenye muwala ambapo vipengele tofauti vya fani na maudhui huingiliana, kujengana na kukamilishana. Sauti ya mwandishi huwa moja na kueleweka kwa misingi ya mantiki. Matukio huelezwa wazi na hufuatana kiusanjari. Hata wakati mbinu rejeshi na mbinu tangulizi zinapotumika, matukio na vitukio hufungamana kwa njia fulani hivi kwamba uhusiano kati ya kisababishi na matokeo hubainika wazi (Khamis 2008). Baadhi ya riwaya za Kiswahili hata hivyo zinatumia mtindo unaokiuka kaida hizi za kihalisia zinazosisitiza uyakinifu, mantiki na muwala katika kazi ya fasihi na badala yake kutumia mtindo wa kimajaribio wa ubaadausasa.

Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa umetumiwa kuyashughulikia masuala kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia kwa namna ambayo uhalisia haungeweza kuyazungumzia (Lewis 2001; Wamitila 2001; Khamis 2005). Wataalam mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili ambao wametumia mtindo huu wa ubaadausasa katika riwaya zao ni pamoja na E. Kezilahabi, E. Mkufya, K.Wamitila, S.A. Mohamed na C. Momanyi (Mwamzandi 2013; Waliaula 2010; Bertoncini 2006; Khamis 2008). Wengi wa waandishi hawa ni maprofesa na wahadhiri katika vyuo vikuu mbalimbali. Kwa mujibu wa Bertoncini (2009) waandishi wa fasihi ya Kiswahili nchini Kenya, Tanzania bara na kisiwani Unguja wenye elimu ya juu, wawe wahadhiri au watafiti, hawajishughulishi na kuandika kazi zenye ploti sahili zitakazowafurahisha wasomaji na kuwapa funzo la kimaadili. Badala yake, wanalenga kuibuka na kazi zenye ubora wa hali ya juu wa kisanaa, zinazozungumzia masuala nyeti ya kijamii na kisiasa na zinazohusisha sio tu maadili ya Kiafrika bali pia athari kutoka nchi za Kimagharibi. Bertoncini (2009) amewaweka waandishi wa fasihi ya Kiswahili katika makundi mawili; kundi la

wanazuoni na waandishi wa fasihi pendwa. Maneno ya Bertoncini (2009) yanadhihirisha kwamba kazi za kifasihi zilizoandikwa na wanazuoni ni za kiwango cha juu zaidi kisanaa na kimaudhui zikilinganishwa na kundi la waandishi wanaoandika kazi za fasihi pendwa. Hata hivyo, ni muhimu kutaja hapa kwamba kuna waandishi wachache kama vile Mohammed Said Abdulla na Mohamed Suleiman ambao kazi zao zimesomwa shuleni na kujadiliwa katika miktadha mbalimbali, licha ya kuwa hawana elimu ya juu ya kiwango cha uprofesa. Kilicho muhimu hapa ni kubainisha kwamba kazi tunazozitafitia na ambazo zimeandikwa na wahadhiri wa vyuo vikuu ni kazi zinazohitaji umakinifu wa msomaji ili aweze kuzielewa. Kama wanavyosema Magaju (2004) na Bakari (2008) mtindo uliotumika katika kazi hizi umezifanya kazi hizi kuwa ngumu kusomeka na kueleweka. Aidha, ingawa waandishi hawa wanauona mtindo wa ubaadausasa kama njia mwafaka ya kuuwasilisha ujumbe wao, mtindo huu umetajwa kama wenye uwezo wa kuitenga hadhira hasa isiyobobea katika fani mamboleo za kifasihi (Mwamzandi 2013).

Pamoja na ithibati iliyotolewa na wataalam mbalimbali kuhusiana na hulka na maumbile ya riwaya mpya ya K21 hakuna utafiti mwingi wa kina uliofanywa wa kufafanua sifa sadifu za tungo hizi za kileo hasa kwa kujikita katika kazi mahususi. Hivyo basi, ipo haja ya kuchanganua umbo la riwaya hizi ili kubaini sifa zake bainifu.

### 1.2 Suala la Utafiti

Kazi za fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali kuanzia mwongo wa mwisho wa K20 na mwanzo wa K21zinaonekana kuwa changamano katika viwango mbalimbali. Katika kiwango cha msuko, riwaya hizi hazina mshikamano na muumano wa hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Badala yake, vipengele katika hadithi vimechupwa huku na kule na kuunda vipande vidogo vidogo vya hadithi, visa na matukio. Aidha, hadithi, matukio na visa havihodhi ukweli katika mantiki ya maisha ya

kawaida kutokana na matumizi ya vipengele vya kifantasia na uhalisiamazingaombwe vinavyoenda sambamba na uhalisia. Isitoshe, riwaya hizi zina matumizi mengi ya mwingilianomatini ambao hutenga kimaksudi hadhira isiyobobea katika fani mbalimbali za kijamii na hivyo kuleta ugumu katika kufuatilia dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika kazi hizi. Riwaya hizi basi zinaonekana kwenda kinyume na riwaya za kimapokeo zilizoandikwa kwa muundo sahili wa ploti uliojikita katika uhalisia ambapo matukio yalikuwa na mshikamano na yalifuatana kiwakati. Aidha, katika riwaya za kimapokeo wahusika, mandhari na matukio yaliakisi uhalisia kama tunavyoujua. Ni kutokana na upya huu unaokaidi mtindo wa uandishi wa riwaya za kimapokeo ambapo utafiti huu umezihakiki riwaya zilizoandikwa katika K21 ili kufafanua sifa zake bainifu kwa kujikita katika riwaya tatu za Kiswahili zilizoteuliwa. Riwaya zenyewe ni *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) za S. A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2008) iliyoandikwa na K. W. Wamitila. Sifa bainifu za riwaya za K21 zilizojadiliwa katika tasnifu hii ni uchopekaji wa vipande vya simulizi, matumizi ya uhalisia mazingaombwe na mwingilianomatini kama vipengele vya mtindo katika riwaya za ubaadausasa. Kwa kutumia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa kama inavyofafanuliwa na Lyotard (1979), tasnifu hii vilevile imehakiki simulizi kuu mbalimbali zinazojitokeza tunapojadili vipengele vya mtindo wa ubaadausasa kama tulivyovitaja hapo juu. Baadhi ya simulizi kuu zilizohakikiwa ni pamoja na simulizi inayohusu maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika na hatimaye simulizi inayohusu uhamiaji kutoka mataifa ya Afrika kwenda Ulaya na athari zake.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti ni kubainisha matumizi ya vipengele vya mtindo wa uandishi wa kijarabati wa ubaadausasa katika riwaya ya Kiswahili, hususan riwaya za *Dunia Yao*

(2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), na *Unaitwa Nani?* (2008). Katika kulitimiza lengo hili utafiti umeongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kufafanua dhana ya ubaadausasa na sifa zake bainifu katika fasihi ya Kiswahili.
ii. Kubainisha kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi kama mtindo wa kiubunifu unaotumika kuhakiki simulizi kuu mbalimbali katika riwaya zilizotafitiwa.
iii. Kuchanganua kipengele cha uhalisiamazingaombwe kama sifa mojawapo ya vipengele vya mtindo katika riwaya zilizoteuliwa.
iv. Kubainisha mtindo wa mwingilianomatini na athari zake katika kufuatilia dhamira tofauti katika riwaya zilizoteuliwa.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, kuna fasili moja faafu ya dhana ya ubaadausasa na sifa zake bainifu ni zipi katika fasihi ya Kiswahili?
ii. Mtindo maalum wa uandishi wa kibaadausasa unaohusu uchopekaji wa vipande vya simulizi umetumika kuhakiki simulizi kuu zipi katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu?
iii. Matumizi ya uhalisiamazingaombwe kama kipengele cha mtindo katika riwaya za kibaadausasa umejitokezaje katika riwaya zilizotafitiwa?
iv. Je, matumizi ya mwingilianomatini kama kipengele cha mtindo yamejitokezaje katika riwaya za utafiti na yana athari gani katika kufuatilia dhamira za riwaya za utafiti?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mtindo wa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa katika riwaya ya Kiswahili haujashughulikiwa kwa kina hasa kwa kulenga kazi mahsusi za kifasihi. Hili ndilo pengo ambalo utafiti huu ulilenga kuliziba kwa kuhakiki riwaya tatu za Kiswahili

zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Riwaya zenyewe ni *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) zilizoandikwa na S. A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2008) ya K. W. Wamitila. Riwaya hizi zimeteuliwa kwa sababu zimedhihirisha upya katika riwaya ya Kiswahili kwa kukiuka mtindo wa kimapokeo wa uandishi uliozoeleka na ambao ulijikita katika uhalisia. Aidha, riwaya zenyewe zimeandikwa na waandishi mashuhuri katika fasihi ya Kiswahili. Bertoncini (2009) kwa mfano anamtaja Wamitila kama mmoja wa waadishi mashuhuri wa enzi hizi anayefuata nyayo za watangulizi wake kama Said A. Mohamed. Umahiri wa waandishi hawa ni kichocheo kikubwa katika kuchagua riwaya za utafiti huu ili kubainisha upya unaojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Uhakiki wa riwaya hizi basi ni dhihirisho kuwa riwaya ya Kiswahili imeanza kuchukua sura mpya na utafiti huu umechangia katika taaluma na uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

Fasihi haiandikwi katika ombwe tupu bali hulenga kuyashughulikia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Kutokana na rai za wataalam kuwa riwaya za kibaadausasa zinayashughulikia masuala haya kwa njia ambayo uhalisia haungeyashughulikia, utafiti umehakiki masuala ya kijamii, masuala ya kisiasa na masuala ya kiuchumi yanayojitokeza kama aina ya simulizi kuu katika riwaya hizi ili kubainisha ni kwa nini simulizi hizo haziwezi kuaminiwa tena kwa kuwa zimeshindwa kuyaboresha maisha ya wananchi katika mataifa ya Afrika. Utafiti huu pia umebainisha njia mbadala zilizotumika kuyasuluhisha kwa muda baadhi ya matatizo yanayoikumba jamii ya kisasa.

Aidha, kutokana na tetesi kuwa riwaya za kimajaribio hazieleweki kwa urahisi, uhakiki wa riwaya teule unachangia katika kuzielewa kazi za kifasihi zilizoandikwa kwa kutumia mtindo wa uandishi wa ubaadausasa, hasa kwa wanafunzi wa Kiswahili wa vyuo vikuu na wapenzi wa fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unalenga kukuza ujuzi na ufahamu wa sifa bainifu za mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya ya Kiswahili. Katika kufanya hivi wasomi wa riwaya hizi wataweza kuzielewa na vilevile kuzihakiki riwaya nyinginezo za Kiswahili zilizoandikwa kwa kutumia mtindo kama huo.Vilevile, utafiti huu utatumika kama msingi wa kuzihakiki kazi nyingine za kisanaa, kama vile tamthilia na ushairi, zilizoandikwa kwa kutumia mtindo wa ubaadausasa.

Uhakiki wa riwaya zilizozoteuliwa umebainisha maudhui na dhamira tofauti zilizopatikana katika simulizi mbalimbali tulizozihakiki katika riwaya hizi, kama njia ya kuakisi hali halisi ya ulimwengu wa sasa, ulimwengu wa ubaadausasa ambao hauna mshikamano.

Uhakiki wa riwaya za utafiti huu umechangia katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili na lugha ya Kiswahili kupitia utafiti na ni sehemu ya mkusanyiko wa maandishi yaliyoandikwa kwa Kiswahili.

### 1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti ulijikita katika riwaya za Kiswahili ambazo zimeandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Kwa kuwa riwaya zilizoandikwa katika mwongo huu ni nyingi, utafiti huu umechunguza riwaya tatu tu ambazo ni, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) za S.A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2008) ya K. Wamitila. Ingawa waandishi hawa wameandika riwaya nyinginezo, utafiti ulijikita katika riwaya hizi pekee kwa kuwa zilitosheleza mahitaji ya utafiti huu katika kubainisha mtindo wa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa katika riwaya za Kiswahili. Aidha, kunaweza kuwa na kazi nyingine za kifasihi, ziwe riwaya, tamthilia au ushairi zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja na

ambazo zingeweza kubainisha uandishi wa kimajaribio katika kazi za kifasihi. Hata hivyo, utafiti huu haukuzishughulikia kazi hizo ila tu ulijikita katika riwaya tatu zilizoteuliwa. Ingawa uchanganuzi wa data inayohusiana na kipengele cha mwingiliano matini ulihusisha marejeleo ya kazi mbalimbali, marejeleo hayo ni yale yanayopatikana katika riwaya tatu zilizotafitiwa.

**1.8 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya ubaadausasa inayohusishwa zaidi na mwanafalsafa, Jean Francois Lyotard (1979) katika makala yake maarufu, *The Post Modern Condition: A Report on Knowledge.* Hata hivyo, mchango wa wanaubaadausaa wengine kama vile Jean Baudrillard (1981), Fredric Jameson (1991), Michel Foucault (1961), pamoja na Gilles Deleuz na Felix Guattari (1972; 1980) pia umezingatiwa kama tulivyobainisha baadaye katika sehemu hii.

Wataalam mbalimbali kama vile Barry (2002), Klages (2006) na Carter (2006) wanakubali kuwa dhana ya ubaadausasa ni tata na hakuna fasili moja toshelevu ya dhana hii. Hii ni kwa sababu wataalamu wamekosa kukubaliana ni lini hasa istilahi hii ilianza kutumika pamoja na kuwa dhana yenyewe imehusishwa na miktadha na taaluma tofauti na hivyo kufasiriwa kwa njia tofauti. Barry (2002) kwa mfano anasema kuwa dhana ya ubaadausasa ilianza kutumika katika miaka ya 1940 kurejelea mtindo wa usanifu wa majengo ambao ulidhihirisha ujumi ulioenda kinyume na usasa na urazini. Baadaye dhana hii ilihusishwa na sanaa nyingine kama muziki, uchoraji na fasihi. Nao Best na Keller (1991) wanasema kuwa ubaadausasa ulianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa uliohusishwa na vita na mabadiliko mengine mengi ya kijamii. Hata hivyo, Waatalam hawa wanakubaliana kuwa Lyotard (1979) ndiye aliyeuweka msingi imara wa kinadharia wa dhana hii katika makala yake , *The Post Modern Condition: A Report on Knowledge.* Ni katika makala haya ambapo Lyotard alianza kutilia shaka ufaafu wa

nadharia na mifumo ambayo hudai kuhodhi ukweli halisi, au kutoa maelezo bia ya namna tunavyopaswa kuutazama ulimwengu au kutoa suluhisho la matatizo yote ya binadamu. Nadharia na mifumo hii ambayo Lyotard aliiona ikiwa kandamizi ndiyo anayoiita simulizi kuu.

Lyotard alikuwa mwanafalsafa aliyejikita katika masuala ya siasa, jambo ambalo lilimpa kichocheo cha kuihakiki mifumo mbalimbali na hasa iliyohusiana na siasa na kuweka msingi wa nadharia yake ya ubaadausasa. Kwa mujibu wa Sim (2013), Lyotard alishikilia wazo kuwa mwanafalsafa anapaswa kujizatiti ili asijihusishe na kundi tawala na badala yake anapaswa kuzihakiki itikadi zinazoenezwa na kundi tawala na kuunda kile Lyotard anakiita 'siasa za kifalsafa'. Katika siasa hizi za kifalsafa, kundi lililokandamizwa na kundi tawala angalau hupata fursa ya kutoa maoni yao na hivyo basi kuhusika kikamilifu katika mchakato wa siasa. Katika kuunda siasa za kifalsafa, Lyotard alilenga kuwatetea waliopuuzwa na mifumo kandamizi ya kisiasa. Makala ya *The Postmodern Condition* basi ndiyo yaliyoweka msingi wa kuhakiki mifumo hii kandamizi ambayo Lyotard aliita simulizi kuu na hatimaye kuzipuuzilia mbali simulizi kuu hizo alipoona kuwa uwezo na nguvu zilizohalalisha zilikuwa zimeanza kufifia. Uhakiki wa simulizi kuu ni mojawapo ya mhimili mkuu wa nadharia ya ubaadausasa na ambayo Lyotard ameishughulika sio tu katika makala ya *The Postmodern Condition* bali pia katika kazi zake za baadaye kama vile *Heidegger and 'the Jews'*(1988). Katika sehemu inayofuata tumeshughulikia mawazo makuu ya Lyotard kama mwasisi wa nadharia ya ubaadausasa.

Mojawapo ya mawazo makuu ya nadharia ya ubaadausasa kama yalivyoelezwa na Lyotard (1979) ni kuzihakiki na kuzipinga simulizi kuu. Neno simulizi kuu hutumika kurejelea nadharia na mifumo jumuishi inayodai kumiliki ukweli halisi, au kutoa maelezo bia ya hali tofauti za tajriba za binadamu, au kutoa suluhisho la matatizo yote

ya binadamu. Kwa hakika, Lyotard (1979) anaueleza ubaadausasa kama hali ya kuzishuku simulizi kuu. Simulizi kuu halisi ambazo Lyotard alizitilia shaka ni mfumo wa Umarx, mwondoko wa Usasa na mradi wa Mwamko wa Kitaaluma kwa kuwa haikuweza kutimiza malengo ambayo iliahidi. Akieleza kuhusu mfumo wa Umarx kwa mfano, Lyotard anasema kuwa Umarx ulisisitiza kuleta ukombozi wa binadamu kutokana na minyororo ya ubepari. Hata hivyo, haukuweza kuleta uhuru na ukombozi ulioahidi na hivyo basi hauwezi kuaminiwa tena. Kwa mujibu wa Lyotard basi, simulizi kuu kama hizi zinapaswa kupuuzwa.

Sim (2001), Barry (2002) na Rivkin & Ryan (2004) wameorodhesha simulizi kuu nyingine ambazo wanaubaadausasa huzihakiki, nazo ni umuundo, elimu, dini na utamaduni. Kuhusiana na nadharia ya umuundo kwa mfano, wanabaadaumuundo wanarai kuwa mifumo ya kitamaduni haiwezi kufungwa katika miundo maalum kama wafanyavyo wanamuundo. Kwa hivyo, wanabaadaumuundo wanakaidi mifumo jumuishi kama umuundo unaopendekeza njia moja ya kuufasiri ulimwengu. Kipengele hiki basi cha kuzihakiki na kuzipuuza simulizi kuu ndicho kinachoingiza nadharia ya baadaumuundo katika nadharia za ubaadausasa kama tulivyojadili kwa kina katika sura ya pili. Katika tasnifu hii mhimili huu umetumika kuzihakiki simulizi kadhaa kama vile simulizi ya, simulizi ya utamaduni, simulizi kuhusu maana ya uhuru wa Mwafrika, simulizi kuhusu ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika na simulizi kuhusu suala la uhamiaji wa Waafrika katika mataifa ya Ulaya.

Kwa kuwa wanabaadausasa huzipuuza simulizi kuu, Lyotard (1979) anapendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo. Katika muktadha wa siasa ambamo Lyotard alijikita, simulizi ndogo zinarejelea vikundi vya muda vya watu vilivyopaswa kusaili na kurekebisha ukandamizaji ulioenezwa na itikadi ya tabaka tawala, itikadi ambazo Lyotard anaziona kama simulizi kuu. Kinachobainika hapa ni kuwa Lyotard

anapendekeza kuhusishwa na kutiliwa maanani kwa sauti na maoni ya watu wengine, na hasa wale ambao hawako katika tabaka tawala. Katika kufanya hivi, mchakato wa siasa utaongozwa na maoni ya watu tofauti bali si sauti ya itikadi tawala pekee. Wakifafanua dhana hii ya simulizi ndogo, Sim (2001); Wegesa na Macharia (2008) na Rivkin na Ryan (2004) wanasema kuwa simulizi ndogo ndogo huzingatia maslahi ya watu binafsi na huelezea matukio madogo ya kila siku yanayohusiana na mambo ya kiasili wala sio yale yanayobainisha mambo ya kiulimwengu. Ni katika simulizi ndogo ambapo watu hung'ang'ana kueleza mitazamo yao kuhusu mambo yanayowakumba. Kuambatana na mantiki hii, utafiti huu umechukulia simulizi ndogo kama njia mbadala za kupambana na hali tofauti za maisha wakati simulizi kuu zimeshindwa kutekeleza malengo yake. Vilevile, katika fasihi kwa jumla mtindo wa uandishi wa ubaadausasa unaweza kuchukuliwa kama njia mbadala ambayo waandishi katika K21 wanautumia kuuelezea ulimwengu wa sasa kwa njia ya kipekee ambayo haijafungwa na uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Kama anavyosema Khamis (2005, 2008) uhalisia haukuweza kueleza mambo yanayoikumba dunia ya sasa - hali ambayo imepelekea waandishi kukiuka kaida iliyozoeleka ya uandishi wa kihalisia na badala yake kutumia mtindo wa kiuandishi wa kimajaribio katika kazi zao ili kueleza ulimwengu wa sasa. Hii ndio maana utafiti umeuchanganua kwa kina mtindo wa kiuandishi wa kimajaribio wa kibaadausasa ili kubainisha namna nyingine ya kuifasili riwaya pamoja na njia mbadala za kuufasiri na kuuelezea ulimwengu wa sasa.

Kipengele kingine muhimu kinachohusishwa na Lyotard katika nadharia ya ubadausasa ni kutetea haki za wanyonge wanaotengwa na kukandamizwa na mifumo ya kisiasa. Kama anavyosema Sim (2013), sifa hii ya kuwatetea wanyonge wanaokandamizwa na mifumo mbalimbali ni mojawapo ya mambo yanayoendelezwa na mwananadharia Michel Foucault, na kumfanya mmoja kati ya wanaubaadausasa. Kulingana na Lyotard

(1979), sifa mojawapo inayobainisha simulizi kuu ni kupuuza wale ambao wanaenda kinyume na itikadi tawala. Lyotard anabuni dhana ya 'tofauti' kubainisha kuwa wanyonge hutengwa kwa kuwa wanaonekana kuwa upande tofauti na kushikilia msimamo tofauti na ule wa tabaka tawala. Akilifafanua suala hili la 'tofauti', Lyotard (1988) katika kitabu chake, *Heidegger and 'the Jews'* anasimulia tukio la kihistoria ambapo Wayahudi walidhulumiwa chini ya utawala wa Nazi, kwa sababu walikuwa 'tofauti' na Wajerumani. Kwake Lyotard, kudhulumiwa kwa Wayahudi chini ya utawala wa Nazi kunadhihirisha sifa mojawapo ya simulizi kuu ya kupuuza wale ambao hawafuati mifumo yao; wale wanaodhihirisha 'utofauti' unaoenda kinyume na kaida zao. Lyotard anapinga mifumo yoyote ambayo haitambui tofauti zilizoko katika tajriba tofauti za binadamu. Kwa mfano, Lyotard anaupinga usasa kwa kuwa ulipendekeza hali ya kujumuisha *(homogenization)* tajriba tofauti za binadamu. Kwake Lyotard, kutokubali kuwepo kwa tajriba tofauti kunaleta dhana ya ukandamizaji ambao anaukataa anaposema kuwa hakuna sheria bia inayofaa kuongoza mawazo yetu. Ni katika ukweli huu wa Lyotard kuhusu dhana ya 'kutokubali sheria bia' ambapo Carter (2006) anasema kuwa wanaubaadausasa hukataa kuwepo na misingi au taratibu zisizopingika za kuongoza mawazo na imani zetu. Kwa hivyo wanaubaadausasa wanapinga mifumo inayodhibiti tajriba tofauti za binadamu kwa njia yoyote ile. Kwa mfano wanazishuku 'nadharia za kimataifa' ambazo hudai kumiliki ukweli halisi badala ya kuzingatia tofauti anuwai katika tajriba tofauti za maisha ya binadamu. Mojawapo ya nadharia za kimataifa ambayo utafiti huu umehakiki ni dini, pamoja na mifumo mingine isiyosailiwa kama vile utamaduni ili kubainisha itikadi kandamizi zilizofichika ndani yake.

Isitoshe, mawazo ya Lyotard yanapinga nadharia jumuishi kama usasa kwa kuwa nadharia kama hizi zinalenga kuleta mshikamano katika jamii. Wanaubaadausasa hata

hivyo wanajali na kusherehekea 'tofauti' na 'uanuwai' katika tajriba tofauti za binadamu wala si mshikamano. Deleuze na Guattari (1980), kwa mfano, wanapendekeza kufutiliwa mbali kwa mifumo iliyozoeleka na tunayojitambulisha nayo, na badala yake kupendekeza watu wawe wabunifu ili waunde mifumo mipya itakayowawezesha kufikia kilele cha kuwepo kwao. Wanachokimaanisha Deleuze na Guatttari ni kuwa kupitia ubunifu, mabadiliko na 'tofauti' ni mambo mawili ambayo hayana budi kutokea. Katika riwaya ya Kiswahili ya K21, wazo hili la 'tofauti' limedhihirika kupitia uandishi mpya wa kibaadausasa ambao ni tofauti na riwaya za kimapokeo. Tofauti hii imetokana na ukosefu wa mshikamano katika riwaya za kibaadausasa kinyume na zilivyokuwa riwaya za kimapokeo zilizokuwa na muumano na mshikamano wa hadithi na matukio kutoka mwanzo hadi mwisho. Ukosefu wa mshikamano katika riwaya za utafiti huu umedhihirika kupitia uchopekaji wa vipande vya simulizi badala ya kuwa na riwaya inayodhihirisha muumano na mshikamano wa hadithi. Aidha, dhana hii ya 'tofauti' vilevile imetumika kujadili mwingilianomatini kama kipengele mojawapo cha mtindo wa uandishi wa ubaadausasa. Katika mwingilianomatini, waandishi wa ubaadausasa hudhihirisha upya katika riwaya za kibaadausasa kwa kukaidi mawazo ya ulimbwende kuhusu uasili wa mawazo.

Wazo la tatu la Lyotard lililotumika kama msingi wa nadharia ya ubaadausasa linahusiana na suala la kufanya maamuzi hasa yanayojikita katika maadili. Lyotard alilenga kutafuta namna maamuzi yanaweza kufanywa bila kuegemea kwenye simulizi kuu yoyote. Alitumia dhana ya 'ukafiri' au *paganism* kwa Kiingereza ambayo haikuegemea kwenye kitovu au msingi wowote wa kubainisha wema na ubaya. Dhana ya 'ukafiri' ililenga kupuuzilia mbali simulizi kuu zinazodai kumiliki ukweli halisi kama vile dini ambayo inatumika kama msingi wa kuyaelekeza maamuzi yetu. Dini kwa mfano, hutumiwa kama msingi wa kubainisha wema na ubaya, na kupendelea

wema kuliko ubaya. Mawazo haya yanaoana kwa kiasi fulani na yale ya Derrida katika nadharia yake ya udenguzi anayekataa kuwepo kwa mipaka mikali kati ya dhana katika jozi kinzani ambapo dhana moja hupendelewa kuliko nyingine. Kwake Lyotard, iwapo maamuzi yatafanywa kwa kuegemeza kwenye msingi maalum, msingi huo utakuwa simulizi kuu ambayo nadharia ya ubaadausasa inapuuza. Kwa hivyo Lyotard anaeleza kuwa katika 'ukafiri' kila kitendo kinafaa kuangaliwa kivyake kwa kuzingatia muktadha wa kutukia kwake. Wakilifafanua suala hili la Lyotard, Sim (2001) na Rivkin & Ryan (2004) wanaeleza kuwa wanaubaadausasa hukataa kufuata sheria au kaida zozote za kidini na ubinadamu au kuchukua msimamo wowote unaohusiana na maadili. Kwa hivyo, kwa wanaubaadausasa, hakuna jambo nzuri au jambo mbaya na kila mtu huwa huru kutenda anavyotaka kwa kuwa hakuna msingi wowote ule wa kuongoza mawazo na imani zetu.

Mawazo mengine muhimu katika utafiti huu ni yale ya Baudrillard (1981) kuhusu athari za kiteknolojia katika kuufasiri ulimwengu wa kibaadausasa. Mchango wake katika suala hili unapatikana katika kazi yake, *Simulacra and Simulations*. Kulingana na Baudrillard ubaadausasa ni kipindi kilichoanza baada ya Vita vya Pili vya Dunia na ambacho kimetawaliwa na ongezeko la umuhimu wa ishara kupitia maendeleo ya kiteknolojia na kuongozwa na ubepari au kile anachokiita jamii tumizi (consumer society). Kulingana na Bauldrillard (1981) ishara zinapaswa kuhusishwa na watu halisi katika hali halisi ili ziweze hufanya kazi na kutimiza malengo yake. Hata hivyo, ishara katika kipindi cha ubaadausasa hazina uhusiano wowote na uhalisi bali zinaambatanishwa na ubidhaishaji wa vitu tofauti hasa kupitia vyombo vya habari. Baudrillard basi anavishambulia vifaa vya kisasa vya kiteknolojia pamoja na vyombo vya habari kwa kuwa ishara katika vyombo hivi hazihusishwi na chochote katika ulimwengu halisi na hivyo basi havibainishi tofauti kati ya ishara na uhalisi. Hii ndio

maana Baudrillard anaueleza ulimwengu wa ubaadausasa kama ulimwengu wa maigizo na uigaji au *simulacra na simulation,* ambapo hatuwezi kubainisha tofauti kati ya uhalisi na wigo au ishara na uhalisia kwa kuwa tumezipa ishara umuhimu sana. Mwingiliano kati ya ishara na uhalisia kama alivyoueleza Baudrillard (1981), ndio msingi wa uhakiki wa matumizi ya uhalisiamazingaombwe katika utafiti huu kama mojawapo ya vipengele vya ubaadausasa katika fasihi. Katika riwaya za utafiti huu, wahusika na matukio yamechanganya vipengele vya ukweli na ubunifu au uhalisia na fantasia au uhalisia na uhalisiamazingaombwe ili kuunda kazi moja kamilifu ya kibaadausasa.

Kwa kuwa fasihi ya Kiswahili imepitia mabadiliko yanayokaidi uandishi wa kimapokeo, mihimili ya nadharia ya ubaadausasa imetumika kuhakiki mtindo huu mpya wa uandishi kama unavyojitokeza katika riwaya zilizotafitiwa. Kwa muhtasari, vigezo vifuatavyo kama vilivyofafanuliwa na Lyotard na wanaubaadausasa wengine vimetumika kama mihimili ya nadharia ya ubaadausasa kuzihakiki matini mahsusi za utafiti huu:

1. Hakuna ukweli halisi: Kwa wanaubaadausasa hakuna ukweli halisi na hivyo wanakataa kuamini kwamba kunayo misingi isiyopingika au taratibu maalum za kutenda jambo. Wanashuku simulizi kuu zinazodai kuhodhi ukweli halisi usioweza kupingika kama vile dini na utamaduni. Aidha wanaishuku simulizi nyinginezo kama Umarx na Usasa kwa kushindwa kuleta mabadiliko na maendeleo ambayo simulizi hizi ziliahidi. Badala yake,wanaubaadausasa hupendelea simulizi ndogo au njia mbadala na anuwai za kushughulikia masuala tofauti yanayoikumba jamii. Katika utafiti huu mhimili huu umetumika kuhakiki simulizi kuu mbalimbali zilizojitokeza kama vile simulizi kuhusu maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya katika

mataifa ya Afrika na uhamiaji wa watu wa mataifa ya Afrika katika mataifa ya Ulaya. Aidha, simulizi kuu zinazohusiana na elimu, dini na utamaduni pia zimejadiliwa zinapojitokeza katika utafiti huu.

2. Ukosefu wa mshikamano: kwa wanaubaadausasa ulimwengu hauna mshikamano. Badala yake kuna njia tofauti na anuwai za kuutazama ulimwengu. Katika kazi ya kifasihi, ukosefu wa mshikamano hudhihirika kutokana na ukosefu wa muumano na mfuatano wa matukio tangu mwanzo hadi mwisho. Badala yake matukio huonekana kama vipengele vidogo vidogo vya simulizi vilivyochopekwa huku na kule, dhana ambayo tumeiita uchopekaji wa vipande vya simulizi katika utafiti huu.

3. Ufutaji wa mipaka kati ya dhana, vitu na hali tofauti: Katika kazi ya fasihi matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mbinu ya kimtindo huonyesha namna mipaka kati ya uhalisia na umazingaombwe hufutika na badala yake kuna matumizi ya uhalisia unaoenda sambamba na umazingaombwe.

4. Mwingiliano wa matini: Wanaubaadausasa hutumia mwingiliano matini kupuuza na kuvuruga itikadi ya usasa kuhusu upekee wa matini, pamoja na uasili wa mawazo ya mwandishi wa matini husika (Grenz 1996; Clayton 2012). Waandishi wa kazi za kibaadausasa hivyo basi hutambua kazi nyingine za awali hasa za kifasihi na huzitumia kama malighafi ya kuunda kazi zao mahsusi.

**1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti**

Sehemu hii inachunguza maandishi mbalimbali yanayohusiana na dhana ya ubaadausasa kwa jumla pamoja na kazi anuwai za kibaadausasa. Tahakiki mbalimbali zinazohusiana na uandishi wa kazi za fasihi zilizoandikwa kwa mtindo wa ubaadausasa pia zimerejelewa na zimemwezesha mtafiti kuyaelewa mawazo ya wataalam

mbalimbali kuhusu mada ya utafiti. Katika kufanya hivi mtafiti aliweza kulibainisha pengo ambalo utafiti ulikusudia kuliziba.

Morgan (2001) anaeleza kuwa matumizi ya dhana ya ubaadausasa ilianza miaka ya 1940 kama mtindo wa usanifu wa majengo uliodhihirisha ujumi ulioenda kinyume na usasa na urazini. Katika kipindi cha usasa wasanifu majengo walilazimishwa kufuata njia na mfumo mahsusi katika kusanifu majengo. Ubaadausasa hata hivyo, unapinga usasa na badala yake hupendekeza uigaji au uundaji upya (pastiche) wa kazi za kisanaa kwa kuchanganya mitindo tofauti katika usanifu wa majengo. Lengo moja la ubaadausasa lilikuwa ni kuvuruga au kuondoa mipaka kati ya tamaduni pendwa na tamaduni za juu ambazo zilisisitizwa na kudumishwa na wanausasa katika kazi za kisanaa (Worfreys na wengine, 2006). Baadaye dhana ya ubaadausasa ilikuja kuhusishwa na maandishi. Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu ulilenga kuangalia namna kazi za kibaadausasa zimechanganya mitindo tofauti katika uandishi wa kisanaa na athari zake katika usomaji na uelewekaji wa kazi hizo.

Kwa mujibu wa Barry (2002) baadhi ya wahakiki huona ubaadausasa kama maendeleo ya baadaye ya dhana au nadharia ya usasa. Wanaoshikilia msimamo huu wanadai kuwa sifa ambazo zilipatikana katika usasa ndizo sifa zile zile ambazo hutambulisha ubaadausasa. Kwa mfano, ubaadausasa, kama ulivyo usasa, hutumia wigobezo pamoja na vipande vipande vya hadithi badala ya kuwa na hadithi moja yenye mtiririko. Hata hivyo, Barry anaeleza kuwa kuna tofauti za kimielekeo kati ya wanausasa na wanaubaadausasa katika matumizi ya vipengele hivi. Kwa mfano, usasa ulilalamikia hali hii ya kuvunjavunja vipengele vya hadithi kwa kuwa kulingana na wanausasa ulimwengu hauwakilishwi kwa njia mwafaka kwa kutumia maumbo yaliyotenganishwa ya kisanaa. Hata hivyo, ubaadausasa husherehekea uvunjaji huu wa maumbo kwani wanaiona kama njia ya kujikomboa kutokana na mifumo ya awali ambayo haikuruhusu

mabadiliko. Utafiti huu umeibainisha sifa hii ya matumizi ya vipande vipande vya hadithi kama mbinu ya uandishi wa kazi za kibaadausasa kama njia ya kufafanua dhamira tofauti zinazoathiri mataifa ya Afrika. Dhamira hizo ni pamoja na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika na uhamiaji wa Waafrika katika mataifa ya ulaya.

Sim (2001) anasema kuwa wananadharia wa baada-umuundo kama vile Jacques Derrida, Michel Faucoult, Luce Irigaray pamoja na Gilles Deleuze na Felix Guattari huchukuliwa kama wanaubaadausasa kutokana na ukiukaji wa kaida au simulizi kuu zilizotawala enzi zao. Kwa mfano, Irigaray anautilia shaka na kuukataa mfumo unaompendelea mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Kulingana na Irigaray, kuhusisha sifa fulani na wanaume na zingine na wanawake ni jambo lisilokuwa na uasili ingawa wanajamii hulitumia kuwakandamiza wanawake. Irigaray basi anakiuka simulizi kuu kuhusu masuala ya kijinsia katika jamii. Ukiukaji wa kaida za kijamii kama vile ndoa za kulazimishwa na kuibuka kwa njia mbadala za kusuluhisha tatizo hili ni mojawapo ya masuala muhimu ambayo utafiti huu unanuia kushughulikia.

Khamis (2006) anaeleza kuhusu vipengele tofauti vya kimtindo na kimuundo katika riwaya ya Kezilahabi inayoitwa *Nagona*. Vipengele hivi ni pamoja na kuwepo kwa vipandevipande vya hadithi, usimulizi usiofuatana kiwakati na uhalisiamazingaombwe. Khamis (2003) anamjibu Gromov (1989) ambaye alirai kuwa riwaya za Kezilahabi, *Nagona* na *Mzingile* zilitumia muundo wenye utata. Khamis anakubali kwamba riwaya ya *Nagona* imekiuka mbinu ya awali ya usimulizi uliofuatana kiwakati. Matumizi ya vipande vipande vya hadithi ambavyo havijaunganika vizuri katika riwaya ya *Nagona* basi ni mbinu ya kimaksudi anayoitumia Kezilahabi kama dhihirisho la ukosefu wa mshikamano katika ya jamii ya kisasa barani Afrika. Kazi hii ya Khamis (2003) ilikuwa muhimu katika utafiti huu hasa katika kukuza ufahamu kuhusu namna Kezilahabi

alivyokiuka kaida za kihalisia na badala yake kutumia vipande vipande vya hadithi na uhalisiamazingaombwe katika uandishi wake. Hata hivyo, kazi ya Khamis (2003) ilieleza tu kwa jumla matumizi ya vipengele hivi bila kujikita katika misingi ya kinadharia namna utafiti huu ulivyofanya. Aidha, kazi ya Khamis ilishughulikia riwaya za Kezilahabi zilizoandikwa kabla ya mwaka wa 2000, ilhali utafiti huu ulishughulikia riwaya za waandishi tofauti yaani, S.A. Mohamed na K. W. Wamitila, zilizoandikwa baada ya mwaka wa 2000. Kuwepo na waandishi tofauti walioandika katika kipindi tofauti na kile cha Kezilahabi hudhihirisha upekee wa mwandishi katika matumizi ya vipengele vya uchopekaji wa vipande vya hadithi na matumizi ya uhalisiamazingaombwe kama mbinu ya uandishi wa ubaadausasa katika riwaya za utafiti huu.

Khamis (2005, 2008) anazungumzia kuhusu riwaya mpya[2] ya Kiswahili iliyozaliwa miaka ya 1990. Anasema kuwa riwaya hizi zinakiuka takriban misingi yote ya kanuni za riwaya za uhalisia zilizotangulia kabla ya hapo na vilevile kuongeza baadhi ya vipengele ambavyo havimo katika riwaya iliyotangulia. Khamis (2008: 21-22) anafafanua baadhi ya vipengele muhimu vinavyopatikana katika riwaya mpya:

> Katika riwaya hii hakuna hadithi inayoshikamana kiwakati kama tuzijuavyo hadithi zilizoandikwa kwa mtindo wa uhalisia…bali kuna vipande vya hadithi, matukio, vitukio na visa ambavyo vimevunjwavunjwa maksudi na kukutanishwa mbali na mnyororo wa safari au utashi wa mhusika fulani kutaka kugundua au kutatua tatizo fulani. Hadithi,visa, matukio na vitukio haviaminiki katika mantiki ya maisha ya kawaida… bali vinasimamia fantasia na mazingaombwe yaliyochanganyika na uhalisia wa aina fulani...kwa wingi wahusika ni vivuli vya watu au dhana zinazopewa uhai ili kusimamia kwa matendo dhamira hoja mtazamo na falsafa ya mwandishi.

Vipengele hivi alivyovizungumzia Khamis ni vile vinavyohusishwa na ubaadausasa ambavyo utafiti huu ulilenga kuvibainisha katika riwaya teule za Kiswahili. Sifa

---

[2] Upya katika muktadha huu ni jina linalotumika kurejelea mtindo unaokiuka kaida zilizozoeleka za kuandika riwaya za Kiswahili (Khamis 2005b)

nyingine za riwaya mpya ambazo Khamis (2005, 2008) amevibainisha ni mwingilano matini, kutokuwepo na mipaka ya wazi kati ya uhalisi na utohalisi, kuchanganya tanzu hivi kwamba baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi vinapatikana katika riwaya Katika usimulizi, nafsi zote tatu zinaweza kutumika kwa pamoja na hakuna sauti moja inayoongoza mawazo ya mhusika mmoja wakati wowote. Kwa hivyo sauti na mitazamo ya mwandishi na wahusika huchanganyika. Aidha, lugha inayotumika huwa gumu kwa kiasi fulani na hukiuka kanuni za kisarufi. Vipengele hivi vilikuwa muhimu sana katika utafiti huu kwani ni sehemu ya yale utafiti huu ulidhamiria kuchunguza. Hata hivyo, Khamis (2008) ameviorodhesha vipengele hivi katika ujumla wake bila kujikita katika riwaya yoyote maalum. Hata wakati amebainisha vipengele hivi katika riwaya mahsusi (Khamis 2005b) kwa mfano katika *Dunia Yao* ambayo inatafitiwa katika utafiti huu, uhakiki wake si wa kina zaidi. Vilevile, utafiti wetu basi utahusisha riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na riwaya ya *Unaitwa Nani?* ambazo hazijafanyiwa utafiti mpaka sasa kuhusu vipengele bainifu vya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa.

Diegner (2005) anaeleza kuwa mwingiliano matini hujitokeza wakati mwandishi anarejelea kimakusudi matini nyingine na pia wakati hajakusudia kufanya hivyo. Kwa kujikita katika riwaya ya *Nagona* na riwaya ya *Ziraili na Zirani* za Kezilahabi na Mkufya mtawalia, Diegner amebainisha aina nne za mwingiliano matini. Aina ya kwanza inahusu marejeleo dhahiri ya kazi zingine kama vile za kidini au kifalsafa ambapo mwandishi hutaja waziwazi kazi, wahusika au waandishi wa kazi zingine katika riwaya husika. Katika aina ya pili, mwandishi hurejelea kwa njia isiyo dhahiri kazi za waandishi wengine. Kwa mfano, mwandishi anaweza kurejelea mawazo yanayopatikana katika matini nyingine lakini bila kumweleza msomaji waziwazi kwamba mawazo hayo yametokana na matini nyingine. Aina ya tatu ya mwingilano matini inahusu namna mwandishi alivyoathiriwa na kazi za wahusika wengine katika

kuiandika kazi yake, huku aina ya nne ikiangalia uhusiano wa matini tofauti katika kiwango cha maudhui. Mawazo haya ya Diegner yalikuwa muhimu katika utafiti katika kubainisha aina tofauti za mwingiliano matini zilizojitokeza katika riwaya zilizotafitiwa. Aina hizo tatu ni, mwingiliano matini dhahiri, mwingiliano matini usodhahiri na mwingiliano matini linganifu.

Kwa mujibu wa Polleheide (2003), matumizi ya mwingiliano matini katika riwaya yamekuwapo tangu jadi. Kimapokeo, mwingilano matini ulichukuliwa kama mbinu aliyoitumia mwandishi kuhusiana na msomaji wake. Mwandishi hivyo basi aliteua kwa makini matini alizozirejelea akiwa na matumaini makubwa kwamba msomaji wake anazifahamu matini hizo alizozirejelea. Hata hivyo, katika kazi za kibaadausasa, wakati mwingine mwandishi hurejelea matini nyingine kwenye kazi yake, bila kupanga kufanya hivyo, na bila kujali iwapo msomaji anazifahamu au la. Mawazo haya ya Polleheide yalikuwa muhimu katika utafiti katika kubainisha athari za mwingiliano matini kwa msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti katika riwaya za kibaadausasa.

Fauka ya hayo, Pollheide (2003), anarai kuwa wanaubaadausasa hutumia mwingiliano matini kudhihirisha kwamba matini haiwezi kuchukuliwa kama kitu kimoja kamilifu kinachojitosheleza. Kulingana na Pollheide (2003), mwingiliano matini huivunjavunja matini katika vipande vidogo vidogo ambavyo huhitaji kuunganishwa baadaye. Mawazo haya yanaambatana na yale ya Lyotard (1979) kuwa dunia haina mshikamano. Matumizi ya mwingiliano kama kipengele mojawapo cha ubaadausasa umetumika kubainisha dhamira mbalimbali zinazojitokeza kupitia marejeleo ainati katika riwaya zilizotafitiwa, kama njia ya kudhihirisha ukosefu mshikamano katika ulimwengu wa sasa.

Childs & Fowler (2006) wanaeleza mwingiliano matini kama “Jina ambalo aghalabu hutumiwa kueleza namna matini za kila aina - ziwe za kimasimulizi, kimaono, kifasihi - hurejelea matini nyingine ambazo huziathiri kwa njia moja au nyingine matini husika (uk 121). Kimsingi, fasili hii ya Childs & Fowler inadhihirisha kuwa mwingiliano matini huhusiana na urejeleaji wa matini nyingine katika kazi husika. Mawazo haya yaliufaidi utafiti huu katika kujadili kipengele cha mwingiliano matini kwa kubainisha kazi anuwai zilizorejelewa katika riwaya zilizotafitiwa.

Aidha, Childs & Fowler (2006) wemeeleza dhima tofauti za mwingilianomatini katika kazi za fasihi. Wanarai kuwa wanaubaadausasa hutumia mwingiliano matini kuvuruga imani ya awali inayohusishwa na mawazo ya ulimbwende kuhusu upekee wa matini pamoja na uasili wa mawazo ya mwandishi wa matini husika. Kabla ya kipindi cha Mwamko wa Kisanaa (Renaissance) na baadaye kidogo, ilichukuliwa na kukubalika kuwa kazi za kifasihi zilikuwa mchanganyiko wa kazi mbalimbali za awali, ambazo zilitumiwa moja kwa moja au zikafanyiwa marekebisho machache kwenye kazi husika. Mwandishi wa kazi hizi za awali hakutambulishwa; hali hii haikuchukuliwa kama wizi wa maandishi (plagiarism) bali kama njia ya kuheshimu utamaduni na ujuzi wa matini asilia zilizorejelewa. Hata hivyo, katika kipindi cha ulimbwende kilichotokea mwishoni mwa karne ya 18, na mwanzoni mwa karne ya 19, kulikuwa na haja ya kumtambulisha mwandishi. Haja hii ilitokana na wazo la wanaulimbwende kuhusu ubinafsishaji wa ubunifu lililolingana na mwondoko wa usasa kuhusu ubinafsi. Matini basi ilichukuliwa kama kitu cha kipekee kama alivyo mwandishi aliyeyazua mawazo katika matini hiyo. Mawazo haya ya ubinafsishaji wa ubunifu yalipingwa na wananadharia wa nadharia za umuundo na baadaumuundo waliodai kuwa lugha ni mfumo, na mwandishi huchota tu kutoka mfumo huo ili kuzieleza tajriba zake. Hivyo basi, kila tunaponena, huwa tunarejelea tu yale ambayo yamewahi kusemwa tayari. Kwa mujibu wa Childs &

Fowler (2006:122) mawazo haya ya wanaumuundo na baadaumuundo yanaweza kuhusishwa na kazi za kisanaa ambapo "Mwandishi hachukuliwi kama mwanzilishi bali mpangaji tu wa mawazo ili kuueleza ulimwengu". Ni kutokana na mawazo haya ambapo kazi za kisanaa huchukuliwa kama mchanganyiko wa matini nyingine zilizoziathiri katika viwango mbalimbali. Mwingiliano matini basi ni kipengele muhimu katika kazi za kibaadausasa kama njia ya kupuuza mawazo ya ulimbwende kuhusu upekee na uasili wa kazi za kisanaa. Matini za fasihi ya kibaadausasa huonyesha namna matini husika ilivyoathiriwa na matini za awali na hulenga kuziandika upya matini hizo za awali na wakati mwingine kwa njia ya kubeza. Kupuuza kwa mifumo na misingi inayolenga kuongoza mawazo yetu ni mojawapo ya mihimili ya nadharia ya ubaadausasa kama inavyofafanuliwa na Lyotard (1979) na ambayo inaongoza utafiti huu.

Isitoshe, Childs & Fowler (2006) wanaeleza kuwa dhima nyingine ya matumizi ya mwingiliano matini ni kumtambua msomaji kama mshiriki katika mchakato wa ubunaji wa kazi ya kifasihi. Kama tunavyofahamu, kazi yoyote ya kifasihi hujumuisha wahusika watatu; mwandishi, matini na msomaji. Kwa kuwa mwandishi ndiye mpangaji wa mawazo, msomaji ana nafasi muhimu ya kuweza kung'amua maana inayotokana na yale ambayo mwandishi ameyapanga. Iwapo mwandishi amerejelea matini nyingine katika kazi yake, ufasiri wa maana wa matini husika utategemea iwapo msomaji anafahamu matini hizo zilizorejelewa au la. Iwapo msomaji hajawahi kupatana na matini hizo zilizorejelewa, atakuwa na ufasiri mwingine ambao, kulingana na Childs & Fowler (2006), pia unaweza kukubalika. Ni kutokana na huu uwezo wa msomaji wa kuweza kung'amua maana katika matini ya kifasihi ambapo msomaji anachukuliwa kama mhusika muhimu katika kazi ya kisanaa. Mawazo haya ya Childs

na Fowler yalitumika katika kubainisha athari za matumizi ya mwingiliano matini kwa msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti za riwaya zilizotafitiwa.

Björnsson (2006) amehakiki vipengele vya ubaadausasa katika filamu inayojulikana kama *The Simpson.* Hii ni filamu iliyoonyeshwa katika runinga huko Marekani. Katika utafiti wake, Björnsson (2006) alilenga kubainisha namna baadhi ya vipengele vya ubaadausasa vinavyodhihirika katika filamu hii. Alijikita katika vipengele vitatau vya ubaadausasa ambavyo ni mwingiliano matini, uhalisia uliopindukia (hyperreality) pamoja na uhakiki wa simulizi kuu. Utafiti wake ulibainisha kwamba filamu ya *The Simpson* ni mojawapo ya vipindi vya runinga vinavyodhihirisha kwa wingi vipengele vya ubaadausasa. Utafiti wa Björnsson (2006) ulikuwa muhimu katika kuelewa namna nadharia ya ubaadausasa inavyoweza kutumika katika kuihakiki kazi ya kifasihi. Hata hivyo, utafiti wa Björnsson ulijikita katika utanzu wa fasihi simulizi ilhali utafiti huu umejikita katika utanzu wa fasihi andishi.

Kwa mujibu wa Gromov (2008) maandishi ya Kiswahili yaliyoathiriwa na mbinu ya ubaadausasa yalianza kutokea katika miaka ya tisini. Baadhi ya waandishi hao walitumia ubunaji wa visasili huku wengine wakitumia uhalisiajabu. Waandishi hao ni pamoja na Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohamed, Kyallo Wadi Wamitila na William Mkufya.Gromov ametaja vipengele viwili tu vinavyopatikana katika maandishi ya ubaadausasa. Hata hivyo, kuna vipengele vingine kama vile ukosefu wa mshikamano na mwingiliano matini. Aidha, hajavihusisha vipengele hivi na kazi mahsusi za kisanaa. Utafiti huu basi ulilenga kuliziba pengo hili kwa kuangalia vipengele mbalimbali vya baadausasa katika riwaya teule za Kiswahili.

Gromov (2008) anaeleza kuwa waandishi wa riwaya ya Kiswahili walioandika katika miaka ya tisini (k.m. S.A. Mohamed na K.W. Wamitila) walitumia mtindo wa

ubaadausasa ambao ni ule wa Kimagharibi. Anaendelea kusema kuwa ubaadausasa wa fasihi ya Kiswahili ni ule wenye kigusahisi (pathos) chanya. Ingawa Gromov hajafafanua ni kwa njia gani ubaadausasa wa Kiafrika ni tofauti na ule wa Kimagharibi, utafiti huu labda utaweza kubainisha namna ubaadausasa wa fasihi ya Kiswahili unavyozua hisia chanya.

Wegesa na Macharia (2008) wametumia nadharia ya ubaadausasa kutathmini mabadiliko ya kijamii na kitamaduni katika hali mbili tofauti nchini Kenya ambazo ni sekta ya uchukuzi wa umma (matatu) na kundi la mungiki[3]. Wamebainisha kuwa makundi haya mawili huenda kinyume na matarajiao ya kijamii yaliyozoeleka. Kwa mfano, wanaohudumu katika sekta ya matatu huujenga utambulisho mpya unaokwenda kinyume na kaida zilizozoeleka za kitamaduni ambapo utambulisho hujikita katika misingi ya kikabila. Aidha, wanakataa kufuata mamlaka ya sheria na ulinzi iliyowekwa nchini. Badala yake wanaunda 'mamlaka' yao ya kipekee yaliyojikita katika ukiukaji wa mamlaka kuu. Vilevile, kundi la Mungiki halifuati kaida zilizozoeleka katika mazishi. Makundi haya mawili yanaonyesha uasi wa wazi dhidi ya mamlaka. Katika muktadha wa kibaadausasa hii ni hali ambayo inaonyesha kushuku kwa mamlaka na simulizi kuu za kitamaduni, dini na sheria. Badala yake wanaunda simulizi zao ndogo zinazowasaidia kwa muda kukabiliana na matatizo yanayowakumba kwa kukiuka sheria zilizowekwa na kuzoeleka. Uhakiki huu wa Wegesa uliufaidi utafiti wetu katika kuweka msingi wa kuhakiki simulizi kuu katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu pamoja na kubainisha matumizi ya simulizi ndogo katika kushughulikia masuala tofauti yanayoikumba jamii ya sasa.

---

[3] Hili ni kundi la watu lililo na mizizi yake katika utamaduni wa jamii ya Wakikuyu ambalo hulenga kuwaongoza wafuasi wake katika kuuasi utamaduni wa kigeni ulioletwa na wazungu na badala yake kuwahimiza kuurejelea utamaduni wa kiasili.

Waliaula (2010) amehakiki riwaya ya *Dunia Yao* ya S.A Mohammed kwa kuzingatia nadharia ya Uhalisia mazingaombwe. Katika makala yake analinganisha riwaya ya *Dunia Yao* ya S.A. Mohamed na ile ya *The Tin Tin Drum* ya Gunter Grass iliyoandikwa kwa Kijerumani na kutafsiriwa kwa Kingereza mwaka wa 1959. Katika makala haya, Walibora anaonyesha ushabaha kati ya riwaya hizi mbili. Anaeleza kwamba riwaya hizi mbili zimetupilia mbali mfumo wa uandishi wenye uhalisia kama tuujuavyo na badala yake zimezingatia mtindo wa ujumi wa ubaadausasa. Ingawa Walibora aliegemea zaidi katika uhalisia mazingaombwe, makala haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu katika kubainisha baadhi ya vipengele vya ubaadausasa katika riwaya teule. Kama anavyosema D'Haen (2005 katika Waliaula (2010:145)

> Uhalisia mazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye[4], linaloonyesha sifa za usasabaadaye kama vile kujirejelearejelea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha udhabiti wa wahusika na usimulizi vilevile, kumchanaganya msomaji kwa maksudi na halikadhalika kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti.

Baadhi ya vipengele hivi alivyovizungumzia Waliaula vilitumika kama msingi wa kuhakiki kwa kina vipengele vya ubaadausasa katika riwaya teule za utafiti huu.

Mwamzandi (2013) anafafanua taswira mpya inayojitokeza katika riwaya za karne ya 21 kwa kujikita katika riwaya tatu: *Musaleo!* (2004) ya K. W. Wamitila, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) za S.A. Mohamed. Makala yake yameangazia namna riwaya za K21 zinavyoasisi nadharia zenyewe na kuzifanya kiini cha kazi hizo kuliko kuzitumia nadharia kama nyenzo ya kuzizungumzia. Ameonyesha namna nadharia za kifasihi kama vile umuundo, udenguzi, nadharia mwigo na ubaadausasa zilivyojitokeza wazi katika riwaya za K21. Aidha, Mwamzandi (2013) anaeleza kwamba riwaya hizi zimebainisha kwamba uandishi wa kazi za kihalisia umepitwa na

---

[4] Baadhi ya wataalam kama vile Waliaula (2010) wanatumia neno usasabaadaye badala ya ubaadausasa kama lilivyotumika katika utafiti huu. Hata hivyo maneno yote mawili yana maana sawa.

wakati na hivyo zimetumia mbinu ya kiuandishi ya kimajaribio. Baadhi ya sifa zinazozitambulisha riwaya hizi ni pamoja na mwingiliano matini, matumizi ya vipande vidogo vidogo vya simulizi, ukosefu wa muumano na muungano wa hadithi tangu mwanzo hadi mwisho pamoja na matumizi ya uhalisia mazingaombwe. Baadhi ya sifa hizi ni zile zinazohusishwa na ubaadausasa ambavyo utafiti huu unalenga kuvibainisha kwa kutumia riwaya teule za Kiswahili. Tofauti na utafiti wa Mwamzandi uliolenga kuonyesha namna riwaya za K21 zinavyohakiki nadharia zenyewe na kuzifanya kiini cha kazi hizo, utafiti huu unahakiki riwaya teule za K21 kwa mujibu wa nadharia ya ubaadausasa.

Mulila-Matei (2014) amehakiki riwaya ya *UNN* kwa kuchunguza namna lugha hutumiwa kuunda na kuonyesha tofauti za mahusiano ya kimamlaka kati ya jinsia tofauti. Aidha, utafiti wake ulilenga kudhihirisha itikadi za kijinsia ambazo husaidia katika kudumisha tofauti hizi za mahusiano ya kimamlaka kati ya jinsia tofauti. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa wahusika wenye hadhi za juu za kimamlaka waliteua msamiati wao kwa namna iliyodhihirisha hadhi yao. Vilevile, wahusika wenye mamlaka ya juu walichukua nafasi kubwa katika kuzungumza huku ikiwapa nafasi finyu wahusika wa mamlaka ya chini. Isitoshe, wenye mamlaka walitumia mikakati yenye mantiki maalum ambayo iliwafanya wahusika wa hadhi ya chini kuutazama ulimwengu kwa mtazamo wa wahusika wenye mamlaka ya juu. Utafiti wa Mulili-Matei (2014) ulikuwa muhimu katika kulielewa suala la utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *UNN* ambalo limeitawala riwaya hii. Hata hivyo, utafiti wake ulijitakita katika kuchunguza kipengele cha lugha kwa kujikita katika nadharia ya Uhakiki Makinifu wa Mazungumzo. Kwa kutumia nadharia hii, Mulili- Matei ameoyesha namna lugha hutumiwa kuunda na kudumisha mahusiano ya kimamlaka kati ya jinsia tofauti. Hii ni tofauti katika utafiti

huu uliojika katika nadharia ya Ubaadausasa ambayo hupinga na kusaili mawazo jumuishi yanayohusiana na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *UNN*.

Ngesa na wengine (2015) wamejadili mwingiliano matini baina ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein na tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) ya Arege. Kwa kutumia mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini inayorai kuwa matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi, wametathmini ukuruba baina ya tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* iliyoandikwa takriban miongo minne baadaye. Makala yao yanathibitisha kuwa tamthilia hizi zinafanana na kudhihirisha mwingilianomatini katika kiwango cha motifu, maudhui, matumizi ya lugha na wahusika. Katika ulinganisho huu, Ngesa na wengine (2015) wanadhibitisha mojawapo ya mhimili wa nadharia ya mwingilianomatini waliouorodhesha unaorai kuwa matini za kifasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine. Mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini kama ilivyoelezwa na Ngesa na wengine (2015) ilikuwa muhimu katika kuhakiki mwingilianomatini kama mojawapo ya mtindo wa uandishi wa kibaadausasa katika riwaya za utafiti huu. Kwa kutumia mihimili hiyo tuliweza kubainisha namna riwaya za utafiti huu zilivyochota, kunukuu, kuiga na kurejelea matini nyinginezo katika viwango tofauti, viwe vya kimaudhui, motifu, lugha na wahusika.

Kimugung (2015) amehakiki mitindo mamboleo ya ubaadausasa kwa kujikita katika nyimbo za jamii ya Kikalenjin zilizoimbwa katika karne ya ishirini na moja. Katika tasnifu yake, Kimugung ameeleza kuwa nyimbo hizi zinadhihirisha mitindo ya ubaadausasa katika kuakisi hali halisi ya jamii ya Kikalenjin. Baadhi ya mitindo aliyojadili ni matumizi ya simulizi ndogo ndogo ili kupinga mamlaka kandamizi yaliyokuwa yamezoeleka katika jamii hii kama vile dini, taasisi za kibinadamu, elimu

na kaida za kisiasa. Aidha, kuna uchopekaji wa vipande vya simulizi unaodhihirika kutokana na ukosefu wa muwala katika nyimbo hizi kama njia ya kuakisi hali halisi ya dunia ya sasa. Vilevile, amebainisha kuwa kuna mwingiliano matini ambapo nyimbo hizi hurejelea kazi za awali ili kujenga maudhui yake. Mtindo mwingine alioujadili ni uigaji wa vipande vya simulizi ambapo kuna usambamba au kuigana kwa nyimbo zilizoteuliwa. Utafiti wa Kimugung unashabihiana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote mbili zinaangazia matumizi ya vipengele vya ubaadausasa katika fasihi ya karne ya ishirini na moja. Hata hivyo, utafiti wa Kimugung ulijikita katika fasihi simulizi kwa kurejelea nyimbo za kikalenji ilhali utafiti huu umejikita katika fasihi andishi kwa kuchunguza vipengele vya ubaadausasa katika riwaya za karne ya ishirini na moja.

Laura (2015) amehakiki uhalisiamazingaombwe kwa kujikita katika riwaya tano za fasihi ya kimagharibi. Katika tasnifu yake, amebainisha kuwa riwaya hizo zimedhihirisha vipengele vya uhalisiamazingaombwe. Ametumia mawazo ya Lyotard (1979) kuwa sayansi pekee haiwezi kuueleza ulimwengu kikamilifu na huacha mapengo ambayo huhitaji kujazwa kwa kutoa masimulizi ya aina fulani. Kwa kutumia riwaya za kimagharibi, Laura ameonyesha namna waandishi wa riwaya hizo wanavyotumia lugha ya kidini kueleza hisia na hali mbalimbali ambazo haziwezi kuelezeka katika misingi ya kisayansi. Mambo hayo ambayo yanajikita katika uwanja wa uhalisiamazingaombwe ni pamoja na kuwepo kwa mizimu pamoja na uwezo wa binadamu wa kuzungumza nayo, uwezo wa binadamu wa kufufuka kutoka kwa wafu, uwezo wa ndege wa kumbeba binadamu katika mbawa zake na kadhalika. Licha ya kuwa Laura (2015) alijikita katika matumizi ya lugha ya kidini kubainisha uhalisiamazingaombwe kwenye riwaya za kimagharibi, kazi yake ilikuwa muhimu

katika kubainisha vipengele vya uhalisiamazingaombwe katika riwaya za utafiti huu uliojikita katika riwaya za Afrika Masharika.

Traore (2015) amejadili ubaadausasa katika riwaya ya Kiswahili kwa kujikita katika riwaya mbili za Said Mohamed, *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006). Katika makala yake Traore anaonyesha namna mwandishi wa riwaya hizi alivyotumia vipengele vya kibaadausasa ambavyo vinaenda kinyume na uandishi wa awali wa kihalisia uliokuwa na mwelekeo chanya kuhusu maendeleo ya kitaifa baada ya uhuru. Baadhi ya vipengele vya kibaadausasa ambavyo Traore amejadili katika riwaya hizi ni matumizi ya wahusika na matukio ya ajabuajabu (uhalisia mazingaombwe), matumizi ya vipandevipande vya simulizi, ukiukaji wa kaida ya wakati, ujirejeleaji na mwingiliano matini. Kulingana na Traore, matumizi ya vipengele hivi yanadhihirisha mtazamo mpya wa mwandishi kuhusu jamii ya kisasa ya Afrika Mashariki. Mawazo haya ya Traore yalitumika kujadili kwa kina vipengele hivi vya ubaadausasa katika riwaya za utafiti huu. Aidha, utafiti huu umejadili simulizi mbalimbali zinazodhihirisha matatizo mbalimbali yanayoyakumba mataifa ya Afrika Mashariki, hususan, Kenya na Tanzania, baada ya uhuru.

Gromov (2019) anaeleza kuhusu riwaya ya majaribio au riwaya mpya katika fasihi ya Kenya kwa kujikita katika riwaya tofauti za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi watatu wa Kenya. Riwaya hizo ni pamoja na *Bina-adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2005) za Kyallo Wamitila, *Mafamba* (2008), *Watu wa Gehenna* (2012) na *Mashetani ya Alepo* (2015) za Tom Olali pamoja na riwaya ya Clara Momanyi, *Nakuruto* (2009). Katika makala yake Gromov anabainisha upya wa riwaya ya Kiswahili kimtindo, kifalsafa na kimaudhui. Anaeleza kuwa riwaya hii mpya inatumia kwa kiwango tofauti cha hila na

mbinu za usasabaadaye[5] na mielekeo mingine ya fasihi ya kisasa. Baadhi ya mbinu za kimtindo alizozijadili ni pamoja na matumizi ya motifu ya utafiti (quest), motifu ya ndoto-uhalisia au uhalisia mazingaombwe, uundaji upya, mwingiliano matini na ukiukaji wa kaida ya wakati. Baadhi ya vipengele hivi vinabainisha mtindo wa uandishi wa ubaadausasa ambao utafiti huu unachunguza. Aidha, Gromov anaeleza kuwa riwaya hii mpya inaonyesha matatizo ya dunia ya leo yenye utawala wa kidikteta, mfumo imara wa kitabaka, dhuluma kali zinazokabiliwa na ajali za kiuchumi na kiekolojia. Kama anavyoeleza Gromov, sifa hizi ndizo zinazoitofautisha riwaya hii mpya na aina nyingine ya riwaya zilizo za kawaida zaidi. Ingawa Gromov amejikita katika riwaya za Kenya pekee, mawazo yake yalikuwa muhimu katika kuchunguza vipengele vya ubaadausasa kama vile matumizi ya uhalisia mazingaombwe, mwingiliano matini na ukiukaji wa kaida ya wakati katika riwaya za utafiti huu zilizotungiwa katika mandhari ya Kenya na Tanzania. Aidha, mawazo yake yalitumika kubainisha simulizi mbalimbali zilizochopekwa kwenye riwaya za utafiti zinazodhihirisha matatizo mbalimbali katika mataifa ya Afrika Mashariki na ulimwengu kwa jumla. Baadhi ya simulizi zilizojadiliwa ni pamoja na ukosefu wa maendeleo katika mataifa ya Afrika katika enzi za baada ya uhuru, kutawaliwa kiuchumi kwa mataifa ya Kiafrika kutokana na nguvu za utandawazi pamoja na dhuluma na changamoto zinazotokana na uhamiaji, miongoni mwa matatizo mengine.

### 1.10 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inashughulikia mbinu zilizotumika katika kuteua sampuli wakilishi, kukusanya na kuchanganua data.

[5] Gromov (2019) ametumia neno usasabaadaye kurejelea ubaadausasa kama tunavyouita katika utafiti huu.

### 1.10.1 Usampuli

Lengo la utafiti huu ni kubainisha matumizi ya vipengele vya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya za Kiswahili za K21. Ili kupata sampuli faafu ya utafiti huu, nilisoma riwaya kadha za Kiswahili zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa K21. Riwaya hizo ni pamoja na *Bin-Adam!* (2002), *Musaleo!* (2004), na *Unaitwa Nani?* (2008) za K.W. Wamitila; *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) za S. A. Mohamed; na *Nakuruto* (2009) ya Clara Momanyi. Usampuli wa kimaksudi ulitumiwa kuteua riwaya zilizoshughulikiwa katika utafiti, yaani, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) zilizoandikwa na S. A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2008) ya K. W. Wamitila. Riwaya hizi ziliteuliwa kwa sababu zinadhihirisha upya katika riwaya ya Kiswahili kwa kubainisha vipengele fulani vya kimtindo vinavyokiuka mtindo wa kimapokeo wa uandishi uliozoeleka na ambao ulijikita katika uhalisia. Aidha, riwaya hizi zilidhihirisha vipengele vingi vya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa na kwa hivyo zingenipa data ya kutosha ya kuukamilisha utafiti.

Ili kupata sampuli wakilishi ya riwaya za Kiswahili niliteua riwaya mbili zilizoandikwa na mwandishi mmoja kutoka Tanzania visiwani (Unguja) na riwaya moja iliyoandikwa na mwandishi kutoka Kenya. Lengo la uteuzi wa aina hii ulisaidia kupata data wakilishi ya uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa katika maeneo tofauti ya Afrika Mashariki. Ingawa utafiti ulikusudia kuhusisha angalau riwaya ya mwandishi mmoja kutoka Tanzania bara, hatukuweza kupata riwaya iliyoandikwa katika K21 ambayo ingekidhi mahitaji ya utafiti huu. Aidha, tulikusudia kupata angalau riwaya moja iliyoandikwa na mwanamke ili kupata usawa wa kijinsia na kubainisha kuwa huu sio mtindo unaotumiwa na waandishi wa jinsia moja pekee. Hata hivyo, hali hii haikuwezekana

kutokana na ukosefu wa riwaya kama hiyo ambayo ingeniwezesha kupata data ya kutosha ambayo ingekithi mahitaji ya utafiti huu.

Vilevile, usampuli wa riwaya zilizoteuliwa uliongozwa na tajriba ambayo S. A. Mohammed na K. W. Wamitila wanayo katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Bertoncini (2009) S. A. Mohamed ni mwandishi mashuhuri aliyebobea zaidi katika uandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili naye Wamitila ni mmoja wa waadishi mashuhuri wa enzi hizi anayefuata nyayo za watangulizi wake kama Said A. Mohamed.

### 1.10.2 Ukusanyaji data

Utafiti unahakiki mtindo wa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa katika riwaya zilizoteuliwa za Kiswahili. Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, tulitumia mtazamo wa utafiti kiustahilifu kuhakiki riwaya tatu teule za Kiswahili. Utafiti ulitumia utafiti wa maktabani ili kukusanya data.

Data ya kimsingi iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa K21. Hizi ni pamoja na *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) zilizoandikwa na S. A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2008) ya K. W. Wamitila. Ukusanyaji wa data ulihusu kusoma kwa kina riwaya zenyewe huku nikinakili kwa daftari vipengele vyote vya kibaadausasa vilivyojitokeza. Vipengele hivi hata hivyo vilikuwa vingi sana na ingekuwa changamoto kubwa kuvichanganua vyote katika tasnifu moja. Nilichagua kwa mbinu ya kimaksudi vipengele vya kibaadausasa vilivyojitokeza kwa wingi katika riwaya zote tatu za utafiti. Vipengele hivyo ni uchopekaji wa vipande vya simulizi, uhakiki wa simulizi huu, matumizi ya uhalisia mazingaombwe na matumizi wa mwingiliano matini. Data

iliyokusanywa ilidadavuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti yanayozibainisha riwaya hizi kuwa za kibaadusasa.

### 1.10.3 Utafiti Maktabani

Ili kufanikisha utafiti huu data yote iliyohitajika ilikusanywa kutoka maktabani. Nilizuru maktaba mbalimbali kama vile maktaba za Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nilidurusu yaliyoandikwa kuhusu ubaadausasa kwa jumla na ubaadausasa katika fasihi. Nilipekua majarida, tasnifu na machapisho mengine yaliyoafiki mada na malengo ya utafiti. Aidha, nilifanya utafiti wa mtandaoni kama vile *Jstor, Swahili Forum* pamoja na *Ensaiklopedia ya falsafa ya Stanford*. Hapa nilipata vitabu, tahakiki na majarida yaliyokuwa na habari muhimu zilizohusiana na mada na malengo ya utafiti. Vilevile nilisoma kwa kina riwaya zilizotafitiwa ili kupata data faafu ya kubainisha mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya hizi.

### 1.10.4 Uchanganuzi wa Data

Data iliyochanganuliwa ilitokana na riwaya teule za utafiti huu. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kupitia maelezo ya kinathari. Ili kuweka msingi imara wa uchanganuzi, sura ya pili ilieleza kwa tafsili dhana ya ubaadausasa na matumizi yake katika fasihi. Ilibainika kuwa, japo dhana hii ni tata, inaweza kuelezwa katika matapo matatu; kwanza, ubaadausasa katika muktadha wa Kihistoria; pili, ubaadausasa katika muktadha wa kinadharia na kifalsafa na tatu, ubaadausasa kama mtindo maalum wa kiuandishi na kisanaa. Uchanganuzi ulibainisha kuwa tapo la kwanza la dhana hii halijahusishwa kamwe na fasihi ya Kiswahili. Tapo la pili lilitumika kama mwongozo wa kinadharia wa utafiti huu huku utafiti ukijikita tapo la tatu la dhana ya ubaadausasa kujadili mtindo maalum wa uandishi wa riwaya za K21 zilizoteuliwa katika utafiti huu kama ilivyojadiliwa katika sura ya tatu hadi tano ya tasnifu hii.

Data kutoka riwaya za utafiti ilichanganuliwa kwa kizingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya ubaadausasa. Utafiti uliainisha sifa mahsusi za kibaadausasa zilizotokana na riwaya za utafiti kama vile uchopekaji wa vipande vya simulizi, uhakiki wa simulizi kuu, matumizi ya uhalisia mazingaombwe na matumizi ya mwingiliano matini. Mtafiti alibainisha namna kila kipengele kinavyojitokeza katika riwaya za utafiti pamoja na sababu maalum za kukitumia. Matokeo ya uchanganuzi huu yamejadiliwa katika sura ya tatu hadi ya tano.

Uchanganuzi wa uchopekaji wa vipande vya simulizi uliongozwa na mhimili wa nadharia ya ubaadausasa kuwa dunia haina mshikamano. Ukosefu wa mshikamano katika riwaya za utafiti ulidhihirika kutokana na matumizi ya vipande vya simulizi badala ya kuwa na hadithi moja iliyo na muwala na muumano wa mawazo. Uchanganuzi ulithibitisha kuwa vipande hivi vya simulizi vilitumika kuhakiki simulizi kuu mbalimbali ili kubainisha kuwa haziwezi kuaminiwa tena. Hii ni kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya ubaadausasa kuwa hakuna ukweli halisi. Matokeo ya uchanganuzi huu yamejadiliwa katika sura ya tatu.

Katika kuchanganua matumizi ya uhalisia mazingaombwe, mhimili wa nadharia ya ubaadausasa unaodai kuwa kazi za kibaadausasa hazibainishi mipaka ya wazi kati ya uhalisia, ndoto, fantasia na umazingaombwe ulitumika. Uchanganuzi ulidhibitisha kuwa riwaya za utafiti zilitumia uhalisia ulioenda sambamba na umazingaombwe katika kuwakilisha wahusika, matukio na matendo mbalimbali. Matokeo ya uchanganuzi huu yamejadiliwa katika sura ya nne.

Uchanganuzi wa mbinu ya mtindo ya mwingiliano matini uliongozwa na mhimili wa nadharia ya ubaadausasa inayorai kuwa kazi za kibaadausasa hurejelea kazi za waandishi wengine waliowaathiri waandishi wa kazi husika kwa njia moja au nyingine

kama njia ya kutambua mchango wao. Uchanganuzi ulibainisha matumizi mengi ya mwingiliano matini uliojitokeza kupitia marejeleo ya kazi mbalimbali za waandishi wengine kama njia ya kuendeleza dhamira tofauti za riwaya za utafiti. Matokeo ya uchanganuzi huu yamejadiliwa katika sura ya tano ya tasnifu hii.

### 1.10.5 Changamoto katika Utafiti

Ingawa nilijizatiti vya kutosha, utafiti ulikumbwa na changamoto kadha. Kwanza, kulikuwa na ukosefu wa maandishi ya kutosha yaliyohusiana na mada ya utafiti, hasa katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kutokana na sababu kuwa mtindo wa uandishi wa ubaadausasa ulikuwa uwanja mgeni katika fasihi ya Kiswahili. Ilinibidi nilizuru maktaba mbalimbali nchini na kupekua maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti bila mafanikio makubwa. Hii ilinigharimu fedha nyingi za usafiri na kunichukua muda mwingi kuliko ilivyotarajiwa kuikamilisha tasnifu hii. Hata hivyo utafiti huu umetoa mchango katika kuliziba pengo hili.

Aidha, haikuwa rahisi kukubaliwa na tawala za maktaba za vyuo vikuu na taasisi mbalimbali kutumia maktaba zao licha ya kuwa na kitambulisho kutoka maktaba ya Chuo kikuu changu. Ilinibiti basi kutafuta barua za kunitambulisha kila mara nilipozuru maktaba hizo, jambo ambalo halikuridhisha kamwe.

Tatizo lingine lilikuwa ni kupata tafsiri zinazofaa za dhana na istilahi zinazohusiana na mada ya utafiti kwa kuwa uwanja huu haujaandikiwa sana katika Kiswahili. Aidha, wataalamu wachache walioandika kuhusiana na uwanja huu wa utafiti wametumia istilahi tofauti kurejelea dhana moja. Ili kutatua tatizo hili, tasnifu hii imeambatanisha orodha ya maneno yaliyotumiwa kurejelea istilahi tofauti kwa Kiswahili pamoja na tafsiri zake kwa Kiingereza ili kumpa msomaji ufahamu wa istilahi hizo kama zilivyotumika katika utafiti na kutoa mchango katika uwanja huu wa utafiti.

Tatizo la mwisho lilihusiana na sababu za kikazi ambazo zilinilazimu kuiweka tasnifu hii kwa muda kwa sababu ya kukosa wakati wa kuishughulikia. Aidha, wakati mwingine shughuli za kikazi ziliwafanya wasimamizi wangu kuchukua wakati mwingi kabla ya kuirejesha kazi hii ili kuifanyia marekebisho. Ilinibidi kuendelea kutafuta marejeleo zaidi ya hivi karibuni yanayoambatana na mada ya utafiti. Tatizo hili limeifanya tasnifu hii kuchukua muda mwingi sana kuliko ilivyotarajiwa.

### 1.11 Hitimisho

Sura hii imeweka msingi wa mambo muhimu yaliyoongoza utafiti huu. Mbali na kubainisha hasa kile utafiti ulikusudia kutekeleza, kiini cha kutaka kuufanya utafiti wenyewe pamoja na umuhimu wa utafiti wenyewe ni baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa. Aidha, sehemu hii imebainisha upeo wa utafiti pamoja na namna utafiti wenyewe ulivyotekelezwa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa.

# SURA YA PILI

# DHANA YA UBAADAUSASA NA SIFA ZAKE BAINIFU KATIKA FASIHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inajadili dhana ya ubaadausasa pamoja na sifa zake bainifu katika fasihi, hususan fasihi ya Kiswahili. Wataalam mbalimbali kama vile Barry (2002), Klages (2006) na Carter (2006) wanakubaliana kuwa sio rahisi kutoa fasili moja jumuishi ya dhana ya ubaadausasa kwa sababu inafasiriwa kwa njia tofauti na wataalamu mbalimbali. Mbali na kuwa dhana hii inatumika katika lugha ya kila siku, dhana hii pia inapatikana katika taaluma tofauti kama sanaa, usanifu majengo, muziki, filamu, fasihi, sosholojia, mawasiliano na teknolojia. Hivyo basi matumizi ya neno ubaadausasa hubadilika sio tu kutegemea mwandishi bali pia muktadha ambapo neno hilo hutumika. Kutokana na hali hii, wataalamu na wahakiki hawajaweza kukubaliana kuhusu fasili yake na badala yake huchukua mitazamo tofauti kuhusu dhana hii. Ni kutokana na utata wa fasili ya dhana yenyewe ambapo sura hii imechunguza na kubainisha fasili tofauti za dhana ya ubaadausasa na sifa zake bainifu katika fasihi. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi nayo sehemu ya pili imefafanua kwa kina dhana ya usasa ambayo baadhi ya wataalamu kama vile Barry (2002) na Klages (2006) wanarai kuwa ndio msingi wa kuelewa ubaadausasa.  Sehemu ya tatu nayo imejadili kwa kina dhana ya ubaadausasa kwa jumla. Sehemu ya nne imejadili ubaadausasa kwa kuzingatia misingi ya kihistoria ili kujaribu kubainisha ni kipindi kipi hasa ambapo ubaadausasa unakisiwa kuwa uliaanza. Katika sehemu ya tano tumejadili ubaadausasa katika muktadha wa kinadharia na kifalsafa. Hapa, mawazo ya wananadharia wawili, Jean Francois Lyotard (1979) na Jean Baudrillard (1981) pamoja na yale wataalamu wanaochukuliwa kuwa wanaubaadausasa yamejadiliwa. Katika sehemu ya sita dhana ya ubaadausasa kama mtindo maalumu wa kiuandishi na kisanaa imejadiliwa. Sehemu ya saba imejadili

ubaadausasa katika fasihi ya Kiswahili nayo sehemu ya nane ikijadili sifa bainifu za ubaadausasa katika fasihi. Sehemu ya tisa ni hitimisho la sura hii.

**2.1 Dhana ya Usasa**

Kwa mujibu wa Klages (2006), aghalabu dhana ya ubaadausasa inaweza kueleweka zaidi iwapo kwanza tutauelewa usasa wenyewe. Sehemu hii basi imejadili kwa tafsili dhana ya usasa kama msingi wa kuielewa dhana ya ubaadausasa. Dhana ya usasa imefasiriwa kwa njia tofauti na wataalamu mbalimbali. Berrett (1997) na Mojola (2002) wanaeleza usasa kama dhana inayotumiwa kurejelea kupindi maalum cha kihistoria kilichoanza pamoja na falsafa ya elimu ya ubinadamu ya mradi wa Mwamko wa Kitaaluma. Mwamko wa Kitaaluma ni kipindi cha kihistoria na pia mradi wa kitaaluma wa K17 na K18 uliokuwa na lengo la kuondoa giza, woga na imani za ushirikina, na badala yake kupata ukweli bia ambao ungeyaeleza maisha katika ukamilifu wake. Mradi wa Mwamko wa Kitaaluma ulipinga nguvu za kitamaduni na imani zilizojikita katika ushirikina. Vilevile, Mwamko wa Kitaaluma ulikataa imani na itikadi za kidini ambazo zilipaswa kufuatwa bila kusailiwa. Usasa basi ulichukuliwa kama mwondoko uliojumuisha mawazo yaliyohusishwa na mradi wa Mwamko wa Kitaaluma. Sifa kuu iliyotambulisha kipindi hiki ni kutukuzwa kwa urazini. Wanausasa waliamini kwamba binadamu angeweza kuyatatua matatizo ya ulimwengu kupitia urazini. Aidha, ukweli halisi ulipatikana kupitia ujuzi wa kisayansi na kuwa kila binadamu alikuwa na haki kujiridhisha na kufikia kilele chake. Kwa viongozi wa kisiasa wa kipindi hiki, urazini ulichukuliwa kama kiini cha maendeleo, na ungetumiwa kuleta haki na kuunda jamii imara. Kwao, maisha ya binadamu yalipaswa kuwa bora kila uchao ili kuleta furaha na maendeleo kwa binadamu, mambo ambayo wanaubaadausasa hurai kuwa hayakutimizwa hivyo kuwa msingi wa kutilia shaka mwondoko wa usasa.

Kipindi kati ya K19 na K20 kilishuhudia maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia - hali iliyoonekana kudhihirisha ufanisi wa usasa na Mradi wa Mwamko wa Kitaaluma. Kwa mfano, Mojola (2002) anasema kuwa kipindi cha usasa kilishuhudia kupanuka kwa mfumo wa viwanda pamoja na mifumo ya vyombo vya habari. Usasa ukajishughulisha na kupata suluhisho la kudumu kuhusu matatizo ya kihistoria na ya kisiasa yaliyoikumba jamii.Wanausasa walilenga kuyaboresha maisha ya binadamu daima kwa kuchukulia kuwa kila kizazi kilikuwa na ujuzi mwingi kuhusu maendeleo ya kiteknolojia kuliko kizazi kilichokitangulia. Katika muktadha wa kisiasa, haikujalisha mfumo wa utawala ambao ungefuatwa, uwe wa kibepari au ujamaa, mradi maisha ya binadamu yangeboreshwa daima. Usasa hivyo basi, ukawa ndio msingi ulioleta tawala zilizopenda maendeleo na mabadiliko. Kinachobainika basi ni kuwa sifa mojawapo inayoutambulisha usasa ni maendeleo ya kiteknolojia kwa lengo la kuyaboresha maisha ya binadamu.

Hata hivyo, usasa ulikuja na changamoto zake hasa kuzuka kwa ubepari na taratibu zilizokuwa za kikatili na zilizowakandamiza wananchi. Kwa mfano, Mojola (2002) anasema kwamba mataifa ya kiulaya yalianza kutawala mataifa ya ulimwengu wa tatu (k.m. ya Kiafrika), wakanyonya rasilimali zao na kuwafanya wenyeji kuwa watumwa au watawaliwa chini ya makoloni yao. Kama anavyosema Mojola (2002), Afrika na mataifa ya ulimwengu wa tatu hayakuwa sehemu ya mradi wa usasa; mataifa haya hayakufaidika bali yaliathirika tu kwa njia hasi na mradi huu. Ni kutokana na hali hii ambapo usasa unachukuliwa kama mradi uliojikita katika utamaduni wa kimagharibi uliolenga kuboresha hali ya kiuchumi na kijamii ya nchi za Magharibi kupitia maarifa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha, kutokana na changamoto za usasa, hiki ni kipindi kinachohusishwa na kuzuka kwa ubepari. Taylor (2004) anadokeza kuwa mifumo ya vyombo vya habari ilisababisha aina fulani ya kuudhibiti umma, na

kuugawanya katika matabaka. Kwa hivyo, licha ya kuwa na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia, usasa ulikuwa na athari hasi hasa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu.

Katika sanaa, Barry (2002) na Klages (2006) wanaeleza usasa kama neno linalotumiwa kurejelea mwondoko wa kisanaa na kitamaduni uliotokea mwishoni mwa karne ya kumi na tisa hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini. Kwa mujibu wa Barry (2002), mwondoko wa usasa ulianza mwaka wa 1890 na ukafika kilele chake kati ya mwaka wa 1910 na 1930. Mwondoko wa usasa ulihusisha aina tofauti za kazi za kiumbuji kama vile sanaa za kimaono, muziki, fasihi, uchoraji na usanifu majengo ambazo zilienda kinyume na kaida za awali zilizokuwa zimewekwa kuhusu namna sanaa inavyostahili kuundwa, kuwasilishwa na hata kumaanisha. Kwa mfano, katika muziki, lahani na ulinganifu wa sauti zilizochukuana vizuri zilitupiliwa mbali; katika usanifu majengo, vifaa na maumbo ya awali kama vile matumizi ya paa zilizoinuka, kuba na nguzo katika ujenzi wa nyumba zilikataliwa. Aidha, wanausasa hawakutaka kutumia nakshi za mbao, mawe au matofali na badala yake wakapendekeza majengo yaliyonakshiwa kwa kutumia vioo au saruji na yaliyochukua umbo la mstatili. Katika fasihi, wanausasa walikataa matumizi ya uandishi wa kijadi uliojikita katika uhalisia na kupendekeza uandishi wa kimajaribio. Inavyobainika ni kwamba, katika sanaa na fasihi, sifa mojawapo ya usasa ni kule kutupilia mbali maumbo ya kizamani na kujaribu kutumia maumbo mapya yaliyoonyesha uasili. Hii ina maana kuwa wanausasa walisisitiza ubunifu wa kimajaribio ambao haukuiga maumbo mengineyo ya awali.

Barry (2002) na Klages (2006) wanaorodhesha sifa zinazoubainisha usasa kwa kujikita katika fasihi. Sifa hizo ni kama zifuatazo:

1. Katika riwaya, mwondoko wa usasa ulisisitiza aina ya uandishi uliopendelea matumizi ya usimulizi katika nafsi ya kwanza. Wanausasa walikataa sio tu

usimulizi katika nafsi ya tatu uliobainisha mtazamo imara wa usimulizi bali pia walipinga kuwepo kwa msimamo mahsusi kuhusu suala la maadili.

2. Katika kazi za usasa, mpaka kati ya tanzu tofauti za kifasihi haukuwa wazi. Kwa mfano, ushairi ungechukua vipengele fulani vya usimulizi wa kinathari huku bunilizi kama vile riwaya zikiwa na chembechembe za ushairi.
3. Usasa ulisisitiza kuwepo kwa vipande vipande vya hadithi na mawazo katika kazi moja ya fasihi pamoja na usimulizi usiokuwa na mshikamano imara.
4. Usasa vilevile ulishikilia maoni kuwa ujumi wa hali ya juu ni ule unaoonyesha uasili unaoweza kupatikana kupitia majaribio. Hali hii iliwafanya wanausasa wakubali ubunifu wa msanii katika kazi za sanaa kupitia mbinu za kimajaribio.
5. Wanausasa walisisitiza kuwepo na mipaka ya wazi kati ya utamaduni wa juu na utamaduni wa chini katika uteuzi wa vifaa vilivyohitajika kuiunda sanaa, na katika mbinu za kuieneza na kuitumia sanaa hiyo.
6. Kazi za sanaa zilichukua mwelekeo wa kujirejelea na kuleta hali ya utambuzi wa kibinafsi. Hii ina maana kuwa kazi yoyote ya kisanaa ingepewa hadhi yake kama toleo au chapisho maalum ambalo limeundwa na linalofaa kutumika kwa njia mahsusi.

Kulingana na Barry (2002) na Lewis (2001), mabadiliko yaliyotokea katika kipindi cha usasa yaliathiri kazi za kifasihi na kuwafanya wasanii kuibuka na tungo za kimajaribio zilizodhihirisha ubunifu mkubwa. Matukio mahususi ya kihistoria kama vile Vita vya Kwanza (na Vya Pili) vya Dunia yalichangia kuibuka kwa tungo mpya za kifasihi. Waandishi kama vile T.S. Eliots[6]wakaandika kudhihirisha fujo na uharibifu uliotokana na athari za vita, na hivyo basi kuleta mabadiliko katika utanzu wa ushairi. Aidha, kama

[6] T. S. Eliots ni mmoja wa waandishi maarufu katika kipindi cha usasa. Shairi lake, *The Waste Land* linadhihirisha magofu ya mji katika ardhi iliyoharibiwa na vita. Shairi lenyewe halina mshikamano; beti zake zimevunjwa katika vipande vipande na sentensi zake zinafanana na vifusi na mabaki ya kitamaduni ambapo msimulizi anapitia kwa shida (Ensaiklopidia ya Wikipedia)

anavyosema Lewis (2001) itikadi zilizotawala wakati huo hazikuwapa watu uhakika wa kutatua matatizo yao. Kutokana na sababu hii waandishi wengi wakaanza kuandika kazi za kifantasia. Lewis (2001) anamnukuu Wolfe (1989) aliyelalamika kuwa waandishi wa riwaya wa usasa walipuuza nafasi ya kazi za kifasihi kama kiwakilishi cha ulimwengu halisi.

Baada ya kufika kilele chake, usasa ulianza kufifia kuanzia miaka ya 1930 hasa kutokana na misukosuko ya kisiasa na kiuchumi katika nchi za Ulaya. Kwa mujibu wa Barry (2002), usasa ulianza kuibuka tena katika miaka ya 1960 ila wakati huu haukuwa na umaarufu kama hapo awali katika miaka ya 1920. Ingawa Barry hajaeleza ni lini hasa usasa ulifika kikomo, tunaweza kuchukulia kuwa usasa unaohusishwa na mataifa ya kimagharibi, ulifika mwisho wake katika mwaka wa 1979 ambapo mwondoko wa ubaadausasa unachukuliwa kuanza rasmi.

## 2.2 Dhana ya Ubaadausasa

Baada ya kuijadili dhana ya usasa kama msingi wa kuuelewa ubaadausasa, sehemu hii imeijadili dhana ya ubaadausasa kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali pamoja na kueleza iwapo ubaadausasa ni mwendelezo wa mawazo ya usasa au mwondoka unaopinga usasa. Kulingana na Sim (2001) ubaadausasa ni neno linalotumiwa sana katika lugha ya kila siku kiasi kwamba matumizi yake wakati mwingine sio sahihi. Ni muhumu basi kueleza maana ya dhana hii kwa kurejelea wataalamu tofauti hasa katika uwanja wa kiakademia. Hata hivyo, wataalamu mbalimbali kama vile Barry (2002), Klages (2006) na Carter (2006) wanakubaliana kuwa sio rahisi kutoa fasili moja jumuishi ya dhana ya ubaadausasa kwa sababu inafasiriwa kwa njia tofauti na wataalamu mbalimbali. Klages (2006), kwa mfano, anaeleza kuwa ubaadausasa ni dhana inayopatikana katika taaluma tofauti kama sanaa, usanifu majengo, muziki,

filamu, fasihi, sosholojia, mawasiliano na teknolojia, na hivyo basi ina maana tofauti kwa kutegemea taaluma mahususi.

Kwa mujibu wa Pollheide (2003) matumizi ya neno ubaadausasa hubadilika sio tu kutegemea mwandishi bali pia muktadha ambapo neno hilo hutumika. Kutokana na hali hii, wataalamu na wahakiki hawajaweza kukubaliana kuhusu fasili yake na badala yake huchukua mitazamo tofauti kuhusu dhana hii. Kulingana na Brodribb (1992) sio rahisi kueleza fasili ya dhana ya ubaadausasa hasa kutokana na sababu kuwa asili na maendeleo ya dhana yenyewe haijaweza kuelezwa kikamilifu. Bernstein (1987) anarai kuwa hakujakuwa na makubaliano iwapo ubaadausasa ni kipindi maalum cha kihistoria, au mwelekeo fulani wa kimawazo katika kipindi fulani, au mwondoko wa kisanaa na kifalsafa; na ni nani au nini kinachoweza kujumuishwa katika kutoa fasili ya dhana yenyewe. Carter (2006: 119) naye anasema:

> Tatizo kuu la ubaadausasa ni kutoa fasili ya dhana yenyewe ya ubaadausasa. Wahakiki hawajaweza kukubaliana kuhusu fasili moja faafu ya dhana ya ubaadasusasa kutokana na maana anuwai zinazohusishwa nayo.

Maelezo ya wataalamu tuliowataja hapa juu ni dhihirisho kuwa dhana ya ubaadausasa ni tata na haina budi kutafitiwa kwa kina. Kutokana na utata huu, Clayton (2012) amerahisisha ufasiri wa dhana hii kwa kutoa fasili yake chini ya mada tofauti. Mojawapo ya mada hizi inahusu kuuangalia ubaadausasa kama mtindo mpya wa uandishi katika sanaa na fasihi. Kwake, mtindo huu mpya uliibuka kutokana na kuchakaa kwa mtindo wa uandishi katika kipindi cha usasa. Katika mada ya pili Clayton (2012) anarai kuwa ubaadausasa unastahili kuangaliwa katika muktadha wa kinadharia na kifalsafa unaohusishwa na nadharia ya baadaumuundo. Katika mada ya tatu, Clayton amejikita katika misingi ya kihistoria kwa kuangalia ni lini hasa ubaadausasa ulianza katika mataifa ya Magharibi. Katika utafiti huu tumejikita katika mgao wa huu wa Clayton kama msingi wa kuifafanua dhana ya ubaadausasa. Yaani,

ubaadausasa katika misingi ya kihistoria, ubaadausasa kama jumla ya mawazo ya kifalsafa na kihakiki na ubaadausasa kama mtindo maalum wa kiuandishi na kisanaa.

## 2.3 Ubaadausasa Katika Muktadha wa Kihistoria

Sehemu hii imejadili kipindi ambacho kinaweza kudaiwa kuwa cha ubaadausasa kwa kuzingatia misingi ya kihistoria. Klages (2006) anaeleza kuwa sio rahisi kubainisha wazi kiwakati na kihistoria ni lini ubaadausasa ulianza. Kinachobainika kutokana na maelezo haya ya Klages ni kuwa kipindi mahsusi cha ubaadausasa ni tata jinsi ambavyo dhana yenyewe ni tata. Kutokana na hali hii kuna mijadala kadha inayojaribu kueleza ni kipindi kipi hasa kinachoweza kuitwa cha ubaadausasa. Kimsingi, neno *baadausasa* linatokana na maneno mawili, yaani *baada* na *usasa*. Kwa mujibu wa TUKI (2018), *baada* ni kielezi kinachotumika pamoja na *ya* kuonyesha kitu au muda ulioko mbele ya kitu hicho. Hivyo basi neno *baadausasa* linaweza kuchukuliwa kumaanisha kipindi kilichofuata kipindi cha usasa, jinsi ambavyo usasa ulikuja baada ya Enzi za Kati.

Kwa mujibu wa Best na Keller (1991) istilahi, ‘baadausasa’ iliundwa na mwanahistoria kutoka Uingereza aliyejulikana kama Toynbee. Wakiyafafanua mawazo ya Toynbee, Best na Keller (1991:6) wanaeleza kuwa ubaadausasa ulianza mwishoni mwa karne ya 19, kipindi ambacho kilihusishwa na vita na mabadiliko mengi ya kijamii. Ingawa hawajaeleza wakati mahsusi ambapo ubaadausasa ulianza, kinachoubainisha ubaadausasa kwa maoni yao ni ukosefu wa maendeleo na utulivu. Mojola (2002) anakubaliana na maelezo ya Best na Keller kuhusu ukosefu wa utulivu hasa kutokana na Vita vya Kwanza Vya Dunia. Hata hivyo, wataalamu hawa wanatofautiana katika suala la maendeleo katika kipindi hiki. Huku Best na Keller (1991) wakidai kulikuwa na ukosefu wa maendeleo, Mojola (2002) anaeleza kuwa kipindi kati ya K19 na K20 kilishuhudia maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia. Huenda ni kweli kuwa kipindi hiki kilishuhudia maendeleo makubwa kama anavyorai Mojola (2002), hata

hivyo ukosefu wa utulivu huenda ulididimiza maendeleo yaliyokuwa yameshuhudiwa hapo awali.

Kulingana na Best na Keller (1991), kipindi cha ubaadausasa kinahusishwa na majanga mawili makuu yaliyotokea katika karne ya 20. Majanga haya ni Vita vya Pili vya Dunia pamoja na maangamizo ya utamaduni, kabila na jamii ndogo ndogo zilizozuiliwa katika kambi za Wanazi. Mawazo haya yanalingana kwa kiasi fulani na ya Clayton (2012) anayesema kuwa ubaadausasa hutumiwa kurejelea kipindi fulani cha kihistoria ambacho kilianza mwishoni mwa Vita Vikuu Vya Pili Vya Dunia. Kwa kuzingatia mawazo ya Best na Keller (1991) na Clayton (2012) ubaadausasa huenda ulianza kati ya miaka ya 1930 na 1940 wakati maangamizi haya yalipofanyika na Vita vya Pili vya Dunia kuanza. Kulingana na Lyotard (1979) majanga haya yaliharibu imani iliyohusishwa na usasa kuwa urazini ndio uliokuwa chanzo cha utu, maendeleo na maadili. Ubaadausasa basi ulitilia shaka urazini kama kiini cha maendeleo kwa kujiuliza ni nani aliyeutumia urazini na aliutumia kuwafaidi kina nani na kwa lengo lipi. Ubaadausasa basi ukatilia shaka simulizi kuu ya usasa uliokuwa umehakikisha kuwepo kwa maendeleo katika kila hatua ya binadamu kwa kuzingatia urazini.

Kwa mujibu wa Barry (2002), dhana ya ubaadausasa ilianza kutumika katika miaka ya 1930, wakati usasa ulipoanza kufifia. Ubaadausasa basi ukaashiria kipindi kipya baada ya kipindi cha usasa kuanza kufifia. Hata hivyo, kama anavyosema Barry (2002), huenda dhana ya ubaadausasa haikupata mashiko sana kwa sababu usasa ulianza kuibuka tena katika miaka ya 1960 ila tu haukupata umaarufu kama ilivyokuwa hapo awali.

Kwa kuzingatia mawazo ya Best na Keller (1991) na Barry (2002) tuliyoyajadili hapo juu, kinachodhihirika ni kwa ubaadausasa kama kipindi cha kihistoria ulianza baada ya

kipindi cha usasa katika miaka ya 1930. Hata hivyo, kati ya mwaka wa 1930 (wakati usasa ulianza kufifia) na mwaka wa 1960 (usasa ulipoanza kuibuka tena) huenda kulikuwa na mwingiliano mkubwa kati ya usasa na ubaadausasa hivi kwamba haikuwa rahisi kukibainisha wazi kipindi hicho. Licha ya kuwa dhana ya ubaadausasa ilianza kutumika katika miaka ya 1930 kama anavyorai Barry (2002), wataalamu mbalimbali kama vile Carter (2006) na Sim (2013) wanakubaliana kuwa ubaadausasa kama mwondoko wa kitamaduni na kisanaa katika mataifa ya Ulaya ulianza kutambulika kirasmi mwaka wa 1979 wakati Jean Fracois Lyotard alipochapisha makala yake, *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Sehemu inayofuata imejadili dhana ya ubaadausasa katika muktadha wa kinadharia na kifalsafa

## 2.4 Ubaadausasa katika Muktadha wa Kinadharia na Kifalsafa

Dhana ya ubaadausasa inaweza kufafanuliwa kwa kujikita katika muktadha wa kinadharia na kifalsafa. Clayton (2012), kwa mfano, anaeleza ubaadausasa kama dhana inayotumiwa kueleza jumla ya mawazo ya kifalsafa na kihakiki yaliyoanza mwishoni mwa miaka ya 1960[7]. Pollheide (2003) naye anaeleza kuwa ubaadusasa katika muktadha wa kifalsafa hutumika kurejelea mwelekeo unaohakiki itikadi na maadili ya kitamaduni. Pia dhana hii hutumika kueleza mwamko au mwondoko unaotilia shaka na kuhakiki elimu ya ufahamu, kama vile mwondoko wa usasa. Fasili hizi zinabainisha ubaadausasa kama dhana inayojumuisha mawazo tofauti ya kifalsafa na kihakiki yaliyolenga kuhakiki mifumo ya kiitikadi na kitamaduni pamoja na elimu ya ufahamu iliyotawala hapo awali.

[7] Ingawa ubaadausasa kama jumla ya mawazo ya kifalsafa na kihakiki unahusishwa na kipindi cha miaka ya sitini, kuna baadhi ya wanafalsafa walioishi kabla ya kipindi hiki ambao mawazo ya yanaweza kuelezwa kama ya kibaadausasa kama vile Friedich Nietzsche, William James, Charles Pierce, martin Hiedegger na Hans-georg Gadamer (Clayton 2012).

Kwa mujibu wa Clayton (2012) na Pollheide (2003) kuna waandishi wengi wanaohusishwa na dhana hii ya ubaadausasa katika muktadha huu wa kifalsafa na kinadharia. Waandishi hao ni kama vile Jean-Francois Lyotard, Jean Baudrillard, Michel Foucault, Jacques Derrida, Gilles Deleuze, Felix Guattari na Roland Barthes. Lyotard na Baudrillard wanahusishwa moja kwa moja na dhana hii kama waandishi waliouweka msingi wa kinadharia kuhusu dhana yenyewe. Ingawa waandishi wengine kama vile Michel Foucault na Jacques Derrida wanahusishwa na nadharia nyingine za uhakiki kama ubaadaumuundo, mawazo yao hudhihirisha kipindi cha ubaadausasa. Hii ni kutokana na namna wanavyohakiki simulizi tofauti zinazohusiana na itikadi, maadili au elimu ya ufahamu, hivyo kuwafanya wachukuliwe kama waandishi wa kibaadausasa. Baadhi ya waandishi nao huzungumzia kuhusu kipindi chenyewe cha ubaadausasa kwa kujaribu kuonyesha namna vipengele tofauti vya ubaadausasa vinavyohusishwa na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Sehemu inayofuata basi inajadili dhana ya ubaadausasa kwa kujikita katika baadhi ya waandishi tuliowataja. Mawazo ya wahakiki wa nadharia hii kama vile Fredric Jameson (1991) pia yameshughulikiwa katika sehemu hii.

### 2.4.1 Jean-Francois Lyotard: Uhakiki wa Simulizi Kuu

Jean Francois Lyotard (1979) ndiye anayechukuliwa kama mwasisi wa nadharia ya ubaadausasa. Mchango wake unapatikana katika andiko lake, *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge* ambapo anaeleza kuhusu hali ya ujuzi na maarifa katika jamii zilizoendelea. Lyotard anaeleza ubaadausasa kama hali ya kuzishuku simulizi kuu. Simulizi kuu hurejelea jumla ya nadharia na mifumo ambayo hudai kuhodhi ukweli halisi, au kutoa maelezo bia ya namna ya tunavyopaswa kuutazama ulimwengu au kutoa suluhisho la matatizo yote ya binadamu. Lyotard anatilia shaka simulizi kuu ya Umarx na ile ya usasa zenye misingi yake katika kanuni za falsafa ya

kimagharibi na elimu ya ufahamu, kwa kukosa kitimiza malengo zilizoahidi. Kwa mfano, simulizi ya usasa kama ilivyo simulizi ya Mwamko wa Kitaaluma zililenga kuleta uhuru na maendeleo kupitia maarifa na ujuzi. Simulizi ya Umarx nayo ilisisitiza ukombozi wa binadamu kutoka minyororo ya ubepari. Lyotard (1979) amezitilia shaka simulizi hizi na kusema kwamba haziwezi kuaminika tena. Kwa mfano, Umarx haukuweza kuleta ule uhuru ulioahidi. Badala yake, ulisababisha kuanguka kwa utawala wa Kirusi pamoja na umwagikaji wa damu katika enzi za Stalin. Kutokana na haya Lyotard anasema kuwa hakuna simulizi kuu inayoweza kuaminiwa.

Kulingana na Lyotard (1979), simulizi kuu zimeundwa kwa jozi zinazokinzana kama vile ubia/ubinafsi, urazini/utorazini, diskosi/mtazamo, ambapo dhana ya kwanza katika jozi hizi hupendelewa bila kuwepo na sababu inayoeleza ni kwa nini ikapendelewa. Kwa mfano, simulizi ya usasa ilipendelea urazini kama kipengele cha kuleta uhuru na maendeleo. Lyotard anasema kuwa, hali ya kupendelea dhana moja katika jozi zinazokinzana hulenga kuunda nadharia au kaida moja jumuishi ambayo inapuuza utofauti na uanuwai katika kutazama hali tofauti za maisha. Hizi nadharia na kaida jumuishi ndizo Lyotard anazoziita simulizi kuu.

Katika uhakiki wake wa simulizi kuu, Lyotard (1979) anajaribu kuonyesha umuhimu wa vipengele vilivyopuuzwa katika jozi zinazokinzana tulizozitaja hapo juu. Anaeleza kuwa maarifa ya kibaadausasa hupatikana kwa kwenda kinyume na mawazo yaliyokubalika tayari. Lyotard basi anapendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo ambazo zinahusisha vikundi vidogo vya watu vilivyopaswa kuwa vya muda ambavyo vingesaili na kurekebisha ukandamizaji ulioenezwa na itikadi ya tabaka tawala. Katika simulizi ndogo, Lyotard anapendekeza kuhusishwa na kutiliwa maanani kwa sauti na maoni ya watu wengine, na hasa wale ambao hawako katika tabaka tawala. Hata hivyo, Lyotard anakataa kuchukua msimamo maalum kuhusiana na suala la maadili katika

kushughulikia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Anatumia dhana ya 'ukafiri' kuonyesha kuwa kila mtu anapaswa kuwa huru kutenda anavyotaka bila kuegemeza kitendo hicho na msingi wowote wa kimaadili.

Katika utafiti huu, simulizi kuu zimetumika kurejelea asasi na mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambayo hapo awali iliaminika kuwa ingeleta mabadiliko na suluhisho la matatizo yanayoikumba jamii ya Kiafrika. Baadhi ya mifumo na asasi zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ni pamoja na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika, uhamiaji kutoka mataifa ya afrika kwenda ulaya elimu, dini na utamaduni. Utafiti huu basi umetumia mawazo haya ya Lyotard kubainisha na kuzihakiki simulizi hizo kuu. Utafiti huu umechukulia simulizi ndogo kama njia mbadala za kuyatatua matatizo yao na kupambana na hali tofauti za maisha wakati simulizi kuu zimeshindwa kutekeleza malengo yake.

Licha ya kuwa utafiti huu utatumia mawazo ya Lyotard kuzihakiki simulizi kuu katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu, ni muhimu kutaja hapa kuwa mawazo ya Lyotard yamepata upinzani kutoka kwa wahakiki kama vile Hutcheon (2005) ambao wanaumulika udhaifu wa nadharia hii. Hutcheon, kwa mfano, anaeleza kuwa msimamo wa Lyotard kuhusu kupendelea dhana iliyopuuzwa katika jozi zinazokinzana vilevile huleta mtazamo bia wa kuutazama ulimwengu, ambao nadharia yake (Lyotard) inaupinga. Kulingana na Hutcheon basi, nadharia ya Lyotard haiambatani na ubinafsi na uanuwai anaoupendekeza. Aidha, Best na Keller (1991) anasema kuwa japo hakuna shida yoyote ya kuhakiki simulizi kuu ya usasa, ni muhimu kukumbuka kuwa tunazihitaji simulizi kuu kuupa maana ulimwengu ambamo tunaishi. Hivyo basi, katika kuzihakiki riwaya za utafiti huu, tumetalii namna waandishi walivyozihakiki simulizi kuu katika kazi zao. Hata hivyo, inapobidi, tumeangazia manufaa ya baadhi ya simulizi zenyewe katika ulimwengu wa sasa.

### 2.4.2 Jean Baudrillard: Uhakiki wa Uwakilishaji wa Ishara katika Ulimwengu wa Kiteknolojia

Jean Baudrillard (1981) ni mwananadharia wa ubaadausasa aliyelenga kuchunguza uhusiano uliopo kati ya uhalisi na ishara katika ulimwengu wa kiteknolojia. Mchango wake katika suala hili unapatikana katika kazi yake, *Simulacra and Simulations*. Katika kazi hii, Baudrillard anazungumza kuhusu athari ya vyombo vya habari kwa utamaduni wa jamii pamoja na namna vyombo hivi hutumika kuwakilisha ishara mbalimbali katika jamii. Baudrillard anasema kuwa ubaadausasa hutumiwa kurejelea nafasi ya vyombo vya habari katika jamii iliyotawaliwa na ubepari katika karne ya ishirini. Kulingana na Baudrillard ubaadausasa ni kipindi kilichoanza baada ya Vita vya Pili vya Dunia na ambacho kimetawaliwa na ongezeko la umuhimu wa ishara kupitia maendeleo ya kiteknolojia na kuongozwa na ubepari au kile anachokiita jamii tumizi. Kulingana na Bauldrillard (1981) ishara zinapaswa kuhusishwa na watu halisi katika hali halisi ili ziweze hufanya kazi na kutimiza malengo yake. Hata hivyo, ishara katika kipindi cha ubaadausasa hazina uhusiano wowote na uhalisi bali zinaambatanishwa na ubidhaishaji wa vitu tofauti hasa kupitia vyombo vya habari.

Kwa kuwa ishara za kitamaduni hazihusishwi na miktadha halisi ya kijamii Baudrillard anasema kuwa ishara hizo hazihusishwi na chochote katika ulimwengu halisi. Kwa hivyo Baudrillard anaueleza ulimwengu wa ubaadausasa kama ulimwengu wa maigizo na uigaji au *simulacra na simulation*, ambapo hatuwezi kubainisha tofauti kati ya uhalisi na wigo au ishara na uhalisia kwa kuwa tumezipa ishara umuhimu sana. Na kama anavyosema Eagleton (1996) mambo ghushi au bandia yamechukua nafasi ya yale yaliyo halisi. Baudrillard basi anavishambulia vifaa vya kisasa vya kiteknolojia pamoja na vyombo vya habari kwa kuwa havibainishi tofauti kati ya ishara na uhalisi. Akizungumza kuhusu vifaa vya kiteknolijia, Grenz (1996) anaeleza kuwa sinema na

runinga huweza kuziba mipaka kati ya mambo ya ukweli na mambo ya kubuni, au kati ya mambo muhimu na yale ambayo si muhimu. Hii ni kwa sababu ishara tofauti kama matangazo ya habari na matangazo ya biashara hupewa nafasi sawa na mtazamaji hupata msusuru wa ishara zisizokuwa na uhusiano ambazo hufululiza kwa kasi kwenye runinga. Kulingana na Grenz haya yanadhihirisha kipengele cha utamaduni na mtazamo wa ulimwengu wa ubaadausasa ambao fasihi ya ubaadausasa hulenga kudhihirisha, yaani, kuchanganya ukweli na ubunifu au uhalisi na fantasia.

Mwingiliano kati ya ishara na uhalisia kama alivyoueleza Baudrillard (1981), ndio msingi wa uhakiki wa matumizi ya uhalisiamazingaombwe katika utafiti huu kama mojawapo ya vipengele vya ubaadausasa katika fasihi. Katika riwaya za utafiti huu, wahusika na matukio yamechanganya vipengele vya ukweli na ubunifu au uhalisia na fantasia au uhalisia na uhalisiamazingaombwe ili kuunda kazi moja kamilifu ya kibaadausasa.

### 2.4.3 Jacques Derrida, Michel Foucault, Luce Irigaray, Gilles Deleuze & Felix Guattari na Fredric Jameson

Kwa kuzingatia mtazamo wa kifalsafa, (Sim 2013), Clayton (2012) na Pollheide (2003) wanakubaliana kuwa dhana ya ubaadausasa huhusisha mawazo ya wanabaadaumuundo kama vile Jacques Derrida, Michel Foucault na Luce Irigaray. Mawazo ya waandishi wengine ambao pia huwekwa katika kundi hili la wanaubaadausasa ni kama vile Gilles Deleuze na Felix Guattari na Rolland Barthes na Michel Foucault miongoni mwa wengine. Baadaumuundo huchukuliwa kama mojawapo ya nadharia za ubaadausasa. Baadaumuundo hurejelea jumla ya mijadala na nadharia zilizoibuka katikati mwa karne ya 20 (kati ya 1950s na 1970s). Nadharia hizi zilipinga mawazo ya nadharia ya umuundo ambao huusawiri ulimwengu kama mfumo imara unaofuata utaratibu maalum. Kama walivyo wanaubaadausasa, wanabadaumuundo huonyesha kuwa

ulimwengu hauna udhabiti na hivyo hauwezi kuelezwa kwa kuzingatia mifumo bia kama wanavyofanya wanamuundo.

Derrida na Foucault kwa mfano waliupinga umuundo kwa sababu ulijikita katika kuangalia ulinganifu wa mifumo wala haukutoa nafasi ya kuangalia tofauti zinazoweza kupatikana katika mifumo hiyo. Kipengele hiki cha 'tofauti' ni sifa mojawapo ya ubaadausasa kama inavyoelezwa na Lyotard (1979). Kwa mfano, Derrida katika nadharia ya udenguzi, alichukua mtazamo wa kifalsafa kuihakiki lugha. Alikiuka utaratibu wa wanaumuundo wa kuzingatia ulinganifu wa mifumo na badala yake akajikita katika utofauti uliokuwepo katika mifumo kama njia mojawapo ya kuufasiri ulimwengu. Derrida anasema kwamba lugha ni mfumo wa kutofautisha na kubainisha maana. Kwa mfano, kitu kimoja hutofautishwa na kingine kutokana na tofauti zake katika kiwango cha vipande sauti na kiwango cha semantiki. Foucault naye alichukua mwelekeo wa kiakiolojia na kinasaba katika kuangalia historia ya Kitamaduni. Mijadala ya Foucault inajikita katika kipengele cha 'utofauti' kwa kupinga utamaduni unaosisitiza kufuatwa kwa kaida na kanuni maalum zinazofaa kuongoza tabia za binadamu. Foucault anaangazia vikundi tofauti vya watu ambavyo vinatengwa kwa sababu ya tofauti zao na binadamu wengine, kama vile wendawazimu, wafungwa na masenge. Kwa mujibu wa Foucault, utamaduni uliotokea baada ya Mwamko uliunda kaida zilizofaa kuongoza tabia za binadamu. Hali hii ilipelekea kutengwa na hata kulaumiwa kwa utofauti, na asasi kama vile magereza, hospitali na vituo vya wendawazimu zikaundwa kama njia ya kukabiliana na hali hii ya utofauti. Kulingana na Foucault (1961), asasi kama hizi hudhihirisha uwezo wa kisiasa ambapo matakwa ya kundi tawala hulazimishwa kwa kundi tawaliwa. Katika masuala yanayohusiana na ngono, ilichukuliwa kuwa ngono iliyokuwa halali ni ile iliyohusisha watu wa jinsia tofauti. Hii ikawa ndiyo kaida iliyopaswa kufuatwa, na mashoga wakaonekana kuikiuka

kaida hii. Kwa mujibu wa Foucault, hali hii ya kusisitiza kufuatwa kwa kaida moja inayoongoza tabia za binadamu ni sehemu ya utamaduni wa kisasa ambao ni wa kimabavu. Hii ni aina ya simulizi kuu ambayo hupingwa na wanabaadausasa. Foucault, kama walivyo wanabaadausasa, anasisitiza haja ya kuzingatia utofauti wala sio kulazimisha watu kufuata kaida fulani katika maisha yao. Aidha, kama Lyotard (1979) anapendekeza uhuru wa binadamu wa kutenda anavyopenda kwa kupinga simulizi kuu zinazoongoza na kudhibiti matendo ya binadamu.

Gilles Deleuze na Felix Guattari (1984) ni wanaubaadaumuundo wanaopinga nadharia ya udodosinafsia inayohusishwa na tanzo ya Edipode (*Oedipus complex)*. Wanadai kuwa nadharia hii ni ya kimabavu kwa sababu inalenga kudhibiti uhuru wa binadamu kuhusu hisia na matamanio yake. Kwa Deleuze na Guattari, binadamu ana matamanio yake ambayo, aghalabu huzuiliwa na mamlaka ya kijamii na kisiasa, na nadharia ya udododsinafsia ni ishara ya namna hisia na matamanio hayo hukomeshwa. Mawazo haya yanalingana na yale ya Lyotard (1979) na Foucault (1961) ya kupinga simulizi kuu zinazodhibiti matendo ya binadamu.

Fredric Jameson (1991) naye alikuwa mwananadharia na mhakiki wa Kimarekani aliyeuhakiki na kuupinga ubaadausasa. Anayafafanua mawazo yake katika kitabu chake, *Postmodernism, or the Cultural Logic of Late Capitalism*. Katika kitabu hiki Jameson anaupinga ubaadausasa katika muktadha wa historia na siasa kwa madai kuwa ubaadausasa ni aina ya ubepari uliofikia hatua zake za mwisho. Kwake Jameson (1991), hakuna tofauti kubwa kati ya usasa na ubaadausasa kwa sababu zote zinarejelea maumbo ya kitamaduni ambayo hudhihirisha hatua tofauti za ubepari. Hatua ya kwanza ya ubepari ilitokea kati ya karne ya 18 na mwishoni mwa karne ya 19 huko Marekani na Uingereza pamoja na maeneo mengineyo yaliyoathiriwa na mataifa haya. Hatua hii inahusishwa na sanaa ya uhalisia pamoja na maendeleo mahsusi ya kiteknolojia (kama

vile uvumbuzi wa gari lililoendeshwa kwa mvuke). Hatua ya pili ilitokea mwishoni mwa karne ya 19 hadi katikati ya karne ya 20. Kipindi hiki kinahusishwa na mitambo iliyoendeshwa kwa stima pamoja na mwondoko wa usasa. Hatua ya tatu ni ya wakati wa sasa. Hiki ni kipindi kinachohusishwa na maendeleo ya kiteknolojia katika vifaa vya stima. Aidha, msisitizo katika kipindi hiki unahusu namna ya kuuza na kutumia bidhaa bali sio namna ya kuzitengeneza. Kulingana na Jameson, hatua hii ya mwisho ya ubepari, ndiyo inabainisha kipindi cha ubaadausasa. Kutokana na maelezo haya ya Jameson basi, ubaadausasa ni mojawapo ya hatua tatu za ubeperi kama ulivyo usasa. Mawazo haya ya Jameson (1991) yametumika katika utafiti huu kuhakiki ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika katika K21. Kama iliyobainika katika utafiti, kutokana na ubepari, mataifa ya Ulaya yameendelea kuyakandamiza mataifa ya Afrika hasa katika masuala ya kiuchumi. Aidha, yametumika kuonyesha namna vyombo vya habari vinavyotumiwa kama uwanja wa kuuzia bidhaa na kueneza utamaduni wa Kimagharibi.

Katika Sanaa hata hivyo, Jameson anaukosoa mtindo mpya wa ubaadausasa. Anaeleza kuwa katika kipindi hiki cha ubaadausasa uundaji wa kazi za kiujumi na kisanaa unalinganishwa na uundaji wa bidhaa nyinginezo. Katika muktadha huu utamaduni wa kibiashara haujatenganishwa na sanaa ya ubaadausasa bali ni sehemu ya sanaa hiyo. Kutokana na hali hii ubaadausasa unaleta hali ya kukosa uhalisia na kuibuka na kazi ambayo ni chapwa. Kutokana na ukosefu wa uhalisi wa kihistoria kupitia kile anachokiita ‘uwanja wa mitindo’ usioongozwa na kaida yoyote, nafasi ya wigobezo inachukuliwa na hali ya uigizaji usio na usanifu. Jameson (1991) anasema kuwa hapo awali uigizaji haukubeza tu bali ulidhihaki, ulikejeli na pia ulihukumu. Leo kupitia ubaadausasa wasanii hulenga tu kuunda upya maumbo matupu yasiyobeza wala kukejeli. Kwa hivyo, Jameson hakupendezwa na mitindo mipya ya ubaadausasa iliyoibuka ambayo utafiti huu umeishughulikia.

**2.5 Ubaadausasa kama Mtindo Maalum wa Kiuandishi na Kisanaa**

Maana ya dhana ya ubaadausasa imeendelea kupanuka na hivyo basi kupita mipaka ya kihistoria na kinadharia katika fasihi. Kama wanavyosema Lewis (2001) na Clayton (2012), ubaadausasa unaweza kuchukuliwa kama mwondoko wa kisanaa uliotokea kati ya mwaka wa 1960 na 1990 uliodhihirisha mtindo wa kipekee wa kiuandishi na kisanaa. Kwa mujibu wa Lewis (2001), baadhi ya waandishi na maandishi ya kibaadausasa yaliyoandikwa katika kipindi hiki ni pamoja na *Willie Masters' Lonesome Wife* (1967) ya William Gass, *Flight to Canada* (1976) ya Ishmael Reed na *Gerald's Party* (1986) ya Robert Coover. Baadhi ya bunilizi maarufu za upelelezi za kibaadausasa ni pamoja na *The Name of the Rose* (1984) ya Umberto Eco, *The New York Trilogy* (1987) ya Paul Auster na *Hawksmoor* (1985) ya Peter Acroyd miongoni mwa kazi nyinginezo. Kama inavyobainika, nyingi ya kazi hizi zilikuwa za Kiulaya na ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Katika fasihi ya Kiswahili, waandishi mbalimbali (Khamis, 2005; Gromov, 2008; Bertoncini, 2009; Traore, 2015) wanakubaliana kuwa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa ulianza kujitokeza katika miaka ya 1960. Maelezo ya kina kuhusu maandishi ya kibaadausasa katika fasihi ya Kiswahili yamejadiliwa katika sehemu ya 2.7 ya sura hii.

Kama mtindo wa kipekee wa kiuandishi, Kusnir (2011), Sharma & Chaudhary (2011) na Clayton (2012) wamebainisha baadhi ya vipengele vya ubaadausasa katika fasihi. Vipengele hivi hudhihirika sio tu katika kiwango cha dhamira na maudhui bali pia katika kiwango cha maana na muundo wake. Kwa mujibu wa Kusnir (2011) baadhi ya dhamira ambazo hujadiliwa katika kazi za fasihi ya kibaadausasa ni pamoja na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya hali ya anga hasa kutokana na kuzuka kwa viwanda ulimwenguni, uhakiki wa hali ya ulimwengu uliotawaliwa na mfumo wa ubidhaishaji wa vitu, dhamira zinazotambua umuhimu wa kuwa huru na kutenda kwa

hiari, pamoja na dhamira zinazoonyesha mtazamo hasi dhidi ya ustaarabu wa kimagharibi, na badala yake kupendekeza kuwepo na mtazamo wa kiasili au wa kawaida kuhusu ulimwengu. Baadhi ya sifa hizi zimejadiliwa kwa kina katika sehemu ya 2.8 ya sura hii.

Hata hivyo, baadhi ya maandishi ambayo yaliandikwa kabla ya 1960 vilevile yanaweza kuchukuliwa kama ya kibaadausasa kutokana na sifa zake zinazoakisi sifa za maandishi mengine kama yalivyofafanuliwa na Kusnir (2011), Sharma na Chaudhary (2011) na Clayton (2012) hapo juu. Kulingana na Carter (2006), mojawapo ya maandishi hayo ni yale ya Mfaransa Francois Rabelias aliyeishi kati ya 1494 na 1553. Bakhtin (1984), katika kitabu chake, *Rabelais and His World* anaeleza kwamba kazi za Rabelais ziliathiriwa kimuundo na kimaudhui na sherehe za kanivali. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), Selden n.w (2005) na Schmitz (2007), kanivali ilikuwa sherehe ya kitamaduni huko ulaya ambapo kaida na taratibu ambazo hupatikana katika maisha ya kawaida huvunjwa. Katika fasihi sifa za kanivali hudhihirika kupitia ukosefu wa mshikamano, mchanganyiko wa uhalisia na fantasia, ukiukaji wa kaida zilizozoeleka na matumizi ya lugha ya kubeza miongoni mwa sifa nyingine. Hizi ni baadhi ya sifa za kibaadausasa na ambazo zinapatikana katika kazi za Rabelais. Kwa mfano, maandishi ya Rabelais yalifuata mtindo wa kifantasia. Aidha, yalikuwa na wingi wa matumizi ya mwingiliano matini kutokana na kuchanganya mawazo kutoka taaluma mbalimbali kama vile dini, utabibu na uanasheria, na hivyo kuyafanya yasieleweke kwa urahisi. Vilevile, yalikuwa na matumizi ya wigo bezo. Hizi zote ni sifa katika maandishi ya ubaadusasa. Katika sehemu inayofuata, tumejadili ubaadausasa katika fasihi ya Kiswahili.

## 2.6 Ubaadausasa Katika Fasihi ya Kiswahili

Baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa katika K21 zinadhihirisha mabadiliko ya kimtindo kwa kuwa zimejikita katika mtindo wa uandishi wa kimajaribio

wa ubaadausasa unaenda kinyume na mtindo wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Wataalamu wengi (Khamis, 2002, 2005; Gromov, 2008, Bertoncini, 2009; Traore, 2015) wanaeleza kuwa uandishi wa kimajaribio wa ubaadausasa katika fasihi ya Kiswahili ulianza kujitokeza katika miaka ya 1960, kupitia kazi za Euphrase Kezilahabi, *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990). Kwa mujibu wa Khamis (2005: 91):

> Baadhi ya riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kuanzia mwaka wa 1990 hadi sasa zimejitenga kwa njia kadhaa na mtindo wa kiuandishi wa kihalisia uliotawala riwaya nyingi za Kiswahili. Mitindo ya kifantasia, uhalisiamazingaombwe na ubaadausasa ndiyo inayoonekana kusambaa katika riwaya hii 'mpya' kama njia ya kudhihirisha mabadiliko na uozo katika jamii za Afrika Mashariki. Mabadiliko haya yametokana na athari za mambo yaliyo ndani na nje ya jamii husika (TY).

Maelezo haya ya Khamis yanaubainisha ubaadausasa kama mtindo 'mpya' wa kiuandishi katika fasihi ya Kiswahili ulioanza kupata umaarufu katika mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini. Maelezo haya ya Khamis yanaakisi yale ya Traore (2015:20) anayeueleza ubaadausasa katika muktadha wa Kiafrika kama "…diskosi na michakato tofauti ya kifasihi ambayo huenda kinyume na urazini, muumano… na hukiuka kaida za uandishi wa kihalisia." Maelezo haya ya Traore yanadhihirisha upya katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili. Neno 'mpya' au 'upya' katika muktadha huu halijatumiwa kumaanisha kwamba mitindo hii haikuwa imewahi kutumika katika kazi za kifasihi. Kwa hakika kama tulivyobainisha katika fasihi ya kiulaya mtindo huu umekuwa ukitumika kwa muda mrefu hata kabla ya dhana ya ubaadausasa kuasisiwa. Hata hivyo, katika fasihi ya Kiswahili huu ni mtindo ambao haukuwa umetumika hapo awali kabla ya miaka ya 1990.

Kwa mujibu wa Khamis (2005), baadhi ya vipengele vinavyoitambulisha riwaya hii mpya ya Kiswahili ni pamoja na kuwepo na vipandevipande vya hadithi, ukosefu wa mshikamano, mwingiliano matini, kuchanganya tanzu mbalimbali katika kazi moja ya kifasihi pamoja na kuchanganya matukio ya kihalisia na ya kiajabu. Hizi zote ni sifa za

ubaadausasa na ndizo zitakazotumika kama nguzo kuu katika uchambuzi wa riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu.

Khamis (2005) na Waliaula (2010) wametaja baadhi ya riwaya za kibaadausasa katika fasihi ya Kiswahili. Hizi ni pamoja na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990) za Kezilahabi; *Walenisi* (1995) ya Mkangi; *Vipuli vya Figo* (1996) ya Mbogo; *Ziraili na Zirani* (1999) ya Mkufya; *Bin Adam!* (2002) ya Wamitila pamoja na *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia yao* (2005) na *Nyuso Za Mwanamke* (2010) za S. A. Mohamed. Wahakiki wa kazi hizi (k.m. Wamitila 2003; Khamis 2003, 2005; Waliaula 2010) wamejikita zaidi katika kipengele cha uhalisiamazingaombwe. Kwa mfano, Waliaula (2010:143) anaeleza kwamba riwaya za *Dunia Yao, Babu Alipofufuka, Nyuso za Mwanamke*, *Mzingile* na *Nagona* "zimetungwa kuusawiri uhalisia kama ulivyo lakini kwa kujumuisha vipengele vya kimazingaombwe". Hata hivyo, sifa wanazozizungumzia katika riwaya hizi ni zile zinazopatikana katika kazi za kisanaa za kiubaadausasa kama vile mwingiliano matini. Hii ni kuonyesha kwamba baadhi ya sifa za uhalisiamazingaombwe pia hutumika kama vipengele vya ubaadausasa. Kwa mfano, Khamis (2005) akirejelea riwaya mpya ya Kiswahili anaeleza kwamba vipengele vya uhalisiamazingaombwe na ubaadausasa vimeingiliana na kuathiriana hivi kwamba sio rahisi kuvitenganisha. Haya yanadhihirisha mwingiliano uliopo kati ya uhalisiamazingaombwe na ubaadausasa. Isitoshe, Waliaula (2010:145) akimnukuu D' Haen analifafanua zaidi suala hili na kusema:

> Uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye[8], linaloonyesha sifa za usasabaadaye kama vile kujirejelearejelea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha udhabiti wa wahusika na usimulizi vilevile, kumchanganya msomaji kwa maksudi na hali kadhalika kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti.

[8] Baadhi ya waandishi kama Waliaula (2010) hutumia neno usasabaadaye kurejelea kile ambacho utafiti huu umekiita ubaadausasa.

Inavyobainika ni kuwa uhalisiamazingaombwe ni kipengele mojawapo cha ubaadausasa. Mbali na vipengele tulivyovitaja hapo juu, utafiti huu umedhihirisha namna uhalisiamazingaombwe ulivyojitokeza katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu.

Wamitila (2003) na Khamis (2005), wanaeleza kwamba kazi za Shabaan Robert, *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* 1946/ 1967) ndizo zilizokuwa riwaya za kwanza katika Kiswahili kukiuka ukawaida wa kiuandishi uliokuwa umezoeleka kwa wakati huo. Kulingana na Khamis (2005) riwaya hizi zilitumia mtindo wa kilimbwende na kifantasia; Robert alijaribu kuunda ulimwengu mkamilifu hali iliyofanya matukio na matendo tofauti kuonekena ya kidhahania na ambayo hayawezi kutokea katika ulimwengu halisi. Ingawa Wamitila (2003) anaona kwamba riwaya za Robert zinadhihirisha sifa fulani za uhalisiamazingaombwe, kwake Khamis (2005) fantasia na uhalisia mazingaombwe (au ubaadausasa unaoambatana na uhalisia mazingaombwe) ni mambo mawili yanayokaribiana lakini yaliyo tofauti. Ni kutokana na sababu hii ambapo kazi za Robert hazichukuliwi kama za kibaadausasa.

Euphrase Kezihahabi ndiye anayechukuliwa kuwa na mchango mkubwa zaidi katika kuleta upya katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili katika kazi zake, *Nagona* na *Mzingile* hasa kuhusiana na matumizi ya uhalisia mazingaombwe na vipengele vya ubaadausasa (Wamitila 2003; Khamis 2005; Traore 2015). Upya anaouzungumzia Wamitila katika kazi hizi za Kezilahabi hasa umejikita katika kipengele cha mwingiliano matini ambao ni mojawapo ya sifa za ubaadausasa katika kazi za kisanaa. Khamis (2003) naye amebainisha sifa nyingine zinazojitokeza katika riwaya ya *Nagona* kama vile kuwepo na vipande vipande vya hadithi pamoja na ukosefu wa mshikamano ambavyo pia ni vipengele vya ubaadausasa katika kazi za kifasihi. Waandishi wengine wa miaka ya

tisini waliofuata mtindo wa kiubaadausasa ni kama vile Katama Mkangi (*Walenisi*), Mbogo (*Vipuli vya Figo*) na William Mkufya (*Ziraili na Zirani*).

Kuanzia mwaka wa 2000, waandishi ambao wameendelea kuutumia mtindo wa kiuandishi unaodhihirisha vipengele vya ubaadausasa katika fasihi ya Kiswahili ni pamoja na S.A. Mohamed, K. W. Wamitila na Clara Momanyi. Waandishi hawa ambao walianza kuandika tungo zao katika mtindo wa kihalisia wamedhihirisha mabadiliko makubwa katika uandishi wao hasa katika kazi walizoziandika katika mwongo wa kwanza wa K21. *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) za S. A Mohamed ni dhihirisho la mabadiliko hayo yanayodhihirisha sifa za kibaadausasa. Aidha, mabadiliko hayo pia yamejitokeza katika kazi zake nyingine kama vile *Babu Alipofufuka* (2001) na baadhi ya hadithi zake katika *Arusi ya Buldoza* (Walibora 2010). Kazi za Wamitila zinazodhihirisha vipengele vya ubaadausasa ni pamoja na *Bin Adam!* (2002) *Musaleo!* (2004) na *Unaitwa Nani*? *(2008)*. Kazi nyingine katika fasihi ya Kiswahili zinavyodhihirisha vipengele vya ubaadausasa ni *Nakuruto* (2009) ya Clara Momanyi, *Mafamba* (2008), *Watu wa Gehanna* (2012) na *Mashetani ya Alepo* (2015) za Tom Olali na *Chozi la Heri* (2017) ya Asumpta Matei miongoni mwa kazi nyingine. Hadithi fupi ya Robert Oduori, *Kikaza*, inayopatikana katika diwani ya *Damu Nyeusi* (2007) pia inadhihirisha matumizi ya ukosefu wa mshikamano katika ploti ambayo ni sifa mojawapo ya vipengele vya ubaadausasa.

### 2.7 Sifa Bainifu za Ubaadausasa katika Fasihi

Ubaadausasa kama mtindo wa uandishi katika baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa katika K21 una sifa zake bainifu zinazoutofautisha na mtindo wa awali wa uandishi uliojikita katika uhalisia. Khamis (2005), Kusnir (2011), Sharma na Chaudhary (2011) na Clayton (2012) wamebainisha baadhi ya sifa bainifu za ubaadausasa katika fasihi katika kiwango cha fani na maudhui. Katika kiwango cha

fani, riwaya za kibaadausasa huwa na matumizi ya vipandevipande vya hadithi, ukosefu wa mshikamano, mwingilianomatini, kuchanganya tanzu mbalimbali katika kazi moja ya kifasihi pamoja na matumizi ya uhalisiamazingaombwe, miongoni mwa sifa nyingine. Katika kiwango cha maudhui, riwaya hizi hushughulikia dhamira zinazohakiki simulizi kuu na kuonyesha umuhimu wa kuwa huru na kutenda kwa hiari. Aidha, zinahakiki nafasi ya vyombo vya habari katika ulimwengu uliotawaliwa na mfumo wa ubepari na ubidhaishaji wa vitu. Hizi zote ni sifa za ubaadausasa na ndizo zimetumika kama nguzo kuu katika uchambuzi wa riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu. Katika sehemu inayofuta tumejadili kwa kifupi baadhi ya sifa hizi.

### 2.7.1 Uhakiki wa Simulizi Kuu

Kwa mujibu wa Sharma na Chaudhary (2011) na Clayton (2012) uhakiki wa simulizi kuu ni kipengele kikuu ambacho hujitokeza katika fasihi ya kibaadausasa. Kulingana na Clayton (2012), neno simulizi kwa jumla hutumika kurejelea hadithi ambazo husimiliwa na watu ili kuweza kuupa ulimwengu wao maana. Hadithi hizi huwezesha watu kuhusiana, kuonyesha tofauti zilizopo baina ya watu au mambo tofauti, kutambulisha matabaka tofauti na kadhalika. Simulizi kuu nazo ni zile 'hadithi kubwa' ambazo watu wengi huamini na kukubali kuwa ni za kweli na zenye umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu. Kutokana na haya, wengi huzitegemea simulizi hizi ili kuweza kufanya maamuzi yao. Hii ni kwa sababu zinaambatana na hisia za kuwepo na ulimwengu mkamilifu ambapo maadili ya kijamii yanaweza kutathminiwa. Aidha, simulizi hizi zinachukuliwa kuwa msingi wa kuelezea hadithi nyingine zote zinazohusiana na maisha yetu. Kutokana na umuhimu ulioambatanishwa na simulizi kuu hizi watu wengi hulazimika kuzifuata, iwe kwa hiari au kwa lazima. Kwa wanaubaadausasa, simulizi hizi hutumiwa kuhalalisha mifumo inayokandamiza na kudhibiti matendo na hisia za wanajamii. Lengo kuu la wanaubaadausasa basi ni

kuzihakiki simulizi kuu kwa nia ya kuzibeza na kuonyesha kuwa hazihodhi ukweli zinazodai kuumiliki. Baadhi ya simulizi kuu ambazo Clayton (2012) ametaja ni kama vile hadithi inayohusiana na dhambi na ukombozi wa dhambi kupitia Yesu Kristo katika dini ya Kikristo, hadithi ya Mwamko wa Kitaaluma iliyoeleza kuhusu maendeleo ambayo yangeleta maarifa kamili, na hadithi ya Marx iliyolenga kuleta usawa, umoja wa kijamii na ukweli. Katika utafiti huu simulizi kuu zilizohakikiwa ni pamoja na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika na uhamiaji wa Waafrika katika mataifa ya ulaya. Aidha, asasi mbalimbali kama vile dini, utamaduni na elimu zimehakikiwa.

Mbali na kuhakiki simulizi kuu, Clayton (2012) anaeleza kuwa wanaubaadausasa pia huhakiki kazi maarufu katika uwanja wa kiakademia au kitamaduni. Clayton anaeleza kuwa kazi maarufu ni zile ambazo hazina budi kutumiwa au kurejelewa na mtafiti katika uwanja husika. Kazi hizi huchukuliwa kama za kipekee na zenye umuhimu mkubwa kwa sababu ukwasi wa maarifa unaopatikana ndani yake. Wanaubaadausasa basi huzihakiki kazi hizi ili kubainisha kuwa vitabu hivi ni vya kawaida tu lakini vilivyotawaliwa na mapendeleo yanayolenga kutimiza matakwa ya kundi fulani la watu, liwe la kijinsia, kirangi au kijamii. Katika kuzihakiki, wanaubaadusasa wanaonyesha namna kazi zenyewe zinavyobagua kikundi fulani cha watu katika jamii. Aidha, wanaweza kubainisha usomaji mpya wa kazi zenyewe unaoenda kinyume na usomaji wa kazi hizo uliozoeleka.

### 2.7.2 Ukosefu wa Udhabiti katika Vipengele vya Ukweli na Maana

Clayton (2012) anaeleza kuwa wanaubaadausasa huamini kwamba ukweli na maana sio mambo dhabiti au imara bali hubadilikabadilika kutegemea muktadha. Wanarai kuwa ukweli hauwezi kuegemezwa katika msingi maalum bali unafaa kufasiriwa kama jambo ambalo huweza kutimiza matakwa fulani katika kipindi fulani. Hivyo basi maana

ya jambo lolote linalohusiana na hali tofauti za maisha ya binadamu haina budi kubadilika katika vipindi tofauti ili kutimiza matakwa fulani katika muktadha husika. Katika sanaa, fasihi ikiwemo, wanaubaadausasa hudhihirisha madai haya (kuwa ukweli na maana sio imara) kwa kukiuka au kubadilisha kaida au nguzo muhimu zinazoambatanishwa na kazi husika. Katika utafiti huu kwa mfano, tumeangazia namna riwaya zilizoteuliwa zinavyokiuka kaida za kihalisia zilizohusishwa na riwaya za kimapokeo na kutumia vipandevipande vya hadithi badala ya kuwa na hadithi yenye mshikamano kutoka mwanzo hadi mwisho.

### 2.7.3 Mwingiliano Matini

Kwa mujibu wa Clayton (2012) kazi za kibaadausasa huwa na wingi wa mwingiliano matini na mwingiliano tanzu. Wanaubaadausasa wanaamini kuwa hakuna kazi yoyote ya kifasihi inayoweza kuchukuliwa kama mpya au asili. Wanaamini kuwa mwanafasihi hutumia tanzu na maumbo mengine ya awali kwa ubunifu ili kuibuka na maana mpya ya kazi zao katika miktadha tofauti ya kiisimu na kitamaduni. Utafiti huu umeonyesha namna waandishi hurejelea maandishi na kazi za wataalamu wengine katika kazi zao. Kwa mfano. Kuna urejeleaji wa vitabu vya fasihi, vitabu vya kidini, filamu, nyimbo na kadhalika. Urejeleaji huu wakati mwingine humuwia vigumu msomaji katika kufuatilia dhamira zinazojadiliwa hasa iwapo msomaji hana ujuzi wowote wa kazi zilizorejelewa.

### 2.7.4 Uanuwai wa Mawazo

Sharma na Chaudhary (2011) wanaeleza kuwa fasihi ya kibaadausasa husisitiza mfumo unaotambua uanuwai au wingi wa mawazo pamoja na uanuwai katika namna ya kuufafanua ulimwengu (plurality and relativism). Uanuwai wa mawazo katika kazi ya fasihi hudhihirika kwa njia tofauti. Kwa mfano, wahusika ambao awali walipuuzwa huanza kusawiriwa kwa njia chanya. Aidha, unaweza kujitokeza kupitia matumizi ya sauti tofauti katika usimulizi ambazo hupishana na kuingiliana, au kupitia matumizi ya

mitindo na tanzu tofauti katika kazi moja. Uanuwai katika namna ya kuutazama ulimwengu hudhihirika kupitia matumizi ya hitimisho wazi badala ya hitimisho funge katika kazi ya fasihi. Hitimisho wazi humpa msomaji nafasi ya kushiriki katika kuiunda maana ya matini husika hivyo kuwezesha kuwepo na mitazamo mbalimbali badala ya kuwa na mtazamo mmoja pekee. Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa uliojadiliwa katika utafiti huu ni mfano wa uanuwai kuhusu maana ya riwaya ya Kiswahili. Awali riwaya ilielezwa kwa kuzingatia mtindo wa uandishi wa uhalisia ambapo matukio yalifuatana kikronolojia. Hata hivyo, katika riwaya za kibaadausasa kama zile zilizojadiliwa katika utafiti huu, matukio hayajafuatana kiwakati bali kuna uchopekaji wa vipande vya simulizi.

### 2.7.5 Uhalisia Mazingaombwe

Kwa mujibu wa Waliaula (2010) uhalisia mazingaombwe ni tawi mahususi la ubaadausasa. Akieleza kuhusu fasihi ya kibaadausasa Kusnir (2011), anasema kuwa wakati mwingine inakuwa vigumu kuweka mipaka kati ya uhalisia, fantasia, bunilizi, na ndoto za mhusika fulani. Hii ina maana kuwa katika fasihi ya ubaadausasa, mipaka kati ya uhalisia na umazingaombwe huzibwa na matukio ya kihalisi huenda sambamba na matukio ya kiajabu na kifantasia. Wakizungumzia kuhusu uhalisiamazingaombwe, Sharma na Chaudhary (2011) wanaeleza kuwa kazi za fasihi zilizotumia mbinu hii aghalabu huwa na matumizi mengi ya mambo ya kufikirika, ya kifantasia na yenye sifa za kindoto. Mambo ya kihalisia huchanganywa na yale ya kifantasia au yasiyo ya kawaida. Kaida ya wakati hukiukwa nao usimulizi na ploti huwa changamano sana. Aidha, kuna matumizi ya mchanganyiko wa ndoto, visasili pamoja na hadithi zenye wahusika wenye uwezo usio wa kawaida (fairy stories). Kwa mujibu wa Kusnir (2011) uhalisia mazingaombwe katika kazi ya fasihi unaweza kudhihirika wakati wahusika ambao waliishi katika ulimwengu halisi katika kipindi fulani cha kihistoria hukutana

na wahusika wa kubuni. Aidha, wahusika halisi walioishi katika vipindi tofauti vya kihistoria hukutana katika ulimwengu wa sasa wa kiubunifu. Vilevile, wahusika halisi wa kihistoria wanaweza kudhihirishwa katika hali ya kiubunifu. Hali hii hudhihirisha kipindi cha ubaadausasa ambapo ulimwengu umejaa fujo na ghasia na sio rahisi kuuelewa wala kupambana nao. Katika utafiti huu, tumedhihirisha namna vipengele vya uhalisia vinavyotumika sambamba na vile vya umazingaombwe na vya kindoto. Kwa mfano, kuna matumizi mengi ya vivuli na mizuka inayowasiliana na watu halisi katika mazingira halisi. Aidha, kuna matumizi ya viumbe halisi wenye sifa zilizozidi uwezo wa binadamu wa kawaida.

### 2.7.6 Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi

Uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mojawapo ya mbinu ya mtindo wa uandishi wa riwaya za kibaadausasa iliyotumiwa na waandishi wa riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu. Wataalamu mbalimbali (Best na Keller, 1991; Sim, 2001; Khamis 2008; Mwamzandi 2013) wanakubaliana kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mtindo mamboleo unaokiuka kaida za awali za uandishi uliokuwa muundo wenye muumano na mshikamano. Kwa mujibu wa Best na Keller (1991), uchopekaji wa vipande vya simulizi unahusu ukiukaji wa muundo maalum, mpangilio na mtiririko wa kazi ya fasihi. Badala yake hupendelea mitindo inayofafanuliwa na kutokuwepo kwa mpango, yenye vurugu na ubahatishaji, isiyo na mfululizo, isiyo wazi na iliyojaa michezo.

Sim (2001) anasema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni ubadilishaji au ukiukaji wa ploti, wahusika, mandhari na maudhui katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtindo huu husababisha mabadiliko katika tanzu za fasihi kutoka mitindo tuliyokuwa tumeizoea. Maelezo haya yanalingana na yale ya Khamis (2008:22) akieleza kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili na kusema kuwa riwaya hii inakiuka takriban misingi yote ya kanuni za riwaya za kihalisia zilizoitangulia:

> [Katika riwaya mpya] hakuna hadithi inayoshikamana kiwakati kama tuzijuavyo hadithi zilizoandikwa kwa mtindo wa kihalisia. Badala yake kuna vipande vipande vya hadithi, matukio, vituko na visa ambavyo vimevunjwavunjwa maksudi na kukutanishwa mbali na mnyororo wa safari au utashi wa mhusika fulani kutaka kugundua na kutatua tatizo fulani.

Mawazo haya ya Khamis (2008) ndiyo yamejitokeza katika riwaya za utafiti huu ambapo ploti katika riwaya hizi hazifuatani kiwakati bali zimeundwa kwa vipande vidogo vidogo vya hadithi. Mtindo wa uandishi wa riwaya hizi pia unaambatana na maelezo ya Mwamzandi (2013) kuhusu riwaya za kibaadausasa anaposema kuwa "Matukio katika riwaya hizi yanaonekana kama vipengele vilivyojitenga na vingine badala ya vipengele hivi kuingiliana na kujengana na kukamilishana". Kwa mujibu wa Ritgerotil (2006) mtindo wa uchopekaji wa simulizi husababisha fasihi kuwa katika vipande vipande, wala hakuna mshikamano tuliokuwa tumeuzoea. Ukweli huu pia umeelezwa na Sim (2001: 127) anayesema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi hufanya usimulizi kutofululiza na matukio kutapakaa kila pahali.

Katika utafiti huu, uchopekaji wa vipande vya simulizi umechukuliwa kama ukiukaji wa kaida za awali za uandishi wa riwaya ya Kiswahili iliyojikita katika uhalisia. Mtindo huu wa awali ulikuwa umependekezwa na akina Plato na Aristotle waliodai kuwa lazima ploti ingekuwa na muumano na muungano kuanzia mwanzo hadi mwisho. Yaani, iwe na mwanzo, kati na mwisho. Hata hivyo, kama inavyodaiwa na wanaubaadausasa, imani hizo zimepitwa na wakati. Wanaubaadausasa hupendelea njia tofauti za kuwasilisha kazi ya sanaa ili kukidhi mahitaji tofauti ya jamii. Uwasilishaji huu ndio uliozua mhimili wa uchopekaji wa vipande vya simulizi ambapo kazi ya kibaadausasa hazina mantiki katika mpangilio wa matukio na visa. Kama anavyosema Lewis (2001) maudhui katika riwaya za kibaadausasa huwa changamano na si rahisi kueleza juu yake. Haya ni kweli katika riwaya za utafiti huu kwa sababu maudhui hayo

yamechopekwa huku na huku bila mpangilio maalum na ni jukumu la msomaji au mtafiti kuyakusanya na kuyaunganisha pamoja ili yaweze kuelezeka.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imefafanua dhana ya ubaadausasasa kwa jumla pamoja na sifa zake bainifu katika fasihi kwa kuzingatia mawazo ya wataalam mbalimbali. Imebainika kuwa si rahisi kuifafanua dhana hii kwa nia moja kwani inahusishwa na miktadha na taaluma mbalimbali. Utafiti huu basi umeifafanua kwa njia tatu kuu; kwa kuzingatia misingi ya kihistoria, kwa kuzingatia mtazamo wa kinadharia na kifalsafa na hatimaye kwa kuuangalia kama mtindo wa kipekee wa fasihi na sanaa. Katika misingi ya kihistoria, ubaadausasa unadhaniwa kuanza kati ya mwaka wa 1930 na 1960 katika mataifa ya Ulaya. Katika msingi wa kinadharia, ubaadausasa umeelezwa kama mwondoko unaopinga simulizi kuu. Hizi ni simulizi ambazo zinadai kuhodhi ukweli halisi au kutoa maelezo bia ya kuufasiri ulimwengu. Katika kujadili ubaadausasa kama mtindo maalum wa kiuandishi, imebainika kuwa mtindo huu hudhihirisha sifa zake bainifu kama vile matumizi ya vipande vipande vya hadithi, mwingilianomatini, matumizi ya uhalisiamazingaombwe na wigo bezo miongoni mwa vipengele vingine

# SURA YA TATU

# MATUMIZI YA MBINU YA UANDISHI YA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI NA UHAKIKI WA SIMULIZI KUU

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imejadili matumizi ya mbinu ya uandishi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi na namna simulizi zenyewe zimetumika kuhakiki simulizi kuu mbalimbali katika riwaya za utafiti huu. Uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mtindo wa kimajaribio unaoenda kinyume na mtindo wa awali wa uandishi wa riwaya uliojikita katika uhalisia. Tangu enzi za Plato na Aristotle mtindo wa uandishi wa kihalisia ndio uliozoeleka na ulitumiwa kama kigezo cha kueleza riwaya ni nini. Mojawapo ya vigezo hivyo ni kuwa riwaya ilipaswa kuwa na mshikamano, na matukio yalipaswa kufuatana kiwakati au kikronolojia. Hii ni tofauti na mtindo wa uandishi wa riwaya za ubaadausasa zinazokaidi kauli hii ambapo tunapata vipande vipande vya simulizi visivyooana, mtindo ambao tumeuita uchopekaji wa vipande vya simulizi katika utafiti huu. Sura hii imekidhi lengo la pili la tasnifu hii la kufafanua mtindo wa kipekee wa uchopekaji wa vipande vya simulizi unaojitokeza katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu. Aidha, kwa kutumia mojawapo ya mihimili ya nadharia ya ubaadausasa kama inavyofafanuliwa na Lyotard (1979), sehemu hii imehakiki baadhi ya simulizi kuu zinazojitokeza katika vipande vya simulizi vilivyojadiliwa. Ili kutimiza malengo haya, sura hii imegawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa sura yenyewe nayo sehemu ya pili imeeleza kwa kifupi kuhusu dhana ya uchopekaji wa vipande vya simulizi. Katika sehemu ya tatu tumeshughulikia simulizi inayohakiki maana ya uhuru kwa kuzingatia hali halisi ya mataifa ya Afrika baada ya uhuru. Sehemu ya nne imeihakiki ajenda za mataifa ya Ulaya kwa mataifa ya Afrika na mbinu

zinazotumiwa kuendeleza ajenda hizo. Simulizi inayohakiki suala la uhamiaji na athari zake imejadiliwa katika sehemu ya tano nayo sehemu ya sita ni hitimisho la sura nzima.

### 3.1 Dhana ya Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi kama Mbinu ya kiubunifu

Uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mojawapo ya mbinu ya mtindo wa uandishi wa riwaya za kibaadausasa iliyotumiwa na waandishi wa riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu. Wataalamu mbalimbali (Best na Keller, 1991; Sim, 2001; Khamis 2008; Mwamzandi 2013) wanakubaliana kuwa uchopekaji wa vipande vya visimulizi ni mtindo mamboleo unaokiuka kaida za awali za uandishi uliokuwa muundo wenye muumano na mshikamano. Kwa mujibu wa Best na Keller (1991), uchopekaji wa vipande vya simulizi unahusu ukiukaji wa muundo maalum, mpangilio na mtiririko wa kazi ya fasihi. Badala yake hupendelea mitindo inayofafanuliwa na kutokuwepo kwa mpango, yenye vurugu na ubahatishaji, isiyo na mfululizo, isiyo wazi na iliyojaa michezo.

Sim (2001) anasema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni ubadilishaji au ukiukaji wa ploti, wahusika, mandhari na maudhui katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtindo huu husababisha mabadiliko katika tanzu za fasihi kutoka mitindo tuliyokuwa tumeizoea. Maelezo haya yanalingana na yale ya Khamis (2008:22) akieleza kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili na kusema kuwa riwaya hii inakiuka takriban misingi yote ya kanuni za riwaya za kihalisia zilizoitangulia:

> [Katika riwaya mpya] hakuna hadithi inayoshikamana kiwakati kama tuzijuavyo hadithi zilizoandikwa kwa mtindo wa kihalisia. Badala yake kuna vipande vipande vya hadithi, matukio, vituko na visa ambavyo vimevunjwavunjwa maksudi na kukutanishwa mbali na mnyororo wa safari au utashi wa mhusika fulani kutaka kugundua na kutatua tatizo fulani.

Mawazo haya ya Khamis (2008) ndiyo yamejitokeza katika riwaya za utafiti huu ambapo ploti katika riwaya hizi hazifuatani kiwakati bali zimeundwa kwa vipande

vidogo vidogo vya hadithi. Mtindo wa uandishi wa riwaya hizi pia unaambatana na maelezo ya Mwamzandi (2013) kuhusu riwaya za kibaadausasa anaposema kuwa "Matukio katika riwaya hizi yanaonekana kama vipengele vilivyojitenga na vingine badala ya vipengele hivi kuingiliana na kujengana na kukamilishana". Kwa mujibu wa Ritgerotil (2006) mtindo wa uchopekaji wa simulizi husababisha fasihi kuwa katika vipande vipande, wala hakuna mshikamano tuliokuwa tumeuzoea. Ukweli huu pia umeelezwa na Sim (2001: 127) anayesema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi hufanya usimulizi kutofululiza na matukio kutapakaa kila pahali.

Katika utafiti huu, uchopekaji wa vipande vya simulizi umechukuliwa kama ukiukaji wa kaida za awali za uandishi wa riwaya ya Kiswahili iliyojikita katika uhalisia. Mtindo huu wa awali ulikuwa umependekezwa na akina Plato na Aristotle waliodai kuwa lazima ploti ingekuwa na muumano na muungano kuanzia mwanzo hadi mwisho. Yaani, iwe na mwanzo, kati na mwisho. Hata hivyo, kama inavyodaiwa na wanaubaadausasa, imani hizo zimepitwa na wakati. Wanaubaadausasa hupendelea njia tofauti za kuwasilisha kazi ya sanaa ili kukidhi mahitaji tofauti ya jamii. Uwasilishaji huu ndio uliozua mhimili wa uchopekaji wa vipande vya simulizi ambapo kazi ya kibaadausasa hazina mantiki katika mpangilio wa matukio na visa. Kama anavyosema Lewis (2001) maudhui katika riwaya za kibaadausasa huwa changamano na si rahisi kueleza juu yake. Haya ni kweli katika riwaya za utafiti huu kwa sababu maudhui hayo yamechopekwa huku na huku bila mpangilio maalum na ni jukumu la msomaji au mtafiti kuyakusanya na kuyaunganisha pamoja ili yaweze kuelezeka. Mohamed (2006) anatilia mkazo ukweli huu katika riwaya yake ya *Dunia Yao*, mojawapo ya riwaya za utafiti huu, anaposema yafuatayo:

> Katika simulizi na mapito yake, vipandevipande – si lazima vishikane. Unavimwaga tu vipande vyenyewe kama unaatika mbegu kwenye shamba la Sanaa. Unafanya hivyo kuwaacha wasomaji waunge

> wenyewe vipande vya maana zao, huku maneno mengine ukiyajengea vivuli ili kuwatenga makusudi watafute maana zao badala ya kuzipata maana kibungabunga…kipande hapa… kipande pale. Vipande vya 'allegory'. Vipandevipande vya ngano mpya. Ngano ya tafrani-za-kileo katika usogori mpya (*DY* uk 9, 68).

Ni dhahiri kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi au matumizi ya vipandevipande vya simulizi kama inavyorejelewa katika dondoo ni mbinu mojawapo ya uandishi katika riwaya za ubaadausasa. Ni jukumu la mwandishi kuunga vipandevipande hivyo vya hadithi ili kuwasilisha maana zao wenyewe. Baadhi ya simulizi hizi hujikita katika 'tafrani-za-kileo'(*DY* uk 68). Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018) tafrani ni fujo, ghasia au hali ya kutokuwa na utulivu. Kwa hivyo, simulizi za tafrani za kileo ni simulizi zinazozungumzia fujo, ghasia na ukosefu wa mshikamano katika ulimwengu wa sasa. Mawazo haya yanaakisi yale Khamis (2003) anayesema kuwa matumizi ya vipande vidogo vya hadithi visivyounganika vizuri ni mbinu ya kimaksudi anayoitumia mwandishi kama dhihirisho la ukosefu wa mshikamano katika jamii ya kisasa barani Afrika. Katika kuujadili mtindo huu wa uchopekaji, maudhui mengi yanayojitokeza ni kielelezo cha ukosefu wa mshikamano katika mataifa mengi ya Afrika kama inavyojitokeza katika riwaya za utafiti huu. Kwa kuwa Maudhui hayo ni mengi sana, tasnifu hii imeteua masuala matatu makuu ambayo aghalabu yamejitokeza katika riwaya zote tatu za utafiti. Masuala hayo ambayo tumeyaita simulizi katika utafiti huu ni uhakiki wa maana ya uhuru kwa kujikita katika hali halisi ya mataifa ya Afrika baada ya uhuru. Aidha, tumehakiki ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika na mbinu zinazotumiwa kuziendeleza ajenda hizo. Hatimaye tumehakiki simulizi inayohusiana na uhamiaji katika mataifa ya ulaya na athari zake.

### 3.2 Uhakiki wa Maana ya Uhuru katika Mataifa ya Afrika

Kama sehemu ya utangulizi wa sehemu hii, ni muhimu kutoa usuli wa riwaya za utafiti pamoja na nchi ambamo riwaya zenyewe zimetungiwa ili kuweka msingi imara wa

kuijadili mada ya sehemu hii. Riwaya za utafiti huu zimetungiwa katika mandhari ya enzi za baada ya uhuru katika nchi za Afrika Mashariki. Riwaya za *DY* na *NZM* kwa mfano, zimetungiwa katika mandhari ya nchi ya Tanzania huku riwaya *UNN* ikitungiwa katika mandhari ya nchi ya Kenya.

Kama tunavyofahamu, kabla ya uhuru nchi ya Tanzania ilikuwa chini ya ukoloni wa Wajerumani na Waingereza mtawalia, nayo Kenya ilikuwa chini ya utawala wa Waingereza. Kwa wakati mmoja Waarabu pia waliwahi kutawala katika maeneo yanayokaribiana na upwa wa nchi hizi. Utawala wa Wajerumani, Waingereza na Waarabu uliandamana na unyanyasaji dhidi ya wenyeji. Akizungumzia kuhusu ukoloni wa Waingereza, Ndege (2009:5) kwa mfano anaeleza namna sera za Waingereza zilivyowaathiri Wakenya kwa njia hasi. Kwa mfano, mashamba ya Mwafrika, hasa yaliyokuwa katika maeneo mazuri yalinyakuliwa na wakoloni ili kuendeleza kilimo. Wakoloni waliwatumia Waafrika kufanya kazi katika mashamba haya kwa malipo duni. Walisimamiwa na wanyapara, na wakati mwingine kucharazwa ili wafanye kazi bila kuzembea. Isitoshe walilipishwa kodi na kutengwa kwa sababu ya rangi yao.. Sio tu wakoloni waliowanyanyasa Waafrika bali pia Waafrika wenyewe waliokuwa wameteuliwa kama viongozi katika ngazi za chini. Kwa mfano, katika riwaya ya *UNN* tunaelezwa kuhusu Sini aliyekuwa chifu katika enzi za ukoloni na namna alivyonyakuwa mashamba kwa njia isiyo halali. Tunaelezwa kuwa Sini alikuwa ‘mmiliki mkubwa wa mashamba mengi ajabu – aliyoyapata kwa kutumia mamlaka yake ya uchifu na kuwatishia wanyonge wengi…’ (*UNN* uk 237). Matumizi mabaya ya mamlaka pamoja na vitisho vinawawezesha viongozi kama Sini kunyakuwa mashamba na kuwanyamazisha raia wasivisaili vitendo hivyo viovu. Hivyo basi, ukoloni ulihusishwa na utumwa na unyanyasaji kwa Mwafrika, mambo yanayodhihirisha ukosefu wa haki na usawa. Hali ya kutaka kujitoa katika utumwa wa Wakoloni na

kuleta haki na usawa ni baadhi ya mambo yaliyochochea Waafrika kutaka kupigania uhuru. Katika muktadha wa ubaadausasa, uhuru wa Mwafrika kutoka kwa mkoloni basi unaweza kuchukuliwa kama aina ya simulizi kuu, kama ulivyokuwa mwondoko wa Mwamko wa Kitaaluma, kwani ulitarajiwa kuleta matumaini na mabadiliko chanya kwa Mwafrika. Hata hivyo, kama wanavyosema wanaubaadausasa simulizi kuu, kama hii ya uhuru na hata mwondoko wa Mwamko, haiwezi kuaminiwa tena, na inafaa kusailiwa kwani haikuleta wala kutimiza matumaini yaliyotarajiwa kama inavyojitokeza katika riwaya za utafiti huu. Kwa mfano, katika riwaya ya *NZM*, tunaelezwa kuhusu lalama za wananchi baada ya uhuru:

> Wanabaki kujiuliza kinatokea nini katika maisha yao? Laana ya Mungu au mapuuza ya binadamu mwenyewe? Ya wapi yale waliyoelezwa kuhusu usawa? Ya wapi yale waliyoahidiwa? Uhuru na kazi. Uhuru na haki. Uhuru na maendeleo. Uhuru na nini sijui… Yako wapi matunda waliyoambiwa watagawiwa akishaondoka Mzungu na Mwarabu? (*NZM* uk 37).

Kama inavyojitokeza kuwenye dondoo hapo juu, uhuru wa Mwafrika kutoka Wakoloni wa Kizungu na Kiarabu ulitarajiwa kuandamana na nafasi za kazi, usawa, maendeleo na haki. Hata hivyo, baada ya kupata uhuru mambo haya hayajatimizwa na ndipo raia wanalalamika wakiuliza 'Ya wapi yale waliyoahidiwa? Uhuru na kazi. Uhuru na haki. Uhuru na maendeleo…Yako wapi matunda waliyoambiwa watagawiwa akishaondoka Mzungu na Mwarabu? Malalamiko haya ni ishara kuwa raia hawajapata matunda ya uhuru. Badala yake wanaendelea kupitia hali ngumu ya maisha chini ya viongozi waliowachagua wenyewe. Sehemu inayofuta basi inaangazia masuala haya kuhusu ukosefu wa usawa, ukosefu wa haki na ukosefu wa maendeleo kama yanavyojitokeza katika riwaya za utafiti huu.

### 3.2.1 Ukosefu wa Haki na Usawa

Kama tulivyokwisha taja katika sehemu iliyotangulia, viongozi huwa katika mstari wa mbele katika kuwakosesha raia haki na usawa katika shughuli zao za kila siku. Riwaya

zilizotafitiwa zinadhihirisha namna ukosefu wa haki na usawa miongoni mwa viongozi umeifanya hali ya raia wa kawaida kuendelea kuzorota huku maisha ya viongozi yakiendelea kunawiri. Mojawapo ya mambo yanayoonyesha ukosefu wa haki na usawa ni unyakuzi wa ardhi unaotekelezwa na viongozi katika nchi huru za Afrika kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Bado mpaka leo wakulima wananung'unika, na hawatasita milele ingawa hawajui wamlalamikie nani. Vipi yule mfuavyoo jana leo awe tajiri mkubwa kiasi hiki? ...hakusomba mali tu, bali kaiba heshima ya wakulima baada ya kuwanyang'anya ardhi na uhuru wao. Na uhuru ni nini kama si kipato? Ghafla amepata nguvu zinazomsimamisha kumsuta kila mtu. Nguvu ambazo watu huziona kila siku zikiharibu, lakini hawawezi kuzizuia. Mwanzo [Bwana Hila] alianza kidogo kidogo kununua vipande vya ardhi zao…wakulima katika ununuzi huu nao wakawa wanasukumwa pembezoni kwa mkono wa kuvunga sheria. Wakasukumwa nyuma kabisa. Ardhi ya bwana huyo taratibu ikawa nyama kubwa lililomeza kila kitu cha watu wengine…hatimaye wakulima wakawa wako mbali naye. Hata hawamwoni wala hawamsikii isipokuwa sauti za majibwa yake… (*NZM* uk 37).

Viongozi kama Bwana Hila katika dondoo wanatumia vyeo vyao kujilimbikiza mali huku wakiwanyanyasa raia. Mali ambayo wanajilimbikizia inatokana na njia zisizo za haki kama unyakuzi wa ardhi. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa Bwana Hila anawanyang'nya wakulima 'ardhi na uhuru wao'. Wanaonyang'anywa ardhi ni wakulima wenye mashamba yaliyo karibu na makaazi ya Bwana Hila. Anatumia mamlaka yake na sheria kuwasukuma 'nyuma kabisa' mbali na makazi yake na hatimaye ardhi ya Bwana Hila inakuwa 'nyama kubwa lililomeza kila kitu cha watu wengine'. Shamba la Bwana Hila kwa mfano, tunaelezwa kuwa lilikuwa 'wanja linalotambaa na kwenda upeo wa macho au kwenda pasi na kikomo (*NZM* uk 35). Ingawa raia hawafurahishwi na udhalimu huu hawana uhuru wa kujieleza na kutetea haki zao kwani viongozi wana nguvu zinazowasaidia 'kumsuta kila mtu na hawawezi kuzizuia'. Hii inaonyesha kuwa viongozi wamejawa na kiburi na watumia vyeo vyao kuwakomesha raia wanaopinga suala la unyakuzi wa ardhi. Viongozi ambao awali

walikuwa watu wa kawaida tu kama topasi au mfuachoo kama anavyorejelewa kwenye dondoo wanaishia kuwa matajiri wakubwa kutokana na unyakuzi wa ardhi. Unyakuzi wa mashamba ni dhihirisho la ukosefu wa haki na usawa ambao ulikusudiwa kupatikana baada ya uhuru. Ukosefu wa haki na usawa uliokuweko enzi za ukoloni mkongwe unachipuka upya kama ukoloni mamboleo, jambo ambalo linausaili uhuru kama ulivyokusudiwa.

Mbali na kunyakua mashamba, viongozi wanajitenga mbali na raia waliowachagua punde wanaposhika hatamu za uongozi. Kwa mfano, kwenye dondoo hapo juu, tunaelezwa kuwa raia hawamwoni wala kumsikia Bwana Hila (*NZM* uk 37). Hii ni kutokana na masafa marefu kati yake na raia kwa sababu ya shamba lake kubwa. Vilevile, milio ya majibwa ni ishara kuwa eneo hilo limelindwa sawasawa. Aidha, tunaelezwa kuwa shamba hili 'limezungukwa na makuta marefu, manene…yaliyokusudiwa kuziba macho maovu yasiingie ndani' (*NZM* uk 36). Raia waliowachagua viongozi wanaishia kuonekana kuwa kero kwao. Hii inaonyesha kuwa viongozi hawatangamani kamwe na raia waliowachagua. Badala yake wanajitenga mbali na kelele na ghasia za raia waliowachagua na kujali tu utulivu na starehe zao.

Hali sawia na hii pia inajitokeza katika riwaya ya *UNN* ambapo tunaelezwa kuwa wabunge hawapatikani nyumbani kwao baada ya uchaguzi. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa Mheshimiwa Kasina huwa 'anafika nyumbani usiku na kuondoka alfajiri' kwa kuwa 'anaogopa kurogwa' (*UNN* uk 66). Naye Mheshimiwa Atiriri hapatikani kwake isipokuwa 'wakati wa mazishi atakapotokeza na kutumia fursa anayopewa kuwafariji wafiwa kuzungumzia siasa' (*UNN* uk 179). Wanapowakosa viongozi nyumbani mwao, baadhi ya raia wanafanya jitahada za kuwatafuta viongozi hao wanaoishi mijini kwenye ofisi zao. Hata hivyo, wanapuuzwa wanapofika huku na hawatimiziwi matakwa yao

kama kilivyo kisa cha Wamae (*UNN* uk 179-181). Huu ni ubinafsi uliokithiri na hali ya kutowajali raia.

Mabadiliko ya kiutawala hayabadilishi hali ya raia. Kwa hakika hali yao hubakia kuwa mbaya zaidi kuliko ya utawala uliotangulia kutokana na ukatili wa viongozi:

> Usisikie wewe, nguvu ndizo zinazotawala kila siku. Lakini nguvu zozote hazidumu milele, kwani nyumba ya nguvu moja huja kukaliwa na nguvu nyingine…kila nguvu ni kama mwambangoma. Kwani kila siku mwambangoma huvutia kwake. Kwa sababu hii kila nguvu ina sehemu kubwa ya uharibifu. Lakini nguvu haidumu…Na inapokuja nguvu mpya kuisukuma nguvu konge, uharibifu huwa maradufu. Katika jambo hili, wanaoteketea kila siku ni watu wa chini. Kwa bahati mbaya, huu ndio mwenendo wa dunia yetu. Hasa dunia ya siku hizi…danganya, piga, chinja, nyang'anya, ua, fisidi, aibisha, dhalilisha… Na eti wale wasio nguvu ndio wanaosaidia kudanganywa, kupigwa, kichinjwa, kunyang'anywa, kuuliwa… (*NZM* uk 9).

Katika dondoo hili hapa juu, viongozi katika mataifa ya Afrika wanarejelewa kama 'wenye nguvu'. Wanalinganishwa na 'mwambangoma anayevutia kwake' kudhihirisha hali yao ubinafsi unaosababisha kila aina ya hila na uovu katika mataifa haya. Kwa mfano, wanahusika katika kudanganya, kuua na kufisidi miongoni mwa maovu mengine. Kila mara uongozi unapobadilishwa raia wanateseka maradufu kwa sababu viongozi wapya wananyakua kile kilichobakishwa na uongozi wa awali.

Wakati mwingine juhudi za raia za kuwatoa mamlakani viongozi dhalimu zinaambulia patupu. Kwa mfano, Kassim anaangamizwa kisiasa na kiuchumi na mbunge wao kwa kutaka kuwania kiti cha ubunge ambacho kingemngo'a mamlakani mbunge huyo (*UNN* uk185-193). Labda juhudi zao raia za kuwaondoa viongozi dhalimu hukwamishwa na ufisadi uliokithiri katika mataifa ya Afrika, ambao huwezesha viongozi kuiba kura na kubaki mamlakani ili waendelee kujitajirisha. Huenda viongozi wanatumia hadhi, nguvu na utajiri kukataa kuondoka mamlakani. Ubinafsi na hali ya kutojali miongoni mwa viongozi unaonyesha namna uhuru haujaweza kuleta haki na usawa kwa sababu

walio mamlakani huwa na nguvu zaidi kuliko raia wa kawaida na wao ndio huamua namna mambo yatakavyokuwa.

Raia pia wamechangia katika kudidimiza haki na usawa katika jamii kwa kukubali kutumiwa na viongozi kuendeleza ukatili wa kila nui. Kwa mfano, tumeelezwa kuwa "wale wasio nguvu ndio wanaosaidia kudanganywa, kupigwa, kichinjwa, kunyang'anywa, kuuliwa (*UNN* uk 9)". Hii ni dhihirisho la hali halisi ya ubaadausasa ambapo mataifa ya Afrika yanajiangamiza yenyewe. Viongozi hawafanyi lolote kuimarisha hali ya raia wake, nao raia wanaungana na viongozi kuangamizana. Uozo wa kila aina umesababisha kutokuwepo na mshikamano na badala yake kumejaa fujo na ghasia katika mataifa haya.

### 3.2.2 Ukosefu wa Maendeleo

Ukosefu wa mshikamano unachangia kudidimiza maendeleo ya nchi na taifa linaanza kurudi nyuma badala ya kwenda mbele. Haya yanadhihirika katika riwaya ya *DY*, Ndi-anapolalamika kwa sababu ya ukosefu wa maendeleo baada ya miaka arubaini na mbili ya uhuru:

> Umebaki utupu wa mambo… Hii ndio hatima ya uhuru wetu wa miaka arubaini na mbili. Sote tumekumbwa na ugonjwa wa ajabu unaotuangusha kwenye maweko ya chini kabisa mwanadamu awezako kuanguka. Ajabu! Sisi ni watu tuliokuwa imara, watundu, wadadisi, watetezi wa nafsi zetu, wapigania heshima ya nchi yetu, watu tuliosimama kidete kwa miguu yetu isiyochoka – kwa fahari na kujisifu! U wapi wakati ule katika dunia yao?... Baada ya miaka **42** ya udhia hakuna kinachoaminika tena. Nilibanduka hapo… Nilikuwa kama kitoto kichanga kinachoanza kwenda tata – kitoto cha miaka **42**. Niliongozwa na mazoea ya miaka 42 ya kwenda gizani kuliko kweupe (*DY* uk 2, 5).

Mataifa ya Afrika hayana chochote cha kuonyesha baada ya uhuru. Kwa mfano, katika dondoo, Ndi- analalamika kuwa katika miaka arubaini na miwili ya uhuru taifa linakwenda 'gizani kuliko kweupe'. Kauli hii inaashiria kuwa taifa halijapata maendeleo yoyote baada ya uhuru na badala yake linarudi nyuma. Hali hii ndiyo

inasababisha ‘utupu wa mambo’, kwa kuwa uhuru haujaweza kutimiza matarajio ya wananchi. Badala yake kumekuwa na udhia, yaani hali ya usumbufu, kero na hofu, mambo ambayo hayangetaraijiwa kuwepo baada ya uhuru. Hii ndiyo sababu Ndi-anatumia neno mageuzi badala ya neno uhuru kuashiria ukosefu wa maendeleo ambayo yalitarajiwa kuambatana na uhuru (*DY* uk 16). Hali sawia na hii pia inajitokeza katika riwaya ya *NZM* ambapo Faisal analalamikia kuzoroteka kwa maisha nchini Tanzania baada ya miaka 37 tangu atoke huku na kwenda Arabuni:

> Njiani Faisal alipeleleza kila kitu kimyakimya… Si kama anajiambia kuwa zamani ilikuwa na raha kwa kila mtu, hapana. Tatizo lake Faisal ni kwamba alihisi sasa imeahidi nafuu ambayo ingeondosha shida. Huu ndio ubaya wa mambo. Faisal alitarajia nafuu sasa, lakini nafuu haipo. Haioni nafuu kamwe… Sasa ndio karudi tena baada ya miaka yote hiyo. Anapita akiutazama mji kwa hofu na huzuni. Una kila alama ya huzuni mji wenyewe. Mengi angesimulia kama angekuwa na kituo, anaweza kujumlisha tu uchapwa wake, uchafu wake, hatari zake, na zaidi, fujo na ukatili wake. Umepoteza utulivu na amani mji. Unavukuta pumzi na harufu mbaya kama kidonda chenye harufu inayokata mianzi ya pua. (*NZM* uk 8, 12).

Inavyobainika kutoka kwenye dondoo ni kuwa hali ya sasa ya mataifa mengi ya Afrika ni mbaya kuliko yalivyokuwa miaka ya mwanzo mwanzo ya uhuru. Kwa mfano, Faisal alitarajia kuwa baada ya miaka thelathini na saba tangu kuihama nchi yake, kungekuwa na ‘nafuu ambayo ingeondosha shida’. Anachomaanisha Faisal ni kwamba alitarajia kuwa hali ya nchi yake na wananchi kwa jumla ingekuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa miaka 37 iliyokuwa imepita. Hata hivyo nafuu yenyewe haipo, na badala yake kuna ‘uchapwa, uchafu, hatari, fujo na ukatili’. Hali hii ya kuzoroteka kwa mambo ndiyo inasababisha huzuni na hofu kwa Faisal anapoutazama mji wenyewe. Baada ya kuangalia kwa jumla hali duni ya mwafrika baada ya uhuru, sehemu inayofuata inaangazia kwa kina masuala mahususi yanayodhihirisha ukosefu wa maendeleo katika mataifa ya Afrika kama yanavyojitokeza katika riwaya za utafiti huu. Masuala hayo ni

pamoja na ukosefu wa usalama, uchafuzi wa mazingira na ukosefu wa kazi na hatimaye miundo misingi duni na umaskini uliokithiri.

#### 3.2.2.1 Ukosefu wa Usalama

Ukosefu wa maendeleo katika mataifa ya Afrika aghalabu hudhihirika katika kila sekta, iwe ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mojawapo ya sekta ya kijamii inayoathirika ni ile ya usalama. Akieleza kuhusu mojawapo ya miji aliyoizuru nchini Tanzania Faisal anasema kuwa mji wenyewe 'umepoteza utulivu na amani' na badala yake umejaa 'hatari, fujo na ukatili' (*NZM* uk 8).Mji uliojaa ukatili na hatari bila shaka hauna utulivu na amani na ni ishara ya ukosefu wa usalama. Vilevile tunaelezwa kuwa mwendo wa dunia ya siku hizi ni 'danganya, piga, chinja, nyang'anya, ua, fisidi, aibisha, dhalilisha…chukua vya watu…' (*NZM* uk 9). Vitendo hivi vyote vya kupiga, kunyang'anya kuua na kadhalika vinaashiria ukosefu wa usalama katika dunia ya sasa, dunia ya ubaadausasa ambayo haina mshikamano wa kijamii.

Ukosefu wa usalama unadhihirika kupitia njia nyingi kama vile wizi wa mabavu. Kwa mfano katika *DY*, tunaelezwa kuwa vijana wanaivamia nyumba ya Sadiki Tumbo na kuiba pesa na vitu vingine vya dhamana:

> Kitambo fulani mbele, nilipofika Mkamasini, jizi lilikuwa limeshawachenga watu waliokuwa wakilifukuza na sasa… wanasimuliana kadhia na kulaani.
>
> "Kaingia ndani kwa Sadiki Tumbo na kumkamatia bastolabandia atoe pesa na vyombo vya dhahabu"
>
> "Naye katoa?"
>
> "Angefanyaje na ile bastolabandia alidhani ya kweli?"
>
> "Eeee, wanatafuta pesa za unga"
>
> "Lo!...Hawaogopi kamwe… mchana wote huu; kweupeeee!"
>
> "Salama yake hatukumpata mwanaharamu yule tungemfirigisafirigisa hapahapa bila kumfikisha polisi wanakoachiliwa…" (*DY* uk 32).

Kichocheo mojawapo cha ukosefu wa usalama ni matumizi ya dawa za kulevya ama 'unga' kama unavyorejelewa kwenye dondoo. Tumeelezwa kuwa vijana wanatumia bastola ambayo ni bandia kuwatishia raia ili waweze kuwaibia. Lengo lao ni kupata pesa za kununua dawa za kulevya labda kutokana na hali ya utamaushi katika mataifa ya Afrika.

Utepetevu katika asasi za kiusalama kama vile polisi ni kichocheo kingine katika kuenea kwa visa vya uhalifu katika jamii. Kwa mfano, katika *DY* raia wanataka kuchukua sheria mikononi mwao ili kupambana na wahalifu kwa kuwa polisi wanawaachilia wahalifu (uk 32). Kwa kawaida, polisi wanastahili kuhakikisha kuwa wahalifu wanafikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka. Kuwaachilia wahalifu bila kuwafikisha mahakamani basi ni ukosefu wa haki hasa kwa raia wanaosumbuliwa na wahalifu hao. Katika muktadha wa ubaadausasa, mwandishi wa riwaya ya *DY* anahakiki simulizi kuu ya asasi inayohusika na masuala ya usalama kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake. Hivyo basi, wanaibuka na simulizi ndogo ndogo au njia mbadala za kukabiliana na shida zilizowakumba kwa sheria mikononi ili kumfunza mhalifu adabu. Ukosefu wa haki bila shaka umezidisha visa vya ukosefu wa usalama ambao hudidimiza maendeleo ya mataifa haya ya Afrika.

### 3.2.2.2 Uchafuzi wa Mazingira na Ukosefu wa Ajira

Uchafuzi wa mazingira ni jambo lingine linalodhihirisha ukosefu wa maendeleo katika mataifa ya Afrika kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Vitalu ambavyo leo havina miti wala maua, lakini zamani vilijaa miti iliyofunua urembo wa maua juu ya vigoo… Hapa na pale, huku na kule, kushoto na kulia, makaro yanabwabwaja maji machafu…mitaro inayochimbwa pasi na kufukiwa…na majaa yaliyofumka ovyo bila ya watu kujua. Mifuko ya plasitiki inayokokotwa na upepo na kurushwa huku na kule…rundo za taka vichochoroni zisizokuwa na matopasi wa kuzichukua (*NZM* uk 8, 12, 13).

Kutokana na uchafuzi wa mazingira tunaelezwa namna miti na maua yaliyovutia hapo awali yalivyoharibiwa. Badala yake kumejaa mifuko ya plastiki iliyotapakaa kila mahali pamoja na uchafu unatokana na makaro ya maji machafu na rundo za taka vichochoroni zisizokuwa na matopasi wa kuzichukua. Hali ni hii hii katika *DY* kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Tangu kuzaliwa kwangu sijapata kuona pahala pachafu na dhaifu kama hapa… Vinyesi vya watu na wanyama vinachekelea… Njia…imepambwa takataka zilizotupwa ovyo. Mifuko ya plastiki ya kila aina iliyotandazika kila pahala; watu waliita 'maua lafi' (*DY* uk 31,32, 35).

Kinachojitokeza kwenye dondoo ni kuwa uchafuzi wa mazingira unatokana na kutowajibika na hali ya kutojali, sio tu kwa viongozi bali pia raia. Kwa upande mmoja, viongozi wameshindwa kutoa nafasi za kazi licha ya kuwa kuna vijana wengi ambao hawana kazi. Kwa mfano katika *NZM* tunaelezwa kuhusu 'vijana wa jobless' ambao wamevifanya 'vipenu vya majumba kuwa maskani yao' (uk 5). Yaani, vijana wasio na kazi na ambao hushinda upenuni mwa majumba pasi na kufanya lolote. Vijana kama hawa wangeajiriwa kama matopasi ambao ambao wangesaidia kuzoa taka na kuchimba mitaro ya maji-taka. Kwa upande mwingine, raia wenyewe hawajawajibika kwa lolote katika kuyaboresha mazingira yao. Kwa mfano, wangeungana pamoja na kutumia nguvu zao kuzoa au kuchoma taka na hata kuchimba mitaro ya maji taka kama njia za kuyanadhifisha mazingira yao. Hii inadhihirisha kuwa uhuru katika mataifa ya Afrika haujaweza kutimiza malengo yake ya 'uhuru na kazi' kwa raia wake kama ulivyoahidi. Katika misingi ya ubaadausasa, riwaya zilizotafitiwa basi zinasaili maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika kwa kushindwa kutimiza malengo yake kwa raia.

Nafasi chache za kazi zinazopatikana zinatolewa kwa mapendeleo kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Baada ya mageuzi (*sipendi kuuita uhuru*)… kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara. Muhimu zaidi wewe ulikuwa nani, mtoto au mjukuu wa bwana gani na kama unaitikia ‘ndiyo’ kila wakati (*DY* uk 16).

Ingawa katika dondoo kazi zinazorejelewa ni zile za ngazi ya juu, vigezo vya kupima ufaafu wa mtu katika kuipata kazi havitegemei elimu, akili au busara aliyo nayo mtu. Badala yake vinategemea unayemjua au anayekujua na aghalabu nafasi hizi hutwaliwa na watu wa tabaka la juu au wastahiki kama wanavyorejelewa katika dondoo. Aidha, tunaelezwa kuwa waliopewa kazi walipaswa kuwa watu ambao “wanaoitika ‘ndiyo’ kila wakati” (*DY* uk 16). Hawa ni watu ambao hawawezi kupinga maamuzi au matendo yoyote hata yakiwa maovu, kwa sababu hata uamuzi wenyewe wa kuwateua haukuwa wa haki. Wanaojaribu kupinga maovu yanayotendeka wanatimuliwa. Mfano mzuri ni ule wa Ndi- katika *DY* ambaye anafutwa kazi kwa kupinga ubadhirifu unaoendelezwa ofisini mwao (*DY* uk 17, 81,188). Iwapo basi wenye vyeo vya juu hawana ujuzi wowote wa kazi wanazozifanya na hawawezi kuyapinga maovu yanayoendelea, bila shaka nchi haiwezi kusonga mbele, na kama anavyosema Ndi- (*DY* uk 5) mataifa ya Afrika yanaendelea kurudi nyuma na kudidimia gizani kuliko yalivyokuwa punde tu baada ya kupata uhuru.

#### 3.2.2.3 Miundo Misingi Duni na Umaskini Uliokithiri

Mbali na mazingira machafu na ukosefu wa nafasi za kazi, kuna miundo misingi duni na umaskini uliokithiri katika mengi ya mataifa ya Afrika. Katika dondoo linalofuata tumeelezwa kuhusu hali mbovu ya miundo misingi katika maeneo tofauti ya mataifa haya:

> Barabara zilizofukukafukuka na vichochoro vilivyobadilika sura, vinanuka badala ya kunukia. Rundo la vifusi vya mawe na dongo jekundu kutokana na majumba yaliyoporomoka na kukosa kutunzwa…vichochoro vyenye wembamba uleule tokea mji huo ulipojengwa… ghorofa zimekwenda tenge, kuta zimegunyukagunyuka, virukia vimeshamiri kwenye mitwiko mibovu

> na mule mwenye nyufa. Madirisha yaliyopoteza rangi na sura, yalikuwa yakiporomosha mbao… (*NZM* uk 12 - 14).

Miundo misingi iliyotajwa kwenye dondoo kama vile barabara na majengo yapo katika hali mbaya inayoashiria ukosefu wa maendeleo katika mataifa mengi ya Afrika. Kwa mfano, tunaelezwa kuhusu 'vichochoro vyenye wembamba uleule tokeo mji huo ulipojengwa' kumaanisha kuwa barabara hazijapanuliwa na hali imebabaki jinsi ilivyokuwa miaka mingi iliyopita. Aidha, hali ya majengo imekuwa mbovu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali kwani yameanza kuporomoka huku mengine yakijaa nyufa. Vilevile majengo hayo hayajapakwa rangi upya na ndio maana tunaelezwa kuhusu 'madirisha yaliyopoteza rangi na sura' kwa sababu hayajatunzwa kwa njia yoyote kwa miongo kadhaa tangu yajengwe. Hali sawia na hii inadhihirika pia katika riwaya ya *DY*:

> Njia ilikuwa mashimo matupu… Njia hizi za mchanga na vumbi ndizo zilizokuwa kanyaga zangu za maisha nilipokwenda miguu chini chuoni, skuli, michezoni, matembezini au nilipotumwa dukani… Katika mkabala huu wa karibu, sasa nilivitazama vijumba na vibanda hivi kwa namna ya ajabu. Jinsi vilivyoshikamana na dhiki na ukubuhu, jinsi vilivyokuwa vikisakarika na maradhi ya kuvumilia, jinsi vilivyoweza kubeba uzito wa miaka mingi namna ile! Mapaa ya makuti mvi tupu. Ya mabati na madebe, ukoko mkongwe wa behedani. Vingine vi hoi nje na ndani ya kuta, fito na nguzo zimeshamung'unyuliwa na wadudu na kung'ong'onwa na wakati. Kuta zenyewe sasa zinalia yombo bila ya kuanguka kwa ujudi wa Mungu tu, huku zikiwanya wapiti njia wasalie mtume na kuchapuka zaidi kuhofu ile hatari ya dhahiri ya kuangukiwa. Ndani lakini, watu wamo wanaishi huku mara wanakumbuka na mara wanasahau hatari inayowakabili. Vingi vya vijumba hivi vinavuja, na michirizi ya mvua na rishai zake za udongo zimefanya ramani zinazozidi kuchafua weupe wa chokaa uliokwisha chafuka. Miaka hamsini au zaidi tokea zipakwe chokaa haujapitia mkono wa pili. Tena pasu na matomo yaliyozibwa kwa matambara, magamba na karatasi. Fito kama mbavu za mbwa mkondefu zinaning'inia nje ya udongo mle mlimobandukabanduka (*DY* uk 35-36).

Ingawa dondoo hili ni refu, linatupatia taswira kamili ya jinsi hali ilivyo. Kwa mfano, barabara nyingi bado ni za mchanga na vumbi na zimejaa mashimo. Hii ina maana kuwa barabara hazikuwa zimetiwa lami, na hata hizo za mchanga hazikuwa zinalimwa

upya ili kuziba mashimo. Makazi nayo si ya maana kwa kuwa mengi ni vijumba na vibanda hoi vinavyokaribia kuanguka. Vibanda hivi vimejengwa kwa malighafi duni kama udongo kwa kuta zake na paa zake ni madebe. Tunaelezwa kuwa chokaa iliyopakwa kwenye kuta hizi zaidi ya miaka hamsini iliyopita 'haujapitiwa mkono wa pili', kumaanisha kuwa kuta hizi hazijapakwa chokaa nyingine tangu zilipojengwa, labda kutokana na umaskini miongoni wa raia wanaoishi maeneo haya. Miundo misingi hii duni ni ishara ya ukosefu wa maendeleo katika mataifa mengi ya Afrika. Huenda ikawa viongozi wanaojilimbikiza mali kama tulivyokuwa tumejadili hapo awali, hawajafanya juhudi zozote kuboresha maisha ya raia wake ili kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Majengo ya hivi karibuni yanayoendelea kuchipuka katika mitaa mbalimbali hayana tofauti kubwa na yale yaliyojengwa takriban miaka hamsini iliyopita. Pia yanadhihirisha umaskini uliokithiri miongoni mwa raia:

> Mbele ya safari yangu nikapita mtaa uliozuka ghafla katika shaghalabaghala mpya… Vibanda vimechipuka ovyo. Labda vibanda si neno zuri, kwani huku kwetu, kibanda kilikuwa na sura na heshima ya aina yke. Hivi ni vichukizi vilivyosimamishwa na shaghalabaghala mpya. Vilivyojengwa kwa kitu chochote. Chochote kisichofaa-kinachofaa: magongo, fito, papi, matambara, mabicha, majamvi mabovu, maboksi, mapande ya mabati yenye kutu, masalia ya madebe yaliyochoka, mbao zilizokwisha mung'unyuliwa na mchwa, majani ya miti… Vyote vichafukizi vimesimama katikati ya tonge la taharuki za kila aina: mpachano, mkurubiano, msuguano, mkimbiano, mfukuzano, mdidimizano, mkengeuko, mtitimo (*DY* uk 31-32).

Miundo misingi duni pia yanadhihirisha umaskini uliokithiri miongoni mwa raia. Kwa mfano, tumeelezwa kuwa majengo yaliyojengwa hivi karibuni si ya kutamanika; ni vibanda vilivyojengwa kwa majamvi mabovu, masalia ya madebe yaliyochoka na mbao zilizomung'unyuliwa na mchwa miongoni mwa vifaa vingine duni. Hii inadhihirisha kuwa raia bado wanaishi maisha duni na uhuru haujafaulu kuwaletea maendeleo

yaliyoahidiwa. Hata hivyo wenye vyeo mbalimbali wanaendelea kutajirika huku maskini wakiendelea kufukarika:

> "…Watu wengi waliimbiwa nyimbo za usawa na wakuu, lakini kumbe katika dhahiri ya mambo wakuu walikuwa wakiimba nyimbo zao wenyewe kujikusanyia mtaji ili kuzijenga nafsi zao. Tazame kuleee!" alinionyesha kwenye ukanda wa mwambao wenye fukwe njema za mchanga mweupe unaomeremeta. "Unaona kule jinsi *vi-Villa* vyema vinavyochipua? Kama uyoga! Vinasimama kwa fahari ya utamaduni mpya. *Its beautiful…fantastic!* Ipeleleze mishahara yao. Utaikuta vibutu kama mikia ya mbuzi… Na kisha geuka huku. Karibu mno… Unaona wingi wa vibanda vya ukorofi vile vilivyojiinamia kwa fedheha (*DY* uk 65).

Taswira inayojitokeza katika dondoo inaonyesha ukosefu wa usawa na mipaka kati ya matajiri na maskini inaendelea kupanuka. Matajiri wenye vyeo wanaishi kwa mitaa mizuri yenye majumba ya kupendeza yanayojulikana kama *Villa*, huku maskini wakiishi katika vibanda.

Mbali na kuwa na majengo duni, vituo vya afya pia ni duni na havitoi huduma bora kwa raia wake. Kwa mfano, katika *DY* tunaelezwa kuwa hospitali ni kama mabanda na hazina dawa, nao madaktari ni wachache (uk 41-42). Katika hospitali zilizo na dawa, dawa zenyewe ni zile za kimsingi kabisa, labda za kutoa huduma ya kwanza kwa raia:

> Zahanati ya pale karibu na kwao, iliyojengwa miaka michache baada ya uhuru, wakati watu walikuwa na msukumo wa kuibadilisha jamii… Siku hizi hakuna dawa zilizopatikana pale isipokuwa aspirini na jivii ya kupaka vidonda… (*UNN* uk 178).

Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, watu walikuwa na 'msukumo wa kuibadilisha jamii' punde tu baada ya uhuru ndiposa wakajenga hospitali na zahanati ili kushughulikia maslahi ya kiafya ya jamii zao. Mabadiliko hayo bila shaka yalikuwa sehemu ya maendeleo ya taifa ili kuwafaidi raia. Lakini malengo hayo yamebadilika na hakuna maendeleo yoyote ya kutamanika. Dawa zilizotajwa hapo juu kama aspirini na jivii ni za kimsingi sana. Kwa mfano, aspirini hutumika kumaliza tu uchungu ambao aghalabu huwa dalili ya ugonjwa wala sio ugonjwa wenyewe. Jivii nayo husaidia

kukausha kidonda haraka lakini haiwezi kuua viini kwenye kidonda. Dawa hizi ni za kale mno na matumizi yake yanaashiria namna nchi huru za Kiafrika zilivyokwama kimawazo na kimaendeleo kama inavyodhihirika kupitia miundo misingi hii duni.

Kando na hayo, shule hazina vifaa muhimu za kuendeleza masomo na kufanikisha elimu. Kwa mfano, katika *DY* tunaelezwa kuhusu shule ambazo 'hazina vikalio wala vifaa na walimu wake wamepungukiwa maarifa' (*DY* uk 42). Iwapo walimu hawana maarifa basi hawatakuwa na uwezo wa kuweka msingi bora wa maendeleo kwa wanafunzi wao. Aidha, shule ambayo haina viti wala vifaa muhimu kama vitabu, chaki na vifaa vingine muhimu haiwezi kuwasaidia wanafunzi kufikia kilele cha ujuzi utakaosaidia kuleta maendeleo. Wanaobahatika kupata elimu ya viwango vya chini wanapata changamoto ya kuingia katika vyuo mbalimbali kutokana na ufisadi na mapendeleo. Kwa mfano, katika *UNN* tunaelezwa simulizi ya Lulu aliyejaribu mara kadha kujiunga na chuo cha walimu lakini hakufaulu kwa sababu 'alishindwa kumpata mtu mwenye nasaba bora wa kumsaidia' (*UNN* uk 197). Simulizi hii inaonyesha kuwa nafasi za kujiunga na vyuo hazikutolewa kwa misingi ya haki na usawa. Walio na hadhi, au nasaba bora ndio wanaotengewa nafasi nyingi katika vyuo huku wale wa maskini wakiendelea kuteseka, hadi watakapopata mtu wa kuwasaidia. Elimu iliyotarajiwa kuwa msingi wa maendeleo baada ya uhuru basi haijatiliwa maanani hivyo kusababisha raia wengi kuzama zaidi katika umaskini.

Ukosefu wa maendeleo unaodhihirika kupitia ukosefu wa usalama, uchafuzi wa mazingira, umaskini uliokithiri, ukosefu wa kazi na kuwepo kwa miundo misingi duni kumeyafanya mataifa mengi ya Afrika kuwa hatua nyingi nyuma kuliko yalivyokuwa wakati yalipata uhuru. Ukweli huu unadhihirika zaidi katika riwaya ya *DY* kupitia mhusika Ndi- anayesema kuwa 'zamani ulimwengu huu ulikuwa jipu na sasa jipu limeshapasuka limekuwa kidondandugu kisichopona – kidonda kinachonuka vibaya

(uk 36-37). Kauli hii ya Ndi- inaashiria kuwa ingawa hali ya Mwafrika kabla ya uhuru haikuwa nzuri, kwa sasa mambo yamekuwa mabaya hata zaidi kiasi kwamba hata matumaini ya kuyabadilisha yanakuwa ndoto tu.

### 3.3 Ajenda za Mataifa ya Ulaya na Mashirika yasiyo ya Kiserikali Barani Afrika

Mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu, hususan mataifa ya Afrika, yako nyuma kimaendeleo yakilinganishwa na yale ya mataifa ya Magharibi. Kwa mtazamo wa nje, mataifa ya Ulaya pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali huonekana kuyajali mataifa ya Afrika na aghalabu hutoa misaada ili "kuyainua" na "kuyaondoa" katika lindi la umaskini. Hata hivyo, uchunguzi wa kina katika riwaya zilizotafitiwa unadhihirisha kuwa hali ni tofauti kwani mataifa ya Ulaya hulenga kuendeleza ajenda zao lakini kwa njia iliyofichika wala sio kuendeleza ajenda za mataifa ya Afrika. Kama anavyosema Sim (2013), wanaubaadausasa hulenga kufichua itikadi potovu zilizofichika katika mifumo mbalimbali, iwe ya kijamii, kiuchumi au kidini. Ili kuweza kubainisha ajenda zilizofichika ndani ya mifumo mbalimbali sehemu hii imejikita katika simulizi zinazobainisha mbinu na mikakati ambayo mataifa ya Ulaya na mashirika yasiyo ya kiserikali hutumia ili kutimiza ajenda hizo. Simulizi zenyewe zimegawanywa katika mada tofauti kama vile uenezaji wa kasumba potovu dhidi ya mataifa ya Afrika, utoaji wa misaada kwa mataifa ya Afrika, uwekezaji katika mataifa ya Afrika na utoaji wa sheria kandamizi dhidi ya mataifa ya Afrika. Vilevile tumejadili simulizi inayoonyesha mchango wa Waafrika katika maendeleo ya nchi zao.

#### 3.3.1 Uenezaji wa Kasumba Potovu Dhidi ya Mataifa ya Afrika

Kama tunavyofahamu, mataifa ya Ulaya kama vile Marekani na Uingereza yamepiga hatua nyingi za kimaendeleo na kiteknolojia yakilinganishwa na yale ya Afrika. Giddens (2002) kwa mfano ametaja Marekani kama nchi iliyo na nguvu zaidi za kiutawala ulimwenguni kote katika vifaa vya kijeshi pamoja na masuala ya kiuchumi

na kitamaduni. Bara la Afrika nalo limetajwa kama mojawapo ya bara lililo na mataifa mengi yaliyo maskini ulimwenguni. Kutokana na tofauti hii kati ya mataifa ya Ulaya na yale ya Afrika, dunia imegawanyika katika makundi mawili makuu; kundi la walionavyo na wasiokuwa navyo kama inavyofafanuliwa na mhusika Ndi- wa *DY* pale anaporejelea mawazo ya Fowles:

> Dunia kweli imegawika mapande mawili. Kwa upande mmoja, wachache wenye nasaba na nguvu. Nguvu za kutawala, nguvu za utajiri na uwezo wa kufikiri, nguvu za kiungu za kuweko mwahala mote kila wakati wote; kuweko na kuamua na kuathiri kila kitu. Kuharibu kila kitu. Na kwa upande mwingine kuna wengi: mahambe, dhaifu, wasio na nasaba wala uzito wa hali wa fikra! Wafuata shangwe! (*DY* uk 44, 172).

Ingawa mgawanyiko kati ya walionavyo na wasiokuwa navyo unaweza kutokea katika kiwango cha watu binafsi, mgawanyiko unaorejelewa katika dondoo umejikita katika kiwango cha mataifa. Hii ina maana kuwa baadhi ya mataifa yana watu 'wenye hadhi' huku mengine yakiwa na watu 'wasio na hadhi' yaani kuna mataifa ya hadhi ya juu na mengine ya watu wa hadhi ya chini. Aidha, mataifa yenye hadhi yana 'nguvu za kiutawala, utajiri na uwezo wa kufikiri'. Hii inaonyesha kuwa mataifa yasiyo na hadhi yanafaa kutawaliwa, kusaidiwa kwa kuwa ni dhaifu na yasiyo na uwezo wa kufikiri. Mataifa haya basi yanahitaji kufikiriwa na kutendewa mambo kwa niaba yao. Ingawa hatujatajiwa ni yapi mataifa ya hadhi ya juu na ya chini, dondoo linalofuata linadhihirisha kuwa mataifa yanayorejelewa ni yale ya Ulaya na Afrika mtawalia:

> "Sisi ndio tuliopewa haki ya kuudhibiti ulimwengu." Nikawahi kumsikia Mzungu mmoja aliyekuwa akibwabwaja kwa jeuri alipokwishaikata chupa ya Gorbachev. "Tulipoona haitoshi Ulaya na mabara ya Mungu matupu duniani na watu wasiofahamu faida ya ardhi kama nyinyi mmeikalia kivivu, tulikuja kuing'wapura!" Waswahili wote walicheka na kupandisha gilasi zao za Gorbachev. "Ndiyo… Ndiyo…aliendelea yule mzungu. "Akili zetu ndizo zilizotupa haki tutawale. Nguvu na ubora wetu wa kimaumbile ndio uliotuwezesha kujitawala. Inafaa mshukuru kukufanyieni mengi katika kujifanyia sisi wenyewe. Sasa mwangaza umezagaa Afrika." Waliokuwepo wote walicheka kwa mzaha huo. Wageni kwa wenyeji (*DY* uk 126).

Anapotumia neno ‘sisi’, Mzungu katika dondoo anarejelea mataifa ya Ulaya yaliyokuja kuitawala Afrika na kuifanya sehemu ya koloni zao wakati wa ukoloni mkongwe. Hapa tunaona namna wazungu wanavyohalalisha ukoloni mkongwe kwa kueneza kasumba potovu kuwa Waafrika ni watu duni na wasiojielewa. Kwa mfano, anasema kuwa sababu yao ya kuja Afrika ni kuweza kuitumia ardhi vizuri kwani wenyeji ni ‘watu wasiofahamu umuhimu wa ardhi’. Hii ni kauli ya kuwadhalilisha Waafrika na kuwafanya wajihisi kuwa duni. Aidha, tunaona kasumba ya kuwatukuza Wazungu kwa kujitambulisha kama watu wenye akili iliyopevuka kuliko ya Waafrika. Kwa mfano Mzungu kwenye dondoo anasema kuwa wazungu waliopewa haki ya kuudhibiti ulimwengu kutokana na akili zao na ubora wao wa kimaumbile. Kwa kiasi fulani, mzungu ameweza kuieneza hii kasumba na kuwafanya Waafrika wajione duni huku wakimtukuza. Tunaona Waafrika wakicheka tu na kufurahia wanapotukanwa na kuonyeshwa kuwa wao ni wajinga tunapoelezwa kwenye dondoo kuwa ‘Waswahili wote walicheka na kupandisha gilasi zao za Gorbachev’. Riwaya ya *DY* inaonekana kukashifu kasumba hii potovu na kujaribu kuwazindua Waafrika kuwa binadamu wote ni sawa ila mazingira ambamo kila mmoja amezaliwa huweza kuathiri namna anavyofikiri na kutenda:

> Kuna mantiki kwa kiasi fulani katika mgao wa watu wa Fowles. Nimeishi kuona umati wa watu ukicheka ovyo huku maafa ya maumivu yakiwakeketakeketa…hata walipoitwa wajinga, walicheka! Walicheka na kufuata kila waliloambiwa. Lakini ninayokataa mimi ni ile rai kwamba uzuri na ubaya unakuja kutokana na urithi tuliokuja nao duniani. Kwamba umma mkubwa zaidi umejikuta tu ndani ya tanuri la mateso na wachache ndani ya kasri za tafrija. La, Fowles; kuna nje inayotungoja tukifika tu duniani. Na nje inaambatana na udhaifu wa kutopata fursa ya kutumia macho yetu kuona ingawa tunatazama. Tena kuona kwenye giza… Watu hukoseshwa mwangaza wa kuhakikisha badala ya kudhani…hakuna binadamu mjinga…hakuna ukweli katika dhana ya Fowles juu ya wengi walioumbiwa uduni na wachache ushupavu na ukwasi… Hakuna kitu safi kabisakabisa, kitu kama nasaba au nguvu au utajiri au awezo wa kufikiri ulioshindikwa na kuchipua ndani za tete za uzazi za mwanadamu yeyote. Hakuna hata kimoja ya vitu hivi kinachotokana

> na urithi wa silka na asili ya mtu tu…Hakuna anayeweza kuthibitisha kwa asahi kwamba akili, kwa sehemu kubwa, ni urithi wa ndani. Hakuna asiyejua kwamba mazingira hupevua akili (*DY* uk 45,47, 172-173).

Ingawa ni kweli kuwa kuna mgao wa mataifa; yale yaliyoendelea na yale yanayoendelea, kinachobainika katika dondoo hapo juu ni kuwa mgao huu haujatokana na urithi. Kwa mfano tunaelezwa kuwa 'hakuna kitu kama nasaba au nguvu au utajiri au awezo wa kufikiri ulioshindikwa na kuchipua ndani za tete za uzazi wa mwanadamu yeyote' (*DY* uk 172). Kauli hii inathibitisha kuwa kasumba ya Wazungu kuwa wao ni watu wa nasaba bora na Waafrika ni wajinga si ya kweli. Hata hivyo tumeonyeshwa kuwa mazingira walimokulia yamewapevua Wazungu akili, tofauti na mazingira wanayojipata Waafrika ambayo yanaambatana na 'udhaifu wa kutopata fursa ya kutumia macho'. Hii ina maana kuwa Waafrika wanaokulia katika mazingira bora huweza kupevuka kiakili sawasawa na anavyofanya Mzungu. Kasumba ya Wazungu ya kujiona bora na kuwaona Waafrika kuwa duni hivyo huwa ya kimaksudi ili kuhalalisha ukoloni mkongwe na daima waweze kuwatawala Waafrika. Aidha, huenda kasumba hii ya kudunisha watu weusi hulenga kueneza na kuhalalisha ubaguzi wa rangi. Kufaulu kwa kasumba hii kutayadhibiti mawazo ya watu wa Mataifa ya Afrika na hawataweza kujisanua. Riwaya zilizotafitiwa basi zinaihakiki Kasumba hii potovu ili kubainisha ajenda za mataifa ya Ulaya zilizofichika ndani yake.

Mbali na kuwadunisha Waafrika, kasumba potovu kutoka mataifa ya Ulaya pia hutumiwa kudunisha vitu na bidhaa zote zinazotoka katika mataifa ya Afrika huku ikipendekeza na kupendelea bidhaa zinazotoka katika mataifa ya Ulaya:

> Kila mtu hapa hujazwa pumzi kutoka mbali huko nje. Pumzi za fitina hujaa vichwani mwa watu. Pendeni vitu msipende utu. Pendeni vitu vyetu msipende vyenu. Ndipo tena usikie miongoni mwetu: Kwa nini huyu kafanya hivi na mimi nisifanye?... kwa hivyo lazima nimwangamize, maana sina uwezo wa kumshinda. Ndani ya uovu wote huu mna tamani iliyosindikwa. Vya London. Vya New York. Vya Paris. Vya Berlin, vya Madrid… lakini si vya Dar-es-salam kama

> vipo. Tunaagiza kutoka nje kwa sababu vyao vyote ni vizuri na vinang'ara, ingawa ving'aravyo vyote si dhahabu. Ndiyo, sawa, hakuna ubaya, lakini vyetu je? Vyetu vyote ni vibaya? Mpaka lini tutanunua tu bila vyetu kununuliwa (*NZM* uk. 194).

Kama inavyobainika katika dondoo, kasumba kutoka mataifa ya nje inadhihirisha mapendeleo ya bidhaa za kutoka nje huku ikipuuza bidhaa za kienyeji. Kwa mfano, Waafrika wanahimizwa kupenda bidhaa za kigeni kutoka miji mikubwa mikubwa kama London, New York, Paris, Berlin na Madrid miongoni mwa miji mingine, kwa maana vitu kutoka huku 'ni vizuri na vinang'ara'. Hata hivyo, bidhaa zinazotoka miji tofauti ya mataifa ya Afrika kama vile Dar-es-salam, vinadharauliwa. Ingawa baadhi ya bidhaa kutoka mataifa ya Ulaya zinaweza kuwa za viwango vya juu zikilinganishwa na zile za kienyeji, hii sio kusema kuwa bidhaa zote za mataifa ya Afrika ni mbovu. Inadhihirika wazi kuwa mataifa ya nje yanatumia kasumba hii ili kupata soko la bidhaa zao katika mataifa ya Afrika. Hii ndio itikadi iliyofichika ndani ya kasumba hii potovu. Wakati kasumba hii inapokita mizizi na kuenea katika mataifa ya Afrika, milango ya kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zimewafikia wateja wake hufunguka.

Mojawapo ya mambo yanayochangia kuwepo kwa bidhaa za kigeni barani Afrika ni mfumo wa soko huria. Ingawa mfumo huu unaweza kuwafaidi Waafrika, Giddens (2002) anatoa tahadhari ya kuukubali bila kuwepo na mikakati inayofaa:

> Taifa lolote linaloukubali mfumo wa soko huria bila kuweka mikakati ifaayo ya kijamii na kiuchumi huenda ikaporomoka kiuchumi badala ya kuinuka. Ni lazima taifa liwe katika mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko katika asasi mbalimbali ili kuinua kiwango cha elimu na kumkomboa mwanamke, kuleta mabadiliko katika sekta ya benki na kuhakiksha kuwa kuna mazingira mazuri ya kuwekeza. Sio rahisi kwa mataifa yenye uchumi wa kiwango cha chini kutekeleza mambo haya. Yatahitaji msaada kutoka mataifa tajiri, sio tu wa kifedha bali pia wa kiteknolojia na ujuzi mwingine utakaoyawezesha kuleta mabadiliko hayo (Giddens 2002:xxxix) (TY).

Ni wazi kuwa mfumo wa soko huria aghalabu hauyasaidii sana mataifa ya Afrika kwani uchumi wao ni wa kiwango cha chini. Kiwango cha Waafrika cha elimu na ujuzi walio

nao huenda usiwawezeshe kuleta mabadiliko yanayokusudiwa ili kuinua uchumi wao katika mfumo wa soko huria. Aidha, mataifa haya bado hayajaweza kumkomboa mwanamke kikamilifu ili awe sehemu ya mabadiliko hayo na aweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa nchi yake. Kwa hivyo, uenezaji wa kasumba potovu unaorahisishwa na mfumo wa soko huria unayawezesha mataifa ya nje kupata soko la bidhaa zao kama tunavyoona katika dondoo linalofuata:

> Sasa [Wamae] akawa na uwezo wa kuipanua biashara yake. Akawa na uwezo wa kifedha wa kuikweza biashara yake kwenye ngazi nyingine… Wakati huu nao ikasadifu kuwa mfumo wa soko huria ulikuwa umeingia nchini. Vikwazo vilivyokuwako zamani vya kuzuia bidhaa kutoka nje vikawa vimeondolewa…. Akaanza kuagiza bidhaa kutoka Dubai, bidhaa za Uchina zilizopendwa na wengi kutokana na bei yake nafuu zikilinganishwa na za Marekani na Ulaya, nguo…kutoka Pakistan na India, vipodozi…kutoka Ufaransa, saa za Uswizi na mikufu ya Ujerumani, mifarishi ya Bahameli, mazulia ya Kiajemi na fulana za sufi zilizopendwa na masekretari kwenye ofisi za kifahari na wake wa matajiri (*UNN* uk 184).

Inavyobainika ni kuwa mfumo wa soko huria huondoa vikwazo vinavyowekwa na serikali vya kuzuia watu kuagiza bidhaa kutoka nje. Mfumo huu una manufaa yake kwa baadhi ya wafanyabiasha kama Wamae kwenye dondoo ambaye anaipanua biashara yake kwa kuweza 'kuagiza bidhaa kutoka nje'. Kwa mfano, anaagiza bidhaa kutoka Dubai, Uchina, Pakistan, India, Ufaransa, Ujerumani na kadhalika. Hata hivyo wanaonufaika kwa biashara kama hii huwa wachache sana, kama Wamae. Wanaoishia kunufaika zaidi ni wale kutoka mataifa ya nje kwani bidhaa zinatoka mataifa yao na kuja kuuzwa katika mataifa ya Afrika. Kama tunavyoelezwa kwenye dondoo hapo juu bidhaa hizi za kigeni zinapendwa na 'masekretari kwenye ofisi za kifahari na wake wa matajiri'. Hii inaonyesha kuwa bidhaa kutoka Ulaya hunasibishwa na watu wa tabaka la juu. Hali kama hii pia inajitokeza katika *UNN* tuponaelezwa kuhusu Mheshimiwa Kasina na mkewe wanaopenda bidhaa kutoka Ulaya – 'saa za Uswizi, Suti za Ujerumani, tai za Ufaransa na viatu vya Italiano, mazulia ya Uarabuni' (*UNN* uk 247).

Mbunge katika mataifa ya Afrika, kama alivyokuwa Mheshimiwa Kasina ni mtu tajiri na wa hadhi ya juu. Kwa kawaida, watu wa tabaka la juu huwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi. Hivyo basi, wanapokosa kununua bidha kutoka nchi zao wanachangia katika kudidimiza uchumi wa nchi yao huku wakisaidia kuinua uchumi wa nchi za kigeni. Hii inadhihirisha namna kufaulu kwa kasumba hii hukita mizizi na hatimaye kufanya mataifa ya Afrika kutawaliwa kiuchumi na kudidimizwa zaidi katika umaskini kwani bidhaa zinazotoka Afrika zinaonekana kuwa duni, na hivyo kukosa soko la kuziuza ndani na nje ya mataifa ya Afrika.

Utandawazi unachangia pakubwa katika kutafuta soko la bidhaa barani Afrika kwa kueneza kasumba potovu inayotukuza utamaduni wa Magharibu na kudhalilisha utamaduni wa Kiafrika. Haya yanadhihirika katika dondoo linalofuata hasa kuhusiana na suala nzima la urembo:

> Vijana wake waliozungusha vipodozi, marashi, kohli na nguo kwenye ofisi mjini na miji ya karibu…wakakamatwa kwa madai ya kuuza dawa za kulevya. Kassim akajitetea kuwa dawa za pekee alizouza ni kama *Xenical*, zilizotumiwa na wanawake kwa ajili ya kuupunguza uzito wao, badala ya kula chakula, ili waonekane wembamba kama wale modeli wa Ulaya na Marekani wanaosifiwa kwenye vyombo vya habari na kuweza kwenda kasi na ulimwengu wenyewe. Akaambiwa…hizo ndizo mbaya zaidi, zina madhara makubwa kuliko ukimwi. Hajawahi kusikia kitu kinachoitwa *anorexia?* ... Na hapo alipo…hajui kuwa wanawake wa Kiafrika wanapaswa kuwa wanene na wakubwa, waliojazana, wanaojua utamu wa chakula (‘wenye nyama za kushikika si magofu ya miili’)? Kwa nini yeye…achukue tezo ya dawa za ajabu ajabu – kwanza amezitoa wapi, labda Uchina bila hata kujua hao husambaza bidhaa duni? – na kuanza kuwapunguzia unene waliojaliwa na biolojia na utamaduni? (*UNN* uk 191).

Kama inavyojitokeza katika dondoo, jamii za Kiafrika huufasiri urembo kwa njia tofauti kabisa na watu wa mataifa ya ulaya. Kwa mfano, katika muktadha wa Kiafrika wanawake wanapaswa kuwa ‘wanene na wakubwa, waliojazana na wanaojua utamu wa chakula’ (*UNN* uk 191). Hii ni tofauti na mizani ya kupima urembo wa wanawake katika muktadha wa Kiulaya. Vyombo vya habari vinatumiwa kueneza kasumba ya

kimagharibi kuwa urembo unapaswa kuandamana na wembamba kwa kuwasifia modeli wa Ulaya na Marekani kwa sababu ya umbo lao. Kuenea kwa kasumba hii kunawafanya wanawake wa Kiafrika ambao kwa kawaida ni wanene, kutumia dawa kama 'Xenical' ili kupunguza uzito wao, licha ya kuwa baadhi ya dawa hizi huwa duni. Vilevile tunaelezwa kuwa dawa hizi za kupunguza uzito huwa na 'madhara makubwa kuliko ukimwi'. Mojawapo ya madhara ni kusababisha wanaozitumia kuwa na *anorexia*, yaani ugonjwa wa kukosa hamu ya chakula. Bila shaka mtu ambaye hali chakula ili aonekane anapendeza kiumbo hana budi kuandamwa na magonjwa mengine kwa kukosa kinga mwilini. Hatima yake ni maafa. Hata hivyo, watu wa mataifa ya nje hawaonekani kuwajali watu wa mataifa ya Afrika, hata kama dawa hizo zitasababisha maafa. Hivyo basi, tunaweza kuzua nadharia kuwa, watu wa mataifa ya kimagharibi hueneza kasumba ya kuupendekeza utamaduni wao kwa lengo la kutafuta soko la bidhaa zao, hata kama dawa hizo zitasababisha maradhi na vifo miongoni mwa watu katika mataifa ya Afrika. Kadri utamaduni wao unavyoendelea kuenea ndivyo soko la bidhaa zao linavyoendelea kupanuka huku idadi ya magonjwa na vifo miongoni mwa watu wa Afrika ikiendelea kuongezeka. Kwa hivyo, kando na kuuchujua utamaduni, kasumba kuhusu suala nzima la urembo husaidia kufanikisha ajenda za mataifa ya nje katika mataifa ya Afrika. Kwa kuzingatia nadharia ya Ubaadausasa, imebainika kuwa riwaya zilizotafitiwa zinasaili simulizi inayolenga kutukuza watu na bidhaa kutoka mataifa ya Ulaya, huku ikitweza watu na bidhaa kutoka mataifa ya Afrika. Utafiti umeonyesha kuwa simulizi hii haiwezi kuaminiwa tena, kwa kuibainisha kama kasumba potovu inayolenga kuyadhibiti mataifa ya Afrika kiuchumi na kitamaduni. Baada ya kuangazia itikadi zilizofichika ndani ya kasumba za kigeni, sehemu ifuatayo imehakiki nafasi ya misaada na miradi mbalimbali kutoka mataifa ya nje pamoja na itikadi zilizofichika ndani yake kwa kujikita katika riwaya za utafiti huu.

### 3.3.2 Utoaji wa Misaada na Uanzishaji wa Miradi Tofauti

Kutokana na kutojimudu kiuchumi, mataifa mengi ya Afrika hutegemea misaada kutoka kwa mataifa ya Ulaya pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa lengo la kujiinua kiuchumi. Kuambatana na maelezo ya Sim (2013) kuwa dhima ya wanaubaadausasa huwa ni kufichua itikadi potovu zilizofichika ndani ya mifumo mbalimbali, sehemu hii imehakiki simulizi inayohusiana na misaada kutoka mataifa ya Ulaya na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kufichua itikadi hizo potovu zilizofichika ndani yake kwa lengo la kuwazindua Waafrika kuhusu misaada hii. Riwaya ya *NZM*, kupitia kwa mhusika, Nana, inabainisha baadhi ya misaada inayotolewa na mataifa ya Ulaya kwa mataifa ya Afrika. Kwa mfano kuna misaada inayotolewa ya 'kuwainua kiuchumi' wanawake maskini katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu:

> Ukijumlisha yote hayo, utajiuliza, Nana ni mwanamke wa aina gani sasa? Bila ya shaka yeye si miongoni mwa wale wanaokusanywa ndani ya *Umoja wa Akina Mama* kupika nyungu za uji, kuchoma maandazi na vitumbua kuviuza kwa senti chache zinazotiwa kwenye kisandukububu kudundulizwa. Siye yeye miongoni mwa wale wanaosukishwa mikoba, vikapu na nyungu kuwauzia watalii wa Kizungu. Yeye si mfumaforonya na mshona vitambaa vya meza. Si mkulima mpigamakoongo ya mhogo au matuta ya viazi na mchimbamashimo ya kupanda kambi za migomba na baadaye kuutangazia ulimwengu: *Haya ndiyo maendeleo ya wanawake* (*NZM* uk 190-191).

Kwa mtazamo wa nje, mashirika yasiyo ya kiserikali yanaonekana kuwaletea wanawake maendeleo. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa wanawake wanasaidiwa kujikimu kiuchumi kupitia kazi na biashara mbalimbali kama vile kupika uji na maandazi, kusuka mikoba na vikapu, na kufanya kilimo cha mihogo, viazi na ndizi miongoni mwa kazi nyingine kama hizo. Hata hivyo, kazi hizi zinazotarajiwa kuleta 'maendeleo ya wanawake' ni kazi duni kwa kuwa mapato yake ni ya chini sana. Kazi hizi duni bila shaka zinamdhalilisha mwanamke wa Kiafrika kwani 'maendeleo' yanayolengwa hayawezi kamwe kuibadilisha nafasi duni ambayo mwanamke

amewekwa katika jamii. Hii ndio maana Nana anasema kuwa yeye si mmoja katika kundi la wanawake 'wanaokusanywa ndani ya *Umoja wa Akina Mama*' wanaofanya kazi hizo duni. Yeye ni mwanamke mwenye nafasi yake na ambaye ameweza kuivuka mipaka duni aliyowekewa mwanamke, hasa katika mataifa yanayoendelea. Kwa mfano, tunaelezwa kwamba Nana amejenga jumba la ghorofa kumi na moja linalojulikana kwa jina, *Karibu Mwanamke*, kutokana na juhudi zake mwenyewe pamoja na msaada wa fedha kutoka kwa mama yake mzazi (*NZM* uk 190). Katika jumba hili, kuna kituo cha redio na televisheni, kituo cha mazoezi na ukakamavu na ofisi kadhaa miongoni mwa mambo mengine. Haya ni mafanikio na maendeleo ya kweli kwa mwanamke ambayo Nana anayaonea fahari, sio kama yale yanayotokana na misaada kutoka nje. Kupitia mhusika Nana, riwaya hii inakashifu misaada hii duni kutoka nje kwa kuwa haiwezi kumsaidia mwanamke katika mataifa ya ulimwengu wa tatu kujiinua na kujitegemea kikamilifu wala kuinua uchumi wa taifa lake.

Ingawa kwa mtazamo wa nje mashirika haya yasiyo ya kiserikali huonekana kujali na kusaidia mataifa yanayoendelea kwa kutoa misaada, kinaya ni kwamba misaada hii huishia kuwanufaisha zaidi watu kutoka mataifa hayo hayo ya nje wala sio Waafrika kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Anapofika hapo Nana hucheka kicheko kikubwa cha wazi kila mtu kusikia. Kisha kujiambia: … Nchi hii imejaa mizaha. Pesa zinazotokana na '*non-governmental organization*', huendelea kukosoa Nana, huwanenepesha waratibu na wasomi wanaoitia mikono ndani ya mifuko hiyo bila ya kumkomboa mwanamke…. Mara Nana alikumbuka mhadhara alioutoa hivi juzi…juu ya mageuzi katika maendeleo ya jamii, ambao, kwa upande mmoja, ulizidi kumpa umaarufu kwa wanawake walengwa, lakini kwa upande wa pili, ulimzidishia uadui miongoni mwa waratibu na wasomi wanaolipwa chungu ya pesa na *non-governmental organisations*. Jambo hili bila shaka lilimshangaza sana Nana. Huwaje vyombo hivi vikawa vinaliwa pesa kila siku, na bado vinakasirishwa na kitendo kizuri cha Nana kutetea pesa zinazoliwa bila ya kuwafikia walengwa? Labda…taasisi hizi zinafanya hivyo makusudi kupotosha malengo ya maendeleo ya watu hawa. Tuseme pesa zao hazikusudiwi hasa kuleta usawa kwa

> wanawake, bali kuigandisha jamii kwenye janga la umaskini milele? Labda jambo hili ni la faida kubwa sana kwao hao wafadhili? Maana wasingetoka huko walikotoka, eti kuja kusaidia wanawake wa huku (*NZM* uk 191).

Inavyobainika ni kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali hayana haja sana ya kumkomboa mwanamke katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, bali huwa na ajenda fulani za kutekeleza. Kama tunavyoelezwa kwenye dondoo misaada ya fedha inayotolewa na mashirika haya 'huwanenepesha waratibu na wasomi wanaoitia mikono ndani ya mifuko hiyo bila kumkomboa mwanamke'. Vilevile tunaelezwa kuwa wasomi na waratibu hawa wanalipwa 'chungu ya pesa' na mashirika haya. Hii ina maana kuwa hazina ya 'pesa za misaada' si za kumkomboa mwanamke hasa, bali kuwalipa waratibu na wasomi mishahara minono minono. Hii ndio maana mhadhara wa Nana kwenye dondoo kuhusu ufujaji wa pesa za msaada unapingwa vikali hasa na wasomi na waratibu wa mashirika haya kwa sababu wanaelewa kuwa fedha hizo sio za kuwasaidia wanawake maskini hasa. Inavyobainika basi ni kuwa misaada hii inatumika kuwafumba macho watu wa Afrika ili kuyawezesha mashirika haya kutimiza ajenda zao kwa mlango wa nyuma. Mojawapo ya ajenda hizo ni kuhakikisha kuwa mataifa ya Afrika yamebaki nyuma kimaendeleo kwa 'kupotosha malengo ya maendeleo…na kuigandisha jamii kwenye janga la umaskini' (*NZM* uk 191). Hii ndio sababu tunapata mataifa haya hayafadhili miradi mikubwa ya maendeleo ya taifa bali huwahimiza wanawake kufanya kazi duni sana ambazo haziwezi kuwainua kiuchumi. Hivyo basi, mataifa ya ulimwengu wa tatu yanagandishwa katika lindi la umaskini na daima yanaishia kutegemea mataifa ya magharibi kwani 'maendeleo' waliyoletewa hayawezi kuinua uchumi wa nchi zao. Kwa mujibu wa nadharia ya Ubaadausasa, misaada inayotolewa na mataifa ya Ulaya kwa lengo la kuyainua kiuchumi mataifa ya Afrika ni simulizi isiyoweza kuaminiwa tena. Hii ni kwa sababu misaada hiyo huishia

kuwanufaisha watu wa mataifa ya Ulaya huku ikiwagandisha watu katika mataifa ya Afrika kwenye lindi la umaskini na utegemezi.

Ajenda nyingine inayoambatana na misaada kutoka mataifa ya ulaya ni kuhakikisha kuwepo kwa utiifu kutoka kwa mataifa ya Afrika kwa lengo la kuyafanya mataifa hayo yafuate amri na sheria zinazotoka katika mataifa ya ulaya. Tunaambiwa:

> Na sasa yupo 'Superboymmoja'…dunia yote imegeuka Magharibi… 'Superboymmoja. Mkamata yote. Haki na uadilifu mkono mmoja. Maangamizo na uharibifu mkono mwingine. Huruma na ruzuku hutolewa kwa kejeli. Chakula ni mchezo wa karagosi unaotoa furaha kubwa au kuchochea utiifu au kuwateka watu akili. Kwenda juu pasi na kikomo ni raha ya ajabu. Kwa sababu unakuwa kileleni ukiketi na kutembea juu ya vichwa na mabega ya watu. Watu wote lazima watii amri zako. Wakifa, wakiangamia potelea mbali. (*DY* uk 45-46).

Neno 'Superboymmoja' katika dondoo linarejelea nchi ya Marekani ambayo ndiyo nchi yenye nguvu zaidi za kiutawala, kichumi na kiteknolojia ulimwenguni kote. Hii ndio sababu tunaelezwa kuwa nchi hii imeketi 'kileleni'…na kutembea juu ya vichwa na mabega ya watu'. Hii ina maana kuwa hakuna taifa lingine lililo juu zaidi kuliko nchi ya Marekani katika kila sekta ya maisha. Ikiwa juu kileleni tunaelezwa kuwa Marekani inatembea 'juu ya vichwa na mabega ya watu', yaani inayadhulumu mataifa yaliyo chini yake kwa kuyawekea amri ambazo 'watu wote lazima watii'. Kutokana na mantiki hii, tunaelewa kuwa mataifa ya ulaya hususan, Marekani inatumia nguvu zake kuyadhulumu mataifa ya Afrika bila kujali matokeo yake. Waafrika 'wakifa, wakiangamia' hawana shida mradi ajenda zao zimetimizwa. Huu ndio mkono 'maangamizo na uharibifu' wa mataifa ya ulaya. Mkono wa 'haki na uadilifu, huruma na ruzuku' hudhihirika kupitia utoaji wa misaada kwa mataifa ya Afrika. Hata hivyo, misaada hii hutolewa kwa kejeli kumaanisha kuwa haitolewi kwa furaha kwa lengo hasa la kusaidia. Kwa mfano tunaelezwa kuwa msaada wa chakula hulenga kuleta 'furaha kubwa au kuchochea utiifu au kuwateka watu akili' watu wa mataifa ya Afrika. Kwa hivyo, utoaji wa misaada sio ishara ya kujali au kusaidia mataifa haya bali

inatumika kama chambo cha kuwafurahisha Waafrika na kuwafanya watii amri zao kandamizi, au hata kuwateka akili Waafrika ili wasitambue kwa urahisi ajenda zao zilizofichika ndani ya misaada wanayoitoa. Hivyo basi, misaada hutolewa kwa mataifa ya Afrika ili mataifa ya ulaya yaweze kutimiza ajenda zao za kuendelea kutawala na kudhibiti mataifa mengine katika kila sekta ya maisha yao. Hii ndiyo itikadi iliyofichika ndani ya misaada inayotoka mataifa ya kigeni.

Misaada ya silaha za vita pia hutolewa na matifa ya Ulaya kwa mataifa yanayoendelea kwa manufaa yao wenyewe kama inavyodhihirika katika dondoo linalofuata:

> Ubinafsi umekuja kuimarishwa na nguvu kubwa mno katika karne hii, nguvu za sayansi na teknolojia ambazo nazo zimekuza utashi wa pesa. Siku hizi vitu hivi ndivyo ishara inayosimamia uwambangoma wa hali ya juu. Wenyewe wanaojua huuita ‘narcissism’. Kufa kwetu sisi ndiyo nusura ya wengine. Hatupo sisi wala hatuishi mbele ya watu hawa. Mbele ya ubinafsi, sayansi, teknolojia na utashi wa pesa sisi ni ombwe tupu… Timor ilionewa. Kosovo ilikandamizwa… Rwanda. Burundi. Angola wajinga wanaokubali kupiganishwa. Silaha zinatoka wapi? Almasi zinakwenda wapi? Wachache wauwane. Wakiwa hai wakifa ni mamoja kwetu. Tutatawala tutatawala tu. Wakitaka wasitake (*DY* uk 46, 48).

Inabainika kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe katika mataifa yanayoendelea kama vile Rwanda, Burundi na Angola (kwenye dondoo hapo juu) huchochewa na mataifa ya Ulaya. Hatimaye misaada ya silaha za vita hutolewa kama njia ya kukomesha vita hivyo. Kinaya ni kuwa silaha hizi huchochea zaidi vita hivi vya wenyewe kwa wenyewe na mataifa ya Ulaya yanapata nafasi ya kuendeleza ajenda yao ya kupora raslimali za mataifa hayo. Hii ndio maana Ndi- kwenye dondoo anauliza, ‘Silaha zinatoka wapi? Almasi zinakwenda wapi? Maswali haya yanadhihirisha ukweli wa kauli kwenye dondoo kuwa, ‘Kufa kwetu sisi ndiyo nusura ya wengine’ *(DY 46)* kuonyesha kuwa pindi mataifa ya Afrika yanapopiganishwa ndivyo mataifa ya Ulaya yanaendelea kunufaika. Hali hii ndiyo inayorejelewa kwenye dondoo kama ‘narcissim’. Neno ‘narcissim’ kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2006) ni hali ya kujipenda au kujihusudu.

Mtu anayejipenda bila shaka ana ubinafsi na kufanya kila jambo kwa madhumuni yake binafsi. Huu ni ubinafsi usiokubalika.

Licha ya hayo, misaada ya mipira ya kondomu inatolewa na mataifa ya Ulaya ili kukabiliana na ugonjwa wa ukimwi kwa mataifa yanayoendelea kwa lengo la kutimiza ajenda zao:

> Kisha waliwatokezea *NGOs* wanaowaonea huruma wanawake wasiojua kujionelea wala kujitetea wenyewe. Alizisikia sauti zinazopinga ngono kwa kukaribisha ngono. Fashion za *tumbo-cut* na *fundi-kasahau-mshono*, na *Rap* za vijana kukobeana na mipasho ya kutukanana, hizi ni feshini tu, huo ni usasa, huo ni utandawazi wewe mpumbavu Nana.Tumia soksi tu. Endeleza utamaduni wa ngono. Aliisikia sauti yake ikimsusuika Nana. Ilikuwa kama Nana akiisikiliza sauti yake ikigombana na nyingine – Hauhusiani usasa na ukimwi wewe. Ukimwi utaondoka kwa kuvaa soksi na mawaidha ya kuhimiza soksi kwenye vyombo vya habari. Ukimwi utaondoka kwa wingi wa fedha na misaada inayotoka nje (*NZM* uk 181).

Ukimwi ni mojawapo ya magonjwa yasiyo na tiba na yaliyoenea sana katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, hasa katika mwongo wa kwanza wa K21. Kama njia mojawapo ya kukomesha kuenea kwa ugonjwa huu mashirika yasiyo ya kiserikali yanapendekeza matumizi ya mipira ya kondomu, au ‘soksi’ kama inavyorejelewa katika dondoo. Hii inaandamana na mawaidha kemkem katika vyombo vya habari kuhusiana na matumizi ya kondomu. Kwa mfano tunaelezwa kuwa ‘ukimwi utaondoka kwa kuvaa soksi na mawaidha ya kuhimiza soksi kwenye vyombo vya habari’. Bila shaka fedha nyingi zinatumiwa na mashirika hayo sio za kusaidia kupunguza makali ya ugonjwa wa ukimwi bali kugharamia matangazo na mawaidha kuhusu matumizi ya kondomu, pamoja na kutoa misaada ya kondomu zenyewe. Kwa hakika, hatuna budi kujiuliza ni nini hasa kinachoyapa mashirika haya msukumo mkubwa hivi kugharamia ugonjwa wa ukimwi, wala si ugonjwa kama saratani ambao pia umewalemea watu katika mataifa ya Afrika.  Tunaweza kuunda nadharia inayobainisha mojawapo ya ajenda za mataifa ya nje kupitia misaada inayotolewa kwa mataifa ya Afrika. Kwanza, huenda Afrika

inatumiwa na mataifa ya nje kama jukwaa la kufanyia utafiti bidhaa mpya wanazoziziunda. Katika kufanya hivyo, wanagharamia utafiti wao kwa kuanzisha miradi ambayo kwa jicho la nje inaonekana kuwasaidia Waafrika. Hii inaeleza basi ni kwa nini juhudi nyingi sana hutumika kutoa mawaidha na kusambaza mipira ya kondomu ili kukamilisha utafiti wao.

Isitoshe, tunaona kuwa hakuna juhudi zozote zile zinazofanywa na mashirika haya kueleza wananchi wajiepushe na ngono au mapenzi ya kiholela. Badala yake tunaelezwa kuwa Nana anasikia sauti 'zinazopinga ngono kwa kuikaribisha ngono'. Hapa tunaona mashirika hayo yakiwatia shime watu wa mataifa ya Afrika waendelee kufanya ngono kwa sababu kuna mipira ya kuwakinga. Hapa tunaweza kuzua nadharia ya pili kuhusu itikadi iliyofichika ndani ya mahimizo hayo ya kuendelea kufanya ngono mradi kuna mipira ya kujikinga. Huenda, mashirika haya yanatafuta soko ya bidhaa zao katika siku za baadaye wakati misaada hii ya kondomu itakapokoma kutolewa. Wakati huo, Waafrika watakuwa wamezoea maisha ya ngono kwa sababu ya kuwepo na njia za kujikinga, hasa kwa kutumia mipira ya kondomu. Kwa kuhofia kuambukizana ugonjwa wa ukimwi, mataifa ya Afrika yatalazimika kuilipia mipira hii kwa gharama ya juu, hivyo kuyawezesha mataifa ya nje kupata soko la bidhaa zao huku wakiwapunja Waafrika.

Katika enzi hizi za utandawazi, tunaona kuwa vyombo vya habari vinatumika kurahisisha na kuendeleza ajenda za mataifa ya Ulaya. Kwa mfano, tumetajiwa kwenye dondoo hapo juu kuwa vyombo vya habari ndivyo vinavyotumiwa kutoa mawaidha na kuhimiza matumizi ya kondomu. Vilevile, vimetumiwa kuendeleza 'Fashion za *tumbo-cut* na *fundi-kasahau-mshono*, na Rap za vijana'. *Tumbo-cut* na *fundi-kasahau-mshono* ni mtindo wa kisasa wa mavazi mafupi kwa wanawake, ambao aghalabu hulenga kuvuta ashiki za wanaume. *Rap* nayo ni muziki wenye mtindo wa kisasa ambao

tumeelezwa kuwa vijana hukobeana na ‘mipasho ya kutukanana’. Hii ina maana kuwa muziki huu husheheni matusi ya kila nui, huku mavazi yakiwa ya aibu kinyume cha utamaduni wa Kiafrika. Hii inadhihirisha hali halisi ya ubaadausasa kama inavyoelezewa na mwananadharia Fredric Jameson katika kitabu chake, *Postmodernism, or the Cultural Logic of Late Capitalism* (1991). Jameson anaiona runinga kama chombo kinachotumiwa kueneza utamaduni wa ubaadausasa unaohusishwa na utumiaji wa bidhaa. Akimnukuu Jameson, Sim (2001:113) anaeleza kuwa runinga ni kama gundi inayotumika kuunganisha jamii tofauti ili kuendeleza utamaduni wa ubaadausasa unaohusu utumiaji wa bidhaa. Kwa hivyo, vyombo vya habari vinatumiwa na mataifa ya Ulaya kama jukwaa la kuuza bidhaa zao, hususan mipira ya kondomu na utamaduni wao kwa kujificha katika matangazo yanayohusu fesheni za *tumbo-cut* na muziki wa *Rap*. Utamaduni huu mpya unaoenezwa kupitia vyombo vya habari unauchujua utamaduni wa Kiafrika na hatimaye unachukuliwa kama ‘usasa’, huku utamaduni wa Kiafrika ukichukuliwa kama ‘ukale’.

Katika kutamatisha sehemu hii, ni dhahiri kuwa misaada kutoka mataifa ya Ulaya huwa na ajenda zilizofichika, hususan, kudidimiza maendeleo ya mataifa ya Afrika, kupata soko la bidhaa na kupata uwanja wa kufanyia utafiti kwa magonjwa mapya yanayotokea ulimwenguni. Kwa hivyo, riwaya zilizotafitiwa zinajaribu kuwazindua Waafrika kuhusu ajenda za mataifa ya kigeni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ambazo huficha itikadi fulani ndani ya miradi ya maendeleo na misaada tofauti ili wawe waangalifu wanapoipokea. Katika sehemu inayofuata tunaangalia nafasi ya uwekezeji katika mataifa ya Afrika na itikadi iliyofichika ndani yake.

### 3.3.3 Uwekezaji katika Mataifa ya Afrika

Njia nyingine ya mataifa ya Ulaya ya kutimiza ajenda zao ni kupitia uwekezaji. Uwekezaji katika makampuni na biashara tofauti tofauti husaidia kumtawala Mwafrika

kiuchumi pamoja na kuuchujua utamaduni wake. Katika *UNN* mataifa ya Ulaya yanawekeza katika majumba ya anasa na starehe kwa ushirikiano na wenyeji wa nchi husika:

> Akamuuliza kama alijua klabu iliyojulikana kama *Avocado Wasp* hapo jijini… Ni klabu ya wanasiasa kadha, na wazungu, nadhani Wamarekani na labda Waingereza – wajua tena jamaa hao wanavyowekeza nchi hii; ni kama wanashindana na Wachina kama wawindaji wanaong'ang'ania nyama, aliambiwa. Maegesho yenyewe yalikuwa yamefurika magari… mataa ya ndani ya ukumbi huo mkubwa yalikuwa ya kila aina (*UNN* uk 222-227).

Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, kuna wawekezaji wengi kutoka mataifa ya nje kama vile Wamarekani, Waingereza na Wachina. Inavyojitokeza ni kwamba mataifa ya Afrika ni uwanja mzuri wa kuwekeza na ndio maana tunaelezwa 'wanashindana …kama wawindaji wanaong'ang'ania nyama', kumaanisha kuwa wanatamani kuwekeza katika mataifa haya labda kutokana na mtaji mkubwa wanaoupata.

Kwa kawaida, uwekezaji kutoka mataifa ya nje unaweza kuathiri uchumi wa nchi pokezi kwa njia chanya au hasi. Akizungumzia kuhusu uhusiano uliopo kati ya uwekezaji kutoka mataifa ya kigeni na ukuzaji wa uchumi wa nchi pokezi, Mencinger (2003) anaeleza kuwa uwekezaji kutoka makampuni ya kigeni aghalabu huleta ushindani mkubwa kwa makampuni ya kienyeji hasa yale madogo. Sababu ni kuwa makampuni makubwa makubwa kutoka mataifa ya kigeni huwa na ujuzi na njia za kisasa za kiteknolojia ambazo huyawezesha kutengeneza bidhaa nyingi kwa gharama ya chini. Kutokana na haya, makampuni ya kienyeji ambayo hayajaendelea sana katika njia za kisasa za kiteknolojia hupata ushindani mkubwa sana na hatimaye hulazimika kuyafunga. Hali hii bila shaka huathiri uchumi wa nchi pokezi kwa njia hasi kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Kwanza ilianza Siasa ya Soko Huria. Makampuni mengi yakaanzishwa nchini. Kampuni yetu ya mafuta ya kupikia, ambayo ilikuwa kampuni ya pekee nchini siku hizo, na kampuni ya wenyeji hasa, kwa hiyo ilipendwa sana na watu wengi, ikakumbana na

> ushindani ambao haikuwa imejiandalia…. Hata watu waliokuwa wakiyachangamkia mafuta yake wakabadili nia… wakaonja mafuta ya kampuni nyingine. Kampuni ikawa ni kama imetiwa kitanzi shingoni. Lakini bado inaweza kushindana. Muda ukapita, kitanzi kikavutwa. Soko likaanza kupungua. Wakuu wa kampuni wakatuita na kutueleza kuwa hali imekuwa ngumu. Inabidi tujitolee zaidi ili kuongeza mauzo ya kampuni. Saa za kazi zikaongezwa kidogo; marupurupu nayo yakapunguzwa. Waliotishia kuwaeleza wakuu wa vyama vya wafanyikazi wakatafutiwa kisingizio na kupogolewa kama matawi ya mbuni yaliyoota yasikotakiwa…kitanzi kikavutwa tena… mara hii vibarua wakaachishwa kazi… hali ikawa mbaya sana. Hofu ikawa imetanda kila mahali. Hata utendakazi nao ukaathirika….Mapato yakashuka. Soko tulilokuwa nalo likawa limeanza kutwaliwa na makampuni mapya ya Ulaya na ya Marekani. Kitanzi kikavutwa zaidi. Kampuni ikatokwa na ngama. Tukaachishwa kazi. (*UNN* uk 157-158).

Kama inavyojitokeza katika dondoo hapo juu, mfumo wa soko huria huwezesha mataifa ya kigeni kuwekeza katika mataifa ya Afrika. Ushindani kutoka makampuni na kigeni hatimaye huathiri makampuni ya kienyeji kwa njia hasi. Jambo la kwanza kuathirika ni soko la bidhaa. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa soko lililokuwa limetawaliwa na bidhaa kutoka makampuni ya kienyeji linaanza kupungua kwa kuwa bidhaa sawia na hizo zinatengenezwa na makampuni ya kigeni na wanunuzi hawakuwa budi kujaribu bidhaa mpya kutoka kwa makampuni ya kigeni. Kwa hivyo wateja wa mafuta ya kienyeji wakapungua na kuathiri mauzo ya bidhaa hizo. Jambo la pili kuathirika ni wafanyikazi. Tunaelezwa kuwa ili kuongeza mauzo, wafanyakazi wanaongezewa saa za kufanya kazi nayo marupurupu yanapunguzwa. Hatua hii ambayo inalenga kupunguza gharama ya kutengeneza bidhaa kwa kampuni inawaathiri wafanyakazi kwa njia hasi kwa kuwa kazi wanayoifanya ni nyingi zaidi lakini malipo yake ni ya chini ikilinganishwa na ilivyokuwa kabla ya uwekezaji kutoka makampuni ya kigeni. Tatu, baadhi ya wafanyakazi wanafutwa kazi kwa kuwa mapato yanaendelea kushuka na hatimaye kampuni linafungwa kwa kuwa soko la bidhaa linaanza ‘kutwaliwa na makampuni mapya kutoka Ulaya na Marekani’. Hii ina maana kuwa makampuni ya kienyeji yanajipata hayawezi kushindana kikamilifu na kampuni kutoka

mataifa ya nje. Kwa hivyo, makampuni kutoka mataifa ya kigeni yananawiri na kuitawala soko la bidhaa huku makampuni ya kienyeji yakididimia. Kudidimia kwa makampuni ya kienyeji kunaathiri uchumi wa wenyeji kwani njia zao za kujikimu kimaisha zinakatizwa wakati kampuni waliyoifanyia kazi inafungwa. Vilevile, faida ambayo ingepatikana kutokana na utengenezaji na uuzaji wa bidhaa za kienyeji inapungua kwa kuwa sehemu ya faida kutoka makampuni ya kigeni inatumika kuendeleza mataifa ya kigeni. Hatima yake ni kuwa uchumi wa nchi pokezi unaanza kudidimia na wananchi kuendelea kuogelea katika dimbwi la uhitaji. Kwa hivyo, uwekezaji kutoka mataifa ya nje hulenga kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi kwa kuwa mataifa ya Afrika hayawezi kushindana kikamilifu na mataifa ya kigeni. Jambo hili huyafanya mataifa ya Afrika daima kuyategemea mataifa ya kigeni na kudidimia zaidi katika umaskini huku mataifa ya kigeni yakimiliki njia zote kuu za uzalishaji mali. Hivyo basi ni dhahiri kuwa ajenda inayoendelezwa katika uwekezaji kutoka mataifa ya kigeni ni kuyatawala mataifa ya Afrika kichumi.

Mbali na kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi, uwekezaji umechangia pakubwa katika kuuchujua utamaduni wa Mwafrika. Kwa mfano katika *UNN* tunaelezwa kuwa mojawapo ya shughuli katika majumba ya anasa yaliyowekezwa na wazungu na wachina ni uchezaji wa densi ambapo wanawake wanawatumbuiza wateja kwa kucheza densi wakiwa 'juu ya meza, nusu uchi' (*UNN* uk 222-227). Jambo hili haliambatani kamwe na utamaduni wa Kiafrika bali utamaduni wa Kimagharibi. Wanaoukumbatia utamaduni huu wa Kimagharibi wanaona kuwa wamejiepusha na ukale na kuingia katika usasa kama inavyothibitishwa na mazungumzo katika *UNN* kati ya Truvessa, mmoja wa wanawake wachezaji densi, na mumewe, Purupesa anayechukizwa na tabia hizi za kimagharibi:

"Mambo gani haya?"

> "Nini? Nataka uhuru wa kujielezea na kuyaishi mawazo yangu. Napenda kuzifurahia njozi zangu bila ya kuzuiliwa na matarajio ya asasi kama ndoa au utamaduni".
>
> "Lakini hatuwezi tu kuyakimbilia mageni…"
>
> "Hapana. Hiyo ni *chronological primitivism*…Profesa hapo ulipo hujamsoma Octavio Paz katika *The Labyrinth of Solitude* na kutambua kuwa kuishi kwenyewe kunahusu chuku, kuvunja kaida na kanuni, kwenda kwenye kilele, kufanya majaribio na hisia zenyewe? Labda tumeishi miaka mingi katika hali ya kudhibitiwa kiasi cha kupoteza uwezo wa kujieleza kwenye mtazamo wetu wenyewe na kwenye mwangaza!... Mambo yamebadilika siku hizi profesa…Hata watu wanaenda *Swinger Clubs* wanakobadilishana wake au waume ili kutia iliki kwenye mahusiano yao yaliyokosa ladha. Ukale hauna nafasi tena katika maisha yetu!"
>
> "Truvessa…Hizo ni tabia za Ulaya na Marekani…Watu ambao wamekosa mwelekeo na kuyachoma maghala ya utamaduni zamani…" (*UNN* uk 232-233).

Kwa mujibu wa dondoo hapo juu, utamaduni, hususan utamaduni wa Kiafrika unamdhibiti binadamu asitende anavyotaka. Hii ndio maana Truvessa anasema kuwa anataka kuwa huru, na kuwa huru huandamana na 'kuvunja kaida na kanuni' pamoja na 'kufanya majaribio'. Hivyo basi binadamu hafai kufungwa na kanuni zozote, hata zile za kitamaduni, na anapaswa kuwa huru kufanya majaribio na kutenda anavyotaka. Uvunjaji wa kaida pamoja na kufanya majaribio ni mojawapo ya mihimili na nguzo muhimu katika nadharia ya ubaadausasa. Kisa hiki cha Truvesaa basi kinadhihirisha hali halisi ya ubaadausasa katika K21 ambapo baadhi ya watu wamevunja kanuni za utamaduni wa Kiafrika na kujaribu mambo mapya yanayoambatana na utamaduni wa Kimagharibi. Hata hivyo, ukiukaji na uvunjaji wa kanuni za utamaduni wa Kiafrika huwa na madhara yake hasa kuhusiana na suala la maadili. Kwa mfano, tunaona masuala ya ngono na uzinifu yakichukuliwa kama mambo ya kawaida tu. Ubadilishanaji wa waume na wake nao unachukuliwa kama njia mojawapo ya 'kutia iliki kwenye mahusiano'. Huu ni uzinifu ambao haukukubalika katika utamaduni wa Kiafrika lakini unaokubalika katika utamaduni wa Kimagharibi. Mambo haya mapya

basi yanaendelea kuuchujua utamaduni wa Kiafrika uliojikita katika maadili na uadilifu. Ingawa nadharia ya ubaadausasa inatilia shaka nadharia kuu ya utamaduni, msimamo wa utafiti huu ni kuwa kutozingatiwa kwa suala la maadili ni mojawapo ya udhaifu katika nadharia hii. Katika utafiti huu tunasisitiza kuwa ingawa kuna mambo katika utamduni wa Kiafrika yanayopaswa kuangaliwa upya, sio mambo yote yanayohusiana na utamaduni huu ambayo ni mabaya, hasa suala linalohusiana na maadili ya kijamii hata katika ulimwengu huu wa ubaadausasa. Katika sehemu inayofuata tumeangazia suala la masharti na amri kutoka kwa mataifa ya kigeni na athari zake kwa mataifa ya Afrika.

### 3.3.4 Amri na Masharti Kutoka Mataifa ya Ulaya

Mataifa ya kigeni aghalabu hutoa amri na kuwekea watu wa mataifa ya Afrika masharti mbalimbali ambayo wanafaa kuyafuata katika shughuli zao mbalimbali. Amri na masharti haya huwekwa na watu wa mataifa ya Ulaya wenye nguvu za kiutawala kama vile Marekani na hulenga kutimiza ajenda zao wenyewe waziwazi au kwa njia iliyofichika. Tazama dondoo lifuatalo:

> Na sasa yupo 'Superboymmoja' dunia yote imegeuka Magharibi… Kila kinachokwenda dunia hii lazima chende kwa pumzi zake. Pumzi moja. Lazima kiwe sehemu ya maslahi yake… Watu wote lazima watii amri zako… Bila shaka wewe unalaani ukandamizaji. Unapinga jinsi moja kuiangamiza jinsi nyingine… Unapigania haki za binadamu. Iraki na Kuwait. 'Sanctions' kiboko kwa wasiofuata. Haidhuru kitakachotokea chochote. Kwa nini isiwe hivyo unapokuwa na nguvu za kiungu? Hakuna atakayedhubutu kukulaumu. Unaweza kuangamiza huku na kunusuru kule, maadamu unajua ari ya utu haimo ndani ya damu za watu waliotupwa jaani. Msingi wa kukataa kudhalilishwa kwao umefukilika. Aibu na fedheha imerushwa na upepo wa haja. Fedha…Pesa…Misaada…Mikopo. Kama husujudu unaangamia (*DY* uk 45-46).

Jina 'Superboymmoja' katika dondoo limetumika kurejelea nchi ya Marekani ambayo mbali na kuwa na nguvu za kiutawala, imejawa na ubinafsi wa hali ya juu. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa kila kitu kinachotendeka ulimwenguni 'huenda kwa pumzi zake' na

huwa ‘sehemu ya maslahi yake’ kudhihirisha nguvu na ubinafsi mtawalia. Ili kuweza kutimiza maslahi yao, wanatumia nguvu na mamlaka waliyo nayo kuweka amri ambazo ‘watu wote lazima watii’. Wanaokosa kutii wanawekewa ‘sanctions’ au vikwazo mbalimbali hasa vya kiuchumi kama njia ya kuwaadhibu. Mataifa ya ulimwengu wa tatu hayana budi kufuata amri zinazotolewa kwa sababu, kwanza hayana uwezo wa kuzipinga ‘nguvu za kiungu’ za *Superboymmoja* na yakithubutu yanaweza kuangamizwa. Pili, mataifa haya yana mahitaji mbalimbali yawe ya ‘pesa, misaada na mikopo’ ambayo yanategemea Superboymmoja ayasaidie. Hii ndiyo sababu tumeelezwa kuwa ‘aibu na fedheha imerushwa na upepo wa haja’ kumaanisha kuwa uhitaji katika mataifa ya ulimwengu wa tatu unayafanya mataifa haya kunyenyekea chini ya huyu Superboymmoja ili kupata usaidizi yanaouhitaji kutoka kwake. Ingawa kwenye dondoo hapo juu hatujaelezwa kuhusu amri na masharti yenyewe, dondoo linalofuata linadhihirisha kuwa mengi ya masharti na amri zinazowekwa na mataifa ya ulaya hulenga kuyatawala kiuchumi mataifa ya Kiafrika:

> Utawasikia wakituambia (sisi wajinga tuliwao): ‘Msifanye hiki na kile, fanyeni kile na hiki. Uzeni viwanda vyenu vyote. Wapeni wanaojua biashara ya kuagiza na kusambaza mafuta nchini mwenu. Tafuteni kampuni ya kuongoza biashara ya huduma za maji na umeme. Zipeni kampuni maarufu hati ya kuendesha forodha na shughuli za bandarini. Nunueni ujuzi. Msiige teknolojia za watu! … Tumieni tu hiyo teknolojia huku mkiilipia fedha… Ndiyo wanasema hivyo!... Wanasema kwa vitendo si kwa maneno. Wanasema kwa sheria wanazozitunga wao wenyewe ili sisi tuzifuate. Sisi tuwe wafuasi daima. Hawasemi bali wanaamrisha watu hasa kufanya mambo ya halali kama vile wao hawajapata kamwe kupora chochote duniani. Sisi sote tunajua kwamba utukufu wao wote unasimama ndani ya misingi yenye kutiliwa shaka (*NZM* uk 193).

Mataifa ya Ulaya huwashurutisha Waafrika kuuza kampuni na viwanda vyao kupitia ‘sheria wanazozitunga wenyewe’ na kuwalazimisha Waafrika kuzifuata**.** Kwa mfano, tunaelezwa kwenye dondoo wanavyowarai Waafrika kuuza viwanda vya mafuta, forodha na kampuni na maji na umeme kwa watu ‘wanaojua biashara’. Hawa watu

wanaojua biashara bila shaka ni wale wanaotoka katika mataifa ya kigeni yaliyopiga hatua katika teknolijia ya kisasa. Hii ni mbinu iliyofichika inayotumiwa na mataifa ya Ulaya kuwekeza katika mataifa ya Afrika na kuendelea kujitajirisha huku ikiwapunja wenyeji. Mojawapo ya sheria zinazoambatana na uwekezaji huu ni kuwa mataifa ya Afrika hayapaswi kuiga 'teknolojia za watu' bali wanafaa 'kununua ujuzi'. Hii ina maana kuwa mataifa ya Afrika yanalazimika kutumia fedha kugharamia ujuzi wa kiteknolojia unaotoka katika mataifa ya Ulaya. Hii ni njia nyingine ya kuyapunja mataifa ya Afrika huku mataifa ya Ulaya yakiendelea kujitajirisha. Kama inavyojitokeza katika dondoo, huduma ambazo wenyeji wanaambiwa wauze ni zile muhimu na ambazo humwathiri mwananchi moja kwa moja kama maji, umeme, mafuta na kadhalika. Mataifa ya Afrika yanapouza huduma hizi, mataifa ya nje yanazinunua na kuzibinafsisha na hivyo kupata uwanja wa kuekeza katika mataifa ya Afrika. Huduma hizi zikiwa mikononi mwao, wana uhakika kuwa watanufaika zaidi kwa kuwa zinahitajika kila wakati. Aidha, zikiwa mikononi mwao, watauza huduma hizi kwa bei ya juu kwa Mwafrika. Katika kufanya hivyo, wanafaulu katika kudhibiti na kutawala mataifa ya Afrika kiuchumi. Wanaendelea kujitajirisha zaidi na kuendeleza uchumi wao huku Mwafrika akiendelea kudidimia katika umaskini.

Mbali na kutawaliwa kiuchumi, hatimaye mataifa ya Afrika hutawaliwa katika kila tone la maisha yao. Hii ndiyo ajenda kuu ambayo mataifa ya ulaya huwa nayo dhidi ya mataifa ya Afrika. Katika dondoo linalofuata tunaona lalama ya Ndi- kuhusiana namna mataifa ya Afrika yanavyotawaliwa na kudhibitiwa na mataifa ya kigeni:

> Wamechukua kila kitu!... Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. Watendaji wetu. Wanaohisi kwa ajili yetu. Wanaona njaa na kiu zetu. Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kwa jumla waendesha maisha yetu yote. Sehemu ya viwiliwili na akili zetu. Kwa ufupi wao ni kila kitu chetu! Sisi wengine ni mapipa matupu. Hatuna rojo la uhai. Hatuna supu ya maisha. Wala nyama ya ubinadamu. Hatuna sehemu

> ya utu. Hatuna rai. Hatuna maoni. Hatuna chetu. Hatuwezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi zetu… Siku hizi kusema kweli ulimwengu hautawaliwi kamwe na wenye akili. Wenye nguvu za utawala, si wenye akili tena, ni wenye mali na pesa na nguvu za kijeshi. Hao ndio wanaohodhi utaratibu wa maisha, nyenzo za mawasiliano, elimu, sayansi, teknolojia… Aaaa, ni nguvu, nguvu na kudhibiti ndio utashi mkubwa wa mwanadamu sasa! (*DY* uk 43, 47).

Ni bayana kuwa mataifa ya Ulaya yameweza kuyatawala na kuyadhibiti mataifa ya Afrika katika kila sekta ya maisha; uchumi, afya, elimu na kadhalika. Kama tunavyoelezwa kwenye dondoo, wao ndio 'wanaendesha maisha yetu kwa jumla'. Kutokana na amri zinazowekwa kama tulivyokwisha jadili hapo awali, Mwafrika hatarajiwi kusema lolote hata kama linamuumiza ama kumwangamiza. Yaani mwafrika ni kama 'mapipa matupu' kumaanisha kuwa yeye ni mpokezi tu wa chochote kinachotupwa kwake na maoni yake hayasikilizwi wala kutiliwa maanani . Kwa hivyo anabaki kuwa mpokezi tu na mfuasi wa mambo yote kutoka mataifa ya ulaya yenye nguvu. Hiki ndicho kilele cha ajenda za mataifa ya ulaya; yaani kuyatawala na kuyadhibiti mataifa manyonge, hususan yale ya Afrika, katika kila sekta ya maisha yao.

Katika kutamatisha sehemu hii, inadhihirika kwamba mataifa ya Ulaya yamejawa na ubinafsi na mambo yote yanayoyafanya hufanywa kwa maslahi yao. Imebainika pia kuwa mataifa haya huwa kama sarafu yenye pande mbili. Kwa upande mmoja yanashika haki na huruma lakini kwa upande mwingine yamebeba maangamizo na uharibifu. Kwa hivyo, misaada na miradi mbalimbali inayotolewa kwa mataifa ya Afrika hujikita katika upande wa haki na huruma. Hata hivyo, misaada hii hutolewa kama chambo cha kufurahisha, kuchochea utiifu na kuteka fikra za watu wa mataifa ya Afrika ili kuyadhibiti na kuyatawala mataifa haya kiuchumi. Aidha, maangamizi na uharibifu hutokea kwa mataifa yanayoasi amri na masharti ya mataifa ya Ulaya kama njia ya kuyaadhibu na kupata namna ya kuendeleza ajenda zao kwa mataifa ya Afrika.

Ingawa mataifa ya kigeni yanafanya kila juhudi kuendeleza ajenda zao barani Afrika, Waafrika wenyewe wanaweza kulaumiwa kwa kuchangia pakubwa katika kutimizwa kwa ajenda kandamizi kutoka mataifa ya ulaya:

> Tatizo kubwa kwetu ni kuthubutu…Tunataka kuendelea, lakini hungojea kupangiwa maendeleo na wanaoitwa mabingwa kutoka nje. Na wafikapo hapa hao mabingwa hawaturuhusu kushiriki katika kuupalilia uchumi wetu. Wao hutaka tufuate amri zao, na amri zao ni amri za kutoka nje zinazofundisha kurudi nyuma badala ya kwenda mbele… lakini sijui kwa nini watu wetu hawaoni wala hawaitambui busara yao wenyewe inayohimizwa kwa methali ya 'Usimwamshe aliyelala, ukimwamsha utalala wewe' Inakuwaje Waafrika huwaajiri mabingwa wa uchumi wenye maslahi yao kuja kuwashauri na kuendeleza chumi zao? … Ndiyo huja na ubingwa, lakini pia na shuruti na ajenda zao wanazozificha. (*NZM* uk 192-193).

Kwanza, Waafrika hawafanyi juhudi zozote kupanga miradi yao ya maendeleo. Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, tatizo kubwa la Mwafrika 'ni kuthubutu'. Hii ina maana kuwa hawa Waafrika hawajizatiti kwa lolote bali hungojea kupangiwa miradi ya maendeleo na mataifa hayo ya nje badala ya kushiriki kikamilifu. Wanawalipa wataalamu kutoka mataifa ya nje ambao hawawashirikishi wenyeji katika miradi hiyo ya maendeleo. Hii inadhihirisha sio tu uzembe bali utegemezi, mapuuza na hali ya kutojiamini. Angalau, ingekuwa afadhali iwapo mataifa ya Afrika yangeweka masharti kuwa wanapowaajiri hao wataalamu wa nje, ni lazima wenyeji wenye taaluma husika wahusishwe ili wapate ujuzi. Kinaya ni kuwa wageni ndio wanawawekea wenyeji masharti na kuwatungia sheria za kufuata, na kama tunavyoelezwa, 'amri zao ni amri kutoka nje zinazofundisha kurudi nyuma badala ya kwenda mbele'. Hii ina maana sheria zinazotungwa ni za kuwanufaisha wageni bali sio wenyeji, lakini wenyeji hawaonekana kutambua hivyo.

Sababu mojawapo inayowafanya Waafrika kutotambua hayo ni kuwa wengi wamefumbika macho kutokana na kufaulu kwa kasumba potovu zinazoenezwa za kumdhalilisha Mwafrika. Kwa hivyo wengi wanaziona sheria hizi kama mambo ya

kawaida yasiyoweza kusailiwa na ambayo hawana nguvu kuyazuia. Hata hivyo kama anavyosema Ndi- watu hawafai 'kuketi na kukamata mikono tu kutazama ulimwengu unavyoangamia' Ni lazima wainuke na 'kuzuia mtutumko' ingawa si jambo rahisi kwa sababu mbegu za ubinafsi zimeatikwa ndani ya uhai wa binadamu' (*DY* uk 48). Kama anavyosema Ndi- ingawa si rahisi kuzipinga nguvu hizi, Waafrika wanafaa kuzinduka na kufanya wanayoweza ili kuzipinga bali wasikae tu na kukubali kukandamizwa na kudhulumiwa.

Katika kutamatisha basi, riwaya za utafiti huu zinalenga kuwazindua Waafrika kuhusu ajenda tofauti za mataifa ya Ulaya zilizofichika. Kwa mfano, wanafaa kutambua na kukataa maenezi ya kasumba potovu kutoka mataifa ya Ulaya zinazolenga kuwadhalilisha. Aidha, wanafaa kuchukua misaada wanayopewa na mataifa ya Ulaya kwa uangalifu zaidi na kufanya kila jitihada za kuleta mabadiliko katika asasi mbalimbali ili kujiinua katika elimu na kupata ujuzi utakaowafaa kuendeleza uchumi wa nchi zao. Kwa jumla Waafrika wanafaa kuzinduka na kuwa katika mstari wa mbele kuchangia maendeleo ya nchi zao bali si kuubomoa wanapongojea kupangiwa miradi yao na mataifa ya Ulaya. Katika sehemu inayofuata, tumejadili simulizi inayohusiana na uhamiaji katika mataifa ya Ulaya athari zake.

### 3.4 Uhamiaji katika Nchi za Ulaya: Kiini na Changamoto Zake

Sehemu hii imejadili simulizi inayohusiana na suala la uhamiaji kama linavyojitokeza kwa kina katika riwaya ya *DY* na pia kutajwa kidogo katika riwaya ya *NZM*. Tumeangazia sababu ambazo hufanya watu kuhamia nchi za Ulaya pamoja na changomoto zinazoandamana na suala nzima la uhamiaji.

### 3.4.1 Sababu za Uhamiaji

Kwa kawaida, binadamu daima hutafuta namna ya kuyaboresha maisha yake katika kila nukta ya uhai wake. Hii ndio sababu watu husoma na kutafuta kazi au kuanzisha biashara ili kuweza kujiinua kiuchumi. Mbali na masuala ya kiuchumi, ukosefu wa usalama hupelekea watu kutafuta mahala tulivu na salama kama njia mojawapo ya kuyaboresha maisha yao. Ni katika ukweli huu ambapo suala la uhamiaji hutokea kama mojawapo wa njia za kuyaboresha maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018) uhamiaji ni hali ya kuingia nchi nyingine kwa kusudi la kukaa. Sehemu hii imeangazia sababu mahsusi zinazowafanya watu hutoka nchi zao, hususan nchi za Afrika, na kuhamia katika nchi za Ulaya, hususan Uingereza kwa kujikita katika riwaya za utafiti huu.

Kupitia kwa mhusika Mtima, riwaya ya *DY* imebainisha umaskini na ukosefu wa nafasi za kazi kama baadhi ya vyanzo vikuu vya watu, hasa vijana, kutaka kuzihama nchi zao na kwenda kutafuta maisha bora katika nchi za kigeni. Tunaona, kwa mfano, Mtima akilalamika kwa sababu ya ukosefu wa nafasi za kazi na hasa kwa vijana:

> Najua ulinikatalia kuja hapa kutokana na hofu yako kwamba na mimi ningekuwa kama Yungi. Hofu ya kuona vijana hatuna jingine la kufanya katika nchi yetu ila ubalaa. Uchungu wa kuona hata elimu yangu bure tu. Hata uhodari na ukakamavu wangu haukufaa. Makundi kwa makundi tuko mabarazani tunazembea. Nafasi za kazi zinachukuliwa na wageni waliojaa nchini. (uk 117).

Kama inavyodhihirika kwenye dondoo, vijana wengi sana hawajapata kazi. Kwa mfano, tunaelezwa kuhusu makundi ya vijana wanaokaa mabarazani wakizembea kwa sababu ya ukosefu wa kazi. Inavyobainika ni kuwa nafasi za kazi zipo lakini ‘zinachukuliwa na wageni waliojaa nchini’. Hii ina maana kuwa waajiri wanawapendelea wageni kuliko wenyeji, hata kama wenyeji wamesoma kama alivyokuwa Mtima. Huenda waajiri wakalaumiwa kwa kuwanyima wenyeji nafasi hizo na badala yake kuwapa wageni kama inavyojitokeza katika dondoo. Aidha, huenda

elimu wanayoipata wenyeji haijaweza kuwatayarisha katika utendakazi katika sekta mbalimbali. Ukosefu wa kazi kwa vijana hasa waliosoma umeongozeka katika enzi za kina Mtima, enzi ya K21. Hii ni tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo vijana waliosoma walihakikishiwa nafasi za kazi, kama anavyoeleza katika maneno yafuatayo ya Ndi-:

> Nami niliipanda [**ngazi ya elimu**] kwa hamu hadi kumaliza digrii yangu ya kwanza – Makerere College, kama ilivyokuwa ikiitwa wakati ule…Ari yangu ilikuwa kujiinua kimaisha nisiadhirike au kuupatisha taabu ukoo wangu kama tulivyopata taabu mimi na mamangu na babangu na mjomba Omari. Wakati ule, si leo, elimu ilikuwa ngazi ya kupanda kwendea maisha ya kipato. Angalau kipato wastani cha kujitosheleza. Mimi…nilkuwa tayari kujisabilia kwa yote kupata elimu. Aaaa, leo hata mtoto anajua kwamba elimu ni upuuzi mtupu. …hapa tulipo, kusoma na kutosoma ni sawa. Elimu haimhakikishii mtu chochote ila mizani za kupimia mambo akilini mwake. Hutegemea unatoka wapi. Unahusiana na nani. Una historia gani (*DY* uk. 15, 115). [msisistizo wetu]

Katika enzi za hapo awali, elimu ilikuwa kama ufunguo wa heri. Kwa mfano, Ndi- kwenye dondoo anasema kuwa katika enzi zao 'elimu ilikuwa ngazi ya kupanda kwendea maisha ya kipato' kuonyesha kuwa waliosoma waliweza kujiinua kiuchumi. Hii ni tofauti katika K21 ambapo tunaelezwa kuwa 'elimu ni upuuzi mtupu'. Yaani, vijana waliosoma kama Mtima hawaonekani kufurahia matunda ya bidii yao kwani hawana kazi.

Katika muktadha wa ubaadausasa, uhusiano kati ya elimu na nafasi za kazi katika K21 unalenga kuhakiki simulizi kuu kuhusu 'elimu kama ufunguo wa heri'. Kama tulivyotaja ni bayana kuwa elimu na matokeo mazuri katika mtihani katika K21 si hakikisho tena la kuishi maisha mazuri wala daraja la kuwa na mapato ya kujitosheleza. Hata hivyo, utafiti huu unayapinga mawazo kuwa elimu katika K21 ni upuuzi mtupu kwani, kama inavyojitokeza kwenye dondoo elimu inampa mtu 'mizani ya kupima mambo akilini mwake'. Kwa hivyo, elimu inapaswa kuwaandaa wanafunzi ili waweze kukabiliana na hali tofauti za maisha yao. Kile tunachoweza kukikosoa hata hivyo, ni

mfumo mzima wa kijamii ambapo nafasi za kazi zinatolewa kwa mapendeleo ambapo wageni wanapendelewa kuliko wenyeji. Aidha, kuna mapendeleo ya kiukoo ambapo nafasi za kazi zinatolewa kwa kuzingatia 'unahusiana na nani' wala hazizingatii 'elimu, akili au busara' (*DY* uk 16). Aidha, tunaweza kuulaumu mfumo wa elimu katika K21 ambao umeshindwa kuwapa vijana mbinu ishi za kukabiliana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo watu katika mataifa ya Afrika. Angalau kuweko kwa mbinu-ishi katika mitaala kunaweza kuwaandaa wanafunzi wake ili watafute njia mwafaka za kujiajiri au kuvumbua njia mpya za kupambana na hali tofauti zinazowakabili.

Ukosefu wa mbinu-ishi unawafanya vijana wengi kuteseka wanapokosa nafasi za kazi, licha ya kuwa wamesoma. Yungi katika *DY* ni mfano mzuri wa vijana kama hao. Analazimika kuingilia ukahaba ili kujikimu kimaisha, na hatimaye anaambukizwa magonjwa ya zinaa. Ni baada ya kutafuta matibabu ambapo anaacha ukahaba na kuanza biashara ndogo ndogo kama kufuma foronya, kutengeneza nywele na kuuza nguo za mitumba ambazo zinamsaidia kujikimu kimaisha (*DY* uk 150-151). Katika muktadha wa ubaadausasa, ukahaba na biashara za Yungi ni simulizi ndogo ndogo au njia mbadala ambazo wanaubaadausasa hupendekeza ili kukabiliana na changamoto zinazowapata wanajamii. Ingawa katika utamaduni wa Kiafrika ukahaba huchukuliwa kama tabia inayodhihirisha ukosefu wa maadili, kwa wanaubaadausasa suala la maadili halipaswi kuzingatiwa. Kila mtu anapaswa kuwa huru kutenda apendavyo. Uzuri au ubaya wa jambo hutegemea kuwepo kwa msingi au kitovu fulani kinachoelekeza maamuzi na matendo yetu, ambacho wanaubaadausasa hupinga. Kwa maoni ya utafiti huu, kutotilia maanani suala la maadili ndio udhaifu mkuu wa nadharia ya ubaadausasa. Kwa kuzingatia maoni haya, msimamo wa utafiti huu ni kuwa, ikiwa elimu ingemfunza Yungi ujasiriamali tangu alipotoka shuleni, huenda angeanza biashara ya kuuza bidhaa

zake ndogo ndogo mapema badala ya kubahatisha tu katika maisha, na huenda hangeingilia ukahaba. Kwa hivyo, ukosefu wa nafasi za kazi pamoja na ukosefu wa mafunzo ya mbinu-ishi ndio sababu kuu ya vijana wengi kutaka kuzihama nchi zao na kutafuta maisha bora katika nchi za ughaibuni. Mmoja wa vijana hao ni Mtima katika riwaya ya *DY* ambaye anahama kwenda Uingereza. Katika sehemu inayofuata tumeangazia changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wahamiaji.

### 3.4.2 Changamoto zinazoambatana na Uhamiaji

Wahamiaji wanaotoka nchi za Afrika kwenda nchi za ulaya hukumbana na changamoto chungu nzima. Changamoto hizo huanza wakati wanapojiandaa hadi wanapofika na kuishi katika nchi wanazozihamia. Katika sehemu inayofuata tumeangazia changamoto mbalimbali kama vile mahitaji ya kifedha, ukosefu wa kazi, ukosefu wa makazi na hatimaye kukumbwa na magonjwa.

### 3.4.3 Mahitaji ya Kifedha

Mojawapo ya changamoto zinazowakumba wahamiaji ni mahitaji ya kiasi kukubwa cha fedha katika maandalizi ya safari na hatimaye matunzo ya mtu binafsi punde tu baada ya kuwasili katika nchi yake mpya. Katika maandalizi, mhamiaji huhitaji fedha za kuwalipa wanaomsaidia kutafuta stakabadhi za usafiri pamoja na kumpa ushauri unaohusiana na safari yenyewe:

> …lakini sikuwacha kukumbuka mengi. Tokea matayarisho ya safari. Unampa mtu dala elfu nne. Hujui atakupatia viza au la. Unatakiwa uamini tu**.** Niliamini. Na kwa bahati nzuri nilipata viza ya uingereza. Nilikuwa nimesahau niliyoambiwa na wakala aliyenitayarishia safari hii ya ujanja ambaye nilimlipa dala za Kimarekani elfu nne. [dala elfu nne] ilikuwa akiba ya maisha yangu ya kudunduliza ambayo ilibidi kuisafisha. Nikifanikiwa nisifanikiwe pesa zimeshakwenda arijojo (*DY* uk 123, 80).

Kiasi cha pesa cha dala elfu nne za Kimarekani ni takriban shilling elfu mia nne za Kenya kwa wakati huu. Hiki ni kiasi kikubwa sana cha fedha kwa mwananchi wa

kawaida ambaye hana kazi ya maana katika nchi yake. Kwa mfano, Mtima anasema kuwa kiasi cha fedha kilichohitajika kuitayarisha safari yake kilimgharimu akiba yake yote. Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, mhamiaji huhitajika kulipa pesa hizo kabla ya maandalizi kuanza na hawezi kurejeshewa kamwe hata kama safari haitafanikiwa. Hii ina maana kuwa baadhi ya wale wanaotarajia kuhamia nchi za nje lakini wakakosa kufanikiwa kupata stakabadhi huishia kupoteza kiasi kikubwa sana cha fedha. Kwa mwananchi aliyepata mafunzo mazuri ya ujasiriamali akiwa shuleni, fedha kama hizi zinaweza kutosha kuanzisha biashara nzuri badala ya kufanya mchezo wa bahati nasibu ili kupata stakabadhi za kusafiri kwenda ughaibuni.

Fedha nyingine zinazohitajika katika maandalizi ya safari ni za kuonyesha ubalozi wa nchi unayotaka kuhamia, hususan Uingereza, kuwa anaweza kujikimu anapofika huko:

> …kwa bahati nzuri nilipata viza ya Uingereza – donge la dhahabu na ufunguo wa peponi. Hata hujui vipi wanaweza kupata viza kwa urahisi hivyo. Halafu uwe na pesa za kuonyesha, ingawa ungeweza kuazima kwa mtu. Nilionyesha dala elfu tano nilizoziazima kwa shoga yangu(*DY* uk 123).

Inavyobainika ni kuwa ubalozi wa Uingereza unafahamu fika kuwa baadhi ya watu wanaodhamiria kuhamia nchi yao hawana uwezo wa kuwa na kiasi hiki cha fedha. Kwa hivyo, wengi hulazimika kuazima kutoka kwa jamaa au marafiki zao, kama alivyofanya Mtima kutoka kwa shoga yake. Fedha hizi pia huwa ni kiasi kikubwa na huenda mhamiaji asipate mtu wa kumwazima. Kwa hivyo, tunaweza kukisia kuwa, fedha hizi hutumiwa na ubalozi wa Uingereza kama kizingiti cha kupunguza idadi ya wahamiaji wanaodhamiria kuhamia Uingereza. Kama inavyojitokeza, wahamiaji hujikakamua kwa ukucha na ujino kutafuta fedha zinazohitajika ili waweze kuipata viza ya Uingereza ambayo ni 'donge la dhahabu na ufunguo wa peponi'. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018) dhahabu ni madini yenye thamani kubwa ilhali peponi ni mahali patukufu ambapo waumini wanaofuata amri za Mwenyezi Mungu wataishi kwa

raha na kulipwa matendo yao. Kwa hivyo, kauli hii inaonyesha kuwa wengi huiona viza ya Uingereza kama kitu cha thamani sana kwa kuwa itawawezesha kuingia Uingereza, mahala penye raha na furaha. Hii ndio simulizi kuu ambayo imeshikiliwa na wengi na ambayo riwaya ya *DY* inalenga kuisali. Kama inavyodhihirika kwenye dondoo sio rahisi kwa mhamiaji kuipata viza hii bila usaidizi wa mawakala, ambao huweza kuipata kwa urahisi sana. Hii ndiyo maana Mtima anashangaa na kusema kuwa 'Hata hujui vipi wanaweza kupata viza kwa urahisi hivyo. Maneno haya ya Mtima huenda yanadhihirisha ulaghai unaofanyika kati ya mawakala na wafanyakazi katika ubalozi wa Uingereza unaowawezesha mawakala kuzipata viza vya wateja wao kwa urahisi huku wakiwapunja wahamiaji.

Isitoshe, mhamiaji huhitaji fedha zaidi za kumlipa wakili atakayebuni kisa kinachoeleza sababu za kutaka kuihama nchi yake na kwenda Uingereza pamoja na kumtetea atakapofika nchi yake mpya. Kama inavyojitokeza kwenye dondoo linalofuata, mchakato huu wa kubuni kisa huandamana na ulaghai mwingi pamoja na matumizi ya fedha zaidi: Aidha, kuandikiwa kwa kesi kama hii huandamana na kubadilisha uraia wa mkimbizi ili uafiki maelezo yaliyotolewa katika kesi yenyewe. Fedha zaidi za kununua cheti cha uraia wake mpya huhitajika. Mtima, kwa mfano, anatungiwa kisa kinachothibitisha namna maisha yake yalikuwa hatarini baada ya jamaa zake kuvamiwa na kuuawa, lakini yeye akabahatika kutoroka:

> Kuna namna nyingi za kuingia hapa. Unaweza kuja kihalali na kisha kuingia mitini – yaani unabadilisha jina lako, unabadilisha uraia wako, unabadilisha jinsi yako ya kuchukua jinsi ya watu wengine ambao wana haki ya ukaazi kwa ukimbizi. Si rahisi kama ninavyoeleza. Wengine ndio akina sisi. Tumeingia tayari tu Wasomali na jina langu Maryan Farah. Tena kuna ya hapa. Ununue cheti cha kuzaliwa cha u-Somali. Upate wakili wa kubuni na kukuandikia kesi yako. Wangu alibuni kisa cha hatari kwelikweli. Nyumbani mwetu tuliingiliwa na wauaji na wazee wangu na ndugu zangu wote waliuawa, lakini mimi niliwahi kukimbia. Msitu na nyika, msitu na nyika, mpaka Kenya (uk123). Baada ya miezi mitatu walikuja kunichukua tena kwa kishindo kingine. Nikapelekwa ofisi moja… nilimngoja wakili, lakini

> hakukutia mguu. Alinikimbia na kunirusha. Nilikwishamlipa pauni 700. Si pesa kidogo (uk 120, 121).

Kubuniwa kwa kesi zisizo za kweli kunadhihirisha ulaghai ambao mhamiaji hulazimika kujihusisha nao. Kwa mfano, kesi ya Mtima inaonyesha ukosefu wa usalama kama sababu kuu ya kuihama nchi yake na kwenda Uingereza. Kwa hakika, swala kuhusu ukosefu wa usalama haliwezi kuhusishwa na nchi ya Tanzania ambayo ndiyo mandhari ambapo riwaya ya *DY* imeandikwa. Kwa hivyo, lazima uongo na ulaghai zaidi utumike ili kisa kinachobuniwa kiweze kuafiki maelezo yanayotolewa kwenye kesi ya mhamiaji. Mojawapo ya ulaghai unaotumika ni kubadilisha uraia wa mhamiaji kwa usaidizi wa wakili wake. Mtima, kwa mfano anabadilisha uraia wake na kuwa mzawa wa nchi ya Somalia, ambayo kwa miaka mingi imejulikana kuwa na ukosefu wa usalama. Vilevile, analazimika kubadilisha jina lake na kuitwa ‘Maryan Farah’, ili lioane na majina ya Kisomalia. Kubadilisha uraia huandamana na cheti na kuonyesha uraia mpya ambacho humgharimu mhamiaji fedha zaidi. Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, kuandikiwa kesi pamoja na kununua cheti cha uraia mpya ndiko kulimgharimu Mtima pauni 700 ambazo ni takriban shilingi tisini elfu za huku Kenya kwa wakati huu.

Kama inavyobainika katika dondoo hapo juu, wahamiaji wanaoingia Uingereza kwa njia halali kama Mtima, hulazimika kuandikiwa kesi za hatari pamoja na kubadilisha uraia ili kuwafanya wawe wakimbizi ambao wana ‘haki ya ukaazi’. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018), mkimbizi ni mtu ajisalimishaye maisha yake kutokana na udhalimu wa mwingine kwa kukimbilia mahali pengine. Kwa hivyo, wakimbizi wanaonekana kuhurumiwa na kushughulikiwa kwa urahisi zaidi kuliko wahamiaji wengine wanaoingia Uingereza. Ili kuficha ushahidi wa uraia wake halisi, mhamiaji huwa ameshauriwa na wakala wake kuzichanachana stakabadhi zake zote punde tu anapoingia Uingereza:

> Tai likagusa lami hatimaye…Polepole, kama silo kabisa, likasogea kwenye domo la mvungu na tai la KLM likaegeshwa…Nilipoingia kwenye jengo la Heathrow nikakimbilia msalani…Nilikuwa nimesahau niliyoambiwa na wakala aliyenitayarishia safari…Haraka nikafungua mkoba na kutoa paspoti yangu na kuanza kuichana. Niliichana vipandevipande na kuvipiga flashi lindini (uk 79-80).

Ingawa kuichanachana paspoti kunalenga kuwasaidia wakimbizi kushughulikiwa haraka, mawakala huwa hawaambii wakimbizi ukweli kuwa paspoti hiyo inaweza kuwafaa na kuwasaidia kurudi kwao iwapo maisha huku Uingereza yatakuwa magumu au kinyume cha matarajio yao. Kama tulivyojadili katika sehemu inayofuata, ni bayana kuwa maisha katika nchi ya ugeni, hususan, Uingereza huwa na changamoto zake ambazo aghalabu huwafanya wengi kutamani kurudi kwao, lakini hawawezi kutokana na makosa ya awali ya kuzichanachana paspoti na kubadilisha uraia. Mojawapo ya changamoto ni ukosefu wa ajira.

### 3.4.3.1 Ukosefu wa Ajira

Ingawa wahamiaji wengi hutoka nchi zao kwenda ughaibuni kutafuta kazi, wengi hujipata hawana kazi licha ya juhudi nyingi walizotia ili kufika huko. Hali huwa ngumu zaidi hasa kwa wahamiaji ambao tayari wamebadilisha uraia wao na kupewa hadhi ya wakimbizi katika nchi walizozikimbilia. Tazama dondoo linalofuata ambapo Mtima anasimulia kuhusu masaibu ya ukosefu wa nafasi za kazi katika nchi ya Uingereza:

> Unaambiwa huruhusiwi kufanya kazi na sheria ya kutoruhusiwa ipo. Lakini hapana asiyejua kuwa kila mgeni hapa huja kutafuta kazi. Kila mtu ana maslahi yake – hatima na baadaye yake. Na jambo hilo maana yake ni kufanya kazi. Tena za nguvu na kututumuka kama mtumwa. Malipo mkia wa mbuzi. Huna bima, huna kitu chochote cha kukulinda. Shauri yako, si umetaka kuingia peponi? Kila siku huwaambia wenzangu…zamani tulikuwa watumwa kwa nguvu, leo tunajiuza wenyewe kwa hiari zetu. Na kazi za utumwa huwezi kupata mpaka uwe na nambari ya bima …Nilianza kutafuta kazi. Kwa muda wa miezi minane sikupata kazi yoyote; na kwa muda wa miaka minne sasa, sina kazi ila ya kufagia na kufuta mavumbi dukani. Kazi zilizopo ni chache na zinagombaniwa na kila mtu, wakiwemo Warusi na jamaa wa Ulaya ya Mashariki. Na hizi ni kazi za nguvu. Mwanamke ana nafasi ndogo ya kupata kazi, na sana ni za aina hii: kufagia, kutandika vitanda hotelini, kuosha vyombo, kupiga pasi… (uk 119,120,123).

Mojawapo ya kizuizi cha kupata kazi ni sheria zilizowekwa na utawala wa Uingereza kuhusu wahamiaji. Katika sheria hizi, wahamiaji hawaruhusiwi kufanya kazi hadi wapate nambari ya kuajiriwa, au nambari ya bima kama inavyorejelewa katika dondoo. Kuipata nambari yenyewe kunaweza kuchukua muda mwingi. Kwa mfano, Mtima hakufanikiwa kupata kazi kwa takriban miezi minane baada ya kuingia Uingereza, kumaanisha kuwa huenda ilichukua miezi hiyo minane kuipata nambari ya bima. Mbali na kuwepo na sheria hizi, inavyobainika ni kuwa kazi zenyewe ni duni kama vile kufagia, kuosha vyombo, kupiga pasi na kutandika vitanda hotelini miongoni mwa kazi nyingine kama hizo. Aidha, malipo yake ni 'mkia wa mbuzi' kumaanisha kuwa ni duni kama zilivyo kazi zenyewe. Isitoshe kazi hizi pia hazipatikani kwa urahisi hasa kwa wanawake. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa 'Kazi zilizopo ni chache…na mwanamke ana nafasi ndogo ya kupata kazi'. Hata kwa wale waliokuwa wamefuzu wakiwa nchini mwao, kama Mtima wanaishia kunga'ang'ana kuzitafuta na kuzifanya kazi hizi duni. Hii inaonyesha kuwa Waingereza hawaithamini elimu ya Mwafrika aliyoipata akiwa kwao. Huu ni ukoloni mamboleo ambapo Waafrika wanaotoka nchi zao wakiwa na matumaini makubwa ya kuyaboresha maisha yao ughaibuni wanaishia kutumikishwa na kufanyishwa kazi duni. Kama anavyosema Mtima, 'zamani tulikuwa watumwa kwa nguvu, leo tunajiuza wenyewe kwa hiari zetu'. Kauli hii ni thibitisho la namna ukoloni umechukua sura mpya; zamani Waingereza ndio waliokuja Afrika na kuwatumikisha Waafrika kwa nguvu lakini siku hizi Waafrika ndio wanaenda Uingereza kwa hiari yao kwa matumaini ya kuyaboresha maisha yao, lakini wanaishia kudhalilishwa na kutumikishwa. Ukosefu wa kazi bora unaandamana na changamoto nyingine kama ukosefu wa makazi.

### 3.4.3.2 Ukosefu wa Makazi Bora

Kutokana na sheria zinazowazuia wahamiaji kufanya kazi kabla ya kupata nambari ya bima, wahamiaji wengi huwa hawana makazi yao binafasi hasa katika miezi michache ya kwanza tangu kuwasili Uingereza. Hii ni kwa sababu wengi huwa hawana pesa za kugharamia kodi na hivyo basi hulazimika kuomba makazi kwa wenzao kabla serikali iwaandalie mahali pa kuishi. Katika dondoo linalofuata, Mtima anamwandikia babake baruapepe na kumsimulia kuhusu ugumu wa maisha yake miezi kadhaa baada ya kuwasili Uingereza:

> Bado sijapata pahala maalum pa kuishi…Nimo tu mpaka sasa nagaragara kwa wenzangu ambao kwa muda mfupi wameshanichoka. Sina budi lakini kung'ang'ania. Ndiyo maisha ya huko yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake…Ikizidi dakika moja ya kuwekwa na mtu nyumbani kwake, basi balaa. Unaikumbika ile nyimbo tuliyoimba shuleni? "Mgeni siku ya kwanza mpe mchele na panza…Mgeni siku ya kumi kwa mateke na magumi…" Lakini utafanyaje unapokuwa huna pengine pa kwenda? Unachuna uso. Unalazimisha mambo. Unajitia ukavu. Ndiyo maisha ya huko; kama unaweza kuyaita maisha. Nyumba nasikia nitapewa na 'mama' – yaani 'Malkia Elizabeth' (uk 7).

Wanaowapatia wahamiaji makazi wanachoka baada ya muda. Hii ni kwa sababu mhamiaji hachangii kwa vyovyote vile ili ajikimu au aikimu familia iliyompa makao. Hata mhamiaji anapofahamu fika kuwa hatakikani tena, analazimika kuwa na ngozi ngumu na kung'ang'ania kuishi humo. Hii ni hali inayomtamausha na kumkatiza tamaa mhamiaji aliyekuwa amesoma na kufuzu katika nchi yake, na aliyenuia kuyaboresha maisha ughaibuni. Katika sehemu inayofuata tumeangazia hali hii ya utamaushi na athari zake kwa wahamiaji.

### 3.4.3.4 Kukumbwa na Magonjwa

Kwa hakika maisha wanayopata wahamiaji wanapoenda nchi za ughaibuni, huwa tofauti kabisa na jinsi walivyokuwa wametarajia walipozihama nchi zao. Wahamiaji wengi hasa kutoka mataifa ya Afrika hufikiria kuwa watapata afueni watakapoenda

ughaibuni lakini ukweli ni kuwa maisha huwa kinyume chake kama inavyojitokeza katika maneno ya Mtima:

> Bila shaka mimi si katika wale niliodhania kwamba Uingereza ni 'the promised land' ambako watu wakifika tu watachuma matunda ya dhahabu. Si mimi; lakini kuna wengi waliofikiri hivyo kabla ya kuingia London. Mimi nilidhani tu kwamba mambo yangekuwa manyoofu na ningeweza kupata kazi ya heshima na kupata pesa zitakazonifaa katika maisha yangu baadaye nitakaporudi nyumbani. Lakini mara nilitambua kwamba nimeingia mtegoni. Hakuna kazi ya maana. Hakuna fedha. Hakuna kurudi nyumbani (uk 121).

Maneno, "The promised land" yanapatikana katika Biblia kurejelea nchi ya Kanaani yenye utele ambako Waisraeli waliahidiwa kuirithi baada ya kutoka Misri (Kumbukumbu la Torati 27:3). Hivyo basi, kuilinganisha Uingereza na Kanaani kunaleta fahawati ya mahali pazuri pasipo na changamoto zozote. Ingawa baadhi ya wahamiaji kama Mtima hawatarajii kuwa maisha ya Uingereza hayawezi kukumbwa na changamoto zozote, wengi hutaraji maisha ya afadhali zaidi kuliko ya kule walikotoka. Hata hivyo, uhalisia wa mambo unakuwa kinyume cha matarajio yao. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa Mtima anapata kuwa Uingereza 'Hakuna kazi ya maana. Hakuna fedha. Hakuna kurudi nyumbani'. Ukosefu wa maisha mazuri wanayotarajia wahamiaji ambayo yangetokana na kuwa na kazi nzuri na yenye malipo mazuri bila shaka ni mambo ya kukatiza tamaa. Zaidi ya hayo, hata nafasi ya kurudi nyumbani ambayo angalau ingemleta afueni mhamiaji pia haiko kutokana na makosa ya awali ya kuichana paspoti ya nchi yake asilia na kubadilisha uraia ili achukue hadhi ya mkimbizi. Hali hii ya utamauishi inaishia kuwaathiri wahamiaji kwa njia tofauti na baadhi hupatwa na magonjwa, yakiwemo yale ya msongo wa akili:

> Ndoto yangu haikuthibiti na moyo wangu ulijaa kibuhuti. Nilianza kukereka. Nilianza kuiona vingine London. Nilianza kumchukia kila mtu. Ingawa hapa kila mtu na lake na choyo na kuchukiana na kupikiana majungu na kufanyiana njama wenyewe kwa wenyewe ni jambo la kawaida… Vipi kwa mfano nitaipata nafuu niliyoijia kuitafuta Uingereza?... Sina budi kuboboja kukata tamaa kwangu. Maisha yameshanipa mgongo!... Kwa hivyo, ninaandika haya

> machache kabla sijala vidonge vya usingizi walivyonipa kupoza kiherehere changu. Hata hivi nisemavyo, nimo katika maruweruwe tu…mwezi wa sita sasa wamegundua naumwa na kiherehere ambacho wao wanakiita *‘depression’*…Kichwa changu kizito. Nimeshabugia vidonge vya dawa. Nikishameza vidonge huona vinanididimiza ardhi ya saba. Macho mazito kwa usingizi. Mdomo umefanya matende. Hata vidole navilazimisha tu… (uk 117, 118, 123, 124, 153).

Ugonjwa unaogandamiza akili au kama unavyorejelewa katika dondoo,‘*depression’* na ‘*kiherehere*’ kwa Kiingereza na Kiswahili mtawalia ni mojawapo ya magonjwa wanayoyapata wahamiaji hasa kutokana na hali ya utamaushi. Kama inavyojitokeza kwenye dondoo, Mtima aliugua ugonjwa huu kwa kuwa ndoto yake ya kuyaboresha maisha yake haikutimia wala hakuwa na njia yoyote ile ya kuitimiza, hali iliyomtamausha. Ili kuupoza ugonjwa huu, mwathiriwa hulazimika kutumia dawa ambazo huwa na madhara yake. Kwa mfano, Mtima anasema kuwa dawa zenyewe humpa usingizi na kufanya kichwa na macho kuwa mazito. Kwa mtu ambaye ana ugonjwa kama huu bila shaka hataweza kufanya kazi yake vizuri, na hata huenda akaipoteza hatimaye.

Katika kutamatisha sehemu hii imebainika kuwa Waafrika wengi wanaohamia nchi za ulaya huchochewa na mambo tofauti kama ukosefu wa kazi pamoja na lengo kutafuta maisha ya afadhali wanakohamia. Katika muktadha wa ubaadausasa basi, simulizi kuu inayoenezwa katika mataifa ya Afrika kuwa maisha ya Ulaya ni mazuri na rahisi si ya kweli na haiwezi kuaminiwa. Kama tulivyojadili katika sehemu hii, imabainika kuwa uhamiaji huambatana na changamoto chungu nzima kuanzia mahitaji ya fedha, ukosefu wa kazi na makazi na hatimaye magonjwa kutokana na utamaushi. Hii inalenga kuwazindua na kuwatahadharisha Waafrika kuhusu kufanya maamuzi ya kuhamia nchi za Ulaya bila kutathmini changamoto zinazoambatana na maamuzi hayo.

### 3.5 Hitimisho

Sura hii imejadili uchopekaji wa vipande vya simulizi kwa kujikita katika simulizi tatu kuu yaani, maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika na uhamiaji kutoka mataifa ya Afrika kwenda Ulaya. Katika sehemu ya kwanza tumejikita katika simulizi ya uhuru wa Mwafrika ambao umechukuliwa kama aina ya simulizi kuu kuambatana na maelezo ya Lyotard (1979). Kama simulizi kuu nyingine, uhuru ulipaswa kuleta afueni na matumaini kwa Waafrika waliokuwa chini ya ukoloni mkongwe; yaani, uhuru uliahidi kuleta haki, usawa na maendeleo. Hata hivyo, simulizi hii haiwezi kuaminiwa tena kwani matumaini yaliyoahidiwa na uhuru hayakuafiki. Badala yake, hali ya Mwafrika baada ya uhuru inaendelea kutawaliwa na ukosefu wa haki, ukosefu wa usawa, na ukosefu wa maendeleo kwa jumla. Kwa upande mmoja, ukosefu wa haki na usawa umedhihirika kupitia kwa viongozi waliojawa na tamaa, ubinafsi, ufisadi, ubadhirifu na kutojali. Viongozi hawa huendelea kujilimbikizia mali na kujitajirisha huku raia wakiendelea kufukarika. Jambo hili linachangia katika kuzidisha pengo lililopo kati ya matajiri na maskini. Kwa upande mwingine, raia wanachangia katika kuleta ukosefu wa haki na usawa kwa kukubali kutumiwa na viongozi kudhulumiana na kuangamizana. Aidha, kuna ukosefu wa maendeleo unaodhihirika kupitia ukosefu wa usalama, kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira, umaskini uliokithiri, ukosefu wa kazi na miundo misingi duni. Imebainika kuwa hali halisi ya Mwafrika katika ulimwengu wa sasa imeendelea kuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa punde tu baada ya uhuru. Kwa hivyo, ingawa wakoloni wanaweza kulaumiwa kwa kuweka misingi ya ubinafsi na kutojali, hali mbaya ya Waafrika baada ya uhuru inaweza kuhusishwa na Waafrika wenyewe, wawe viongozi au raia wa kawaida. Iwapo mabadiliko chanya yatatokea, wananchi wenyewe ndio wanapaswa kubadilika kwanza na kuacha ubinafsi, tamaa, ufisadi na aina nyingine za uozo.

Katika simulizi ya pili, tulijadili kuhusu ajenda za mataifa ya kigeni kwa mataifa ya Afrika pamoja na mbinu wanazozitumia kuendeleza ajenda hizo. Utafiti huu umebainisha kuwa, kwa mtazamo wa nje mataifa ya Ulaya huonekana kuyajali na hata kuyasaidia mataifa ya Afrika hasa kwa kutoa misaada na kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Hata hivyo, uhakiki wa simulizi hii umebainisha kuwa ufadhili unaotolewa kwa mataifa ya Afrika hulenga kuyanufaisha mataifa ya Ulaya. Kwa hivyo, mataifa haya huwa kama sarafu yenye pande mbili; upande wa huruma na upande wa maangamizi kwa lengo la kuweza kutimiza ajenda zao kwa njia iliyofichika. Ajenda hizo ni kama vile kutafuta soko la bidhaa zao, kutafuta uwanja wa kufanyia utafiti wa bidhaa na magonjwa mapya kama ukimwi na hatimaye kuyatawala kiuchumi mataifa ya Afrika. Ili kutimiza ajenda hizi, mbinu tofauti hutumika. Kwa mfano, wanaeneza kasumba potovu inayolenga kuwatukuza watu na bidhaa kutoka Ulaya huku ikiwatweza watu na bidhaa kutoka Afrika. Aidha, wanatoa misaada na kuanzisha miradi mbalimbali inayotumika kama chambo cha kufurahisha, kuchochea utiifu na kuteka fikra za watu wa mataifa ya Afrika ili wasitambue kwa urahisi ajenda za mataifa ya Ulaya na kuzisaili. Vilevile wanawekeza katika mataifa ya Afrika na kuunda sheria zinazolenga kuwanufaisha watu wa mataifa ya ulaya. Mataifa yanayopinga ajenda za mataifa ya Ulaya na kukosa kutii amri na masharti waliyowekewa yanawekewa vikwazo kama njia ya kuyaadhibu. Katika enzi hizi za utandawazi, vyombo vya habari vinatumika kueneza baadhi ya ajenda za mataifa ya Ulaya pamoja na kuueneza utamaduni wao unaorahisisha kutimizwa kwa ajenda hizi kandamizi. Hatimaye mataifa ya Ulaya yanafaulu katika kuyadhibiti na kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi na kitamaduni. Hata hivyo, imebainika kuwa mataifa ya Afrika pia yamechangia pakubwa katika kufaulu kwa ajenda hizi za mataifa ya Ulaya. Waafrika hivyo basi wanapaswa kutilia shaka simulizi inayohusiana na ajenda za mataifa ya kigeni barani Afrika kwa

mujibu wa mojawapo ya mihimili ya nadharia ya baadausasa kama ilivyoelezwa na Lyotard (1979). Badala yake Waafrika wanapaswa kuunda simulizi ndogo kwa kutafuta mbinu zitakazowawezesha kujishughulisha kikamilifu katika kuujenga uchumi wa nchi zao.

Katika simulizi ya tatu tumejadili kuhusu uhamiaji na athari zake. Tumeona wahamiaji wengi wanaotoka nchi za Afrika huenda nchi za Ulaya kutafuta kazi na maisha bora. Hii ni simulizi kuu inayoaminiwa na Waafrika wengi kuwa maisha katika mataifa ya Ulaya ni bora kuliko yale ya Mataifa ya Afrika. Hata hivyo imebainika kuwa wahamiaji hawayapati maisha hayo mazuri waliyoyatarajia. Badala yake wanapatana na changamoto nyingi kuanzia maandalizi ya safari hadi kwenye maisha yenyewe huko ulaya. Baadhi ya changamoto hizo ni mahitaji ya kiasi kikubwa cha fedha, ukosefu wa kazi na inapopatika huwa duni na yenye malipo duni. Hii huambatana na ukosefu wa makazi na hatimaye kupatwa na magonjwa kama msongo wa kimawazo kwa sababu ya kutamauka. Utamaushi unatokana na kutotimizwa kwa ndoto ambazo wahamiaji walikuwa nazo wakienda Ulaya, yaani, kuwa maisha yao yangekuwa afadhali. Aidha, makosa ya wahamiaji ya kuzichanachana paspoti zao asilia na kuchukua uraia mpya kama wakimbizi unakatiza ndoto yao ya kuwahi kurudi nyumbani tena. Kwa hivyo, wahamiaji wanaotoka Afrika huishia kuwa watumwa katika nchi za Ulaya. Kuambatana na mihimili ya nadharia ya ubaadausasa kama ilivyofafanuliwa na Lyotard (1979), simulizi inayohusiana na uhamiaji ili kutafuta maisha bora haiwezi kuaminiwa tena. Hivyo basi, Waafrika wanafaa kuzinduka na kutafuta njia mbadala za kukabiliana na hali zao ili kujikimu na kujiendeleza.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UHALISIA MAZINGAOMBWE

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inajadili matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mojawapo ya vipengele vya mtindo unaotambulisha riwaya za kibaadausasa. Lengo kuu la sura hii ni kubainisha namna matumizi ya mbinu hii ya kimtindo inazipa upekee riwaya za kibaadausasa na kuzitofautisha na riwaya nyingine zilizoandikwa kwa misingi ya kihalisia. Matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mtindo wa uandishi katika riwaya za kibaadausasa basi dhihirisho la ukiukaji wa kaida za uhalisia. Katika kutekeleza lengo hili sura hii imegawanywa katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa sura nayo sehemu ya pili imejadili kwa kifupi dhana na sifa za uhalisa mazingaombwe. Katika sehemu ya tatu tumejadili uhalisia mazingaombwe kama kipengele cha mtindo katika riwaya za kibaadausasa kwa kujikita katika riwaya za utafiti huu. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na matumizi ya binadamu wa kawaida wenye sifa za kiajabu, matumizi ya wahusika wa kiajabu na matendo na matukio ya kiajabu. Hitimisho la sura linapatikana katika sehemu ya nne.

## 4.1 Dhana na Sifa za Uhalisia Mazingaombwe

Wataalam mbalimbali wakiwemo Zamora & Faris (1995), D’haen (2005) na Waliaula (2010) wamekubaliana kuwa uhalisia mazingaombwe ni mojawapo ya mikondo katika mwondoko wa ubaadausasa. Akifafanua uhusiano uliopo kati ya ubaadausasa na uhalisia mazingaombwe, D’haen (2005) anaeleza kuwa baadhi ya sifa ambazo hubainisha matini za kibaadausasa pia hupatikana katika uhalisia mazingaombwe. Sifa hizo ni kama vile uanuwai au mseto wa vitu, mwingiliano matini, kuvuruga udhabiti wa wahusika na usimulizi, ufutaji wa mipaka kati ya vitu na hali tofauti pamoja na hali ya kutofuata kaida zilizozoeleka. Mwingiliano huu wa sifa huufanya uhalisia

mazingaombwe kuwa tawi mahususi katika mwondoko wa ubaadausasa. Aidha, D'haen (2005) anaeleza kuwa mvutano unaotokana na kuwepo na vipengele halisi na visivyo halisi (au vya kiajabu) katika matumizi ya uhalisia mazingaombwe huuunda simulizi-mseto au vipande vipande vya simulizi kwa wakati mmoja; simulizi ya kihalisia, simulizi ya kimazingaombwe na simulizi ya kihalisia mazingaombwe. Matumizi ya vipande vipande vya simulizi ni sifa kuu katika nadharia ya ubaadausasa.

Kwa mujibu wa Baldick (2008:194) uhalisia mazingaombwe ni istilahi inayotumika kurejelea "riwaya za kisasa ambazo hukiuka mipaka ya uandishi wa kihalisia. Pollheide (2003) na Goring n.w. (2010) nao wanasema kuwa mojawapo ya mhimili muhimu wa fasihi ya kibaadausasa ni kule kutokubaliana na wanamapokeo kuwa uhalisia ni kipengele muhimu cha kuifafanua riwaya. Mawazo ya wataalamu hawa yanadhihirisha kuwa wanaubaadausasa wanatumia uhalisia mazingaombwe kama mtindo wa kiuandishi kama njia mojawapo ya kukiuka kaida za wanamapokeo kuhusu maana ya riwaya. Kama tunavyofahamu, ukiukaji wa kaida zilizozoeleka ni sifa mojawapo ya nadharia za ubaadausasa. Ni muhimu basi kueleza kwa kifupi kuhusu mtindo wa uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia ili kubainisha ni nini hasa wanaubaadausasa wanachokikaidi katika riwaya hizo.

Waandishi na wahakiki tofauti kama vile Watt (2000), Wamitila (2002), Ntarangwi (2004) na Goring n.w. (2010) wanakubaliana kuwa uhalisia ni kipengele mojawapo ambacho wanamapokeo walitumia ili kuibainisha riwaya. Wamitila (2002:114) kwa mfano, anasema:

> Uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hivi kwamba haiwezekani kuizungumzia riwaya bila ya kuyarejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia.

Maelezo ya Wamitila hapo juu yanabainisha kuwa lazima riwaya za kimapokeo zingeandikwa kwa kutumia mtindo wa uhalisia ili zikubalike kuitwa riwaya. Uandishi

wa kihalisia uliandamana na sifa mbalimbali katika vipengele vyote vya fani kama vile ploti, wahusika, lugha, mandhari na urefu. Goring n.w. (2010) kwa mfano wanaeleza riwaya za kihalisia kama "bunilizi iliyosimuliwa kwa lugha ya kinadhari na ambayo ina urefu wa kadri na ambapo wahusika na matendo yao huwakilisha hali halisi ya maisha yanayowasilishwa kwenye ploti sahili au changamano."Forster (2002), Watt (2000) na Wamitila (2002) nao wanabainisha sifa zifuatazo za riwaya za kihalisia. Kwanza, katika riwaya za kihalisia wahusika, matukio na madhari yanapaswa kuoanana na uhalisia wa jamii husika. Kwa mfano, bunilizi hizi aghalabu hutumia wahusika watu ambao wanaweza kupatikana katika mazingira na hali halisi na hutambulishwa kwa majina halisi. Aidha, matukio na visa hupangwa kufuatia wakati na kwa njia ambayo chakula cha mchana huja baada ya chamsha kinywa, Jumanne baada ya Jumatatu, kuoza baada ya kifo na kadhalika. Mandhari nayo huwa ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii. Kinachobainika katika fasili hizi ni kuwa uandishi wa kihalisia huwiana na ukweli wa jamii husika kwa upande wa mandhari, wahusika na matendo yao.

Wamitila (2002) vilevile anasema kuwa riwaya ya kihalisia hulenga kufikia tamati au hitimisho ambapo suluhisho la matatizo yaliyojadiliwa linapatikana mwishoni mwa riwaya. Lengo kuu la riwaya hizi huwa ni kupata suluhisho na kudhibitisha kwamba kuna mshikamano katika jamii na kumhakikishia msomaji kwamba mifumo ya maadili na itikadi za kitamaduni bado zina mashiko katika jamii husika. Aidha, fasihi inafaa kufikiwa na kila mwanajamii na wala sio tu wasomi au watu wa tabaka la juu. Kwa hivyo, lugha ambayo hutumika pamoja na uteuzi wa msamiati unafaa kuelekea kwenye mtindo sahili.

Wanaubaadausasa wanatumia uhalisia mazingaombwe kama mtindo wa kiuandishi kama njia mojawapo ya kukiuka kaida za wanamapokeo kuhusu maana ya riwaya.

Lyotard (1979:81) akizungumza kuhusu wasanii wa kubaadausasa na kazi zao anasema:

> Msanii au mwandishi huwa kama mwanafalsafa: matini anazoziandika na kazi anazozibuni haziongozwi kamwe na kaida zilizowekwa tayari…wala hatuwezi kuhusisha kazi au matini fulani na kategoria zinazojulikana tayari. Kwa hivyo, msanii au mwandishi anafanya kazi yake bila kuongozwa na kaida au sheria yoyote ile, ili aweze kuunda kaida za kile ambacho tayari atakuwa amekiandika.

Uandishi wa riwaya kwa kutumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe basi ni njia ya kimajaribio ya wanaubaadausasa ya kuunda kazi zao bila kuongozwa na kaida za awali zilizojikita katika uhalisia. Na kama anavyosema Lyotard (1979) kuwa ubaadausasa husaili mamlaka ya simulizi kuu, vivyo hivyo uhalisia mazingaombwe husaili mamlaka ya uhalisia na hivyo basi kudhihirisha kuwa uhalisia mazingaombwe ni mtindo wa kiuandishi katika nadharia ya ubaadausasa. Aidha, uhalisia mazingaombwe ni ishara ya mabadiliko katika uwanja wa fasihi kuambatana na maneno yafuatayo ya Lyotard (1979: xxiii) akieleza kuhusu dhana ya ubaadausasa:

> [Ubaadausasa] hurejelea hali ya utamaduni uliyopo kwa sasa ambao, tangu mwisho wa karne ya kumi na tisa, umebadilika na kubadilisha kaida zilizozoeleka za kutenda mambo katika uwanja wa sayansi, fasihi na sanaa.

Ni bayana kuwa fasihi, hususan riwaya ya Kiswahili ya K21 imedhihirisha mabadiliko mengi, na matumizi ya uhalisia mazingaombwe ni dhihirisho la mabadiliko hayo. Kama anavyosema Khamis (2005), baadhi ya mambo yanayodhihirsha upya katika riwaya ya Kiswahili ya K21 ni matumizi ya uhalisia mazingaombwe pamoja na vipengele vingine vya kimtindo kama vile matumizi ya vipande vipande vya simulizi, ploti zisizokamilika au zisizohitimishwa na usimulizi ambao hauonyeshi wazi kichocheo au kiini cha usimulizi huo. Katika sehemu inayofuata, tumejadili baadhi ya sifa za uhalisia mazingaombwe kwa kurejelea wataalamu mbalimbali na namna zinavyokaidi uandishi unaotumia mtindo wa uhalisia.

Kwa mujibu wa Salenius (2009) wahakiki hawajaweza kukubaliana kikamilifu kuhusu sifa bainifu za uhalisia mazingaombwe. Hata hivyo, kuna sifa ambazo aghalabu hurejelewa mara kwa mara kama vile kuwepo kwa mambo na matukio yasiyo ya kawaida na ambayo hukinzana na kaida zilizozoeleka za kuutazama na kuueleza uhalisia. Hivyo basi ili kuelewa uhalisiamazingaombwe, ni muhimu kuzitambua baadhi ya sifa za uhalisia mazingaombwe kwa kujikita katika kazi ya fasihi, hususan riwaya ya Kiswahili.

Baldick (2008:194) anaelezea uhalisia mazingaombwe kama istilahi inayotumika kurejelea "riwaya za kisasa ambazo hukiuka mipaka ya uandishi wa kihalisia kwa kutumia vipengele vya ngano, hekaya na visasili na wakati huo huo kuweza kuangazia maisha katika jamii ya kisasa". Katika kuwawakilisha wahusika Baldick (2008) anasema kuwa riwaya zenye vipengele vya uhalisia mazingaombwe huwapa wahusika wao sifa za kifantasia kama vile uwezo wa kupaa na kuelea angani, uwezo wa baadhi ya wahusika wa kuweza kuwasoma wengine (telepathia) pamoja na uwezo wa kuunda au kubomoa vitu kwa nguvu za kiungu.

Kwa mujibu wa Waliaula (2010:4), "Uhalisia mazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadri fulani, kama mkabala wa kuuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha". Kinachobainika kutokana na fasili hii ni kwamba uhalisia mazingaombwe huchanganya vipengele vya uhalisia na umazingaombwe. Sifa hizi za uhalisia mazingaombwe zimejitokeza katika riwaya zote nne za utafiti huu, lakini kwa njia tofauti. Katika uwakilishaji wa wahusika, baadhi ya wahusika ni binadamu wa kawaida ambao wanatenda mambo kwa njia isiyo ya kawaida, ilhali wahusika wengine sio binadamu wa kawaida bali viumbe vya ajabuajabu kama vile mizuka na vivuli.

Zamora na Faris (1995) nao wanaeleza kuwa uhalisia mazingaombwe hudhihirika katika bunilizi yoyote kupitia matumizi ya mizuka (ghosts), jambo ambalo huwezesha kuwepo kwa muungano wa mambo au mifumo, ambao haungewezekana katika aina nyingine ya bunilizi. Kwa mujibu wa Salenius (2009) mojawapo ya sifa za uhalisia mazingaombwe ni kuwepo kwa mambo na matukio ya kimiujiza na ambayo hukinzana na kaida zilizozoeleka za kuutazama na kuueleza uhalisia. Strecher (1999) naye anasema kuwa uhalisia mazingaombwe hudhihirika wakati mandhari halisi huingiliwa na jambo la kiajabu na ambalo haliwezi kuaminika kwa urahisi katika ulimwengu halisi. Bowers (2004) anaeleza kuwa uhalisia mazingaombwe hujitokeza wakati vipengele vya mambo halisi, mambo ya kufikirika au ya kimiujiza huwasilishwa kwa pamoja kana kwamba yanawasilisha uhalisia. Fasili hizi basi zinabainisha kuwa uhalisia mazingaombwe hujikita katika uhalisia, lakini kwa namna ambayo uhalisia huo umepita mipaka ya kile kilichokubalika kama halisi.

Bowers (2004) na Waliaula (2010) wanakubaliana kuwa uhalisia mazingaombwe hujitokeza wakati vipengele vya mambo halisi na vya kimiujiza huwasilishwa kwa pamoja kana kwamba yanawasilisha uhalisia, hivyo basi kuziba mipaka ya wazi kati ya vipengele hivi. Waliaula 2010:143) akimnukuu Abrams (1999) kwa mfano, anaeleza yafuatayo kuhusu waandishi wanaotumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe:

> Waandishi hawa husukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yanayotokana na visaasili na hekaya.

Kinachobainika hapa ni kuwa uhalisia mazingaombwe hutumia vipengele vya uhalisia sambamba na vile vya kifantasia au vya kindoto, au vipengele vinavyotokana na visaasili na hekaya za jamii fulani, hivi kwamba hakuna mipaka ya wazi kati ya vipengele hivi. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza katika riwaya za utafiti

huu ambayo yanaambatana na maelezo ya Baudrillard (1981) ambayo yametumika kama mojawapo ya mihimili ya nadharia ya ubaadausasa katika utafiti huu.

Baada ya kutalii fasili za wataalamu mbalimbali kuhusu dhana na sifa za uhalisia mazingaombwe, utafiti huu umeufasiri uhalisia mazingaombwe kama mtindo wa kuiandishi wa riwaya za kibaadausasa unaoenda kinyume na kaida za kimapokeo za uandishi uliojikita katika uhalisia. Mtindo huu wa uhalisia mazingaombwe hutumia vipengele vya uhalisia unaoenda sambamba na vile vya umazingaombwe au vya kindoto. Vipengele vya umazingaombwe hubainishwa kupitia matukio ya kiajabu, viumbe wa kiajabu kama vile mizuka pamoja na kuwepo na binadamu wa kawaida wenye sifa na uwezo wa kiajabu. Sifa hizi ndizo tumejadili katika sehemu inayofuata kwa kujikita katika riwaya zilizotafitiwa.

## 4.2 Uhalisia Mazingaombwe katika Riwaya za Utafiti

Riwaya zilizotafitiwa zimedhihirisha upya kutokana na matumizi ya vipengele vya uhalisia mazingaombwe kama dhihirisho la mtindo wa kipekee wa uandishi wa kibaadausasa. Katika sehemu hii tumejadili namna uhalisia mazingaombwe hudhihirika kupitia binadamu wa kawaida lakini wenye uwezo wa kiajabu, matumizi ya viumbe wa ajabu na matumizi ya matukio ya ajabu.

### 4.2.1 Binadamu wa Kawaida wenye Uwezo wa Kiajabu

Mojawapo ya sifa za umazingaombwe hujikita katika uwakilishaji wa wahusika kwa kutumia binadamu wa kawaida wenye uwezo wa kiajabu. Uwakilishaji huu umejitokeza katika riwaya za *NZM* na *DY*. Katika riwaya hizi binadamu wa kawaida wamepewa uwezo wa kuwasoma na kuwajua wahusika wengine bila kutumia njia za hisia za kawaida kama vile kuona, kugusa, kunusa na kadhalika. Katika riwaya ya *NZM*

mhusika Nana anawaingia na kuwasoma washindani wenzake waliokuwa wamefika kwa mashindano ya waimbaji chipukizi katika mkahawa ulioitwa *Hoteli Selwa*:

> Niligeuka kulia kuwatazama washindani wenzangu, lakini kipembe changu cha mwono kilikuwa kimebainika. Ikanibidi ghafla nitoe bongo langu nje. Nikaenda kulining'iniza juu, mbele ya wale washindani wangu walioketi pale. Nikaanza kumwingia ndani mmoja baada ya mwingine. Aaa, usishangae. Mimi nimeshajifunza mbinu nyingi kuumudu wakati wa kuruka. Hii ndiyo hatua pekee siku hizi ya kuweza kumpiku mwenzako. Lazima umwingie ndani kumjua yeye nani, ana ufundi gani, na uwezo upi utakaolekea kushinda au kushindwa. Nilianza kumwingia ndani mmoja mmoja. Nilisikiliza sauti zao zikiimba kimyakimya, nikakadiria kuwa hakuna sauti ambayo ingeweza kutia fora mbele ya yangu. Nilipima mizani ya kuthubutu kwao, nikatambua kuwa hapana ambaye angeweza kuifunika heba yangu. Wote walikuwa na wasiwasi na mimi. Hawakunijua tokea zamani, hawanijui hivi sasa. Na mimi sikuwajua tokea zamani, lakini nawajua mpaka ndani ya hisia zao hivi sasa (*NZM* uk. 140-141).

Nana anadhihirisha uwezo usio wa kawaida wa kuingia ndani ya wahusika wengine na hata kuzisikia sauti zao zikiimba licha ya kuwa wahusika hao hawakufungua vinywa vyao kuimba. Aidha, anapousikiliza uimbaji wao ana uwezo wa kuujua ufundi walionao na kuelewa bayana kuwa hakuna hata mmoja ambaye angeweza kumpiku. Inavyobainika pia ni kwamba sio wahusika wote walio na uwezo kama huu wa Nana. Kwa mfano, Nana anasema kuwa washindani wenzake hawakuweza kumjua au kumsoma, lakini yeye aliwaingia na kuwasoma wote waliokuwepo. Ingawa Nana anaonekana kama binadamu wa kawaida, uwezo huu wake unadhihirisha uhalisia uliochanganywa na umazingaombwe katika muktadha mmoja hivyo kufuta mipaka ya wazi kati ya hali hizi mbili, ambayo ni sifa mojawapo ya ubaadausasa.

Hali sawia na hii inadhihirika katika *DY* kupitia mhusika Bisudi. Akiwa na umri wa miezi mitatu tu, Bisudi anaweza kufahamu mambo ambayo hajaelezwa na mtu yeyote. Pia ana uwezo wa kuzungumza na hata kusoma vitabu, jambo ambalo si la kawaida

katika ulimwengu halisi. Sifa hizi za Bisudi zinafafanuliwa Bi M, mamake Bisudi, akimweza Ndi- aliyekuwa babake Bisudi:

> Ndivyo kilivyo…kitoto cha kimiujiza…sura yake ni kama yako…lakini sura yake pia ni sura ya kila mtu. Sura yake inabadilikabadilika kama kinyonga. Na mambo si hayo tu…Jana nilikiweka chini juu ya kifarsha chake, kufumba na kufumbua nikakikuta kimebingirika mpaka jikoni nilikokuwa nikichoma maandazi…Juzi, juzi ya kijomba, nilisikia kama kinaniita – "Mama, mama, yu wapi baba?" Nikashtuka. Kitoto cha miezi mitatu kitawezaje kusema? Kitawezaje kuuliza na kumtaka babake? Nikaona labda njozi zangu mwenyewe tu. Lakini usiku nilipokuwa nikikilaza, mara kilitaka kitabu, nikakipa, kikawa kinasoma. Mwisho wa kusoma nilikisikia kinasema tena maneno yaleyale. Na tena kikaongeza, "Najua baba kafungwa. Najua kasingiziwa kuua na wazimu bure, lakini mimi nitakuja kumkomboa siku moja. Nitamkomboa kila mtu!" (*DY* uk 196-197).

Tunaona uhalisia na umazingaombwe ukienda sambamba katika maisha ya Bisudi. Mbali na kuwa na uwezo wa kuzungumza na kusoma akiwa na umri wa miezi mitatu, Bisudi anaelewa kuwa babake amefungwa na kufungwa kwake hakukutekelezwa kwa misingi ya haki. Hii ndio maana anaahidi kumkomboa babake na wote ambao hawajatendewa haki. Katika muktadha wa ubaadausasa, Bisudi ametumia kudhihirisha ukosefu wa mshikamano wa jamii katika ulimwengu wa sasa, hasa katika mataifa ya Afrika ambapo haki za wengi hukiukwa. Kama ilivyo muujiza kupata kitoto kama Bisudi katika ulimwengu halisi, vivyo hivyo ndivyo ilivyo vigumu kupatikana kwa ukombozi kamili katika mataifa mengi ya Afrika, hasa kuhusiana na ukiukaji wa haki miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, Ndi- anafungiwa kwa seli bila hatia. Aidha, mwandishi amemtumia Bisudi kimaksudi kama kielelezo cha mapindizi yanayohitajika ili kuleta mshikamano wa kijamii. Mapinduzi haya hata hivyo yapo katika hatua zake za awali kabisa, jinsi kitoto Bisudi kilivyo kichanga, na huenda yakachukua muda ili kufikiwa kikamilifu.

Hali nyingine ya umazingaombwe inahusu uwezo wa baadhi ya wahusika wa kuona mambo yaliyo katika ulimwengu wa kiroho. Kwa mfano, katika *NZM* Nana na Bi Mau wana uwezo wa kuona mambo ambayo yangekuja kutendeka baadaye. Isitoshe Bi. Mau ana uwezo wa kuona na hata kuzungumza na vizuu na mizuka:

> Kila mtu hapo mtaani alikuwa akitambua kwamba Bi. Mau ameolewa na jini au ruhani. Na jini hilo limemchunuka mno Bi. Mau, na kwa sababu Bi. Mau amekuwa akilitii jini hilo kama si kuliabudu, basi jini hilo limemfunza mambo fulani ya maana. Moja katika mambo hayo ni kumfunulia miujiza ambayo binadamu wa kawaida hawawezi kuiona. Ndilo hilo jini linalosemekana kumwonyesha yeye Bi. Mau mambo ya vizuu na mizuka yanayotokeza ndani humo. Nani kwa hivyo, ndani ya nyumba hiyo asiyetambua uwezo wa Bi. Mau wa kuona visivyoonekana? Au nani aliyeweza kuthubutu uwezo wake wa kutabiri yasiyotabirika? Mara ngapi hapo nyuma yeye alikwisha tambua kuwa siku moja kitukuu chake kingerejea kuishi kwao licha ya Bw. Hila kikizuia kisikaribie nyumbani humo. Na leo si hiki kitukuu chenyewe kimekuja… (*NZM* uk. 174).

Tunaelezwa kuwa Bi. Mau alibashiri kuwa siku moja angeishi na kitukuu, Nana, jambo ambalo lilikuja kutimia. Uwezo huu wa Bi. Mau unatokana na jini lililomuoa. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI jini ni kiumbe asiyeonekana, asiye shetani wala pepo. Jini hili vilevile linamwezesha kupenya katika ulimwengu wa kiroho ambapo anaona na kuzungumza na vizuu na mizuka. Matumizi ya majini, vizuu na mizuka katika maisha ya Bi. Mau yanadhihirisha umazingaombwe unaoenda sambamba na uhalisia.

Nana, kitukuu chake Bi. Mau, pia ana uwezo wa kuingia katika ulimwengu wa kiroho, aliourithi kutoka kwa Bi. Mau (uk. 174). Uwezo huu unawawezesha wote wawili kupatana katika ulimwengu wa kiroho wakijaribu kujielewa na kuwaelewe wenzao katika nyumba yao. Aidha, akiwa katika ulimwengu huu wa kiroho, Nana anakutana na vivuli vya wanawake tofauti na kuzungumza navyo jinsi binadamu wa kawaida wanavyoweza kuwasiliana. Kwa mfano, anakutana na vivuli vya Mwanamkuu, Hawa na Maskati ambao wanalalamikia kwa sababu ya dhuluma wanazozipitia kwa sababu ya jinsia yao, kama vile kubakwa, ndoa za kulazimishwa, kutalikiwa bila sababu na

kadhalika. Mwanamkuu kwa mfano analalamika kwa sababu ya kubakwa na anakutana na Nana na Bi. Mau katika ulimwengu wa kiroho ili kumfariji. Tunaelezwa yafuatayo kuwahusu:

> Leo kivuli cha kwanza anachokiona Nana, ni cha Mwanamkuu. Kinahaha na kupaparika kama kuku anayetafuta mahala pa kutaga na kuotamia. Kiliibuka chumbani, kule Mwanamkuu anakolala. Huku kilianza kwa kuanua mashuka kitandani, na kupangua mito godoroni…Mara nyingine kilisikilizana kikisaili: “U wapi? U wapi?”...Nana alipokisogelea kivuli cha Mwanamkuu, ghafla kilikuja kumvaa na kumkumbatia. Kikaangusha kilio kikubwa kilichomwaga mvua ya machozi. “Unatafuta nini Mwanamkuu?” aliuliza umbea Nana. “Natafuta n’nachotafuta milele, kile ambacho nilinyanganywa nilipokuwa kitoto kidogo na mjomba wangu.”…Hapo tena Bi. Mau hufika hima kumsaidia Nana kukiinua kivuli cha Mwanamkuu ili kukipoza. Na Mwanamkuu hupata nafuu… (*NZM* uk. 178/9).

Mbali na kuwa Nana na Bi. Mau ni wahusika wenye mashiko ya uhalisia, wana uwezo wa kusafiri masafa marefu katika ulimwengu wa kiroho, ingawa miili yao haibanduki mahali ilipo katika hali halisi. Kwa mfano, katika dondoo hapa juu tunaelezwa kuwa wako nyumbani kwao lakini wanasafiri katika ulimwengu wa kiroho hadi chumba cha kulala cha Mwanamkuu na hata kuanza kuwasiliana naye. Uwezo huu wa Nana na Bi. Mau umepita mipaka ya uhalisia kama tunavyoujua, na hivyo kuingia katika tapo la uhalisia mazingaombwe. Mbali na kuwapa binadamu wa kawaida uwezo uliokithiri mipaka ya uhalisia, mwandishi ametumia wahusika wa ajabu ajabu kama vivuli, mizuka, vifuu na kadhalika. Matumizi ya wahusika hawa wa ajabu yamejadiliwa katika sehemu inayofuata kama kiwakilishi cha uhalisia mazingaombwe katika riwaya za utafiti huu.

### 4.2.2 Matumizi ya Wahusika na Matukio ya Ajabuajabu

Riwaya zilizotafitiwa zimetumia wahusika wa ajabu ajabu wanaowakilisha binadamu halisi katika ulimwengu halisi lakini kwa njia iliyokiuka uhalisia. Mojawapo ya wahusika kama hao ni vivuli. Vivuli sio watu walio na mwili kama binadamu wa

kawaida, namna ambavyo wahusika katika riwaya za kihalisia wanavyohitajika kuwa. Badala yake hawa ni wahusika wa kuhisika tu lakini wanaowakilisha hali halisi ya maisha. Katika *NZM* na *DY*, vivuli wanapatikana katika ulimwengu wa kiroho na ulimwengu halisi mtawalia. Katika *NZM*, sio binadamu yeyote anayeweza kuona au hata kuwasiliana na vivuli bali wale tu wenye uwezo wa kupenya katika ulimwengu wa kiroho kama Nana na Bi. Mau. Katika ulimwengu huu wa kiroho, watu halisi kama Nana na Bi. Mau pia hubadilishwa na kuwa vivuli ili waweze kuwasiliana na vivuli vyenzao. Kwa mfano, tunapata mawasiliano kati ya vivuli vya Nana, Bi. Mau na Hawa, baada ya kitoto cha Hawa kuuawa kinyama, kwa sababu kilizaliwa nje ya ndoa. Nana na Bi. Mau wanajaribu kumtuliza Hawa baada ya kitendo hiki cha kikatili:

> "Nyamaza… Nyamaza…" Kivuli cha Nana na cha Bi. Mau vilikipoza kile kivuli cha cha Hawa kwa huzuni.
>
> "Mpaka lini?" Kiliuliza kivuli [cha Hawa] ndani ya kilio na kwikwi.
>
> "Mpaka kila mtu atakapofahamu, mpaka sheria zitakaposimamishwa kututetea na kutulinda," kivuli cha Nana kilihakikisha (*NZM* uk. 180).

Ingawa mwandishi ametumia vivuli katika dondoo hili, vivuli hivi katika muktadha huu vimetumika kuwakilisha hali halisi ya maisha ambapo wanawake wanadhulumiwa kwa sababu ya jinsia yao. Wanawake hawapewi nafasi ya kupinga matendo ya kikatili kama aliyotendewa Hawa. Sheria nazo haziwatetei wala kuwalinda wanawake, hivyo kudhihirisha ukosefu wa haki katika jamii. Katika muktadha wa ubaadausasa kisa hiki cha Hawa kinaonekana kuihakiki nafasi ya sheria za nchi katika kulinda na kutetea haki za raia wake, hasa wanawake. Aidha, kinaonyesha namna ukosefu wa haki husababisha ukosefu wa mshikamano katika jamii, kwa maana baadhi ya wanajamii hupendelewa huku wengine wakipuuzwa.

Matumizi ya wahusika ambao ni vivuli vilevile yanapatikana katika riwaya ya *DY*. Tofauti na ilivyo katika *NZM*, vivuli hivi vinaishi katika ulimwengu halisi na ndio

maana Ndi- anasema anapishana navyo kila mara anapotoka nje. Hata hivyo, kama ilivyo katika *NZM*, vivuli hivi havionekani kwa macho bali vinahisika tu. Kwa mfano Ndi- anasema namna anavyopatana na vivuli vya watu wengi, anavyovijua na asivyovijua:

> Sasa nikitoka nje, hupishana na vivuli. Sikuviona hasa kwa namna ya mtu anavyoona vitu vya mashiko. Nishai labda. Magube. Mazingaombwe! Nilihisi aina fulani ya mapito kama mazigazi. Kama sarabi. Hisia majimaji ya vivuli vya watu vinavyoambaa…bado ingawaje, nilibaki na uwezo fulani wa kukihisi kivuli kipi kilikuwa cha nani, iwapo mtu hakuwa mgeni kwangu. Nadhani na mimi watu wengine waliniona hivyo hivyo. Kivuli tu! Wale waliokuwa wapembuzi bila ya shaka. Hii haina maana kwamba hakukuwa na watu, watu. Walikuwepo, wachache ingawaje… (*DY* uk. 28-29).

Katika *DY*, vivuli vinawakilisha hali ya utupu baada ya kuporomoka kimaisha kwa baadhi ya wanajamii kama Ndi-. Awali, Ndi- alikuwa mtu mwenye nafasi katika jamii lakini hatimaye akaporomoka kimaisha. Kwa mfano alikuwa amesoma hadi chuo kikuu, aliwahi kuwa mwalimu mkuu katika shule za sekondari na pia karani katika ngazi za juu serikalini (*DY*, uk 15-16). Nyakati hizo alikuwa anaipata riziki yake kwa urahisi lakini kwa sasa hali imebadilika. Aibu inayotokana na kuporomoka huku inamfanya ajifungie katika chumba chake na kutoka nje kwa nadra sana. Ingawa Ndi-ni binadamu halisi, tunaelezwa katika dondoo hapo juu kuwa huenda watu wengine walimwona kama kivuli tu, kumaanisha kuwa, waliuona utupu ndani ya maisha yake kwa sababu ya kuporomoka kimaisha, hivi kwamba inamuia vigumu hata kupata riziki (*DY* uk. 22).

Kando na yeye, Ndi- anaonyesha hali hii ya utupu kupitia vivuli vingine alivyopatana navyo njiani. Mojawapo ya kivuli anachokifamu ni cha mwalimu wake wa zamani aliyekuwa mfano wa kuigwa lakini baadaye akalipaka jina lake tope kwa kufanya matendo yasiyo ya haki (uk 30-31). Aidha, anakutana na kivuli cha Vuai Mapozi aliyekuwa mtu mkubwa katika Wizara ya Habari lakini baadaye akafukarika. Hatimaye

anakutana na kivuli cha Daudi aliyetoka katika ukoo wa kitajiri lakini akaporomoka na kuwa maskini hohehahe. Hawa wote walikuwa watu waliokuwa na nafasi zao hapo awali, lakini wameporomoka kimaisha na utukufu waliokuwa nao hapo awali hauonekani tena, unahisika tu kwa mbali. Hivyo basi maisha yao ya sasa ni kama kivuli tu cha maisha yao ya awali.

Uhalisia mazingaombwe vilevile unajitokeza wakati wahusika wafu wanahuishwa na kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu halisi katika mazingira halisi. Kwa mfano, katika riwaya ya *NZM* Bimkubwa aliyekuwa amekufa miaka kadha iliyokuwa imepita anamjia mtoto wake, Nana, aliyekuwa hai na kuonyesha mapenzi yake kwake, jinsi ambavyo angefanya kama angekuwa hai:

> …Bimkubwa mamake, ndiye aliyemjia bintiye Nana hapo alipoganda….Alikuja tu akaketi naye sako kwa bako, pachapacha. Akanyoosha mikono yake kumshika kichwa chake na kukiinamisha mpaka kikagusa midomo yake ambayo ilibusu kipaji chake…alimtazama Nana kwa muda mrefu huku yeye mama mtu akikifululiza kicheko kisichokatika. Baadaye, Bimkubwa alitoa ziwa lake lililojaa na kulitia kinywani mwa binti yake….Wakati huu mama mtu alikuwa kiumbe kamili: si maiti, si mzuka. Ni Bimkubwa aliye hai, kiumbe kamili kisicho na ishara ya ufu (uk. 284-285/9).

Kama tunavyoelezwa kwenye dondoo, Bimkubwa anamtokezea binti yake kama kiumbe halisi wala si kama mfu au mzuka. Anatenda kama binadamu wa kawaida anapoenda kuketi karibu na bintiye, anamshika kichwa na kumbusu, anacheka na hatimaye kumnyonyesha Nana. Tunaelezwa kuwa Bimkubwa anamjia Nana mara kadhaa katika hali hii. Kwa mfano, anamjia Nana na kumpongeza kwa kuupigania uhuru wake kama mwanamke (uk. 285), na wakati mwingine anamjia kumwonya dhidi ya kuolewa kutokana na dhuluma mbalimbali anazoweza kupatana nazo kama mwanamke katika ndoa (uk.286-289). Anamsimulia Nana kisa chake mwenyewe kuhusu dhuluma alizozipitia katika maisha yake ya ndoa pamoja na mahusiano yake na wanaume mbalimbali. Uwezo huu wa wafu wa kuweza kutenda kama binadamu halisi

katika mazingira halisi unadhihirisha umazingaombwe unaoandamana na uhalisia katika riwaya hii.

Baadhi ya wahusika wa ajabu ajabu wanachukua sura za binadamu kwa kiasi fulani lakini kwa namna ambayo imekiuka uhalisia. Kwa mfano, katika *DY* kuna mhusika anayechukuwa maumbile tofauti tofauti, yawe ya binadamu au ya wanyama na kutenda vitendo vya ajabu kama anavyoeleza Ndi- katika dondoo linalofuata:

> Sikujua la kufanya mpaka pale nilipokuwa nimeketi kungojea kuingia kwa daktari. Ubavuni kwangu alikuwa bibi mmoja mkongwe. Taabani kwa ugonjwa na uzee. Niligeuka kumtazama kwa muda huku nikitungwa na huzini naye. Lakini ghafla lilitokezea jambo la ajabu. Ilinijia tu kumwona bibi huyu kuwa kajigeuza umbo la kutisha. Uso wa kiboko wenye kuzingwa na manyoya ya mbuzi. Kichwani katoa pembe na kinywani aliposema alitoka moto (*DY* uk. 86).

Kiumbe kinachorejelewa hapo juu kina uwezo wa kujigeuzageuza. Kwanza, kinajitokeza kama binadamu aliye na sura ya mwanamke; ajuza aliyekuwa amedhoofika kiafya kwa sababu ya ugonjwa na uzee. Ghafla ajuza huyu anabadilika na kuchukua sura ya mnyama mwenye mseto wa mnyama wa porini na wa kufugwa. Isitoshe, kiumbe hiki kinatenda mambo ya kiajabu. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa kinaposema, kinatoa moto kutoka kinywani. Licha ya kuwa kiumbe cha ajabu, kina uwezo wa kuwasiliana na binadamu wa kawaida. Kwa mfano, kinajibizana na Ndi- aliyekuwa ameketi karibu nacho na hatimaye wanapigana na Ndi- anakiumiza vibaya (uk.86). Maelezo haya kuhusu Ndi- na kiumbe hiki cha ajabu yanadhihirisha uhalisia unaoenda sambamba na umazingaombwe hivi kwamba mhusika halisi anatangamana na yule wa kimazingaombwe na hivyo kuifuta mipaka ya wazi kati ya uhalisia na umazingaombwe.

Katika *NZM*, tunaelezwa kuhusu mhusika wa ajabu mwenye umbo la binadamu. Hata hivyo, mhusika huyu ni kiwiliwili tu ambacho hakina kichwa, yaani ni kibutu mtu kama kinavyoitwa katika riwaya hii. Hata hivyo, kina uwezo wa kutenda kama binadamu wa kawaida:

> Tokeo lile la ajabu lilitokea siku ile [Nana] alipokuwa njiani kutoka kazini akizungusha usukani wa gari lake… Alipotazama kulia yake aliliona lile gari la *Rolls Royce*. Dereva wake kibutu cha mwili; kiwiliwili kilichobutuka kichwa. Hakuwamini Nana. Aliinama kupagusa kile kioo cha dirisha la gari yake. Naam kwenye dirisha la *Rolls Royce* lenye kioo cha kiza, aliona kibutu cha mtu. Na hapo hapo hicho kibutu cha mtu kilichokuwa kikendesha gari kilimpungia mkono Nana. *Nani yule? Miujiza gani ile?* Alijiuliza (*NZM* uk. 217).

Kwa kawaida, kichwa ni sehemu muhimu sana katika mwili wa binadamu. Katika kichwa kuna viungo muhimu vinavyotusaidia kuona, kusikia na kuzungumza. Aidha, ubongo wa binadamu hupatikana kwenye kichwa na hutuwezesha kufikiria na kufanya maamuzi. Kwa kifupi, kichwa huwa kama injini inayoendesha mwili wa binadamu, na bila kichwa uhai wa binadamu hukatika. Hivyo basi kiumbe anachokiona Nana ni cha ajabu kwani hata bila kuwepo na kichwa bado ki hai, kinaona, kinazungumza na kusikia, kuwapungia watu mkono na hata kuendesha gari. Isitoshe, inaonekana kuwa wakati mwingine kiumbe hiki hujitokeza kama kichwa kilichotengana na kiwiliwili, yaani kichwa kibutu kama anavyokiita Nana. Wakati kinajitokeza katika hali hii huwa kinajibadilishabadilisha na kuchukua sura za watu tofauti:

> Siku hizo zote, Nana alifanya upekuzi sana kukitafuta kile kichwa butu, lakini hakufanikiwa. Siku moja kwa miujiza, alikiona kimetokeza waziwazi kichwa hicho, kwa sura ya Mwarabu, ingawa hakuwa na hakika kama kilikuwa cha Mwarabu kweli au la. Baadaye, siku nyingine, kichwa kilitokeza kwa wasifu wa Mjerumani. Pia hakuweza kusema kwa asahi kama kilikuwa cha Mjerumani au Mchina au Mhispania. Kuna siku kilijitokeza kwa sura ya Mwingereza aliyevaa shati la bendera ya Kiingereza. Kisha siku nyingine cha Mmarekani aliyejizonga kanda la *Cow Boy* shingoni. Kisha ikaja sura ya mtu mweusi. Na mwisho kichwa kikawa cha Mwitaliano kabla hakijageuka Kaburu wa Afrika ya Kusini. Jambo hili sasa halikumshangaza tu Nana, lilimpa hofu. … Nani huyu

> kiumbe anayejigeuzageuza kama kinyonga? Anayeanza kwa kitendawili cha ubutu na kuishia kubadilisha nyuso? (*NZM* uk. 218).

Ingawa kiumbe hiki kinajitokeza kama mazingaombwe, kinaashiria matukio halisi katika ulimwengu halisi. Kama anavyosema Baldick (2001) sifa za uhalisiamazingaombwe hutumiwa kutoa taswira ya jumla ya mabadiliko ya kisiasa katika karne ya 20. Tunaweza kusema basi kuwa sura mbalimbali la kiumbe hiki zinaashiria aina tofauti ya wakoloni na ukoloni katika Afrika na maeneo mengineo ulimwenguni kote yaliyotokea kabla na baada ya karne 20. Hivyo basi, tunarejelea ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Katika karne hii ya 21 tunatawaliwa na ukoloni mamboleo ulio na msingi wake katika ukoloni mkongwe. Kutawaliwa huku hakujitokezi wazi wazi bali kumejificha na kunaendelea kuwaathiri watu hasa walio katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Hii ndio maana kiumbe hiki kinajitokeza kama kiwiliwili kibutu ili kuuficha uso wake kuashiria ukoloni ambao bado upo lakini kwa njia ilyofichika. Kama mhusika kwenye kazi ya kifasihi, matumizi ya kibutu mtu na uwezo wake wa kubadilishabadilisha sura unakiuka uwezo wa binadamu wa kawaida na hivyo kuonyesha mabadiliko katika utanzu huu wa riwaya.

Mhusika mwingine wa kimiujiza ni Muse[9] katika riwaya ya *DY.* Mwandishi pia ametumia jina Mize kama njia ya kuswahilisha jina Muse ili lioane na mazingira ya Uswahilini. Tunapopatana naye kwa mara ya kwanza riwayani, Muse anajitokeza kama dhana tu katika akili na kumbukizi za Ndi-. Hata hivyo anaanza kumtokezea Ndi- akiwa amejipa umbo la mwanamke wa kutamanisha. Aidha ana mbawa kama ndege au malaika. Kutokana na urembo wake, Ndi- anaanza kutamani kufanya ngono naye ili kutimizi ashiki. Kupitia kwa Mize, Ndi- anapata uwezo uliokiuka ule wa binadamu wa

[9]Waliula (2010) anaeleza kuwa jina Muse liliazimwa kutoka visaasili vya Kiyunani na lilitumiwa kurejelea miungu wa sanaa na ubunifu. Muse aliaminika kuwa chanzo za kariha na ubunifu katika ushairi na kadhalika.

kawaida. Akieleza uwezo huu wa Ndi- kupitia kwa Muse, Waliaula (2010: 8-9) anaeleza yafuatayo:

> Mize ndiye anamwelekeza Ndi kwa kukaidi mpito wa nyakati na mipaka ya mahali, mipaka kati ya roho na mwili, mipaka kati ya kuwepo na kutokuwepo, mipaka kati ya kuonekana na kutoonekana, mipaka kati ya ukoloni na baada ukoloni, mipaka kati ya ugiriki wa kale na unguja.

Kwa mfano, Bi Muse anamtokezea Ndi- akiwa chumbani mwake. Anamtoa Ndi- kwenye kitanda na kumwongoza hadi kwenye tarakilishi na kisha anajitambulisha (uk. 60-61). Baadaye wanakuwa na majadiliano marefu kisha Bi. Muse anatoweka. Kabla ya kutoweka anamuasa Ndi- kwa kusema haya:

> "Lazima utafute asili ya mambo. Sababu ya kuzama kwako topeni. Chanzo cha balaa," aliniambia Bi Mize, huku nikimhisi akinishuka ghafla. Kama pepo wa ruhani aliyekwisha nidondoshea tamu, kwa kunionjesha tone lake moja la asali. Nilikuta vidole vyangu vimesita juu ya vibofya vya kompyuta, mawazo nayo yamekwenda na yule bibi-wa-sanaa. Shibe ya fikra na mawazo ikatoweka… (uk. 76).

Bi. Muse anaonekana kumtokezea Ndi- wakati wowote na mahali popote na baada ya kuikamilisha kazi yake anatoweka.

Baadhi ya matukio katika riwaya za utafiti huu yanakaidi mipaka ya kihalisia na kudhihirisha matukio ya kimazingaombwe yanayoenda sambamba na uhalisia. Kwa mfano, Ndi- anapoitazama albamu ya aila yake, picha za aila yake zilizoko kwenye albamu hii zinahuishwa na kufanywa wahusika wenye uwezo wa kuwasiliana na kutenda kihalisia. Ndi- ambaye ni mhusika halisi katika riwaya hii anaanza kuwasiliana na wahusika wake wapya waliohuishwa ambao ni Dubwa, Yungi na Bi M. Katika dondoo lifuatalo tunapata mawasiliano kati ya Ndi- na picha ya Dubwa iliyohuishwa:

> Albamu li wazi. Dubwa anaibuka na kutoka nje ya karatasi. Ajabu! Miaka yote hii picha yake ilikuwa imefichama kwenye albamu. Leo imezuka na kusimama kwa mapana na marefu….
>
> "Ninajua unawaza nini," aliniambia alipokuwa amesimama mbele yangu…

> *Kwa nini nisiwaze ninavyostahiki kuwaza?* Aliponitazama alihisi macho yangu yakisema maneno haya…"
>
> "Kwa sababu huna haki ya…" alijibu (*DY* uk. 137/8).

Tunaona kuwa Dubwa anajitokeza kwenye albamu na anaanza kuwasiliana na baba yake, Ndi-. Anamshtumu Ndi- kwa kujitia wendawazimu na kujitenga na familia yake, hivyo basi kukimbia jukumu lake kama mume wa mke wake na baba ya watoto wake. Kwa kuwa hata yeye Dubwa alipatikana nyumbani kwa nadra sana, anamwomba Ndi- watubu kwa Mwenyezi Mungu, na anaanza kujitayarisha kuswali:

> Sasa [Dubwa] alikuwa akitandika chini ule mswada aliokuja nao. Akasimama juu yake na kuelekea kibla. Baadaye nikamwona ananyanyua mikono kufunga swala. Aliswali rakaateni. Baada ya kwisha kuswali, alikaa palepale mswalani kwa muda akiomba dua (uk 138).

Ingawa Dubwa ni picha tu kwenye albamu, picha yenyewe inahuishwa na kuwa mhusika anayetenda kama binadamu halisi. Kwa mfano, anatandika mswada chini na kuanza kuswali. Kama anavyosema Waliaula (2010), albamu inageuzwa na kuwa kama kiwambo cha sinema ambapo maigizo ya wahusika tofauti yanaonyeshwa, na Dubwa na Ndi- wanakuwa baadhi ya wahusika hao.

Matukio mengine yanayodhihirisha uhalisia mazingaombwe yamejikita katika uwakilishaji wa matukio ya kawaida yaliyojikita katika misingi ya visaasili vya jamii fulani. Katika riwaya ya *UNN* tunaelezwa kuhusu Nyakor, mhusika wa kawaida, mwenye asili ya kizazi cha Mwanamke wa Ziwa.

> Nyakor, mwanamke mwenye ngozi ya rangi nyeusi iliyoshiba Uafrika – ule unaong'aa kama ngozi ya jongoo, macho ya kikombe, midomo iliyotuna siha, meno meupe yenye mwanya katikati, vidu usoni, pua pana, ndonya ya kipekee, shingo ya mwanzi na masikio ya wastani, alitokana na kizazi cha Mwanamke wa Ziwa (*UNN* uk. 72).

Kisa cha Mwanamke wa Ziwa ni kisaasili katika jamii ya mhusika huyu kinachotumia kuwafunza wanajamii umuhimu wa kuwa na shukrani na kushtumu matendo hasi kama kiburi na ujeuri. Kinamtumia Mwanamke wa Ziwa aliyeibuka kutoka ziwani kama

chanzo cha utajiri wa Nyalgondho. Hatimaye Nyalgondho anapoingiwa na kiburi Mwanamke wa Ziwa anarudi ziwani alikotoka akiwa amefuatwa na utajiri wote aliokuwa amempa Nyalgondho na kumwacha mwanamume katika hali yake ya awali ya umaskini:

> Ni mimi Mwanamke wa Ziwa naja ziwani
> Huku ndiko nilikotoka majini
> Fungua sote tuingie kwenye wako undani
> Ili tusionekane tena kwa Nyalgondho nyumbani
> Huyu mwanamume asiyekuwa na shukrani (*UNN* uk. 75)

Kisa cha Mwanamke wa Ziwa ana Nyakor kinadhihirisha ukweli wa maelezo ya Abrams katika Waliaula (2010) anayesema kuwa katika uhalisia mazingaombwe matukio ya kawaida yanawasilishwa sambamba na mambo yanayotokana na visaasili na hekaya. Usambamba huu unadhihirika wakati Nyakor ambaye ni mhusika wa kawaida anasemekana kutokana na kizazi cha muhusika wa kisaasili, yaani Mwanamake wa Ziwa.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imejadili uhalisiamazingaombwe kama kipengele mojawapo cha mtindo katika riwaya za kibaadausasa. Imebainika kuwa uhalisiamazingaombwe ni mtindo wa uandishi unaokiuka kaida za kihalisia zilizokuwa zimezoeleka na kutumiwa na wanamapokeo kama msingi wa kuifafanua riwaya. Ukiukaji huu ambao huchanganya uhalisia na umazingaombwe umedhihirika kupitia matumizi ya wahusika wa ajabu ajabu kama vile mizuka, vivuli, wafu ambao wanatenda kama viumbe katika ulimwengu halisi. Aidha, binadamu wa kawaida wenye sifa na uwezo wa ajabu kama vile kuwasoma watu pia ni ishara ya uhalisia mazingaombwe. Vilevile uhalisia mazingaombwe umeshihirika kupitia matukio mbalimbali ya ajabu. Matumizi ya mtindo huu ni dhihirisho la upya katika fasili ya riwaya inayopinga fasili ya awali na kudhihirisha njia anuwai za kujieleza bila kufungwa na simulizi kuu ya wanamapokeo.

Aidha, mtindo huu umetumika kuwakilisha ulimwengu wa sasa uliojaa fujo, ghasia na mambo mengine ya ajabu ambayo yamesababisha kutokuwepo na mshikamano katika K21.

# SURA YA TANO

# UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA MWINGILIANO MATINI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imebainisha matumizi ya mwingiliano matini kama kipengele mahsusi cha mtindo wa ubaadausasa kwa kujikita katika riwaya tatu za utafiti huu. Mwingiliano matini hutumika kukaidi itikadi ya mwondoko wa Usasa uliopendekeza uasili wa kazi za sanaa. Badala yake, wanaubaadausasa hutambua kazi nyingine za awali na kuzitumia kama malighafi ya kuunda kazi zao. Matumizi ya mwingiliano matini basi yanaambatana na maelezo ya Lyotard (1979) ya kuzipuuza simulizi kuu, kama vile Usasa, na badala yake kuibuka na njia anuwai za kujieleza. Aidha, kuambatana na maelezo ya Khamis (2005) kuwa riwaya za ubaadausasa husheheni maudhui yanayoakisi matatizo yanayoikumba bara la Afrika, sura hii imedhihirisha namna vipengele vya mwingiliano matini vimechangia kuendeleza dhamira tofauti za riwaya zenyewe. Licha ya hayo, sura hii imejadili namna mwingiliano matini unavyoweza kumwathiri msomaji katika kufuatilia dhamira za riwaya husika. Katika kufanya hivyo, sura hii itatimiza lengo la nne la utafiti huu. Ili kufanikisha malengo haya sura hii imegawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambapo muhtasari wa sura umeelezwa. Sehemu ya pili imejadili kwa kifupi dhana ya mwingilano matini nayo sehemu ya tatu ikiangazia dhima ya mwingiliano matini katika kazi ya fasihi. Katika sehemu ya nne tumejadili kwa kina mwingiliano matini katika riwaya zilizotafitiwa kwa kubainisha matini mbalimbali zilizorejelewa. Hizi ni pamoja na marejeleo ya fasihi ya Kiswahili, marejeleo ya fasihi ya Kiingereza, marejeleo ya filamu, marejeleo ya kidini, marejeleo ya mashujaa wa Kihistoria na hatimaye marejeleo ya wanasaikolojia na wanafalsafa mbalimbali. Kwa kila marejeleo tumejadili namna mwingiliano matini umechangia dhamira za riwaya husika pamoja na athari

zake katika kuzifuatilia dhamira zenyewe. Hitimisho la sura linapatikana katika sehemu ya tano.

### 5.1 Dhana ya Mwingiliano Matini katika Fasihi

Sehemu hii imejadili maana ya dhana ya mwingiliano matini kama ilivyoelezwa na wataalamu tofauti, pamoja na matumizi yake katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Childs & Fowler (2006) na Fairclough (2006), mwingiliano matini ni dhana iliyotumiwa kwa mara ya kwanza mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanaisimu wa Kifaransa, Julia Kristeva kurejelea kazi ya Bakhtin kuhusu usemezano. Ingawa Bakhtin mwenyewe hakuitumia istilahi hii, Kristeva alitumia mawazo yake kama msingi wa kuelezea mwingiliano matini. Kristeva anaeleza kuwa, mwingiliano matini unahusu hali ya kuingiza historia katika matini, na kuingiza matini husika katika historia. Hii ina maana kuwa matini yoyote ile huundwa kutokana na matini za awali, huku matini ya sasa ikiwa kama msingi wa kuunda matini za baadaye. Kwa hivyo, matini yoyote ile huwa na sifa ya mwingiliano matini, yaani, kila matini ina vipengele vya matini nyinginezo. Ingawa maelezo ya Kristeva yalikuwa muhimu katika kuweka msingi wa dhana ya mwingiliano matini, maelezo yake ni ya kijumla sana hivi kwamba hatuwezi kueleza ni vipengele vipi hasa vinabainisha mwingiliano matini. Kama anavyosema Diegner (2005), dhana ya mwingiliano matini katika nadharia ya fasihi imekiuka mipaka hii ya kimsingi kama alivyoieleza Kristeva na kupata maana pana zaidi inayojikita katika uhusiano wa kiusemi wenye maana kati ya matini tofauti.

Katika fasihi, wataalamu mbalimbali (k.m. Polleheide 2003; Diegner 2005; Childs na Fowler 2006; Bjornsson 2006) wamekubaliana kuwa mwingiliano matini hutumiwa kueleza namna matini moja hurejelea matini nyingine ambazo huziathiri kwa njia moja au nyingine. Diegner (2005), kwa mfano, anaeleza kuwa mwingiliano matini hujitokeza

wakati mwandishi anarejelea kimakusudi matini nyingine na pia wakati hajakusudia kufanya hivyo.

Mohammed (2006) katika *DY* amechangia katika kuonyesha kuwa kila matini huwa na vipengele vya mwingilao matini anaposema:

> Kila utunzi, kila andiko la kisanaa ni aina moja ya mchanganyondimi. Huwezi kuepuka hilo. Hata ukipata bahati ya kukutana na Bi Muse na uzuri wake wa ajabu, bado huwezi kuuepuka mchanganyondimi (*DY* uk 42).

Katika dondoo hapo juu, Mohamed (2006) anarejelea mwingiliano matini ambao yeye anauita mchanganyondimi. Anadhihirisha kuwa kazi za kisanaa, hususan riwaya za kibaadausasa huwa na wingi wa mwingiliano matini, kipengele ambacho sura hii inashughulikia.

Polleheide (2003) naye anaeleza kuwa katika kazi za kibaadausasa, wakati mwingine mwandishi hurejelea matini nyingine kwenye kazi yake, bila kupanga kufanya hivyo, na bila kujali iwapo msomaji anazifahamu au la. Mawazo haya ya Polleheide yalikuwa muhimu katika utafiti katika kubainisha athari za mwingiliano matini kwa msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti katika riwaya za kibaadausasa.

Utafiti huu umejikita katika aina tatu za mwingiliano matini kama zilivyofafanuliwa na Diegner (2005). Aina ya kwanza ya mwingiliano matini, ambayo tumeiita mwingiliano matini dhahiri katika utafiti huu, inahusu urejeleaji wa vipengele mahsusi kutoka matini nyingine na ambavyo vimeingizwa katika riwaya za utafiti huu. Aina ya pili ya mwingiliano matini ambayo imeshughulikiwa katika utafiti huu tumeiita mwingiliano matini usodhahiri. Katika mwingiliano matini usodhahiri, kuna urejeleaji wa vipengele mbalimbali kutoka matini nyingine bila kutaja ni wapi ambapo vimetolewa. Aina ya tatu ya mwingiliano matini ambayo tumeishughulikia inazingatia usharabu na ulinganifu wa kimawazo kati ya riwaya hizi na matini nyinginezo ambazo zimerejelewa

na ambazo zimeathiri mwandishi wa riwaya hizi kwa njia moja au nyingine. Aina hii ya mwingiliano matini tumeuita mwingiliano matini linganifu. Ingawa utafiti huu haukushughulikia mwingiliano matini kati ya riwaya zenyewe za utafiti huu, wakati mifano ya matini zilizorejelewa ilijitokeza katika riwaya mbili au zaidi za utafiti huu, mifano hiyo ilishughulikiwa kwanza na kulinganishwa. Kabla ya kushughulikia mwingiliano matini katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu, ni muhimu kwanza kujadili dhima ya mwingiliano matini katika kazi za kifasihi, hususan, riwaya za kibaadausasa.

## 5.2 Dhima ya Mwingiliano Matini katika Kazi za Kibaadausasa

Katika kazi za kibaadausasa, mwingiliano matini hulenga kutimiza malengo tofauti ambayo sehemu hii imeyajadili. Malengo hayo ndiyo msingi wa uhakiki wa mwingilano matini katika sura hii kwa kuzingatia riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu.

Wataalamu mbalimbali (k.m Grenz 1996; Lewis 2001; Barry 2002; Klages 2006; Childs & Fowler 2006; Clayton 2012) wamebainisha kuwa wanaubaadausasa hutumia mwingiliano matini kuvuruga imani ya awali inayohusishwa na mawazo ya usasa na ulimbwende kuhusu upekee wa matini, pamoja na uasili wa mawazo ya mwandishi wa matini husika. Barry (2002), kwa mfano, anaeleza kuwa sifa mojawapo ya usasa katika sanaa na fasihi ilikuwa ni kutupilia mbali maumbo ya kizamani na kujaribu kutumia maumbo mapya yaliyoonesha uasili. Hii ina maana kuwa wanausasa walisisitiza ubunifu wa kimajaribio ambao haukuiga maumbo mengine ya awali. Kama anavyosema Grenz (1996), wanaubaadausasa hulenga kupuuza itikadi ya usasa inayompa mwandishi mamlaka makuu ya kuunda kazi asili ya fasihi. Wanaubaadausasa huamini kuwa hakuna kazi yoyote ya fasihi inayoweza kuchukuliwa kama mpya au asili. Clayton (2012), kwa mfano, anaeleza kuwa wanaubaadausasa huamini kuwa mwanafasihi hutumia tanzu na maumbo mengine ya awali ili kuibuka na

maana mpya ya kazi zao katika miktadha tofauti. Kwa hivyo, matini za fasihi ya kibaadausasa huonyesha namna matini husika ilivyoathiriwa na matini za awali, na hulenga kuziandika upya matini hizo za awali na wakati mwingine kwa njia ya kubeza. Hiki ndicho kiini cha matumizi ya mwingiliano matini katika kazi za fasihi kama mojawapo ya mhimili mkuu katika nadharia ya ubaadausasa. Katika utafiti huu kipengele hiki cha mwingiliano matini kimejadiliwa kwa kuonyesha namna waandishi wa riwaya zilizotafitiwa wamerejelea kazi za wataalamu wengine na kuzitimia kazi hizo kama malighafi ya kuunda kazi zao.

Kulingana na Childs & Fowler (2006) dhima nyingine ya matumizi ya mwingiliano matini ni kumtambua msomaji kama mshiriki katika mchakato wa ubunaji wa kazi ya kifasihi. Kwa kuwa mwandishi ndiye mpangaji wa mawazo, msomaji ana nafasi muhimu ya kuweza kung'amua maana inayotokana na yale ambayo mwandishi ameyapanga. Iwapo mwandishi amerejelea matini nyingine katika kazi yake, ufasiri wa maana katika matini husika utategemea iwapo msomaji anafahamu matini hizo zilizorejelewa au la. Iwapo msomaji hajawahi kupatana na matini hizo zilizorejelewa, atakuwa na ufasiri mwingine ambao, kulingana na Childs & Fowler (2006), pia unaweza kukubalika. Ni kutokana na huu uwezo wa msomaji wa kuweza kung'amua maana katika matini ya kifasihi ambapo msomaji anachukuliwa kama mhusika muhimu katika kazi ya kisanaa. Dhima hii imetumika katika kubainisha athari za mwingiliano matini kwa msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti za riwaya zilizotafitiwa.

Pollheide (2003; Diegner 2005; Childs na Fowler (2006), wanakubaliana kuwa mwingiliano matini hulenga kubomoa imani kuhusu ukamilifu na upekee wa kazi ya kisanaa. Kwa mfano, Pollheide (2003) anasema kuwa mwingiliano matini huivunjavunja matini katika vipande vidogo vidogo ambavyo huhitaji kuunganishwa baadaye. Kwa hivyo, wanaubaadausasa hutumia mwingiliano matini kudhihirisha

kwamba matini haiwezi kuchukuliwa kama kitu kimoja kamilifu kinachojitosheleza. Mohamed (2006) anadhihirisha ukweli wa mawazo haya katika *DY* anaposema hivi:

> Katika simulizi na mapito yake. Vipandevipande – si lazima vishikane. Unavimwaga tu vipande vyenyewe kama unaatika mbegu kwenye shamba la sanaa. Unafanya hivyo kuwaacha wasomaji waunge wenyewe vipande vya maana zao, huku maneno mengine ukiyajengea vivuli ili kuwategea makusudi watafute maana zao badala ya kuzipata maana kibungabunga. Maneno yawe wahusika, picha, watu, wanyama, au mashetani (uk. 9).

Maneno haya ya Mohamed (2006) katika *DY* yanabainisha kwamba matini huundwa kwa vipandevipande vya simulizi na ni jukumu la msomaji kuviunganisha ili kuunda maana. Mwingiliano matini ni mojawapo ya mbinu ambayo huvunja usimulizi katika vipande vipande, jambo ambalo huweza kusababisha changamoto kwa msomaji katika kufuatilia dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya husika. Sehemu inayofuata imejadili mwingiliano matini dhahiri, mwingilano matini usodhahiri na kwa kiasi fulani mwingiliano matini linganifu kwenye riwaya za utafiti huu kwa kujikita katika marejeleo ya nyanja mbalimbali kama vile fasihi, filamu, dini, historia pamoja na uwanja wa saikolojia na falsafa.

### 5.3 Mwingiliano Matini katika Riwaya Zilizotafitiwa

Riwaya za utafiti huu zimedhihirisha wingi wa mwingiliano matini katika nyanja na taaluma mbalimbali. Katika sehemu hii tumejikita katika mwingiliano matini unaotokana na urejeleaji wa matini za fasihi ya Kiswahili, fasihi ya Kiingereza, muziki na filamu, marejeleo ya kidini, marejeleo ya matukio ya kihistoria pamoja na marejeleo ya wanafalsafa na wanasaikolojia mbalimbali. Katika sehemu hii, matini na mawazo yaliyorejelewa aghalabu yameonyeshwa kwa kutumia maandishi yaliyokolezwa rangi ili kuyatofautisha na maelezo mengine ya riwaya zenyewe.

### 5.3.1 Urejeleaji wa Kazi za Fasihi ya Kiswahili

Riwaya zilizotafitiwa zimedhihirisha mwingiliano matini unaotokana na fasihi ya Kiswahili, hususan, tamthilia, riwaya na ushairi. Katika riwaya ya *NZM* kwa mfano, kuna urejeleaji wa tamthilia ya Kiswahili ya *Mashetani,* iliyoandikwa na mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili, Ebrahim Hussein:

> Lakini nyumbani humu nilimo hivi sasa ni shule kamili kwangu…hapa, mara moja nilijifunza kwamba hata vitu vidogo kama kikombe na kisahani, hututofautisha sisi binadamu. Hubainisha mwenendo pande mbili. Upande mmoja, ni ule wa wale wanaoshika vitu kwa dhati ya kushika na upande wa pili, ni ule wa wasioshika kamwe au wanaoshika bila hisia yoyote au kwa ulazima wa kushika tu. Hutuwekea mipaka vitu, baina ya ukubwa na udogo, uke na uume, umaskini na utajiri, mwamko na ujinga, na **chambilecho Hussein wa *Mashetani*, baina ya mpanda ngazi na mshuka ngazi (*NZM,* uk. 73).**

Riwaya ya *NZM* imetumia mwingiliano matini dhahiri kwa kuitaja matini inayorejelewa, mwandishi wa matini hiyo pamoja na mawazo yake ambayo yamerejelewa. Katika riwaya ya *Mashetani,* Hussein anayatumia maneno haya kuonyesha utabaka katika jamii ambapo matajiri wanaendelea kutajirika huku maskini wakiendelea kufukarika. Anamtumia mhusika Juma aliyekuwa wa tabaka la chini kumwambia Kitaru aliyekuwa wa tabaka la juu kuwa '**Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono**…Leo yako ni kidato cha kesho…leo yangu ni kidato cha jana' (*Mashetani* uk 56). Kauli hii ya Juma katika Mashetani inabainisha namna ilivyo vigumu kuziba mipaka ya kitabaka, kwani kila kuchao, matajiri wanaendelea kupanda kidato kingine kwenye ngazi ya maisha, huku maskini wakishuka. Kwa msomaji wa *NZM* anyefahamu muktadha wa matumizi ya kauli hili katika *Mashetani*, itakuwa rahisi kwake kung'amua kuwa Nana anazungumzia suala la utabaka. Anaonyesha tofauti iliyoko kati ya maisha ya kifahari aliyoyaishi nyumbani kwao na maisha ya kimaskini wanayoyaishi kina Bi. Chuma ambako amehamia na kuyafanya makao yake mapya. Hata hivyo, kwa msomaji ambaye hana ufahamu wa

riwaya ya mashetani, huenda ikamwia vigumu kuing'amua maana ya kauli hii na itambidi ategemee muktadha wa matumizi yake na kufasiri maana ambayo huenda ikawa tofauti na iliyokusudiwa. Hata hivyo, kama wanavyosema Childs & Fowler (2006), ufasiri wa maana mpya iliyo tofauti na iliyokusudiwa pia hukubalika kwani msomaji pia ni mhusika katika kuunda kazi ya fasihi.

Mbali na urejeleaji katika tamthilia, riwaya za utafiti huu zimedhihirisha mwingiliano matini kupitia urejeleaji wa riwaya za Kiswahili. Kwa mfano, katika *DY* kuna urejeleaji riwaya ya Kezilahabi, *Dunia Uwanja wa Fujo*:

> "Unatarajia nini baba katika ulimwengu uliokwisha kufa?"
> Ingawa najua kwamba hata mimi nimeshakufa, ukweli ni kwamba siamini juu ya fikra ya kwamba maisha tunayoishi yanatustahili. **Dunia si uwanja wa fujo! Si zogo lisilosarifika. Sikubaliani kabisa na Kezilahabi.** Namjua anayeharibu. Namwona akisukuma watu katika lindi refu. Uchungu wangu ni kuwa siwezi kumzuia… (*DY*, uk. 144)].

Ingawa kwenye dondoo hapo hatujatajiwa kitabu kinachorejelewa, bado huu ni mwingiliano matini dhahiri kwani mwandishi wa riwaya inayorejelewa, yaani Kezilahabi, ametajwa pamoja na mawazo yake. Katika riwaya yake, *Dunia Uwanja wa Fujo*, Kezilahabi anasema kuwa dunia imejaa fujo, ghasia na migogoro. Kila binadamu basi yuko katika harakati za kutosheleza maslahi yake binafsi ili aweze kuishi maisha mazuri zaidi kuliko wenzake. Katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, kama zilivyo kazi nyingine zake, Kezilahabi anaongozwa na falsafa ya jaala (Fate). Katika falsafa hii, Kezilahabi anaonyesha kuwa kilichoandikwa kuhusu maisha ya binadamu hakina budi kutokea hata kama binadamu atajitahidi kiasi gani. Riwaya ya *DY* inayahakiki mawazo haya ya Kezilahabi kwa kukataa kukubali kuwa dunia ni uwanja wa fujo. Mwandishi wa *DY* kupitia kwa mhusika Ndi- hata hivyo analenga kutoa ufasiri mpya kuhusu maisha. Anaonyesha kuwa matatizo wanayowapitia wanadamu hayatokani na dunia wala jalaa bali wanadamu wanaowakandamiza wanadamu wenzao. Tofauti na

anavyoeleza Kezilahabi, mwandishi wa *DY* anaonyesha kuwa hali hiyo ya ukandamizaji na ukandamizwaji inaweza kubadilika. Haya yanajitokeza kupitia kwa mhusika Ndi- ambaye tayari ameshaporomoka kimaisha. Licha ya kuwa anaifahamu na kuikubali hali yake, anakataa kukubali kuwa hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Anashikilia kuwa iwapo binadamu watawajali binadamu wenzao, mabadiliko yanaweza kutokea. Mawazo sawia na haya vilevile yanajitokeza kutokana na mhusika Nana katika *NZM*. Tazama dondoo lifuatalo:

> Neno ‘oa’ lilimtia hofu Nana. Amesoma vitabu vingi vya uana na jinsia vya kimagharibi vinavyosisitiza ndoa kuwa si chochote bali utumwa tu kwa mwanamke. Dhana hii lakini kila siku humtisha Nana….Ndoa, kitu gani ndoa? Hajui mengi kuhusu neno hili, lakini moja analitambua, ndoa ndiyo iliyomleta yeye hapa duniani, kama kweli iliyomleta yeye duniani ilikuwa ndoa. **Lakini Nana alikataa katakata kwamba dunia ni uwanja wa fujo** (*NZM*. uk 223).

Tofauti na ilivyo katika *DY*, urejeleaji wa kazi ya Kezilahabi katika *NZM* kwenye dondoo hapo juu unadhihirisha mwingiliano matini usodhahiri. Katika urejeleaji huu, jina la mwandishi halikutajwa wala anwani ya kazi yake, bali mawazo ya Kezilahabi yamepachikwa tu. Kwa kuzingatia kuwa S. A. Mohamed ndiye mwandishi wa riwaya zote mbili, yaani *DY* na *NZM*, tunaona namna mawazo yake yanaoana hasa katika kuyahakiki mawazo ya Kezilahabi. Kama ilivyo katika *DY*, riwaya ya *NZM* pia anakataa kuwa dunia ni uwanja wa fujo. Kwa mujibu wa Khamis (2005: 95) riwaya mpya ya Kiswahili hulenga kubainisha maudhui yanayoonyesha vita halisi na vya kisaikolojia ambavyo wanajamii katika bara la Afrika hupitia. Waandishi basi huandika kudhihirisha hasira yao kutokana na matokeo ya vita hivi kama njia ya kuwashawishi wanajamii wainuke na kuibadilisha hali yao. Katika dondoo hapo juu, riwaya ya *NZM*, kama mojawapo ya riwaya mpya ya Kiswahili, inadhihirisha vita vya kisaikolojia vilivyojikita katika utamaduni unaowadhalilisha wanawake kupitia mhusika Nana. Nana anaonyesha namna wanadamu walivyoidhalilisha asasi ya ndoa na kuiona kama

utumwa hasa kwa mwanamke. Hata hivyo, Nana anashikilia kuwa hali hii inaweza kubadilika na ndoa ikaweza kuchukuliwa kama kitu adimu. Kupitia mhusika Nana, mwandishi huenda analenga kuwazindua wanajamii na wasomaji wa riwaya hii kuhusu utamaduni unaowadhalilisha wanawake hasa katika asasi ya ndoa, ili wainuke na kuubadilisha kwa kuinua hadhi ya mwanamke. Katika urejeleaji huu, mwandishi anaelekea kujadili dhamira inayohusiana na utu na uwajibikaji katika jamii.

Mbali na kuwa na mwingilano matini ambapo waandishi wa riwaya za utafiti huu wanarejelea kazi za waandishi wengi, kuna mwingilano matini wa aina nyingine ambapo waandishi wa riwaya hizi wanazirejelea kazi zao wenyewe. Kwa mfano, katika riwaya ya *DY*, S. A. Mohamed amerejelea riwaya yake ya awali ya *Dunia Mti Mkavu:*

> Nilipolala usiku niliota nchi nzima iko katika kile ambacho hapa huitwa fensi, au aina ya *carnival*…. Lakini ghafla mmoja wao alianza kumpiga panga mwingine na mwingine…. Fensi haikutambulikana tena. Burudani ikaondoka. Watu walipigana vibaya vibaya. Damu ikaenea nchi nzima. **Mikondo ya damu ilimiminika kama katika *Dunia Mti Mkavu*. Damu ikamalizikia kutiririkia bahari ya Hindi** (*DY*, uk. 70).

Urejeleaji wa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* unatokea katika *DY* wakati Ndi- anasimulia mojawapo ya ndoto akiwa kwenye fensi ambapo walianza kupigana na kuuana na kusababisha umwagikaji wa damu unaolinganishwa na ule uliotokea katika riwaya ya *Dunia mti Mkavu*. Katika *Dunia Mti Mkavu*, kulikuwa na msururu wa mauaji yanayotokea katika siku moja na kusababisha umwagikaji mwingi wa damu. Inspekta Farouk anaamrisha polisi kuwafyatulia risasi waandamanaji waliokaidi amri yake na kumi kati yao wakafariki papo hapo. Waliouawa walikuwa viongozi wa Kiafrika walioupinga utawala wa mzungu na walioandama ili kuwatoa wenzao kwa jela kwa madai kuwa walifungwa bila hatia. Wakati uo huo, mhusika anayeitwa Masika anamuua mumewe. Inasadifu kuwa gari lililombeba Masika ili kumpeleka kwenye kituo cha polisi kwa shutuma za mauaji linapita karibu na mahali viongozi wale

wameuliwa. Inspekta Farouk analisimamisha ili apate msaada wa kuzibeba maiti. Ghafla, Masika anachukua bunduki ya askari mmoja na kumuua Inspekta Farouk. Maji ya mvua iliyokuwa inanyesha inaiosha damu ya waliouliwa na kuiporomosha mikondo ya damu (*Dunia Mti Mkavu* uk. 111-121). Mwandishi wa *DY* basi anatumia mwingiliano matini kulinganisha umwagikaji wa damu katika fensi na ule uliotokea katika *Dunia Mti Mkavu*. Msomaji anayeifahamu riwaya ya Dunia Mti Mkavu anaipata taswira kamili ya hali inayorejelewa katika riwaya ya *DY*. Hata hivyo, kama anavyosema Mwamzandi (2013), riwaya hii itaitenga hadhira isiyobobea katika fani mamboleo za kifasihi, na hivyo kutatiza ufuatiliaji wa dhamira zinazojitokeza.

Kama tulivyokwisha kutaja, riwaya ya *DY* imetungiwa katika mazingira ya Afrika katika enzi za baada ya uhuru. Kuambatana na maelezo ya Khamis (2005) kuwa riwaya za kiubaadausasa huangazia matatizo yanayakumba mataifa mengi katika bara la Afrika katika ulimwengu wa sasa. Huenda fensi anayoizungumzia Ndi- kwenye dondoo imetumika kitamathali kurejelea nyakati za mwanzo punde tu baada ya uhuru katika mataifa mengi ya Afrika. Katika dondoo, Ndi anarejelea ndoto zake za utotoni katika muktadha ambapo anaeleza namna dunia ya sasa ilivyojaa fujo na maangamizi yanayotufanya kushuhudia mambo ambayo hatujawahi kuyashuhudia (uk 68). Aidha, katika ndoto zake za utotoni, Ndi- anaeleza kwamba watu walimcheka na kumwita Nabii Yusufu mpya alipowaambia kuwa kungetokea njaa, kiu, ufukara, fitina, chuki na uchafu wa kila aina (uk. 70). Tunaweza kukisia kuwa furaha ya uhuru basi ilikuwa ya muda tu na baadaye watu wakaanza kupigana na kuuana kutokana na chuki, na uozo wa kila aina. Katika muktadha wa ulimwengu wa sasa, vita anavyoshuhudia Ndi- kwenye dondoo vinaweza kuchukuliwa kama vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vimewahi kushuhudiwa katika mataifa tofauti ya Afrika. Kwa mfano, katika mwaka wa 1994 kulikuwa na vita kati ya Wahutu na Watutsi nchini Rwanda. Aidha,

nchini Kenya kulikuwa na vita vilivyotokea baada ya uchaguzi wa 2007 ambavyo vilijikita katika misingi ya kikabila na kusababisha umwagikaji mwingi wa damu.

Urejeleaji wa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* katika *DY* unatupatia ushabaha uliopo kati ya dunia ya sasa (baada ya uhuru) na enzi za awali (wakati wa ukoloni) ambapo katika kila hali, kuna umwagikaji wa damu unaodhihirisha kuwa ulimwengu umejaa fujo, ghasia na maangamizi. Tofauti ni kwamba, katika *Dunia Mti Mkavu*, vita vilikuwa kati ya Wazungu na Waafrika ambapo Waafrika waliamini kuwa Wazungu ndio walikuwa kiini cha matatizo yaliyowakumba. Hii ndiyo sababu waligoma na hatimaye kuweza kumpinga mkoloni. Hata hivyo, katika *DY* kuna vita kati ya Waafrika wenyewe kupitia vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyotokana na misingi ya kikabila. Katika muktadha wa kibaadausasa, riwaya ya *DY* inaonekana kuhakiki simulizi kuu ya awali ambapo Waafrika wengi walishikilia kwamba matatizo yao yalitokana na Wazungu. Labda kwa kuyabainisha wazi matatizo yaya haya katika ulimwengu wa sasa, mwandishi wa *DY* atawachochea wasomaji kutafakari upya kiini cha matatizo yao ili wakabiliane nayo kikamilifu. Kwa msomaji anayeifahamu riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ulinganisho huu utabainika wazi kuliko ilivyo kwa msomaji ambaye haifahamu riwaya yenyewe.

Mwingiliano matini pia umejitokeza katika riwaya za utafiti huu kupitia marejeleo katika utanzu wa ushairi. Katika *UNN*, Utenzi wa Mwanakupona umerejelewa katika hadithi ya “Ndoa ya Giza” wakati babake Kasekesi anampa wosia bintiye anayeitwa Kasekesi. Kwa mujibu wa King’ei (2000) Mwana Kupona alikuwa mwandishi mashuhuri wa ushairi wa Kiswahili katika karne ya 19. Alimwandikia binti yake, Mwana Hashima, wosia kwa mtindo wa utenzi ambao unajulikana kama *Utenzi wa Mwanakupona*, ambao umerejelewa katika dondoo lifuatalo:

> Kumbuka mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba na ndiye anayekufadhili katika maisha yako; anayekuongoza kwenye mapito ya giza katika ulimwengu huu katili; anayekuelekeza unapokwenda kombo; anayekunasihi jinsi ya kuishi na wengine. Na uso wa kufadhiliwa u chini binti yangu. Mnyenyekee mumeo ili maisha yako yakunyookee mwanangu, **nadhani umesoma *Utenzi wa Mwana Kupona*** uliotungwa na mwanamke na anavyoeleza hayo! Mtunze vyema kabisa… (*UNN*, uk. 48).

Kama Mwana Kupona alivyomwasa bintiye, babake Kasekesi naye anamsihi bintiye amnyenyekee na amtunze mumewe vizuri. Katika dondoo, babake Kasekesi ametaja baadhi ya mamlaka aliyo nayo mwanamume juu ya mwanamke. Kwa mfano, tumetajiwa kuwa mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba na humwelekeza mwanamke anapopitia katika hali ngumu ya maisha. Aidha, yeye ni mshauri na nasaha zake humsaidia mwanamke kutangamana vyema na wenzake. Kutokana na mamlaka hayo, msomaji ambaye hajausoma utenzi anaweza kuelewa kwa kiasi tu sababu zinazomfanya baba mtu amwombe Kasekesi amtunze na amnyenyekee mumuwe. Hata hivyo, hataelewa ni kwa njia gani mwanamke humtunza mumewe na kumnyenyekea. Ili kupata ufasiri kamilifu wa wosia msomaji hana budi kurejelea utenzi wenyewe wa *Mwana Kupona.*

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* takriban beti kumi na nne za utenzi huu, hususan ubeti 23-36, zinahusu mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika ndoa (Shitemi 2010:174). Kwa mfano, ubeti wa (26) na (27) unaonyesha mamlaka aliyo nayo mume juu ya mke; kwamba, mwanamume ndiye huamua iwapo mkewe ataenda peponi au motoni, labda kutokana na namna mke alivyomtunza mumewe hapa duniani. Katika beti zinazofuata, Mwana Kupona basi anamshauri bintiye namna ya kumtunza mumewe baada ya kuolewa. Kwa mfano anapaswa kumyenyenyekea na kumheshimu mume wake. Asimkasirishe mume wake, amkaribishe vizuri afikapo nyumbani, amwandalie chakula na mahali pa kukaa, ampapase na ampepee hadi atakapolala.

Ufahamu wa awali wa utenzi huu basi ni muhimu katika kuifuatilia dhamira ya riwaya yenyewe kwa kuuelewa kikamilifu wosia wa bake Kasekesi kwa bintiye kuhusu sababu za mke kumtunza mume na namna anavyopaswa kumtunza. Hata hivyo, wosia huu umejikita katika utamaduni unaoongozwa na mfumo wa ubabedume ambao riwaya za utafiti huu zinauhakiki na kuusaili.

Katika *NZM*, tunapata mwingiliano matini dhahiri wakati mwandishi ameirejelea diwani ya *Sauti ya Dhiki* ya Abdilatif Abdallah. Hapa mwandishi, kazi yake na mawazo yake yametajwa kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> "Unatabiri nini?" Nilimuuliza amrijeshi wangu.
>
> "Sitabiri kitu," aliniambia, "najaribu tu kuieleza mbele ilivyo kwa kuitazama nyuma – kule kwenye jipu la tamaa lilikoanza kutunga usaha; **jipu la Abdilatif Abdalla wa *Sauti ya Dhiki*** ambalo limepasuka njiani na kuambua donda ndugu linalonuka na lisilopona. Ghafla nilichomwa na maumivu moyoni mwangu. Maumivu makali kushinda jipu la Adilatif Abdalla (*NZM* uk. 83).

Katika *Sauti ya Dhiki*, Abdilatif Abdalla amefafanua hili jipu katika shairi analoliita "Jipu". Katika shairi hili, msimulizi anaeleza uchungu unaouhisi kutokana na jipu lililokuwa makalioni mwake. Anasema kwamba mchana hawezi kufanya lolote na jioni hawezi kulala. Anatazamia siku ambapo jipu litaiva, aliminye hadi litumbuke. Ingawa atauhisi uchungu katika kufanya hivyo, huu ndio utakaokuwa mwisho wa dhiki yake. Jeraha litakalotokana na jipu hilo nalo atalitia dawa hadi litakapopona na aweze kuifurahia afya njema tena (Abdalla 1973:7-8). Kwa kuwa Abdilatif aliyaandika mashairi ya diwani hii akiwa gerezani, tunaweza kuliangalia shairi hili kama jazanda ambapo analinganisha jipu na dhiki au masaibu ya kuwa gerezani, huku akitazamia siku ambayo kifungo chake kingekamilika aweze kuurejea uhuru wake.

Katika *NZM* hali ya maisha ya msimulizi katika nchi yake ya Tanzania na Afrika kwa jumla yanalinganishwa na jipu la Abdilatif Abdalla katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki*.

Msimulizi anaeleza kwamba, Waafrika wanaonekana kurudi nyuma badala ya kwenda mbele. Tofauti na ilivyo katika *Sauti ya Dhiki* ambapo mwandishi anaonyesha matumaini ya dhiki yake kufika kikomo, msimulizi katika *NZM* anaonyesha hali ya kukata tamaa anaposema kuwa jipu "limepasuka njiani na kuambuka *donda ndugu* linalonuka na lisilopona". Anaiomboleza dhiki ya mataifa ya Kiafrika kwa kuilinganisha na jipu lililo na uchungu zaidi kuliko lile la *Sauti ya Dhiki*. Ufahamu wa jipu katika *Sauti ya Dhiki* unatuwezesha kupata taswira ya uchungu anaouhisi msimulizi katika *NZM* kuhusu hali ya kukatiza tamaa katika mataifa mengi ya Afrika.

### 5.3.2 Urejeleaji wa Fasihi ya Kiingereza

Mbali na fasihi ya Kiswahili, mwingiliano matini umejitokeza kupitia urejeleaji wa fasihi ya Kiingereza. Kwa mfano, riwaya za *DY* na *NZM* zimerejelea riwaya ya John Fowles, *The Collector,* lakini kwa njia na miktadha tofauti. Katika *DY* mwandishi amewarejelea wahusika wakuu wa *The Collector* ambao ni Clegg na Miranda:

> Lakini mimi kuwa laghai? Mimi kuwa mjanja na myang'anyi. Niliichukia hali hii nzima. Utafanyaje lakini, maji yanapojaa na kukuzunguka? Leo nilichelewa kurudi, zaidi kwa sababu baada ya kupata zile fedha, niliketi barazani mimi na shaibu tukawa tunasimuliana hadithi ya ukata, ukapa na upweke uliomzunguka Clegg na Miranda katika riwaya ya Fowles, *The Collector*. Ilinifungulia mawazo mapya kuhusu ulimwengu wetu ulivyogawika (*DY*, uk. 20).

Hadithi ya Ndi- katika riwaya ya *DY* ina mshabaha wa karibu sana na hadithi ya Clegg na Miranda katika The *Collector*, hasa kuhusiana na mambo matatu yaliyotajwa kwenye dondoo; ukata, ukapa na upweke. Kuhusiana na suala la upweke, Clegg katika *The Collector* alijitenga na ulimwengu kutokana na hali yake ngumu ya maisha aliyolelewa baada ya kifo cha wazazi na mjomba wake na kuishia kulelewa na shangazi yake aliyemtesa. Hali hii ni sawia na ya Ndi- katika *DY* anayejitenga na ulimwengu na kujifungia katika chumba kidogo baada ya kuporomoka kimaisha. Aidha, kama alivyo

Clegg, Ndi- analelewa na mjomba wake baada ya wazazi wake kufariki na mke wa mjomba akawa anamyanyasa. Kwa wakati fulani, Clegg aliwahi kuwa karani, lakini maisha yakamwendea kinyume na akafukarika, hali ambayo inashabihiana na ya Ndi-. Kwa hivyo, tunayaona maisha ya ukata katika malezi na maisha ya baadaye ya Ndi- sawia na yale ya Clegg. Katika dondoo Ndi- anaeleza kuhusu pesa alizozipata kwa bahati nasibu akiwa njiani, hali ambayo inashabihiana na ya Clegg ambaye alicheza mchezo wa bahati nasibu na akashinda kitita kikubwa cha pesa. Ushabaha huu unabainisha mwingiliano matini linganifu ambao Diegner (2005) anasema unahusu namna mwandishi anavyoathiriwa na kazi za waandishi wengine katika kuiandika kazi yake. Katika mwingiliano matini wa aina hii, tunaona namna Said Mohamed wa *DY* alivyoathiriwa na kazi ya msanii wa Uingereza, John Fowles(1963) aliyeiandika *The Collector.*

Katika riwaya ya *NZM* urejeleaji wa *The Collector* umejitokeza kwa njia nyingine lakini kwa kuwarejelea wahusika wao hao, yaani, Clegg na Miranda kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuta.

> Labda, kama nilivyo mimi hodari wa kusoma nyuso za watu, na Faisal alikuwa hodari hivyohivyo….Alikuwa mtu gani huyu? **Ni *psychic* kama Clegg[10] wa *The Collector*, au bazazi kama Idi wa *Kiu* au mwokota *bunga-yao* kama Sulubu wa *Nyota ya Rehema?*** Kwa nini nilimchunuku tu…kwa nini nilimfuata u mbali huu? Mbali na kitovu changu? Mbali na asili ya uzazi wangu? Mbali na salama yangu? (*NZM* uk. 115).

Katika dondoo, msimulizi ametaja uhodari wa Clegg wa kutumia akili, ubazazi wa Idi na upumbavu wa Sulubu. Ingawa Idi na Sulubu wanapatikana katika fasihi ya Kiswahili, sifa za wahusika hawa pamoja na zile za Clegg zimetajwa tu bila

[10] Riwaya ya *NZM* imetumia jina Gregg badala ya Clegg kama ilivyonukuliwa katika dondoo. Hii ni kwa sababu riwaya ya *The Collector* haina mhusika kwa jina Gregg bali kuna Clegg. Kutokana na haya, utafiti huu umechukulia kuwa mwandishi alimaanisha Clegg wala si Gregg, na hivyo basi kutumia jina Clegg katika utafiti huu.

kufafanuliwa, lakini zinamwafiki Faisal katika *NZM*. Kwa mfano, tunajiuliza nini hasa Clegg au Idi au Sulubu alichokifanya kiasi cha Nana kumlinganisha Faisal nao. Au ni vipi ulimwengu umegawanyika kwa mujibu wa Fowles katika *The Collector*. Majibu ya maswali haya yanategemea ufahamu wa riwaya zenyewe. Kwa msomaji wa riwaya ya *NZM* ambaye hajazisoma riwaya za *The Collector*, *Kiu* na *Nyota ya Rehema*, ulinganisho wa Faisal na wahusika Clegg, Idi na Sulubu mtawalia hautakuwa wazi. Katika dondoo hapo juu, Faisal alikuwa amemwezesha Nana kutoroka kwao na kumpeleka mahali ambapo Nana hakupajua. Ingawa baadaye tunakuja kufahamu kuwa Faisal alikuwa amemwelekeza Nana hadi kwa watu wa ukoo wake, katika muktadha ambapo anamtaja Clegg, Nana na hata msomaji hafahamu huko alikopelekwa na Faisal ni wapi na uhusiano wake na watu aliowapata huko. Jambo hili ndilo linalomtia wasiwasi Nana na anaanza kujiuliza Faisal ni mtu wa aina gani na alimpeleka huko kwa nia gani. Kwa kumlinganisha Faisal na Clegg, Nana anaona kwamba labda Faisal amempeleka mbali na nyumbani kwao kama mbinu ya kuweza kumshawishi ampende kama Clegg alivyomfanya Miranda. Kwa kumlinganisha na Idi, Nana anaona kwamba huenda Faisal anataka kumtumia ili ajinufaishe yeye mwenyewe, namna Idi alivyomtumia Bahati kwa manufaa yake binafsi. Anapomlinganisha na Sulubu huenda Nana anamwona Faisal kama mtu asiye na nia yoyote ya kumdhuru. Badala yake anaweza kuwa mtu mpumbavu tu anayeweza kudanganyika kwa urahisi na kuzifuata hisia na matakwa ya Nana namna Sulubu alivyodanganyika na hufuata hisia na matakwa ya Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Tunapoelewa muktadha ambao wahusika hawa wametumika, yaani Clegg, Idi na Sulubu, msomaji anaingiwa na hali ya taharuki sawa na ile aliyo nayo Nana kuhusu dhamira ya Faisal kwake. Tayari msomaji anafahamu kuwa Nana alikuwa na maradhi fulani alipofika huku alikopelekwa na Faisal. Msomaji anayeifahamu riwaya ya *The Collector* hana budi kuwa na kiwewe

na kuhofia kuwa huenda Nana atafariki namna Miranda alivyofariki. Jambo hili linampa msomaji hamu ya kutaka kuendelea kusoma ili afahamu kitakachomfika Nana katika makao haya mapya. Hivyo basi, dhamira ya mwandishi ya kujenga taharuki inaongezeka kwa msomaji anayeifahamu riwaya ya *The Collector*.

Mbali na kuonyesha mwingilaiano matini kati ya *DY* na *The Collector*, Ndi- anasema kuwa riwaya hii ya *The Collector* ilimfungulia mawazo mapya kuhusu namna ulimwengu wetu ulivyogawanyika (*NZM* uk. 20). Kwa kuwatumia wahusika Clegg na Miranda, Fowler katika *The Collector* alilenga kuonyesha athari za utabaka katika jamii. Kwa mfano, Miranda, aliyetoka katika tabaka la juu, anamdharau Clegg kwa sababu alikuwa wa tabaka la chini. Clegg naye anapomiliki mali anapata ujasiri wa kumteka nyara Miranda, hali ambayo hatimaye inaishia kumwuua Miranda. Katika *DY*, Ndi- anaposema kuwa aliposoma *The Collector* alielewa namna ulimwengu ulivyogawanyika, labda anarejelea mgawanyiko huu wa kitabaka kwa kurejelea viongozi wa Kiafrika waliochukuwa hatamu za uongozi na kutumia vyeo vyao kujitajirisha, ilhali wale walioongozwa na maadili kama yeye (Ndi-) wanafutwa kazi na kusababishiwa madhila ya kimaisha. Vilevile, tunaweza kukisia kwamba Ndi- anajisaili na kujiasa mwenyewe pale anapoona dosari na udhaifu wake mwenyewe. Licha ya kwamba alishikilia haki na usafi, Ndi- anaeleza kwamba amekuwa laghai na mnyang'anyi – jambo ambalo halimfurahishi. Kufuatana na mawazo haya ya Khamis (2005) marejeleo ya kazi ya Fowles katika *DY* yanaweza kuchukuliwa kama mtindo unaotumiwa na riwaya katika kuwazindua wanajamii, hususan Waafrika, waache kuelekeza kidole cha lawama kwa watu wengine (labda wazungu na viongozi) lakini pia wajisaili wenyewe na waone ni wapi wanapoweza kulaumiwa ili waweze kubadilika. Mabadiliko ya jamii nzima bila shaka yatatokana na mabadiliko ya watu binafsi.

### 5.3.3 Urejeleaji wa Filamu

Riwaya za utafiti huu zimerejelea filamu za aina mbalimbali. Kwa mfano riwaya ya *UNN* imerejelea filamu ya vichekesho ya *Cedric the Entertainer (uk. 93)*, filamu ya vibonzo ya *Tom and Jerry* (uk. 69), filamu za kimagharibi zinazotokea katika runinga kama vile *El Cuerpo Del Deseo (uk. 85)* miongoni mwa filamu nyingine. Katika dondoo linalofuata tumejikita katika filamu ya *El Cuerpo Del Deseo*, ambayo ni filamu kutoka Mexico iliyoandikwa kwa lugha ya Kihispania lakini pia imetafsiriwa kwa Kiingereza na kuitwa *The Body of Desire.*Tafsiri yake ya Kiswahili basi inaweza kuwa *Mwili wa Matamanio* kama inavyorejelewa kwenye dondoo linalofuta:

> Akaambiwa hao wasio na elimu ndio hatari zaidi. Anaishi nchi gani? Hajaangalia vipindi vya runinga hasa *Soap Operas* za Marekani ya Kusini vinavyopendwa, vinavyopapatikiwa hasa, nchini na kila mtu? Hajamwona Salvado Cerinza, mkulima aliyekuwa mbu mbu mbu mzungu wa reli, jitu lililoburutwa mbele na silka ya mnyama na kuongozwa kama ng'ombe wa shemere na mkewe Cantalicia, aliyekufa, akatoka kwenye jeneza kwa kishindo kabla ya mazishi yake na kutimua mbio, akaongea Kilatini akamshinda kasisi na hata akakisoma Kifaransa? Akawa bingwa wa kucheza piano? Hajui *El Cuerpo Del Deseo* (Mwili wa Matamanio)? (*UNN* uk. 85).

Filamu ya *El Cuerpo Del Deseo* ambayo pia hujulikana kwa jina *Second Chance* (Nafasi ya Pili) ilionyeshwa hapa nchini Kenya katika runinga ya Citizen mwaka wa 2005. Filamu hii inahusu mhusika mkuu wa kiume anayeitwa Pedro Jose Donoso na aliyekuwa tajiri kupindukia. Pedro anapokufa roho yake inaingia ndani ya mwili wa Salvador Cerinza, mwanamume maskini lakini mtanashati aliyeishi sehemu za mashambani akiwa na mkewe, Cantalicia. Kwa hivyo, kupitia roho ya Pedro, Salvador anawezeshwa kurithi mali nyingi. Kisa hiki kimerejelewa kwa ufupi katika *UNN* kwenye hadithi ya "Vuta n'kuvute" kumlinganisha Farouk na Salvador. Mamake Zahra aliyekuwa nduguye Farouk anakamatwa na polisi kwa madai kuwa Farouk, alikuwa gaidi. Mamake Zahra anaulizi ni vipi Farouk anavyoweza kuwa gaidi ilhali hata hajawahi kuingia shuleni akajua kusoma na kuandika. Katika kulijibu swali la mamake

Zahra, polisi wanarejelea kwa kifupi wahusika Salvado Cerinza katika filamu ya *El Cuerpo Del Deseo* kuonyesha kuwa hata watu ambao hawajasoma au wanaodhaniwa kutojua lolote wanaweza kutenda mambo ambayo hawatarajiwi kuyatenda. Jinsi ambavyo Salvador Cerinza aliishia kumiliki mali nyingi licha ya kuwa alikuwa mtu maskini, na hatimaye akaweza kuzungumza Kifaransa kinyume na matarajio ya wengi, vivyo hivyo, Farouk anaweza kuwa gaidi hata kama ndugu zake hawamtarajii kuwa vile. Kisa hiki kumetumika kuiendeleza dhamira ya hadithi hii ya "vuta n'kuvute" kuhusu ukosefu wa haki kwa walio wanyonge. Mbali na kutowatendea haki wanyonge, tunawaona wenye nguvu wakitumia mbinu tofauti kuhalalisha matendo yao maovu. Ingawa hatuwezi kueleza kwa uhakika kama kweli Farouk alikuwa gaidi au la, tunaweza kukisia kwamba Farouk alisingiziwa kuwa gaidi kutokana na wingi wa visa vya wanyonge wanaodhulumiwa katika hadithi hii ya "Vuta n'kuvute". Kwa mfano, hatuelewi ni kwa nini mamake Zahra akamatwe na kutiwa jela kwa makosa ya kusingiziwa, na hasa akiwa mja mzito. Hata hivyo, polisi wanatumia filamu ya *El Cuerpo Del Deseo* kuhalalaisha tendo lao la kumhusisha Farouk na ugaidi bila kuwepo na ithibati yoyote.

### 5.3.4 Marejeleo ya Kidini

Marejeleo ya wahusika au mawazo yanayohusiana na dini yamejitokeza katika riwaya za *UNN* na *DY*. Waandishi wa riwaya hizi wametoa marejeleo yao hasa kutokana na misingi ya dini ya Kikristo na Kiislamu kwenye Biblia na Koran mtawalia. Labda jambo hili limetokana na sababu kuwa waandishi wa riwaya hizi wana misingi yao ya kidini katika Ukristo au Uislamu. Mengi ya marejeleo hayo hasa yamezingatia wahusika na matukio ambayo wasomaji wenye misingi katika dini hizo wanayaelewa kwa urahisi. Baadhi ya matukio yametajwa waziwazi huku mengine yakiashiriwa tu

hivi kwamba msomaji ambaye hana msingi wowote wa dini hizi hawezi akatambua kuwa yana misingi ya kidini. Tazama mifano ifuatayo:

> Huyu ni **Jezebel**i wa pili" alisema Pasta. Kisa cha Jezebeli nilikikumbuka kutoka zamani nilipokwenda kanisani kutokana na amri ya baba ambaye alivutiwa sana na mhubiri mwenyewe, babake Kaminda. Alikuwa mke wa Mfalme Ahab. Siku moja alimwendea jirani yake Nabothi, aliyekuwa na shamba la mizabibu. Akatamani kuligeuza shamba la mboga na kumwahidi Nabothi shamba jingine au hata fedha. Nabothi naye hakutaka kuutoa urithi wa wazazi wake. Ahabu akakasirika na kwenda zake nyumbani. Hata chakula hakuweza kula. Jezebeli alipomdadisi akatambua kisa cha huzuni yenyewe. Akamwambia ni rahisi, Nabothi afanyiwe mashtaka ya ghushi. Watafutwe watu watakaomsingizia. Hatima yake Nabothi ashtakiwe kwa kumtukana Mungu na mfalme. Hatima yake: kupigwa mawe hadi afe (*UNN* uk 60).

Kisa kuhusu Jezebeli kinapatikana katika Biblia (1 Wafalme 21: 1-13) na kimerejelewa na kufafanuliwa kikamilifu katika hadithi ya "Ndoa ya Giza" ya riwaya ya *UNN* kama inavyojitokeza katika dondoo hapo juu. Kwenye hadithi hii, Kasekesi analinganishwa moja kwa moja na Jezebeli kurejelea ukatili wake ambao umebainishwa wazi wazi. Haya yanawezesha msomaji kuifuatilia dhamira ya hadithi hii. Hii ni tofauti na ilivyo katika mifano inayofuata ambapo ni majina ya wahusika pekee yaliyotajwa:

> Tunachotaka ni jina ehh… tunataka jina kama la wanawake tunaowajua…majina wanayopewa wanawake kama **Hawa, Jezebel, Delilah**…(*UNN* uk 15)

Hawa na Delilah na Jezebel ni majina ya wahusika wa kike wanaopatikana katika Biblia na ambao waliwalaghai wanaume kwa njia moja au nyingine. Yanapotumika katika riwaya ya *UNN*, yanaonyesha mtazamo hasi walionao wanaume kuhusu wanawake. Tunaelezwa kuwa wahudumu wa kiume wanaomhudumia mwanamke aliyekuwa kwenye hali mahtuti walitaka ajitambulishe. Ingawa kitu cha pekee anachokikumbuka mgonjwa huyu ni jinsia yake (kwamba yeye ni mwanamke) wanamtaka ajitambulishe kwa kutumia majina halisi, na hapa ndipo wahudumu wanataja baadhi ya majina ya wanawake ambayo wangetaka mwanamke huyu ajinasibishe nayo kama vile Hawa,

Jezebeli na Delilah. Dhamira kuu katika *UNN* inahusiana na suala la utambulisho. Mwandishi inalenga kupinga mawazo jumuishi ambayo wanajamii hutumia kutambulisha watu kutokana na jinsia yao. Aghalabu utambulisho jumuishi, kama ulivyo katika dondoo, unaishia kumbeza na kumdhalilisha mwanamke kwa kumsawiri kama kiumbe katili, jambo ambalo si la kweli kwa kila mwanamke. Mwandishi basi anapendekeza kuwa watu wanapaswa kutambulishwa kama watu binafsi, au hata kupewa nafasi ya kujitambulisha wao wenyewe.

Mhusika mwingine wa Biblia aliyerejelewa katika riwaya ya *DY* ni Samson kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Ndi- alikuwa kakamata mifumbati ya chuma iliyosimama kwa kedi na inda kumtenganisha yeye na ukoo wake pale jela-ya-wendawazimu. Upande huu na huu, kulikuwa na askari waliosimama na bunduki kumlinda Bi M na Yungi, pindipo Ndi-, kama mbabe katika hadithi ya **Samson na Delilah**, angevunja lile tundu la chuma na kutoka nje… (*DY* uk. 195).

Katika dondoo hapo juu, kisa cha Samsoni na Delilah kimerejelewa ili kumlinganisha Ndi- na Samsoni wa Biblia anayefahamika kutokana na nguvu zake: Kwenye Biblia kisa cha Samson ni aina ya mighani inayotumika kueleza kuhusu nguvu za kiajabu alizokuwa nazo. Kwa mfano, anatumia nguvu zake kung'oa milango ya lango la maadui zake alikokuwa amefungiwa, na kuibeba kwa mabega hadi kileleni cha mlima (Waamuzi 16: 2-3). Msomaji anayekifahamu kisa hiki cha Samsoni atapata taswira nzuri zaidi ya kufungiwa alikofungiwa Ndi- ndani ya gereza, jinsi Samsoni alivyojipata amefungiwa ndani ya mji wa maadui zake. Aidha, taswira ya Ndi- kuikamata mifumbati ya chuma inampa msomaji taswira sawia na ile ya Samson ya kukamata milango ya lango la maadui zake na kuiong'oa. Hata hivyo, ulinganisho huu unajitokeza kama kinaya kwa sababu Ndi-, tofauti na Samsoni, alikuwa dhaifu na hata hakuhitaji ulinzi wa askari wenye bunduki mradi tu alikuwa amefugiwa sawasawa kwenye jela.

### 5.3.5 Marejeleo ya Mashujaa wa Kihistoria

Mashujaa tofauti wa kihistoria, wanaotoka ndani na nje ya mipaka ya bara la Afrika wamerejelewa hasa katika *DY* na *NZM*. Mashujaa hawa ni pamoja na Patrice Lumumba, Jomo Kenyatta, Julius Nyerere, Mahatma Gandhi, W.E.B. Du Bois, Frantz Fanon**,** Kwame Nkuruma, Nelson Mandela, Cabral, Ben Bella na Rodney:

> Ninyi [Ndi- na wengine] ni mfano mzuri wa kutaka kujiua kwa ajili ya wengine…ndio maana mnaitwa wakorofi na wale wakaidi wanaotaka kujenga nyumba bila ya kubarikiwa au wanaokusanya mali kwa nafsi zao na jamaa zao tu. Dunia yetu haikuwa hivi. Yenu, isiwe wala haitaweza kuwa kama yetu, lakini mmewacha mengi mazuri tuliyokurithisheni. Mtaangamia. Sasa [joshijitu] lilikwenda tena kwenye kivuli cha meza, likainua kile kibuyu cha kilewevu, likainua pembe ya urithi ya faru na kuijaza kilewevu. Likawa linapita likimwaya matone ya kilewevu huku likisema. **Hii ya Lumumba, hii ya Neto, hii ya Cabrel, hii ya Rodeny, hii ya Samora**…Na…na …na… Orodha ya waliopewa kinywaji pasi na kuonekana ilikuwa ndefu (*DY* uk. 193). [msisitizo wetu]

Katika *DY*, Lumumba, Cabrel, Rodeny na Samora wanarejewa katika kago la wazee. Kwenye faharasa ya *DY*, S. A. Mohamed ameeleza kago kama kinga dhidi ya uchawi au jicho mbaya. Lumumba na wengine waliotajwa katika dondoo ni baadhi tu ya wanajamii mashuhuri katika historia ambao hawakuwa na ubinafsi wa kujilundika mali kwa ajili yao binafsi na jamaa zao. Badala yake walijitolea kufa kwa ajili ya jamii nzima. Ingawa riwaya inaeleza kuhusu watu kuirejelea asili yao, hii haimaanishi kwamba wanajamii wanapaswa kurejea yote yanayohusishwa na ukale na kuupuuza usasa. Mwandishi anakikejeli kizazi kinachouchukulia ukale kama jambo lisilo la maana na kukumbatia usasa bila kuchuja lolote. Badala yake anawataka wanajamii kukumbatia ukale na usasa ulio na manufaa na kujiepusha na athari hasi za ukale na usasa. Kwa hivyo, lengo kuu la kago lilikuwa ni kuwakinga wanajamii kutokana na athari hasi za usasa na utandawazi uliosababisha ubinafsi na maangamizi. Katika mtazamo wa ubaadausasa, tunaweza kuchukulia kwamba mwandishi anataka kuvuruga imani kwamba usasa ni mzuri huku ukale ukichukuliwa kuwa mbaya na uliopitwa na

wakati. Badala yake, anataka wasomaji watafakari upya ukweli kuhusu ukale na usasa kwa kukumbatia yaliyo mazuri na kupuuza yaliyo mabaya.

Ingawa katika *DY* mwandishi anaonekana kutambua juhudi za mashujaa hawa wa kihistoria, na hasa kujitolea kwao katika kuwakomboa Waafrika kutoka pingu za wakoloni, jambo hili linaonekana kuchukua mtazamo tofauti katika *NZM*:

> Sasa lakini inambidi alipatie maana neno mapinduzi. Alitaka kulizamia upya neno hili. Afikie vivuli vyake na mbali kwa fikra za karibu. Je, kwa mfano, kumewahi kuwa na wanamapinduzi wowote huku kwetu? **Lumumba? Cabral? Ben Bella? Nkuruma? Kenyatta? Nyerere? Mandela? Rodney? Dubois? Fanon, Gandhi? Malcolm X? Nani?** Nani? Nani? Fasili nzuri ya neno hili labda ni kubadilisha maovu na kuleta mema. Kama hakuna mema katika mabadiliko yoyote, mapinduzi huwa hayakufanyika na wanaojinasibu, bure wanajivika vilemba vya ukoka (*NZM* uk. 220) [msisistizo wetu].

Licha ya kuwa wahusika hawa walitoka katika nchi na tofauti, walikuwa na jambo moja linalowatambulisha. Wote walikuwa katika mstari wa mbele katika kupigania haki za wanyonge na waliodhulumiwa hasa kwa misingi ya rangi. Wengi kati yao hasa walikuwa viongozi wa kisiasa waliopigania uhuru katika nchi zao dhidi ya wakoloni, kama vile Kenyatta (Kenya), Nyerere (Tanzania), Mandela (Afrika Kusini), Fanon (Algeria), Gandhi (India) na Lumumba (Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo). Du Bois ambaye alikuwa Mmarekani mweusi alisaidia katika kuandaa mikutano ya *Pan African Congress* kwa nia ya kuwakomboa Waafrika kutokana na nguvu za wakoloni. Aidha, alitetea kuwepo na haki sawa kwa watu weusi waliobaguliwa na utawala wa wazungu katika Marekani ya Kusini. Mwandishi katika *NZM* anamtaka msomaji atafakari upya maana ya neno mapinduzi hasa kwa kuwarejelea hawa mashujaa wa kihistoria. Mwandishi anakubali kwamba mashujaa hawa walihusika kwa njia moja au nyingine katika kuleta mabadiliko hasa ya kisiasa katika nchi zao. Hata hivyo, mwandishi anataka msomaji kujiuliza iwapo mabadiliko hayo yalikuwa na athari yoyote chanya kwa wanajamii au ni mabadiliko tu ya viongozi wa kisiasa, ilhali maovu yaliyokuweko

yaliendelezwa katika enzi zao. Kwa mfano, Gooding- Williams (2020) anaeleza kwamba Du Bois alikuwa na shauku kubwa ya kuwahamasisha watu dhidi ya matumizi ya vifaa vya kinyuklia. Mengi ya mapendekezo yake aliyoyatetea yalitekelezwa mwaka wa 1964, mwaka mmoja baada ya kifo chake. Utekelezaji wa mapendekezo ya Du Bois unaonyesha mabadiliko yaliyoleta mema sio tu katika nchi yake bali ulimwengu kwa jumla.

### 5.3.6 Marejeleo ya Wanafalsafa na Wanasaikolojia

Riwaya za *UNN* na *NZM* zimewarejelea wanafalsafa wa kimagharibi kama vile Fredrich Nietzsche, Aristotle, Plato, Karl Marx pamoja na mwanasaikolojia, Sigmund Freud. Kwa mujibu wa Clayton (2012:7), mojawapo ya mihimili ya ubaadausasa ni kuhakiki mawazo yanayopatikana katika vitabu vinavyotambulika katika nyanja tofauti za maisha kama vile kiakademia au kitamaduni. Akieleza zaidi kuhusu vitabu vilivyotambulika (canon), Clayton anasema kuwa:

> Hizi ni kazi ambazo zimetengwa na kuonekana kuwa muhimu sana na za kipekee hivi kwamba yeyote anayehitaji kufanya utafiti katika uwanja husika hana budi kuzirejelea kutokana na wingi wake wa maarifa (TY).

Kulingana na Clayton (2012) wakakiki wa kibaadausasa hujaribu kudhihirisha kuwa kazi hizi ni orodha tu ya vitabu vyenye mawazo kandamizi yanayolenga kuendeleza mahitaji ya kikundi fulani cha watu, kiwe cha kijamii, kijinsia au kirangi. Katika kuzihakiki kazi zenyewe wanaubaadausasa huonyesha namna kazi zenyewe hupendelea kikundi fulani huku kikundi kingine kikibaguliwa. Aidha, wanajaribu kutafuta njia mbadala ya kuzisoma kazi zile ili kupindua usomaji uliozoeleka wa kazi hizo. Sehemu hii itashughulikia kwa undani mawazo ya mwanasaikolojia, Sigmund Freud, na mwanafalsafa, Fredrich Nietzsche ili kubainisha namna mawazo yao yanavyojitokeza kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya ubaadausasa.

Sigmund Freud ni mmoja wa wanasaikolojia ambaye mawazo yake hayana budi kurejelewa na wasomi wanaofanya saikolojia. Hivyo basi mawazo yake ni mojawapo ya kazi maarufu iliyotambulika katika uwanja wa saikolojia. Katika riwaya ya *UNN* mawazo ya mwanasaikolojia huyu yamerejelewa kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> "… Kumbuka huu ni ukweli wa kisayansi! Mwanamke ni mwepesi wa hisia tu…Chuoni hukumsoma Sigmund Freud wewe?"….
> " Ni watu dhaifu kabisa hawa! Wanyonge katika nyanja zote na si kwa sababu nyingine ni kwa sababu ya upungufu fulani… "Kinachowatawala hawa ni hisia, hisia na hisia, yaani *eros*!!! (uk. 17-18).

Kutokana na dondoo hili, mawazo ya Freud yanadhihirisha mambo matatu kumhusu mwanamke, yaani, mwanamke ana upungufu fulani, ni kiumbe dhaifu na kuwa anaongozwa na hisia. Ingawa huu ni mfano wa mwingiliano matini dhahiri ambapo jina na mawazo ya mwanasaikolojia huyu yametajwa, uelewa kamili wa dhamira ya hadithi hii unaweza kutatizwa kwa mtu ambaye hajamsoma Sigmund Freud. Tumefafanua kwa kifupi mawazo haya ya Sigmund Freud kumhusu mwanamke katika sehemu inayofuata.

Katika dondoo tumeelezwa kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu kutokana na upungufu fulani lakini upungufu wenyewe haukutajwa. Katika nadharia zake maarufu za tanzo la Edipode na tanzo la Elektra zinazohusiana na mtoto wa kiume na mtoto wa kike mtawalia, Sigmund Freud anaeleza kuwa mwanamke ana upungufu unaohusishwa na ukosefu wa zubu (McLeod, 2013; Zakin (2011). Kwa mujibu wa Freud wakati mtoto wa kike anatimiza umri wa miaka mitatu anatambua kuwa hana zubu na katika ung'amuzibwete wake anaanza kutamani kuwa angelikuwa mvulana. Ukosefu huu wa zubu unamfanya mtoto wa kike kujihisi kama kiumbe dhaifu kwa kufikiria kuwa alihanithishwa na anapata kile Freud anachokiita *wivu wa zubu*. Ukosefu huu wa zubu ndio unaorejelewa katika dondoo kama upungufu alio nao mwanamke na ambao

unamfanya kuwa kiumbe dhaifu akilinganishwa na mwanamume. Aidha, Freud anaeleza kuwa udhaifu wa mwanamke unatokana na sababu kuwa dhamiri yake ni dhaifu kwa sababu yeye huongozwa na hisia (Eros). Akifafanua maelezo haya ya Freud, Zakin (2011), anaorodhesha viwango vitatu vya utu wa binadamu ambavyo huathiri matendo yake. Vipengele hivi ni silika, nafsi na dhamiri (id, ego and superego) na hukua na kuimarika katika hatua tofauti za maisha ya binadamu. Silika ndicho kipengele cha kimsingi kinachopatikana katika ung'amuzibwete. Silika huongozwa na hisia za papo hapo za kutaka kutimiza shauku za binadamu na matamanio yake tofauti bila kuzingatia hali halisi ya maisha, maadili au matokeo ya matendo yake. Hii ni kwa sababu lengo la silika ni kujifurahisha na kujistarehesha. Silika imegawika katika matapo mawili; *eros* na *thantos*. *Thantos* inahusishwa na hisia za ushari, ugomvi na kifo. *Eros* nayo inahusishwa na hisia za uhai ambazo ni pamoja na hisia za kufanya ngono, matamanio ya kuishi au kuwa hai, pamoja na hisia za kutimiza mahitaji mengine ya kimingi kama vile kula chakula na kukata kiu. Kulingana na Freud, wakati mtoto wa kike anapotambua kuwa hana zubu anashindwa kuacha kuyang'angania mapenzi ya baba yake, na hivyo basi daima anaongozwa na hisia hizi. Kwa hivyo dhamiri yake inakuwa dhaifu kwa sababu inashindwa kudhibiti matakwa ya silika.

Ni bayana kuwa mawazo ya Freud yanashughulikia suala la jinsia kwa mtazamo wa jozi kinzani la kiume/kike. Katika jozi hii mwanamume huchukuliwa kuwa bora na mkamilifu huku mwanamke akichukuliwa kuwa dhaifu na aliyepungukiwa kwa kukosa zubu. Kwa hivyo mwanamke anaelezwa na kufafanuliwa kwa misingi ya jinsia ya kiume. Haya yanaoana na mawazo ya wahakiki wa kibaadausasa kama Luce Irigaray wanaorai kuwa kazi zilizotambulika katika nyanja tofauti za kiakademia na kitamaduni huwa na mapendeleo ya kikundi fulani huku kikundi kingine kikikandamizwa na kubaguliwa (Zakin, 2011; Clayton 2012). Akiihakiki nadharia ya udodosinafsi ya

Freud, Irigaray kwa mfano anaeleza kuwa nadharia hii humfasiri mwanamke kwa misingi ya jinsia ya kiume. Yaani, mwanamke hufasiriwa kama mwanamume aliyekosa zubu au aliyehanithiwa, hivyo kufanya jinsia ya kike kutowakilishwa au kutambulishwa kwa njia yoyote ile. Irigaray basi anapendekeza kuwa inafaa kuieleza na kuifafanua kila jinsia kivyake bila kuihusisha na jinsia nyingine. Ingawa Irigaray hajaeleza utambulisho wa jinsia ya kike ungetokana na nini, anawahimiza wanawake kuutangaza utambulisho wao kwa njia iliyo hakika na inayofaa. Mtazamo huu wa Irigaray na wanaubaadausasa kwa jumla ndio unaoelekea kujitokeza na kuendelezwa katika riwaya nzima ya *UNN* kwa kujaribu kuivunja jozi kinzani ya mwanamume/mwanamke. Kwa mfano katika riwaya ya *UNN* tunawapata wanaume wanaomhudumia Mwanamke hospitalini. Wanasisitiza kuwa wanataka kulijua jina lake halisi linaloonyesha utambulisho wake halisi kama vile kusema yeye ni binti ya mwanamume gani au mke wa mume yupi (*UNN* uk.33). Mawazo ya wanaume hawa yanaonekana kuegemea katika nadharia ya Freud ya udodosinafsi ambapo utambulisho wa mwanamke unaelezwa kwa misingi ya jinsia ya kiume. Kwa mfano wanataka ajitambulishe kama binti ya mwanamume fulani au mke wa mwanamume fulani. Hata hivyo, mwanamke anachukua mtazamo wa kibaadausasa kwa kuonyesha kuwa mwanamke anaweza kutambulishwa kivyake bila kuambatanishwa na mwanamume kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Wanasema ninalolikumbuka ni moja tu: kwamba ni mwanamke. Je, kwa nini wanaliona dogo hilo? Kwa nini wanadhani hilo dogo? Kuwa mwanamke dogo? Hawa vizuu walizaliwa na mwanamke kweli au walianguliwa? Au...walipotosha historia kwa utamaduni kujipendelea, walizaliwa na mwanamume? …Kuna njia nyingine ya kujitambulisha inayozidi hii. Hawajui kuwa jina ni kitu unachopewa na mtu mwingine? Kwamba jina ni mtazamo wa mtu wa nje? Mtazamo wa ndani ni huu wanaoukataa? (uk.8).

Kutokana na dondoo hili Mwanamke anakataa kutambulishwa kwa mtazamo wa nje ambao hauna budi kumhusisha na mwanamume kwa njia moja au nyingine. Badala

yake anataka kutambulishwa kwa mtazamo wa ndani kama kiumbe kamilifu anayeweza kuelezewa kivyake. Aidha, katika dondoo na riwaya nzima kwa jumla tunayaona mawazo ya wanawake wakionyesha nafasi yao katika kuzaa na kuwalea watoto, wale wa kiume wakiwemo (uk 140), hali inayowapa utambulisho wao wa kipekee. Ni bayana basi kuwa ufahamu wa nadharia ya Freud ya udodosinafsi pamoja na uelewa wa mawazo ya wahahkiki wa nadharia hii utampa msomaji nafsi nzuri zaidi ya kuelewa dhamira inayohusiana na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *UNN* kinyume na ilivyo kwa msomaji asiye na ufahamu huo.

Riwaya ya *NZM* inadhihirisha mwingiliano matini unaorejelea wanafalsafa maarufu kama vile Plato, Aristotle, Hegel na Nietzsche kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Kuthubutu kulianzishwa na Nietzsche alipotangaza *God is Dead*. Baada ya hapo rutuba ya wema ilipangusika haraka haraka juu ya udongo kuanzia wakati ule. Na watu, bila ya kujua pengine, walianza kutafuta vitu vingine kuvitawaza badala ya Mungu. Ikawa kama wametafuta Miungu mingine kusimamishia matakwa yao badala ya kuabudu na kumcha Mungu waliyemjua tokea zamani. Mungu mkubwa wa sasa ni pesa, na ukitaka ukwasi wa pesa unahitaji uwe na nguvu za Kiungu. Ukitaka unaweza kujifaharisha na *sagacity* na *traditional philosophy* iliyomo kwenye methali, wakati watu wanajikuza na kujitutumua zaidi na zaidi: *juu, juu, juu zaidi* kwa kukusanya pesa. Pia ukitaka kupumbazwa na kubaradhulika na Plato, Aristotle na Hegel shauri yako, lakini mtowe Nana. Nana siye. Hayumo. Yeye ameshawasoma hawa, anawajua vizuri, hawambabaishi (*NZM* uk. 195-196).

Katika dondoo hapo juu, kuna mwingiliano dhahiri na mwingiliano matini usodhahiri. Katika mwingiliano matini usodhahiri majina ya wanafalsafa kama Plato, Aristotle na Hegel yametajwa tu. Japo tumetajiwa kuwa wanafalsafa hawa wanaweza kumpumbaza mtu, mwandishi hajafafanua ni kwa njia gani au kile hasa walichokifanya kiasi cha kumpumbaza mtu. Urejeleaji kama huu unaweza kumtatiza msomaji asifahamu mawazo ya wanafalsafa hawa katika kufuatilia kikamilifu dhamira inayolengwa na

mwandishi. Sehemu hii hata hivyo imejikita katika mwingiliano matini dhahiri ambapo jina la mwanafalsa Nietzsche limetajwa pamoja na kauli yake, *God is Dead*, ambayo tumeelezwa kuwa iliathiri mtazamo wa watu kuhusu Mungu na utendaji wa wema. Hata hivyo, maelezo haya yametolewa kwa muhtasari sana hivi kwamba msomaji anahitaji kufanya utafiti zaidi kumhusu Nietzsche ili kufuatilia dhamira inayolengwa na mwandishi.

Kwa mujibu wa Anderson (2022), Fredriech Wilhelm Nietzsche alikuwa mwanafalsafa maarufu wa Kijerumani aliyeishi kati ya mwaka wa 1844 na 1900. Baadhi ya mawazo yake yalihusiana na uhakiki wa suala la urazini (reason) na ukweli pamoja na uhakiki wa masuala ya kidini, hususan suala la maadili katika dini ya Kikristo. Nietzsche aliamini kuwa falsafa ilipaswa kushughulikia kwa kina zaidi mahitaji ya kibinafsi ya kila binadamu. Hii ingewezekana kwa kutupilia mbali maadili na amali za kitamaduni na kidini. Kauli yake maarufu, *God is Dead*, ambayo tafsiri yake kwa Kiswahili ni *Mungu Amekufa*, inapatikana katika baadhi ya kazi zake hasa *The Gay Science* (Anderson 2022). Kauli hii inadhihirisha mtazamo wa Nietzsche kuhusu maisha ambapo alipinga mawazo ya wanafalsafa wa kimapokeo pamoja na yale ya maadili ya kidini, hususan dini ya Kikristo. Nietzsche alishkilia kuwa dini ya Kikristo hutuelekeza katika msingi fulani ambapo maamuzi yetu kuhusu kilicho chema/kiovu huegemezwa. Kwake, Nietzsche maamuzi yetu hayafai kuegemezwa katika msingi wowote ule bali kila binadamu anafaa kuruhusiwa kufuata sheria zilizoko ndani yake. Kauli yake basi kuwa *Mungu Amekufa* iliashiria kuwa Nietzsche alitupilia mbali imani ya dini ya Kikristo kuhusu suala la maadili, kwa kupinga kuwepo mtazamo bia kuhusu suala hili.

Mawazo haya ya Nietzsche yanaambatana na mawazo ya wanaubaadausasa ambao hukataa kuwepo kwa msingi mmoja ambao tunauegemea katika kufanaya uamuzi wetu au kueleza ukweli wowote. Ni kutokana na kauli hii ambapo Nietzsche huchukuliwa

kama mmoja wa watangulizi wa ubaadausasa hata kabla ya istilahi yenyewe kuasisiwa. Katika dondoo (hapo juu) kauli ya Nietzsche imerejelewa na Nana katika riwaya ya *NZM* anayesema kuwa kuthubutu kulianza na Nietzsche alipotangaza kuwa *Mungu Amekufa*. Anaitumia kauli hii kama jazanda ili kuwazindua Waafrika ambao wametumikishwa na watu wa mataifa ya Kimagharibi kwa kuonyeshwa kuwa hawawezi kuendelea mbele bila kutegemea mataifa haya ya Kimagharibi. Anawataka Waafrika wadhubutu, kama walivyodhubutu Nietzsche, kwa kukoma kutegemea 'ukweli wa Kimagharibi' na badala yake wajiamini kuwa wanaweza kuyatatua matatizo yao. Ingawa msomaji anaweza kung'amua maana inayorejelewa na maneno ya Nietzsche kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake, ufahamu wa maelezo yake utampa msomaji uelewa zaidi na wa haraka wa dhamira hii ya utegemezi na athari zake.

**5.4 Hitimisho**

Sura hii imejadili namna mwingiliano matini ulivyojitokeza kama kunga ya uandishi katika riwaya tatu za utafiti huu. Imebainika kwamba riwaya zote za utafiti huu zimedhihirisha mwingiliano matini kwa kurejelea matini za aina mbalimbali kama zile za fasihi ya Kiswahili, fasihi ya Kiingereza, filamu, marejeleo ya kidini, marejeleo ya mashujaa tofauti wa Kihistoria, pamoja na marejeleo ya wanafalsafa na wanasaikolojia mbalimbali. Urejeleaji wa matini hizi unakaidi itikadi ya mwondoko wa usasa uliopendekeza uasili wa kazi za sanaa. Matumizi ya mwingiliano matini basi yanaambatana na maelezo ya Lyotard (1979) ya kuzipuuza simulizi kuu kama vile Usasa na badala kuibuka na njia anuwai za kujieleza. Imebainika kuwa waandishi wa riwaya za utafiti huu wametumia viwango vitatu vya mwingiliano matini, yaani, wametumia mwingiliano matini dhahiri na mwingiliano matini usodhahiri na mwingilaano matini linganifu ili kuendeleza dhamira tofauti katika kazi zao. Baadhi ya dhamira hizo ni pamoja na utabaka, utu na uwajibikaji, ukabila na vita vya wenyewe

kwa wenyewe, mahusiano ya kijamii na utambulisho wa kijinsia miongoni mwa dhamira nyingine. Dhamira hizi zimetumika kuonyesha baadhi ya matatizo yanayoyakumba mataifa ya Afrika katika karne ya ishirini na moja.

Aidha, matumizi ya mwingiliano matini katika riwaya za utafiti huu yamefanikisha dhima ya wanaubaadausasa ya kutambua nafasi ya kazi za waandishi wengine ambazo zimewaathiri waandishi wa riwaya za utafiti huu kwa njia moja au nyingine katika kuunda kazi zao. Hata hivyo, matumizi ya mwingiliano matini wakati mwingine humtatiza msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti iwapo msomaji hana ufahamu wowote wa kazi zilizorejelewa. Inapotokea hivyo, msomaji hana budi kuunda maana ya kazi zilizorejelea kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Hii inaaambatana na dhima ya mwingiliano matini kwa wanaubaadausasa ya kumtambua msomaji kama mshiriki katika mchakato wa ubunaji wa kazi ya kifasihi. Hivyo basi, msomaji hana budi kuunda maana zake anaposoma kazi ya fasihi zilizotumia mwingiliano matini. Baadhi ya marejeleo hata hivyo ni sahili na yamefafanuliwa moja kwa moja na msomaji anaweza kufuatilia dhamira zilizokusudiwa kwa urahisi.

Vilevile, imebainika kuwa mwingiliano matini hutumika kama njia ya kukosoa na kuhakiki kazi na mawazo ya watu mbalimbali katika nyanja tofauti. Kwa mfano katika marejeleo ya fasihi na saikolojia, mawazo ya Kezilahabi na Sigmund Freud mtawalia yamehakikiwa kama njia ya kuleta usomaji mpya wa mawazo yao. Haya yanaambatana na dhima ya wanaubaadausasa kuhusu mwingiliano matini ya kuonyesha namna matini husika ilivyoathiriwa na matini za awali. Aidha, mwingiliano matini hulenga kuziandika upya matini hizo za awali, wakati mwingine kwa njia ya kubeza.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.0 Utangulizi

Utafiti huu umebainisha mtazamo wa kibaadausasa kama kunga ya uandishi katika riwaya tatu za Kiswahili za K21, yaani, *Dunia Yao*, *Nyuso za Mwanamke* na *Unaitwa Nani*? Katika sura ya kwanza tulieleza usuli wa utafiti, suala la utafiti pamoja na madhumuni yaliyodhamiriwa kuafikiwa na utafiti. Aidha, tulifafanua misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu, mapitio ya maandishi pamoja na mbinu zilizotumiwa kukusanya na kuchanganua data. Katika sura ya pili tulifafanua kwa kina dhana ya ubaadausasa pamoja na sifa zake bainifu katika fasihi kama njia ya kuweka msingi madhubuti wa kuchanganua vipengele vya ubaadausasa katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu. Katika sura ya tatu hadi tano tulichanganua kwa kina data yetu kwa mujibu wa nadharia ya ubaadausasa. Sura hii ya sita imeangazia muhtasari wa matokea, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

## 6.1 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu uliongozwa na malengo manne makuu. Kwanza, tulidhamiria kufafanua dhana ya ubaadausasa pamoja na sifa zake bainifu katika fasihi. Pili, tulilenga kubainisha kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi na namna simulizi zenyewe zimetumika kuhakiki simulizi kuu mbalimbali. Tatu, tulilenga kuchanganua kipengele cha uhalisia mazingaombwe kama mojawapo ya vipengele vya mtindo wa ubaadausasa katika riwaya za utafiti. Hatimaye tulidhamiria kubainisha matumizi ya mwingilianomatini kama mbinu ya kimtindo na athari zake katika kufuatilia dhamira tofauti katika riwaya zilizoteuliwa za utafiti huu.

Fasili ya dhana ya ubaadausasa pamoja na matumizi yake katika fasihi yalijadiliwa katika sura ya pili. Kutokana na utafiti, ilibainika kuwa si rahisi kuifafanua dhana ya

ubaadausasa kwa njia moja kwani inahusishwa na miktadha na taaluma mbalimbali. Utafiti huu ulibainisha njia tatu kuu ambazo zinaweza kutumika kuifafanua dhana hii ya ubaadausasa. Kwanza, kwa kuzingatia misingi ya kihistoria, pili, kwa kuzingatia mtazamo wa kinadharia na kifalsafa na hatimaye kwa kuuangalia ubaadausasa kama mtindo wa kipekee wa uandishi wa fasihi. Katika misingi ya kihistoria, ilibainika kuwa ubaadausasa ulikuwa mwondoko katika mataifa ya Ulaya uliokuja baada ya mwondoko wa usasa. Mwondoko huu wa ubaadausasa unadhaniwa kuanza kati ya mwaka wa 1930 na 1960 katika mataifa ya Ulaya. Kwa hivyo, mwondoko huu haukuhusishwa kamwe na mataifa ya Afrika ambapo utafiti huu umejikita.

Katika msingi wa kinadharia, utafiti huu ulidhihirisha ubaadausasa kama mwondoko unaopinga simulizi kuu za aina yoyote ile. Hizi ni simulizi ambazo zinadai kuhodhi ukweli halisi au kutoa maelezo bia ya kuufasiri ulimwengu. Kwa mfano, ubaadausasa hupinga mamlaka kandamizi kama vile umarx, dini, utamaduni pamoja na simulizi zinazoaminiwa kuwa za kweli. Mtazamo huu wa dhana ya ubaadausasa ndio mhimili mkuu wa nadharia ya ubaadausasa. Nadharia hii imetumika katika utafiti huu kuhakiki simulizi kuu mbalimbali zilizojadiliwa katika sura ya tatu ya tasnifu hii kama kama vile maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika na uhamiaji wa Waafrika katika mataifa ya ulaya kwa lengo la kutafuta maisha bora.

Katika kujadili ubaadausasa kama mtindo maalum wa kiuandishi, ilibainika kuwa mtindo huu hudhihirisha sifa zake bainifu katika fasihi. Sifa hizo ni kama vile uchopekaji wa vipande vipande vya hadithi, mwingiliano matini, matumizi ya uhalisia mazingaombwe, matumizi ya wigo bezo, uhakiki wa simulizi kuu, uanuwai wa mawazo na ukosefu wa udhabiti katika vipengele vya ukweli na maana miongoni mwa vipengele vingine. Sifa hizi ndizo zilikuwa msingi wa kukusanya na kuchanganua data yetu katika sura ya tatu hadi ya tano. Uchanganuzi wa data hata hivyo ulijikita katika vipengele

vinne pekee, yaani, uchopekaji wa vipande vya simulizi, matumizi ya uhalisia ajabu na matumizi ya mwingiliano matini. Aidha, utafiti ulihakiki simulizi kuu mbalimbali kama zilivyojitokeza katika mchakato mzima wa utafiti.

Sura ya tatu ilichanganua matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi na uhakiki wa simulizi kuu mbalimbali. Uchanganuzi wa uchopekaji wa vipande vya simulizi uliongozwa na mhimili wa nadharia ya ubaadausasa kuwa dunia haina mshikamano. Utafiti uligundua kuwa riwaya zote za utafiti zilidhihirisha ukosefu wa mshikamano kupitia matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi badala ya kuwa na hadithi moja yenye muwala na inayofululiza kutoka mwanzo hadi mwisho kwa kila riwaya. Ilibainika kuwa kila riwaya ilisheheni vipande vidogo vidogo vya hadithi vilivyochupwa huku na kule. Aidha, matukio hayakuwa na mshikamano na muumano kutoka mwanzo hadi mwisho. Kutokana na wingi wa vijihadithi vilivyochopekwa katika kila riwaya, utafiti ulijikita katika simulizi tatu pekee zilizotawala riwaya zote tatu za utafiti. Simulizi hizi ni pamoja na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika na uhamiaji kutoka mataifa ya Afrika kwenda Ulaya. Hizi ziliteuliwa kwa maana zilikithi mahitaji ya utafiti huu kwa kujitokeza kama aina ya simulizi kuu ambazo haziwezi kuaminiwa tena. Utafiti ulizihakiki simulizi hizi kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya ubaadausasa uliotumika katika utafiti huu unaodai kuwa hakuna ukweli halisi. Katika utafiti huu simulizi kuu ilifasiliwa kama aina yoyote ya mifumo inayodai kuhodhi ukweli halisi na kutoa maelezo bia kuhusu tajriba za binadamu. Aidha, simulizi kuu ilichukuliwa kama aina yoyote ya simulizi ambayo watu wengi huiamini na kuikubali kuwa ni ya kweli na yenye umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu, hivi kwamba wengi huitegemea ili kufanya maamuzi yao.

Katika kuchanganua simulizi iliyohusiana na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, utafiti ulibainisha kuwa matarajio na matumaini ambayo Waafrika walikuwa nayo endapo wangepata uhuru kutoka kwa mkoloni hayakuafiki. Kwa mfano, uhuru katika mataifa ya Afrika uliahidi kuleta haki, usawa na maendeleo. Hata hivyo, utafiti huu ulibainisha kuwa riwaya za utafiti zimeihakiki simulizi kuu ya uhuru wa Mwafrika na kuonyesha kuwa haiwezi kuaminiwa tena. Hii ni kwa sababu matumaini yaliyoahidiwa na uhuru hayakuafiki na badala yake mataifa ya Afrika yameendelea kutawaliwa na ukosefu wa haki, ukosefu wa usawa, na ukosefu wa maendeleo kwa jumla hata baada ya uhuru. Ilibainika kuwa ukosefu wa haki na ukosefu wa usawa huendelezwa na viongozi waliojawa na tamaa, ubinafsi, ufisadi, ubadhirifu na kutojali. Viongozi hawa kujilimbikizia mali na kujitajirisha huku raia wakiendelea kufukarika, jambo ambalo huchangia katika kuzidisha pengo lililopo kati ya matajiri na maskini. Baadhi ya raia hata hivyo hushirikiana na viongozi katika kuleta ukosefu wa haki na usawa kwa kukubali kutumiwa na viongozi pamoja na kudhulumiana na kuangamizana wenyewe kwa wenyewe. Utafiti pia uligundua kuwa mataifa ya Afrika yana ukosefu wa maendeleo unaodhihirika kupitia ukosefu wa usalama, uchafuzi wa mazingira, umaskini uliokithiri, ukosefu wa kazi na miundo misingi duni. Utafiti ulibainisha kuwa hali halisi ya Mwafrika katika ulimwengu wa sasa imeendelea kuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa punde tu baada ya uhuru. Uhakiki wa simulizi hii ya uhuru ulibainisha kuwa, hali mbaya ya Waafrika baada ya uhuru inaweza kuhusishwa na Waafrika wenyewe, licha ya kuwa wakoloni ndio waliopanda mbegu za ubinafsi na kutojali. Iwapo mabadiliko chanya yatatokea, wananchi wenyewe ndio wanapaswa kubadilika kwanza na kuacha ubinafsi, tamaa, ufisadi na aina nyingine za uozo.

Mfano wa pili wa uchopekaji wa vipande vya simulizi ulihusiana na ajenda za mataifa ya kigeni kwa mataifa ya Afrika pamoja na mbinu wanazozitumia kuendeleza ajenda

hizo. Utafiti huu ulibainisha kuwa, kwa mtazamo wa nje mataifa ya Ulaya huonekana kuyajali na hata kuyasaidia mataifa ya Afrika hasa kwa kutoa misaada na kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Hata hivyo, uhakiki wa simulizi hii umebainisha kuwa ufadhili unaotolewa kwa mataifa ya Afrika hulenga kuyanufaisha mataifa ya Ulaya na kutimiza ajenda zao kwa njia iliyofichika. Kwa hivyo, mataifa ya Ulaya huwa kama sarafu yenye pande mbili; upande wa huruma ambao unadhihirika kutokana na utoaji wa misaada kwa mataifa ya Afrika, na upande wa maangamizi, ambapo misaada inayotolewa hutumika kuyadhibiti mataifa ya Afrika kiuchumi. Kutokana na utafiti ilibainika kuwa baadhi ya ajenda za mataifa ya Kigeni kupitia utoaji wa misaada ni pamoja na kutafuta soko la bidhaa zao, kutafuta uwanja wa kufanyia utafiti wa bidhaa na magonjwa mapya kama ukimwi na hatimaye kuyatawala kiuchumi mataifa ya Afrika. Ili kutimiza ajenda hizi, utafiti ulibainisha mbinu tofauti ambazo mataifa ya kigeni hutumia. Kwa mfano, wanaeneza kasumba potovu inayolenga kuwatukuza watu na bidhaa kutoka Ulaya huku ikiwatweza watu na bidhaa kutoka Afrika. Aidha, wanatoa misaada na kuanzisha miradi mbalimbali inayotumika kama chambo cha kufurahisha, kuchochea utiifu na kuteka fikra za watu wa mataifa ya Afrika ili wasitambue kwa urahisi ajenda za mataifa ya Ulaya na kuzisaili. Vilevile wanawekeza katika mataifa ya Afrika na kuunda sheria zinazolenga kuwanufaisha. Mataifa yanayopinga ajenda za mataifa ya Ulaya na kukosa kutii amri na masharti waliyowekewa yanawekewa vikwazo kama njia ya kuyaadhibu. Katika enzi hizi za utandawazi, vyombo vya habari vinatumika kueneza baadhi ya ajenda za mataifa ya Ulaya pamoja na kuueneza utamaduni wao unaorahisisha kutimizwa kwa ajenda hizi kandamizi. Hatimaye mataifa ya Ulaya yanafaulu katika kuyadhibiti na kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi na kitamaduni. Hata hivyo, imebainika kuwa mataifa ya Afrika pia yamechangia pakubwa katika kufaulu kwa ajenda hizi za mataifa ya Ulaya.

Waafrika hivyo basi wanapaswa kutilia shaka simulizi inayohusiana na ajenda za mataifa ya kigeni barani Afrika kwa mujibu wa mojawapo ya mihimili ya nadharia ya baadausasa kama ilivyoelezwa na Lyotard (1979). Badala yake Waafrika wanapaswa kuunda simulizi ndogo kwa kutafuta mbinu zitakazowawezesha kujishughulisha kikamilifu katika kuujenga uchumi wa nchi zao.

Katika simulizi ya tatu tulijadili kuhusu suala la uhamiaji na athari zake. Tuliona wahamiaji wengi wanaotoka nchi za Afrika huenda nchi za Ulaya kutafuta kazi na maisha bora. Hii ni simulizi kuu inayoaminiwa na Waafrika wengi kuwa maisha katika mataifa ya Ulaya ni bora kuliko yale ya Mataifa ya Afrika. Hata hivyo ilibainika kuwa wahamiaji hawayapati maisha hayo mazuri waliyoyatarajia. Badala yake wanapatana na changamoto nyingi kuanzia maandalizi ya safari hadi kwenye maisha yenyewe huko ulaya. Baadhi ya changamoto hizo ni mahitaji ya kiasi kikubwa cha fedha, ukosefu wa kazi na inapopatika huwa duni na yenye malipo duni. Hii huambatana na ukosefu wa makazi na hatimaye kupatwa na magonjwa kama kiherehere kwa sababu ya kutamauka. Utamaushi unatokana na kutotimizwa kwa ndoto ambazo wahamiaji walikuwa nazo wakienda Ulaya, yaani, kuwa maisha yao yangekuwa afadhali. Aidha, makosa ya wahamiaji ya kuzichanachana paspoti zao asilia na kuchukua uraia mpya kama wakimbizi unakatiza ndoto yao ya kuwahi kurudi nyumbani tena. Kwa hivyo, wahamiaji wanaotoka Afrika huishia kuwa watumwa katika nchi za Ulaya. Utafiti hivyo basi ulibainisha kuwa simulizi kuu inayohusiana na uhamiaji ili kutafuta maisha bora haiwezi kuaminiwa tena kwa sababu wahamiaji hatimaye huishia kuwa kama watumwa katika mataifa ya ulaya. Utafiti hivyo basi ulibainisha kuwa Waafrika hawana budi kuzinduka na kutafuta njia mbadala za kukabiliana na hali zao ili kujikimu na kujiendeleza.

Katika kujadili simulizi zote tatu, yaani, maana ya uhuru kwa mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya kwa mataifa ya Afrika pamoja na mbinu wanazozitumia kuziendeleza ajenda hizo na hatimaye uhamiaji na athari zake, utafiti uligundua kuwa kila simulizi ilisheheni matumizi mengi ya mbinu rejeshi. Hii ilimbidi mtafiti kwenda mbele na nyuma katika usomaji ili kuweza kufuata msuko wa kila kijihadithi. Utafiti basi uligundua kuwa matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi unaweza kuwa kikwazo katika kufuatilia dhamira na matukio katika riwaya za kibaadausasa na kizifanya zionekane kuwa ngumu kueleweka.

Mbali na kuzihakiki simulizi zilizochopekewa huku na kule, ilibainika kuwa matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi kwa jumla ni mbinu ya uandishi wa kibaadausasa inaopinga simulizi kuu iliyohusiana na uandishi wa riwaya kama ilivyopendekezwa na akina Aristotle na Plato kuwa matukio yanafaa kuwa na mshikamano na muumano wa hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Nadharia ya ubaadausasa hupinga mifumo na mawazo yote yanayolazimisha watu kufuata kaida fulani, kama walivyopendekeza kina Plato na Aristotle kuhusu namna ya kuifasiri riwaya. Mawazo kama haya huchukuliwa kuwa kandamizi. Badala yake wanaubaadausasa hupendekeza matumizi ya njia anuwai katika kueleza tajriba za binadamu. Utafiti ulibainisha kuwa matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mojawapo ya njia za kijarabati zinazotumiwa na waandishi za riwaya za utafiti kubainisha njia tofauti ya kuiandika na kuifasiri riwaya.

Isitoshe, ilibainika kuwa matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi ni dhihirisho la hali halisi ya mataifa ya K21 ambayo hayana mshikamano bali yamejaa fujo na ghasia za kila aina. Kwa mfano, katika riwaya za utafiti fujo na ghasia katika mataifa ya Afrika zilidhihirika kupitia changamoto ambazo mataifa haya yanapitia kama vile kama ukosefu wa kazi, umaskini uliokithiri, miundo misingi duni, kudhibitiwa na

kutawaliwa kiuchumi na kufanywa watumwa miongoni mwa masaibu mengine yanayoyakumba mataifa ya bara la Afrika.

Sura ya nne ilichanganua matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama kipengele mojawapo cha mtindo wa uandishi wa ubaadausasa ulivyojitokeza katika riwaya za utafiti. Uchanganuzi wa matumizi ya uhalisia mazingaombwe uliongozwa na mhimili wa nadharia ya ubaadausasa unaodai kuwa kazi za kibaadausasa hazibainishi mipaka ya wazi kati ya uhalisia, ndoto, fantasia na umazingaombwe. Uchanganuzi ulidhibitisha kuwa riwaya za utafiti zilitumia uhalisia ulioenda sambamba na umazingaombwe katika kuwakilisha wahusika, matukio na matendo mbalimbali. Haya yalidhihirika kupitia matumizi ya wahusika wa ajabu ajabu kama vile mizuka, vivuli na wafu ambao wanatenda kama viumbe katika ulimwengu halisi. Aidha, binadamu wa kawaida wenye sifa na uwezo wa ajabu kama vile kuwasoma watu pia ilikuwa dhihirisho la uhalisia mazingaombwe katika riwaya za utafiti. Vilevile uhalisia mazingaombwe ulidhihirika kupitia matukio mbalimbali ya ajabu kama vile kuwepo na mawasiliano kati ya watu halisi na watu katika albamu.

Utafiti uligundua kuwa matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mbinu ya kimtindo katika riwaya za utafiti ni dhihirisho la upya katika fasili ya riwaya inayopinga fasili ya awali iliyojikita katika uhalisia. Katika riwaya za kimapokeo, wahusika na matukio yalihitajika kuakisi ulimwengu halisi kama tuujuavyo. Wanamapokeo basi walitumia kigezo cha uhalisia kama msingi wa kuifafanua riwaya. Hata hivyo, riwaya za utafiti huu zilizojikita katika uandishi wa kibaadausasa zimekiuka kaida hii ya kihalisia kwa huchanganya uhalisia na umazingaombwe. Haya yanaambata na mojawapo ya mhimili mkuu wa nadharia ya ubaadausasa inayopinga aina yoyote ya simulizi kuu, hususan uhalisia, na kupendekeza matumizi ya njia anuwai za kueleza tajriba za binadamu. Ilibainika kuwa matumizi ya uhalisia mazingaombe katika riwaya za utafiti basi ni

dhihirisho la njia anuwai za kujieleza bila kufungwa na mbinu ya uandishi wa kimapokeo iliyojikita katika uhalisia.

Aidha, ilibainika kuwa mtindo huu wa uandishi umetumika kuwakilisha ulimwengu wa sasa uliojaa fujo, ghasia na mambo mengine ya ajabu ambayo yamesababisha kutokuwepo na mshikamano katika K21. Mambo haya ya ajabu yanadhihirika kupitia namna mataifa ya ulaya hutumia nguvu zisizopingika ili kuyadhibiti mataifa ya Afrika kiuchumi na kitamaduni kama ilivyojadiliwa katika sura tatu ya tasnifu hii. Kwa mfano, katika *DY* tunaelezwa kuwa mataifa ya ulaya, hususan Marekani, yanawekea mataifa ya ulimwengu wa tatu masharti ya kufuatwa, na yanapojaribu kuyapinga masharti hayo, yanaadhibiwa (uk.45-46). Jambo hili ni dhihirisho la ukoloni mamboleo katika K21unaoathiri mataifa ya Afrika kwa njia ya ajabu. Kwa hivyo, riwaya za kibaadausasa hazina budi kutumia uhalisia unaenda sambamba na umazingaombwe ili kudhihirisha hali halisi ya ulimwengu wa sasa iliyojaa mambo mengi ya kiajabu, kama ilivyojitokeza katika riwaya za utafiti huu.

Katika sura ya tano, tulichanganua matumizi ya mwingilianomatini kama kunga ya uandishi katika riwaya za utafiti huu. Uchanganuzi uliongozwa na nadharia ya Ubaadausasa ambayo hupuuza simulizi kuu, kama vile Usasa, na badala yake kuibuka na njia anuwai za kujieleza. Ilibainika kuwa mwingiliano matini ulitumika kukaidi itikadi ya mwondoko wa Usasa uliopendekeza uasili wa kazi za sanaa. Badala yake, riwaya zilizotafitiwa zilitambua kazi nyingine za awali kupitia matumizi ya mwingiliano matini. Ilibainika kwamba riwaya zote za utafiti huu zilidhihirisha mwingiliano matini kupitia matumizi ya marejeleo ya kazi mbalimbali za waandishi wengine. Baadhi ya matini zilizorejelewa ni pamoja na marejeleo ya fasihi ya Kiswahili, marejeleo ya fasihi ya Kiingereza, marejeleo ya filamu, marejeleo ya kidini,

marejeleo ya mashujaa tofauti wa Kihistoria, pamoja na marejeleo ya wanafalsafa na wanasaikolojia mbalimbali.

Utafiti ulibainisha kuwa waandishi wa riwaya za utafiti huu walitumia viwango vitatu vya mwingilianomatini, yaani, mwingiliano matini dhahiri, mwingiliano matini usodhahiri na mwingiliano matini linganifu. Katika mwingiliano matini dhahiri, tulipata urejeleaji wa vipengele mahususi kutoka matini nyingine zilizoingizwa katika riwaya za utafiti. Hapa, mawazo yanayorejelewa yaliambatanishwa na jina la mwandishi au/na jina la kitabu. Kwa mfano, katika *NZM* tunaelezwa kuwa, "…nilijaribu tu…kuileza mbele… kwa kuitazama nyuma…kule kwenye jipu…jipu la **Abdilatif Abdalla wa *Sauti ya Dhiki*.**.." (uk 83). Hapa jina la mwandishi, Abdilatif Abdalla, pamoja na kitabu ambapo mawazo hayo yametokea, yaani, *Sauti ya Dhiki*, yametajwa. Katika mwingiliano matini usodhahiri, mawazo au majina ya wahusika walitajwa tu bila kuelezwa yaliponukuliwa. Kwa mfano, katika *UNN* tunapata marejeleo haya " …tunataka jina la wanawake tunaowajua … kama **Hawa, Jezebel, Delilah**… (uk 15). Hapa tunapata majina tu ya wahusika, yaani Hawa, Jezebel na Delilah lakini hatujaelezwa walichokifanya au wanahusishwa na mwandishi au kitabu kipi. Katika mwingiliano matini linganifu, kulikuwa na ulinganifu wa kimawazo kutoka riwaya ya *NZM* na riwaya ya Kiingereza ya *The Collector*. Hapa matendo ya wahusika Nana na Faisal katika *NZM* yana ushabaha wa karibu na yale ya Clegg na Miranda katika *The Collector* mtawalia.

Utafiti uligundua kuwa mwingiliano matini ulitumiwa kuendeleza dhamira tofauti katika riwaya za utafiti. Baadhi ya dhamira hizo ni pamoja na utabaka, utu na uwajibikaji, ukabila na vita vya wenyewe kwa wenyewe, mahusiano ya kijamii na utambulisho wa kijinsia miongoni mwa dhamira nyingine. Kwa mujibu wa nadharia ya ubaadausasa, dhamira hizi zimetumika kudhibitisha ukosefu wa mshikamano katika

dunia ya sasa kwa kuonyesha baadhi ya matatizo yanayoyakumba mataifa ya Afrika katika karne ya ishirini na moja. Aidha, ilibainika kuwa matumizi ya mwingiliano yalidhihirisha namna waandishi wa riwaya za utafiti walivyoathiriwa na matini za awali na namna walivyotumia kazi za waandishi wengine kama malighafi ya kuunda kazi zao.

Utafiti vilevile ulibainisha kuwa matumizi ya mwingiliano matini wakati mwingine yanaweza kumtatiza msomaji katika kufuatilia dhamira tofauti iwapo msomaji hana ufahamu wowote wa kazi zilizorejelewa. Inapotokea hivyo, msomaji huwa hana budi kuunda maana ya kazi zilizorejelewa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Hii inaaambatana na dhima ya mwingiliano matini kwa wanaubaadausasa ya kumtambua msomaji kama mshiriki katika mchakato wa ubunaji wa kazi ya kifasihi. Hivyo basi, msomaji hana budi kuunda maana zake anaposoma kazi ya fasihi zilizotumia mwingiliano matini.

Vilevile, utafiti uligundua kuwa mwingiliano matini ulitumika kama njia ya kukosoa na kuhakiki kazi na mawazo ya watu mbalimbali katika nyanja tofauti. Kwa mfano katika marejeleo ya fasihi, S.A Mohamed katika *DY* anayahakiki mawazo ya Euphrase Kezilahabi kuwa dunia ni uwanja wa fujo. Licha ya kuwa Mohamed anakubali kuwa dunia imejaa fujo na ghasia anasaili mawazo ya Kezilahabi kuhusu falsafa yake ya jaala na kuonyesha kuwa binadamu wenyewe ndio chanzo cha fujo na ghasia hizo na wenyewe ndio wanaoweza kuzimaliza. Aidha, Kyallo Wamitila katika *UNN* anayasaili mawazo ya Sigmund Freud kuhusu suala la utambulisho ambapo mwanamke anatambulishwa kwa misingi ya mwanamume. Katika msingi huu mwanamke anaelezwa kama kiumbe dhaifu kwa sababu hana zubu. Wamitila anayasaili mawazo haya kwa kupendekeza kila kiumbe kipewe utambulisho wake binafsi bila kuhusishwa na kiumbe kingine. Ilibainika kuwa mwingiliano matini ulitumiwa kama mbinu ya

uandishi katika riwaya za ubaadausasa ili kuhakiki, kubeza na kusaili simulizi kuu za waandishi watajika kwa lengo la kuleta usomaji mpya wa mawazo mbalimbali.

### 6.2 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, imebainika kuwa mtindo wa uandishi wa ubaadausasa ni kunga kuu ya uwasilishaji wa riwaya Kiswahili za katika K21. Ubaadausasa umejitokeza kama nadharia ya uhakiki na pia kama mtindo maalum wa uandishi katika fasihi, hususan, fasihi ya Kiswahili. Nadharia ya ubaadausasa ndiyo imeongoza utafiti huu kupitia mihimili yake mikuu. Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa umetumika kama mtindo wa kimajaribio wa uandishi wa riwaya za Kiswahili za K21 unaokaidi uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Sifa zake bainifu zimedhihirika kupitia matumizi ya uchopekaji wa vipande vya hadithi, uhalisia mazingaombwe na mwingiliano matini. Katika uchopekaji wa vipande vya simulizi imebainika kuwa hadithi katika riwaya za utafiti hazina mshikamano na muumano kutoka mwanzo hadi mwisho kama ilivyopendekezwa na akina Aristotle na Plato. Badala yake kuna vipande vipande vya hadithi ambavyo vimechupwa huku na kule. Vipande hivi vya simulizi vimeelezwa kupitia matumizi mengi ya mbinu rejeshi na inambidi msomaji kwenda mbele na nyuma ili kufuata msuko wa hadithi. Hali hii aghalabu humtatiza msomaji katika kufuatilia ujumbe unaokusudiwa na mwandishi. Aidha, matumizi ya uhalisia mazingaombwe unakiuka uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia ambapo wahusika na matukio yaliakisi ukweli kama tunavyoujua. Badala yake tunapata uhalisia unaoenda sambamba na umazingaombwe hivyo basi kufuta mipaka kati ua uhalisia na umazingaombwe. Matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi na uhalisia mazingaombwe ni dhihirisho la hali halisi ya ubaadausasa ambayo haina mshikamano na imejaa mambo mengi ya ajabu yasiyoelezeka. Mwingiliano matini umetumika kwa wingi katika riwaya za utafiti ambapo matini nyinginezo zimerejelewa kama njia ya

kutambua kazi za waandishi wengine walioathiri waandishi wa riwaya za utafiti. Matini zilizorejelewa ni zile za kifasihi kidini, kifasihi, kihistoria, filamu, pamoja na matini za kisaikolojia na kifalsafa. Mwingiliano matini umetumika kuendeleza dhamira mbalimbali katika riwaya. Aidha, umetumika kama malighafi ya kuunda riwaya zenyewe kwa kuyahakiki mawazo ya waandishi wengine.

Kimaudhui, riwaya za ubaadausasa hukakiki simulizi kuu mbalimbali na kuonyesha kuwa haziwezi kuaminika tena. Simulizi hizo ni kama vile maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya kigeni barani Afrika na uhamiaji. Kutokana na uhakiki wa simulizi kuu hizi imebainika kuwa watu wa mataifa ya Afrika wanapitia changamoto ainati kama vile ukosefu wa haki, ukosefu wa usalama, ukosefu wa maendeleo, kudhibitiwa kiuchumi na mataifa ya ulaya, pamoja na kutumikishwa kwa wahamiaji wanaoenda nchi za ughaibuni. Changamoto hizi zinadhihirisha hali halisi ya ulimwengu wa sasa ambao hauna mshikamano bali umejaa fujo na ghasia za kila nui. Hivyo basi, riwaya zinawazindua Waafrika ili waweze kutafuta njia mbadala za kuyatatua matatizo yanayowakumba. Aidha, mwingiliano matini umetumika kuyahakiki mawazo ya waandishi tajika katika nyanja tofauti kama vile fasihi na saikolojia ili kuyasaili mawazo yao. Lengo kuu ni kubainisha kuwa simulizi hizo haziwezi kuaminiwa tena. Hivyo basi, waadishi wa riwaya za utafiti wanadhamiria kuleta usomaji mpya wa kazi hizo za awali.

Kwa kutamatisha, utafiti huu umefaulu katika kukuza ujuzi na ufahamu wa sifa bainifu za mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya ya Kiswahili. Ujuzi huu utawafaidi wasomi na wapenzi wa Kiswahili katika kuzielewa na vilevile kuzihakiki riwaya na kazi nyinginezo za fasihi ya Kiswahili, zilizoandikwa kwa kutumia mtindo wa uandishi wa Ubaadausasa.

Hali kadhalika, tasnifu hii imechangia katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili na lugha ya Kiswahili kupitia utafiti, na ni sehemu ya mkusanyiko wa maandishi yaliyoandikwa kwa Kiswahili.

## 6.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia ubaadausasa kama kunga ya uandishi katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa K21. Hata hivyo, utafiti huu uliacha mapengo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi. Kwanza, ni muhimu utafiti mwingine ufanywe wa riwaya zilizoandikwa baada ya mwongo wa kwanza wa K21 ili kubainisha iwapo kuna mabadiliko zaidi ya riwaya ya Kiswahili ya K21. Pili, ni muhimu utafiti ufanywe katika tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili kama vile tamthilia na ushairi ili kubainisha namna vipengele vya ubaadausasa vinavyojitokeza katika tanzu hizo. Tatu, utafiti ulijikita katika vipengele vinne tu vya ubaadausasa, yaani, uhakiki wa simulizi kuu, uchopekaji wa vipande vya simulizi, uhalisia mazingaombwe na mwingiliano matini. Kuna haja ya kutafitia vipengele vingine vya ubaadausasa katika fasihi ya Kiswahili kama vile ukosefu wa udhabiti katika ukweli na maana, ujirejeleaji, ubunaji na ubandikaji.

## MAREJELEO

Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Oxford: Oxford University Press.

Anderson, R. L. (2022) Fredich Nietzsche. Katika: Zalt E. N. (mhr). *The Stanford Encyclopedia of Philosophy*. Stanford: Stanford University.

Bakari, M. (2008). "Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za Babu Alipofufuka (2001), Bina_Adam! (2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa Sadiki Ukipenda (2002)". Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya MA (Haijachpishwa).

Bakhtin, M. (1984). *Rabelias and His World*. Bloomington, IN: Indiana University Press

Baldick, C. (2008). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York: Oxford University Press.

Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester: Manchester University Press.

Baudrillard, J. (1981). *Simulacra and Simulation*. Ann Arbor, MI: University of Michigan Press.

Bernstein, C. (1987). Centering the Postmodren In the Middle of Modernism in the Middle of Capitalism on the Outskirts of New York…*Socialist Review* 17(6) 45-56.

Berrett, T. (1997). Modernism and Postmodernism: An Overview with Art Examples. Katika: Hutchens, J. & Suggs M. (whr). *Art Education: Content and practice in a Postmodern Era.* Washington, DC: NAEA.

Bertoncini, Z. E. (2002). When Grandfather came to Life Again: Said Ahmed Mohamed's New Novel beyond Realism. *Swahili Forum* IX: 25-33.

Bertoncini, Z. E. (2006). Globalization unmasked in Two Kiswahili Novels (A Posmodernists Challenge). *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI*. Dar es Salaam: TUKI pp. 85-94.

Bertoncini, Z. E., Gromov, M. D., Khamis S. A. na Wamitila, K. W. (2009) *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction and Drama.* Leiden: Brill.

Best, S. na Keller, D. (1991). *Postmodern Theory: Critical Interrogations*. London: Routledge.

Biblia (1952). *The Holy Bible in Kiswahili* (Union Version). United Bible Societies.

Bjornsson, B. (2006). Postmodernism and the Simpsons: Intertextuality, Hyperreality and Critique of Metanarratives. An unpublished Bachelor of Arts Thesis. Iceland: University of Iceland Press. Mtandao: www.snpp.com/other/papers/bf.paper.pdf.

Bowers, M. A. (2004). *Realism*. New York: Routledge.

Brodribb, S. (1992). *Nothing Mat(t)ers: A Feminist Critique of Postmodernism*. North Melbourne: Spinifer Press Ltd.

Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Harpenden, Pocket Essentials.

Childs, P. na Fowler, R. (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. London: Routledge.

Clayton, J. W. (2012). Some Common Themes and Ideas within the Field of Postmodern Thought. A Handout for HIS 389. Mtandao: http://webs.wofford.edu/whisnantcj/his389/postmodernism.pdf. Last modified Nov 19, 2022.

D'haen, T. L. (2005). "Magical Realism and Postmodernism: Decentreing Privileged Centres". Katika: Zamora, L. P. & Faris W. B. (1995) (whr). *Magical realism: Theory, History, Community*. Durham: Duke University Press.

Deleuze, G. na Guattari, F. (1980). *A Thousand Plateaus*. London: Bloomsbury Academic.

Deleuze, G. na Guattari, F. *Anti-Oedipus:* (1972). Kimetafsiriwa na Hurley, R., Seem, H. M. & Lane, H. R. (1983). London: The Athlone Press.

Diegner, L. (2005). Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel: Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and William Mkufya's *Ziraili na Zirani*. *Swahili Forum* vol 12: 25-35.

Eagleton, T. (1996). *Literary Theory: An Introduction*. Malden, Blackwell Publishing.

Fairclough, N. (2006). *Discourse and Social Change*. Cambridge: Polity Press & Blackwell Publishing Ltd.

Forster, E. M. (2002). *Aspects of the Novel*. New York: RosettaBooks LLC.

Foucault, M. (1961). *Madness and Civilization: A History if Insanity in the Age of Reason.* Watafsiri: Murphy, J. na Khafla, J (1964). New York: Vintage Books.

Fowles, J. (1964). *The Collector*. London: Reprint Society.

Giddens, A. (2002). *Runaway World: How Globalisation is shaping our Lives*. London: Profile Books.

Gooding-Williams, R. (2020). W.E.B. Du Bois Katika: Zalt E. N. (mhr). *The Stanford Encyclopedia of Philosophy*. Stanford: Stanford University.

Goring, P., Hawthorn, J. na Mitchell, D. (2010). *Studying Literature (2nd Edition)*. London: Bloomsbury Publishing PLC.

Grant, I. H. (2001). 'Postmodernism and Politics'. Katika: Sim S. (mhr). *The Routledge Companion to Postmordernism*. London: Routledge.

Grenz, S. J. (1996). *A Primer on Postmodernism*. Cambridge: William B. Eerdmans Publishing Company.

Gromov, M. D. (1989). Nagona and Mzingile: Novel, Tale or Parable?Afrikanistische Arbeitspapiere (AAP) 55 *Swahili Forum* V: 73-78.

Gromov, M. D. (2008). Fasihi ya Kiswahili na Nadharia ya Fasihi. Katika: N.O.Ogechi, N. L. Shitemi na K. Simala. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi Univresity Press.

Gromov, M. D. (2019). “Riwaya mpya”, majina mapya, changamoto mpya: kuhusu maendeleo ya “riwaya ya majaribio” katika fasihi ya Kenya. Katika: *Eastern African Literary and Cultural Studies,* 5:3-4, 200-213.

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learners Dictionary, 7th Edition*. New York: Oxford University Press.

Hussein, E. N. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Hutcheon, L. (1988/2005). *A Poetics of Postmodernism: History, Theory, Fiction*. New York: Routledge.

Jameson, F. (1991). *Postmodernism, or, the Cultural Logic of Late Capitalism*. Durham: Duke University Press.

Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Khamis, S. A. M. (2003). Fragmentation, Orality and Magic Realism in Kezilahabi’s Novel, Nagona. *Nordic Journal of African Studies*. 12(1): 78-91.

Khamis, S. A. M. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel. *Research in African Literatures* 36(1): 91-108. Project Muse: Indiana University Press.

Khamis, S. A. M. (2005b). Book Review by Alain Ricard (2000). Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism. *Nordic Journal of African Studies*. 14(3): 409-418.

Khamis, S. A. M. (2007). The Swahili Novelist at the Crossroad: The Dilemma of Identity and Fecundity. *Swalihi Forum,* 14: 165-180.

Khamis, S. A. M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili. Katika: N.O.Ogechi, N. L. Shitemi na K. Simala. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi Univresity Press.

Kimugung, S. K. (2015). Mitindo Mamboleo ya Ubaadausasa katika Nyimbo Teule za Jamii ya Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja. Eldoret: Chuo kikuu cha Moi. Tasnifu ya MA (Haijachapishwa).

King’ei, K. (2000). *Mwana Kupona: Poetess from Lamu*. Nairobi: Sasa Sema Publication.

Klages, M. (2006). *Literary Theory: A Guide for the Perplexed.* London: Continuum.

Kusnir, J. (2011). *Postmodernism in American and Australian Fiction*. PULIB, University of Presov. Online publication: http/:www.pulib.sk/elpub2/FF/kusnir1/index.html. Accessed 14/7/2015 at 12.30 p.m.

Laura, L. D. (2015). “Believe in these Things”: Magical Realism’s use of Religious Language. Tennessee: Chuo Kikuu cha Tennessee. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).

Lewis, B. (2001). ‘Postmodernism and Literature’. Katika: Sim S. (mhr) (2001). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge

Lyotard, J. F. (1979). *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Kimetafsiriwa na Bennington, G. & Massumi, B. (1987). Manchester: Manchester University Press.

Lyotard, J. F. (1988). *Heidegger and "the Jews*". Kimetafsiriwa kwa Kiingereza na Michel, A. na Roberts, M.S. (1990) London: University of Minnesota Press.

Magaju, J. K. (2004). "Uhalisiajabu katika Riwaya ya Babu Alipofufuka (2001) ya S.A.Mohamed na Bina-Adam! (2002) ya K. W. Wamitila". Nairobi: Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).

Matei, A. K. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet and Media services Ltd.

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

McLeod, S. A. (2013). Freud's Theory of Personality: Id, Ego and Superego. *Simply Psychology*. London: Psychology Press. Mtandao: http://www.simplypsychology.org/psych.html. Retrieved Mei, 23, 22023 at 1:30pm.

Mencinger, J. (2003). Does Foreign Direct Investment Always Enhance Economic Growth? *Kyklos* vol 56 (4): 491-508.

Mohamed, M. S. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, M. S. (2000). *Kiu*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S. A (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*.

Mohamed, S. A. (2006 [1980]). *Dunia Mti Mkavu Mkavu*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mojola, A. O. (2002). Modernity, Post-Modernity and the Information Age: Prospects and Challenges for African Theological Education in the Twenty-First Century. *Chemchemi Internationa Journal of the School of Humanities and Social Sciences* vol 2(1): 1-21.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto.* Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Morgan, D. (2001). 'Postmodernism and Architecture'. Katika: Sim S. (mhr) (2001). *The Routledge Companion to Postmordernism*. London, Routledge.

Mulila-Matei, A. K. (2014). "Discourse, Gender Identity and Gender Power Relations in Fiction. A Critical Discourse Analysis and Systemic Functional Grammar Reading of Wamitila's *Unaitwa Nani*?" Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamifu (Haijajapishwa).

Mwamzandi, I. Y. (2013). Riwaya za Karne ya 21 na udurusu wa nadharia za Fasihi. *Swahili Forum 20 (48-66).*

Ndege, P. O. (2009). "Colonialism and its Legacies in Kenya". Lecture Delivered during Fulbright – Hay Group Project Abroad Program: July 5th-August 6th 2009. Eldoret: Moi University.

Ngesa, A. K., Enock Matundura na John Kobia (2015). Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: Mashetani na Kijiba Cha Moyo. *Swahili Forum* 22(2015): 42-71

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Kifasihi. Tasnifu ya Ph.D. (Haijachapishwa).

Oduori, R. (2007) "Kikaza". Katika Walibora, K. na Mohamed S. (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Macmillan.

Olali, T. (2008). *Mafamba*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2015). *Mashetani ya Alepo*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Pollheide, J. (2003). Postmodernist Narrative Strategy in the Novels of John Fowles. Unpublished Ph.D Thesis. Bielefeld: Bielefed University.

Ritgerotil, B. A. (2006). *Postmodernism and The Simpsons: Intertextuality, Hyperreality and Critique of Metanarratives.* London: Routledge.

Rivkin na Ryan (2004). *Literary Theory – An Anthology* (Second Edition). Malden: Blackwell Publishing.

Salenius, C. (2009). From the Margins to the Mainstream: Magical realism and Feminism in Alice Hoffman's *Practical Magic* and Joanne Harns's *Chocolat*. Unpublished MA Thesis, University of Tampere.

Schmitz, T. A. (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: An Introduction*. Malden: Blackwell Publishing.

Selden, R., Widdowson, p. na Brooker, p. (2005). *A Readers Guide to contemporary Literary Theory.* Harlow, Pearson Education Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU

Sharma, R. na Chaudhary, P. (2011). Common Themes and Techniques of Postmodern Literature of Shakespeare. *International Journal of Educational Planning and Administration*, 1(2): 189-198.

Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.

Sim, S. (2001). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge.

Sim, S. (2013). *Fifty Key Postmodern Thinkers*. London: Routledge.

Strecher M. C. (1999). Magical Realism and the Search for Identityin the Fiction of Murakami Haruki. *Journal of Japanees Studies* Vol 25(2) pp 263-298.

Taylor, C. (2004). *Modern Social Imaginaries*. Durham: Duke University Press.

Tilak, R. (1993). *History & Principles of Literary Criticism.* New Delhi: Rama Brothers.

Traore, F. A. (2015). Postmodernism as seen through the Swahili Novel: A reading of *Babu Alipofufuka* and *Dunia Yao* by Said Ahmed Mohamed. Katika: *Journal of African Cultural Studies*, 27(1): 20-29.

TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary (3rd Edition)*. Dar es Salam: Institute of Kiswahili Research.

TUKI (2018). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Waliaula, K. W. (2010). Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum. Swahili Forum*, 17: 143-157.

Wamitila K. W. (2002). *Bina- Adam*! Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo*. *Kiswahili* 66: 49-58.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Musaleo!* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Unaitwa Nani?* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Watt, I. (2000). *The Rise of the Novel: Studies in Defoe, Richardson and Fielding*. London: PIMLICO.

Wegesa, B. na Macharia, S. N. (2008). Postmodernism or Chaos? Theoretical Considerations in Reading New Directions in Some Cultural Practices in Kenya. Katika: N. O. Ogechi, N. L. Shitemi na K. Simala (whr). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press, pp 319-329.

Wolfreys, J., Robbin, R. na Womack, K. (2006). *Key Concepts in Literery Theory*. Edinburgh, Edinburgh University Press Ltd.

Zakin, E. (2011). Psychoanalytic Feminism. Katika: Zalta, E. N. (mhr). *The Stanford Encyclopedia of Philosophy*. Stanford: Stanford University.

Zamora, L. P. na Faris W. B. (1995). *Magical realism: Theory, History, Community*. Durham: Duke University Press.